**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 5 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):**

Taarifa ya Mwaka ya Benki ya Rasilimali ya Tanzania kwa Mwaka 2004 *(The Annual Report of the Tanzania Investment Bank Limited for the Year 2004)*

Taarifa ya Mwaka na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation of Tanzania* kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2004 (*The Annual Report and Audited Financial Statements of Consolidated Holding Corporation of Tanzania for the year ended 31ST December, 2004).*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM (K.n.y. MHE. KHAMIS ALI SALEH) - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI:-**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 196

**Vyombo vya Habari**

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (K.n.y. MHE. WILFRED M. LWAKATARE)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa utaratibu wa Taasisi za Umma za habari ni wa kibiashara ili kujipatia mapato:-

(a) Je, ni utaratibu gani umewekwa kwa vyombo vya habari kama TVT na Redio Tanzania wa kurusha matangazo yanayohusu vyama vya siasa?

(b) Je, ni fedha kiasi gani hulipwa kwa dakika pindi wahitaji wanapotaka kurusha habari zao kupitia vyombo hivyo?

(c) Je, ni vyama vipi vya siasa tangu mwaka 2004 – 2005 vimebahatika kutumia vyombo hivyo na vimelipa kiasi gani cha fedha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB )** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a), (b)na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari kama vile TVT na *RTD* hurusha habari zote kwa kuzingatia misingi ya taaluma ya Uandishi wa Habari, Sheria na Kanuni za Nchi, Sera ya Habari na pia kwa kuzingatia maslahi ya Nchi yetu. Kwa maana hiyo, vyombo vya habari vya utangazaji vitarusha habari za vyama vya siasa ambazo zinalinda maslahi ya Taifa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna malipo kwa habari zinazorushwa katika kipindi cha taarifa ya habari na matukio kama vile Majira au Harakati. Hata hivyo, vyombo

habari hupokea matangazo ya biashara na huduma za jamii, ambayo hulipiwa kwa viwango vinavyozingatia wakati na muda wa kutangaza.

Aidha, vyombo hivi hutoa matangazo yanayolipiwa kwa vipindi maalum kwa maombi ya wateja kama vile Vyama vya Siasa, Mashirika, Wizara na Idara za Serikali. Viwango vya matangazo hayo vipo wazi na vinapatikana katika *rate cards* ambazo ziko kwenye Idara ya masoko ya Taasisi ya Utangazaji (TUT)

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2004 hadi mwaka huu wa 2005, ni Vyama vya *CUF* na CCM tu ndivyo viliomba kutangaziwa Mikutano yao Mikuu kupitia vyombo vya habari vya umma. CCM iliendesha Mkutano wake Mkuu tarehe 4 Mei, 2005 Mjini Dodoma na *CUF* iliendesha Mkutano wake Mkuu tarehe 28 Aprili, 2005 Jijini Dar es Salaam. TVT na *RTD* havikuweza kutangaza moja kwa moja Mkutano Mkuu wa *CUF* kwa kuwa vifaa vinavyotumika kwa madhumuni hayo vilikuwa Mjini Singida na hapa Dodoma.

Vyombo hivyo vilitakiwa kurusha moja kwa moja maadhimisho ya siku ya Malaria Duniani yaliyofanyika Kitaifa Mjini Singida tarehe 25 Aprili, na hali kadhalika maadhimisho ya Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo Kitaifa yalifanyika hapa Mjini Dodoma tarehe 26 Aprili, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha *CUF* kilitakiwa kilipe shilingi 2,400,000/= kwa mtindo wa *special charge package*. Hata hivyo, hadi leo hawajalipa gharama hizo Serikalini. Chama cha Mapinduzi kilitakiwa kilipe *special rate* ya shilingi milioni 8,000,000/= fedha ambazo zimeishalipwa. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri katika sehemu (a) na (b) yalikuwa ni ya uficho sana ambapo alitakiwa kutoa takwimu na akasema waende wakazisome huko nje kwa kukiuka utaratibu wa Bunge. Je, sasa kama CCM ndiyo iliyotoa matangazo tu na ikalipa na*CUF* wakanyimwa hiyo nafasi kwa picha ya watu wa kawaida hawawezi kuona kwamba kulikuwa na hujuma?

(b) Je, ni kweli kwamba kwa muda wote huo wa siku mbili ambapo CCM ilifanya Mkutano wake hapa Chimwaga sh. milioni 8,000,000/= tu ndiyo zilistahili kulipwa au kulikuwa na upendeleo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB ):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa sababu ambazo zilifanya waziwazi kwa nini CCM ilipata nafasi ya kutangazwa moja kwa moja na kwa nini *CUF* haikufanywa hivyo. Nimefanya hivyo kwa makusudi kwa sababu hizi ni dhama za uwazi na ukweli sikuficha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa kwamba CCM iliomba na ikapewa nafasi hiyo na nimeelezea fedha ambazo ililipa kwa *special rate* ambazo hata *CUF* pia ilifanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ni kwamba katika mambo haya ya biashara mmiliki anaweza kutoa *rate* maalum kwa madhumuni maalum. Kwa mfano, CCM haikutumia TVT na Redio kwa muda wa siku mbili, ilitumia kwa siku moja na kwa saa maalum. Wakati mwingine unaweza ukatoa *rate* maalum ukiangalia faida itakayopatikana kwa mfano, kwa muda ambao CCM ilitangaza matangazo yale mamilioni ya Watanzania waliangalia TVT na kwa hiyo kuipa faida kubwa zaidi TVT kuliko faida ambayo ilitolewa na CCM. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa vyombo hivi viwili TVT na Redio Tanzania wanafanya kazi nzuri sana hapa nchini na kwa kuwa Redio Tanzania inasikika karibu nchi nzima lakini TVT inaonekana katika baadhi ya Mikoa. Je, ni lini chombo hiki cha TVT kitaonekana katika nchi nzima? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB ):** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa TVT inaweza kuonekana katika nchi nzima kwa kutumia ungo ambao kila mmoja anaweza kuuona. Lakini tumesema hapa katika Bajeti yetu kwamba nia ya Serikali ni kueneza vituo hivi kwa nchi nzima na mwaka huu hadi mwezi Oktoba, tutaongeza idadi ya Mikoa saba na mwakani tukijaliwa tutaeneza kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Na. 197

**Magari ya Wagonjwa – Vituo vya Afya**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Bumbuli lenye wakazi wapatao 150,000 baada ya kuanzishwa ilibainika kuwa lingekuwa na Vituo vya Afya vitatu (3) lakini vituo hivyo havikujengwa na kwa kuwa sasa Serikali imekubali kupandisha hadhi zahanati za Soni (Tarafa ya Soni), Mgwashi (Tarafa ya Mghwashi) na Tamota kuwa Vituo vya Afya:-

(a) Je, ni lini vituo hivyo vitapatiwa magari ya wagonjwa?

(b) Je, mpaka sasa Serikali imetoa msaada gani kuunga mkono nguvu za wananchi katika upanuzi wa zahanati hizo?

(c) Je, Kituo cha Afya kinatakiwa kuwa na wataalam wa Afya wangapi na sasa wapo wangapi katika vituo nilivyovitaja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imekuwa na utaratibu wa kuboresha huduma za afya kwa kuzipandisha hadhi baadhi ya zahanati kuwa Vituo vya Afya kwa kuzingatia ongezeko la watu na umbali uliopo kutoka ama Vituo vya Afya, Zahanati au Hospitali ya Wilaya. Kwa sasa zahanati za Soni na Mghwashi zilizopo katika Jimbo la Bumbuli zimepandishwa hadhi na kuwa Vituo vya Afya. Kwa mujibu wa Sera ya Afya, Kituo cha Afya kinaweza kujengwa mahali ambapo kuna idadi ya watu wasiopungua 50,000. Hivyo, iwapo pendekezo la kuipandisha hadhi zahanati ya Tamota litakubaliwa, kituo hiki kitakuwa kinahudumia watu 30,000 tu wa kata za Milingano, Funta na Tamota.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vituo vya afya saba vilivyopo katika Halmashauri ya Lushoto, ni vituo viwili tu vya Mnazi na Mlola ndivyo vyenye magari ya wagonjwa. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari moja kwa madhumuni hayo. Halmashauri itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa mwaka hadi mwaka hadi tatizo hili litakapomalizika kabisa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuunga mkono nguvu za wananchi katika upanuzi wa zahanati hizo, Serikali Kuu imekuwa ikitoa fedha kupitia Bajeti za Halmashauri kama ifuatavyo:-

Kwa zahanati ya Soni katika kupanua zahanati hiyo kuwa Kituo cha Afya hadi sasa jumla ya Shs. 32,404,000/= zimetolewa na Serikali Kuu kati ya mwaka 2000/2001 na 2002/2003. Fedha hizo zimetumika kujenga wodi moja ya wanaume na moja ya wanawake, choo cha wagonjwa na kununua samani. Kuhusu zahanati ya Mghwashi kati ya mwaka 2003/2004 na mwaka 2004/2005 Halmashauri imepokea kutoka Serikali Kuu jumla ya Shs.29,658,550/= ili kupanua zahanati ya Mghwashi kuwa Kituo cha Afya. Jengo moja la wodi ya akinamama limekamilika.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mwongozo wa Wizara ya Afya, vituo vya Afya vinatakiwa kuwa na watendaji wafuatao:-

- Madaktari Wasaidizi *(AMO)* 2
- Tabibu (*Clinical Officer*) 4
- Wauguzi (*Nursing Officer*) 1
- *Public Health Nurse B* 2
- Wauguzi Wakunga (*Nurse Midwife*) 4

- *Laboratory Technician* 1
- *Medical Recorder* 1
- Mfamasia 1
- *Dental Therapist* 1
- *Health Officer* 1

Wilaya ya Lushoto ina Vituo vya Afya saba na hakuna hata Kituo cha Afya kimoja kilichotimiza Ikama ya wataalam niliowataja hapo juu. Halmashauri inaendelea na jitihada za kuwapata watumishi hawa kwa kuomba vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kama ilivyo katika Zahanati na Vituo vya Afya vingine; Zahanati za Mghwashi, Soni na Tamota zinahudumiwa na *Clinical Officer* mmoja mmoja na wahudumu wengineo.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kwa majibu ya kutia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kama tulivyouliza katika kipengele cha (c), tatizo kubwa la ufunguzi wa zahanati na Vituo vya Afya ni ukosefu wa watumishi pamoja na kwamba Serikali imeeleza kwamba kuna kuomba vibali, lakini lipo bado tatizo la kupatikana watumishi wenye ujuzi na fani inayotakiwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulishughulikia tatizo hili ili liweze kupata ufumbuzi kama vile Wizara ya Elimu na Utamaduni inavyoshughulikia tatizo la uhaba wa walimu kwa kuweka mpango wa MMES na kuweka *crash Programme*?

(b)Kwa kuwa umeme ni kitu muhimu sana katika maeneo haya je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vituo kama hicho cha Mghwashi, Tamota na Mlola katika Jimbo la Lushoto vinapata umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi katika zahanati na Vituo vya Afya ni kweli ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni tatizo ambalo linatukabili katika Majimbo yetu mengi wala siyo Lushoto tu karibu katika kila Majimbo ambapo tulikuwemo kwenye Mradi wa *TASAF* tumejenga zahanati nyingi na nyingi katika hizo hazijapata watumishi. Lakini kama juzi ambavyo alikuwa anajibu maswali hapa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi, kwamba Serikali kwa kutambua tatizo hili sasa imelivalia njuga ili kuhakikisha kwamba vile vituo vya afya na zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi zitoe huduma ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuhakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tatizo hili Serikali inalifahamu na limevaliwa njuga katika kutafuta waganga na manesi wa kutosha kuhudumia zahanati hizo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la umeme ni kweli. Tatizo la umeme si tu katika zahanati za Lushoto, lakini katika zahanati nyingi na vituo vya afya vingi.

Katika hili niseme tu kwamba tukisubiri umeme wa *grid* kila mahali, ufike ila mahali tutachelewa. Kwa hiyo, njia mbadala na nimeona katika baadhi ya Wilaya nyingi sasa wanaanza kuweka umeme wa *solar* katika vituo vya afya na zahanati nadhani huo ndiyo mwelekeo sahihi. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa moja ya tatizo sugu katika Vituo vyetu vya Afya nchini na zahanati ni maabara na tunazungumzia kwamba hiki ni kipindi cha Sayansi na Teknolojia na wagonjwa wengi mara nyingi wanapokwenda katika zahanati hizo hasa katika vituo vya afya ambavyo ndiyo *referral* hospitali wanazozitegemea wanakosa huduma hii. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa kwa kila Vituo cha Afya na zahanati kuwa na maabara na wataalamu ili wagonjwa wetu wapimwe kisayansi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika nyakati hizi inafaa sasa Vituo vya Afya na hata Zahanati kuwa na maabara. Ni hoja sahihi kabisa na Serikali tunalitambua hilo na kama nilivyojibu swali la msingi kwamba pamoja na jitihada za kutafuta wataalamu katika zahanati zetu na vituo vya afya juhudi hizi vilevile Serikali inazielekeza katika kutafuta vifaa kwa sababu maabara ni vifaa. Kwa hiyo, haya masuala mawili yanaenda sambamba kutafuta wataalamu wa maabara, wakunga, matabibu pamoja na vifaa kama darubini, magari na vifaa vinginevyo ambavyo vinaendana na kazi za matibabu.

Na. 198

**Uendeshaji wa Daladala kwenye Miji Mikuu**

**MHE. SOPHIA M. SIMBA (K.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA)** aliuliza:-

Kwa kuwa uendeshaji wa magari ya abiria maarufu kwa jina la daladala kwenye Jiji la Dar es Salaam na Miji Mikuu hapa nchini haufuati taratibu na kwamba madereva wa magari hayo wameanzisha mtindo wa kuendesha magari hayo kwa kasi kubwa wakishindania abiria na wakati mwingine hutoka kwenye misururu ya magari kwenye barabara na kupita nje kabisa ya barabara kwa lengo la kuyavuka magari mengine yaliyoko kwenye mstari, hali inayoweza kusababisha ajali na vurugu nyingi barabarani;

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kukomesha kabisa mwenendo huo ili kuepusha ajali za mara kwa mara za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vitendo vya magari ya abiria kuendeshwa kasi na nje ya barabara zinazoruhusiwa hutokea kwenye maeneo mengi katika Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine mikubwa nchini. Vitendo hivi ni uvunjaji wa sheria za barabarani na ni kero na hatari kwa usalama wa abiria na kwa waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupambana na tabia hii ya kihuni, isiyo ya kiungwana, na ya hatari, Serikali ilitunga sheria ya Usalama barabarani Na.30 ya mwaka 1973 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.16 ya mwaka 1996. Chini ya Sheria hii ni makosa kwa dereva yeyote kuendesha gari kwenye njia za waendao kwa miguu au maeneo mengine ambayo hayaruhusiwi kwa matumizi ya magari.

Vilevile kwa sheria hiyo hiyo dereva haruhusiwi kulipita gari la mbele yake kwa upande wa kushoto ila tu kama gari hilo lilo mbele yake linaonyesha ishara ya kupinda kulia. Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali dhidi ya madereva wanaokiuka sheria hii. Hatua hizo ni pamoja na kuwakamata na kuwatoza faini za papo kwa papo *(notification*) au kuwafikisha Mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kutoa onyo kali kwa madereva wenye tabia hii ya kihuni waiache mara moja; na pia naagiza Askari Polisi waendelee kuwa wakali na makini zaidi katika kuwashughulikia madereva wanaoendeleza tabia hii ya kihuni. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Pamoja na kukubaliana naye kuhusu hizo kero na sheria mbalimbali ambazo zimetungwa, atakubaliana nami kwamba tatizo kubwa sana ufinyu wa barabara ambapo magari ya daladala ni mengi sana yanahitaji kuwa na barabara zake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua au kutengeneza barabara za juu ili kupunguza tatizo hili?

(b) Katika kero hii tunajua Dar es Salaam imejitahidi ilivyoweza kupitia Mwenyekiti wake wa Bodi ya Leseni ya Mkoa, Bwana David Mwaibula, kwa kutengeneza utaratibu mzuri. Je, Serikali itakubaliana nami kumpongeza Mwenyekiti wetu David Mwaibula, kwa utaratibu mzuri aliyouunda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y . WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufinyu wa barabara wa Dar es Salaam

na si  Dar es Salaam tu karibuni Miji yote ambayo  ilikuwa imepangwa zamani haikutilia maanani kwamba kutahitajika upanuzi wa barabara hizo baadaye.

Kwa hiyo, barabara zetu ni finyu kwa sababu zimejengewa nyumba karibu karibu. Umuhimu wa kujenga barabara za juu upo, lakini nilijibu swali hapa ndani  ya Bunge juu ya barabara za juu ni kwamba kitu  aghali sana.

Lakini kwa misaada ya kila   Mji kupanga mipango yake na kuomba misaada kusaidiwa inawezekana kabisa.  Kwa Dar es Salaam nafikiri mikakati hiyo ipo ya hali ya juu.  Majiji  mengine na   Manispaa nyingine wanashirikiana ili kuweza kuangalia ni jinsi gani. Pale watakapohitaji msaada wa Wizara ya Ujenzi tutakuwa tayari kusaidiana nao. *(Makofi)*

**NAIBU  WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli juhudi zinafanywa pale Dar es Salaam na Bodi ya Leseni ambayo sasa hivi imekuwa *SUMATRA* na Halmashauri ya Jiji lenyewe kwa jumla maana hiyo kazi siyo ya  mtu mmoja wanafanya kazi nzuri katika kuweka utaratibu wa usafiri kwa kupunguza kero za usafiri Dar es Salaam.

Daladala kukatisha *rote*, daladala wanaita kuchomekeana na  wapiga debe kuwaathiri abiria.  Jiji limeweka utaratibu. Nataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia kwamba Serikali Kuu itaunga mkono juhudi hizo ambazo Jiji la Dar es Salaam na vyombo vingine kama *SUMATRA* wanavyofanya katika kuboresha usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.  *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:**  Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja  dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linahusu  ajali za mabasi; na kwa kuwa ajali nyingi ambazo zinatokea abiria wanaojeruhiwa na kupoteza maisha hupata matatizo hayo kwa kukanyagana  na kwa kuwa mabasi mengi hayana madirisha au milango ya dharura. Je, Serikali inatoa tamko gani?

**NAIBU  WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  Mheshimiwa Naibu Spika,   ni kweli kwamba ajali zinapotokea moja  ya athari kubwa ni katika namna ya abiria kutaka kujiokoa, tatizo hilo tunakubaliana kwamba lipo.  Lakini Shirika la viwango *TBS* wameishatoa maelekezo ya aina gani ya bodi ziweje, madirisha ya kutokea yaweje na  milango ya  dharura iweje. Kwa hiyo, suala hili linashughulikiwa kwa namna hiyo na mabasi yatakayokuwa yanaagizwa sasa lazima  yakidhi matakwa na vigezo vilivyowekwa na *TBS*

.

Na. 199

**Uvunjaji wa Sheria za Barabara**

**MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. MHE. PETER KABISA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekiri kuwa imeongeza uwezo zaidi kwa Polisi na vitendea kazi vya kudhibiti na kupunguza uhalifu nchini ikiwa ni pamoja na kudhibiti ajali za barabarani lakini bado uvunjaji wa sheria za barabarani unaendelea:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya uendeshaji wa daladala katika barabara ya Shekilango – Tegeta ambako daladala zinaendeshwa pembeni mwa barabara hiyo upande wa kushoto na kulia hadi kwenye kona ya barabara iendayo *White Sands Hotel* kwenye barabara ya *Old* Bagamoyo kutoka Makutano ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na barabara ya Kawawa - Kawe ambako daladala zinapita kwenye *road reserve* ya barabara hizo kulia na kushoto na hivyo husababisha *road block?*

(b) Je, Serikali imeshindwa vipi kurekebisha na kuwaadhibu wanaohusika na vitendo hivyo.

Je, Polisi wa Usalama barabarani wanakuwa wapi wakati hayo yanafanyika na hivyo vifaa walivyopewa pamoja na taaluma zao vinatumikaje ili kupunguza ajali na adha barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali inatekeleza mpango wa kuongeza uwezo wa Jeshi la Polisi wa kupambana na uhalifu nchini ikiwa ni pamoja na kudhibiti ajali za barabarani. Hata hivyo, ajali zinaendelea kutokea kutokana na baadhi ya watumiaji wa barabara kuvunja sheria za usalama barabarani. Miongoni mwao ni madereva wa daladala ambao huacha barabara na kupita pembeni kwenye njia za waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu 95 (10) cha Sheria ya Usalama Barabarani Na.30/1973 ni kosa kwa Dereva wa Daladala au Dereva wa gari yoyote kuendesha gari pembeni kushoto au kulia mwa barabara hasa kwenye *road reserve*.

Jeshi la Polisi limekuwa linapambana na madereva wa aina hii kwa kuwakamata na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria hii. Mwaka 2004 jumla ya madereva 194 wa

daladala za barabara ya Shekilango - Tegeta walikamatwa kwa kupita pembeni mwa barabara.

Aidha, jumla ya madereva wengine 457 wa daladala ambazo zilikuwa zinapita pembeni mwa barabara katika Jiji la Dar es Salaam walikamatwa na Polisi wa Trafiki na walitozwa faini ya jumla ya Shs.19,240,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kusimamia sheria za usalama barabarani na itaendelea kuwaadhibu madereva wakorofi na wahuni wanaoendesha magari bila kuzingatia sheria za usalama barabarani. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na mimi nataka niulize swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa katika barabara hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri, vipo vigingi ambavyo vimewekwa kwenye sehemu za hifadhi za barabara na wengine wanaweka kabisa kuzuia hiyo *road reserve*, Je, inapotokea ajali kama moto au magari kupata ajali, magari yatapitaje wakati kuna vigingi kama magurudumu na kadharika, je hilo nalo sio kosa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, vigingi ambavyo vinawekwa kwenye *road reserve* ni kuzuia magari yasipite kwenye sehemu ambayo waenda kwa miguu wanapita na hatuweki kwenye barabara. Kwa hiyo mara nyingi inapotokea ajali ya moto, magari ya zimamoto sehemu hiyo yenye vigingi ni ndogo sana hayawezi kupita lazima yapite barabarani. Sisi hatuweki vigingi kwenye barabara, tunaweka vigingi kwenye sehemu ambayo waenda kwa miguu wanapita, ni njia za waenda kwa miguu. Kwa hiyo magari hayaruhusuwi na ndiyo maana daladala zikipita huko zinakamatwa.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika swala lililotangulia yamaeonyesha kutokuwepo kwa mikakati ya muda mfupi na muda mrefu kwa sababu mimi naona hili ni suala la kimikakati, na kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam linaendelea kukua kila kukicha, pamoja na matatizo aliyoyataji yanayosababisha msongamano wa magari barabarani, lakini kikubwa kimojawapo ni daladala na hasa vipanya. Je, ni lini watapunguza hayo magari madogo na kuingiza magari makubwa ya abiria wengi 65 na zaidi kama utatuzi wa muda mfupi kuondokana na msongamano wa magari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya kupunguza tatizo la usafiri katika Jiji la Dar es Salaam ipo na mengine ameitaja sasa hivi Naibu Waziri wa Ujenzi, kama ile ya kupanua barabara za Dar es Salaam na kujenga barabara za juu kwa juu katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza

msongamano uliopo. Lakini vile vile kauliza: Je, lini utaratibu utawekwa wa kupunguza hivi vipanya vinavyochukua abiria wachache na kuleta magari makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam wanao mpango ambao awali ulikuwa unaitwa *Bus Rapid Transit* (*BRT)* sasa wanauita *Dar es Salaam Rapid Transit* (*DART).* Chini ya mpango huu magari makubwa yatakuja kwa hiyo vipanya havitaruhusiwa sasa katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Vipanya vitachezea pembeni pembeni, katikati ya Jiji kutakuwa na mabasi makubwa ambayo katika zile barabara itatengwa *line* moja, upande mmoja wa barabara yatapita haya mabasi makubwa tu, ili wewe ukitaka kusafiri haraka panda basi kwa sababu itakuwepo *line* yao moja ya mabasi sisi wengine tutakuwa na *line* yetu. Kwa hiyo, dawa inakuja hii ya mabasi makubwa na nafikiri mipango ikienda vizuri mpaka kufika mwakani mabasi makubwa yaataanza kufanya kazi katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Na. 200

**Barabara ya Morogoro – Kisaki**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa *TANROADS* inasimamia barabara ya Morogoro – Kisaki inayounganisha Majimbo matatu ya Morogoro Mjini, Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Kusini: Maeneo yenye uchumi na utajiri mkubwa wa matunda mengi yanayolisha nchi; na kwa kuwa inasemekana barabara hiyo imetengewa fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami:

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?

(b) Kwa kuwa, habari hizo zinaonyesha matakwa halisi ya wananchi wa maeneo husika jinsi inavyowakera. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwekea lami barabara hiyo ambayo kipande cha eneo la Mlima wa Ng’alo tayari ilipewa tabaka la lami ya majaribio.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika , kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Thobiasi Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Morogoro hadi Kisaki ni ile inayoanzia mzunguko wa Posta hadi Kisaki yenye urefu wa Kilometa 144.5 ambayo ni barabara ya Mkoa ambapo Kilometa 12 za Mlima Ng’alo ziliwekewa lami nyepesi (*Otta Seal*) kwa lengo la kuondoa kero iliyokuwa ikisababisha magari kushindwa kupanda hasa wakati wa mvua na hivyo kurudi nyuma na kuanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshijmiwa Oscar Mloka, kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali haijawahi kutenga kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya kuiwekea lami barabara hiyo kuanzia Bigwa hadi Kisaki.

(b) Kama nilivyojibu katika swali (a) hapo juu, hakuna mpango wa kuiwekea lami barabara hii kutokana ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, ambayo mbali na kupita katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa matunda lakini pia inaelekea katika Hifadhi ya *Selous* ambayo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia sekta ya utalii. Serikali imefanya na inaendelea kufanya juhudi mbalimbali za kutengeneza barabara hiyo kuhakikisha kuwa inapitika kwa kipindi chote cha mwaka. Matengenezo hayo ni ya kiwango cha changarawe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa juhudi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi mpya wa sehemu ya barabara ya Dakawa – Kisaki ya Kilometa 12, daraja jipya la Kisanga katika Mto Mgeta na Kafa pamoja na madaraja mengine saba madogo madogo kati ya Gomero na Kisaki.

Mradi huu ulibuniwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kufadhiliwa na *Japan Food Aid Counterpart Fund* na Shirika la *KFW* la Ujerumani ili kuimarisha barabara za Ukanda wa Kaskazini kuelekea Hifadhi za *Selous* ili iweze kupitika kwa urahisi kipindi chote cha mwaka. Mradi huu ulikamilika mwaka 2004 na uligharimu kiasi cha Shilingi 848.3 milioni.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 Serikali kupitia Wakala wa Barabara *TANROADS*, ilizifanyia matenngenezo sehemu kadhaa za barabara hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Pangawe hadi Mlima Ngo’le; kilometa 7 imefanyiwa matengenezo ya muda maalum, *Periodic Maintenance* ili iweze kupitika kwa urahisi kwa kipindi chote cha mwaka. Miongoni mwa kazi zilizofanyika ni pamoja na kuumba upya barabara na kuweka changarawe. Jumla ya shilingi 70.77 milioni zilitumika.

(ii) Sehemu ya Mlima wa Kibungo Chini – Ruvu Km. 5 ukarabati unaendelea na baadhi ya kazi zilizokamilika ni pamoja na upanuzi wa barabara kwa kupasua miamba na kupanua madaraja. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kuweka changarawe, kazi ambayo inakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi 50 milioni kutoka katika mfuko wa maendeleo.

(iii) Sehemu ya Mlima Chamanyani – Mvuha, Km. 7 ukarabati unaendelea na baadhi ya kazi zilizokamilika ni kuumba upya barabara, kuweka changarawe na kujengwa makalvati. Kazi hii itakapokamilika inategemea kugharimu kiasi cha shilingi 70 milioni kutoka katika mfuko wa maendeleo.

(iv) Serikali ilitenga pia jumla ya shilingi 66 milioni kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya Matengenezo ya kawaida *Routine/Current Maintenance.* Miongoni kwa kazi

zilizofanyika ni pamoja na kuchonga barabara, kufyeka majani, kufukua mifereji na kuzibua makalvati yaliyoziba ili kuiwezesha barabara hiyo kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini matakwa ya wananchi wa maeneo husika na pindi hali ya fedha itakapo ruhusu Serikali haitasita kuziwekea lami barabara mbalimbali za Mikoa ikiwemo barabara husika kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo. Lakini kwa sasa Serikali haijawahi na haijapanga fedha za kuitengeneza barabara ya Morogoro hadi Kisaki kwa Kiwango cha Lami. Serikali haina uwezo kwa sasa. barabara hii kwa sasa inapitika mwaka mzima kwa kiwango cha changarawe.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu marefu ya swali langu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza madogo.

Kwa kuwa barabara hii ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Morogoro Mjini na kusimishwa ilipofikia eneo la Bigwa na kuruka Kata nzima ya Bigwa hadi kwenda kuweka lami ya majiribio pale Mlima wa Ng'alo na kwa kuwa inafahamika kwamba upo uhaba wa fedha za kujenga miradi mikubwa mikubwa kwa Serikali kama alivyosema lakini vipande vidogo vidogo ingewezekana kabisa kuondoa tatizo hili. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuunganisha kipande hichi kilichorukwa ambacho kina urefu usiozidi Kilometa nne kungetimiza azma ya usemi wa Kiswahili kwamba haba na haba hujaza kibaba?

Pili, upo upanuzi mkubwa kama alivyosema pale sehemu za Kibungo karibu na daraja la Ruvu ambayo sehemu hii ni korofi kidogo. Je Serikali itachukua ushauri wangu kwamba ile lami ya majaribio ya *Otta Seal* ambayo wameiweka pale Mlima wa Ng'alo pia iwekwe kwenye eneo hili linalofanyiwa ukarabati sasa hivi pamoja na maeneo ya mji mdogo wa Mtamba na Mlima wa Chamanyani kama alivyosema?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kutoka Posta hadi Bigwa ilipangiwa rasmi kuwekewa lami na imewekewa lami sio *Otta Seal* ambayo ni ya magari mazito na tumekwenda kutia *Otta Seal*, lami nyepesi katika Mlima Kola kwa sababu magari yalikuwa yanaanguka sana na tumeona ni vizuri kuokoa pale ambayo ni njia pekee yakuweza kupafanya pawe pazuri na ni kuweka *Otta Seal.*

Serikali itakapopata uwezo tutaunganisha *Otta Seal* hiyo kati ya Bigwa na Mlima Kola na ushauri wake kuhusu Kibungo- chini, Mtamba na Chamanyani, tumeupokea tutakapokuwa na uwezo tutatekeleza hapo Serikali itakapokuwa na pesa.

Na. 201

**Fedha za *STABEX* – Kwa Zao la Kahawa**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** alijibu:-

Kwa kuwa taarifa zinonyesha kwamba fedha za *STABEX* kwa ajili ya kahawa yaani bilioni 42, bilioni 12 kati ya hizo zilipelekwa kwenye kituo cha utafiti wa kahawa cha Lyamungo, Moshi.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimetumika kwa shughuri hiyo na ni wakulima wangapi wamepatiwa miche ya kahawa inayostahimili magonjwa kwa kituo hicho?

(b) Je, ni lini wakulima watafahamishwa kuwa fedha hizo za *STABEX* ya kahawa zimepelekwa kwenye kituo cha utafiti cha Lyamungo kwa ajili ya shughuri za utafiti ili wasiwe na mategemeo ya kuzipata?

(c) Kwa kuwa kuna maelekezo toka Serikalini kuwa fedha hizo hutumika katika matengenezo ya barabara za Mikoa. Je, hayo yalikuwa ni matakwa ya wafadhili na kama hivyo ndivyo, Serikali haioni kuwa inaua kilimo cha kahawa hapa nchini?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako naomba kutambua vijana 31 wa shule ya Kiluvya walioko kwenye *gallery* yako hapa Bungeni asubuhi hii, kutoka kwenye Jimbo langu la Uchaguzi.

*(Hapa vijana wa Kilivya walisimama na kuonekana kwenye gallery)*

Mheshimiwa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:

Kama nilivyoeleza kwenye kauli ya Serikali kuhusu utaratibu wa fedha za *STABEX* ya kahawa iliyotolewa katika Bunge hili Tukufu tarehe 30, Julai 2003, utafiti wa kahawa na misaada ya teknolojia yaani C*offe Research and Technology Support Programme* ilitengewa *Euro* milioni 9, na fedha hizi zilipangwa kutumika katika muda wa miaka mitano kugharamia shughuri tano zifuatazo:-

*(i)* *Euro* milioni 4.62 kwa ajili ya *Endowment Fund* ambayo amewahi kuizungumzia Mheshimiwa Ngawaiya hapa Bungeni.

*(ii)* *Euro* milioni 1.1 ni kwa ajili ya ukarabati wa vituo na miundombinu na majengo katika vituo vya utafiti Lyamungo, Mbimba, Ugano na Maruku.

*(iii)* *Euro* milioni 1,48 ni kwa ajili ya matumizi ya kila mwaka kwa shughuri za utafiti.

(iv) *Euro* 1.1 kwa ajili ya vifaa vya maabara.

(v) *Euro* 700,000 kwa ajili ya kununulia huduma za kiufundi

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia tarehe 4 Juni, 2005 *TaCRI* walikuwa wamepokea *Euro* 716,264.49. Fedha hizi zimetumika kujenga miundombinu ya kiutafiti ambayo imewezesha kuharakishwa kuchaguliwa kwa aina bora tano za kahawa inayostahilimili magonjwa ya Chule buni yaani *CDB* na kutu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa miti 300,000 imesambazwa kwa vikundi vya wakulima 92 na mashamba makubwa 14. Miti mama hutumiwa kuzalisha miche mingi kwa jaili ya kuwasambazia wakulima. *TaCRI* imelenga kuzalisha miche mama milioni tano ifikapo mwaka 2007 na inatarajia kwamba ifikapo mwaka wa 2010 miche ya kahawa milioni 50 itazalishwa na kuuzwa kwa wakulima naomba kurudia kwamba itauzwa kwa wakulima.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa taarifa mara kwa mara, juu ya matumizi ya fedha za *STABEX* hapa Bungeni. Kwa mfano. taarifa hizo zilitolewa katika vikao vya 14, 15 na 35 vya Mkutano wa 12 wa Bunge lako Tukufu na katika kujibu maswali hapa Bungeni mara kwa mara yaliyoulizwa na Mheshimiwa Ngawaiya na Mheshimiwa Mutungilehi. Maelezo ya kina kuhusu matumizi ya fedha za *STABEX* yalitolewa katika kauli ya Serikali yaliyotolewa kwenye Kikao cha 35 cha Mkutano za 12 na naomba taarifa hiyo irejewe.

(c) Maelekezo ya kutumia fedha za *STABEX* ya kahawa katika kukarabati barabara za maeneo yanayozalisha kahawa nchini yalitolewa na kikao cha wadau wa zao la kahawa kilichofanyika mwezi wa Novemba, 2000. hakikutokana na shinikizo wala maagizo ya mhisani. Utengenezaji wa barabara hizo utaimarisha huduma za usafiri katika maeneo hayo na hivyo kuchangia ukuaji wa zao la kahawa na siyo kuua uzalishaji wa zao hilo kama anavyodai muuliza swali.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwanza kabisa niseme tu kwamba maswali mengi yanayoulizwa hapa Bungeni yanayohusu *STABEX* sio tunamshambulia Mheshimiwa Waziri isipokuwa ni kweli kwamba kuna mkataba ambao ulitiwa saini *Berlin* kuhusu matumizi haya ya fedha za *STABEX* na bahati nzuri mkataba huo ninao. Aidha nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba katika Mawaziri wazuri waliofanya kazi vizuri hapa Tanzania yeye ni mmoja wapo.(*Makofi*)

Kwa hiyo tunaiuliza Serikali sio yeye tu peke yake, kwamba mkataba huu ambao ninao nitamkabidhi walisema kwamba fedha milioni 42 kwa maana ya *Euro* milioni 39 zimetolewa *over and above* ya pesa za kawaida ambazo wange-*allocate* Tanzania kwa ajili ya *short fall* ya kahawa ambayo ni mauzo ya miaka mitatu. Kwa maana hiyo walihitaji hizi fedha zitumike kwa ajili ya kuwasaidi wale wakulima waliouza kahawa

zao na mkataba huu ninao hapa na nitamkabidhi. Sasa naomba niulize swali: Je, ni kwa nini? Ni nani mwingine aliyekuja akabadilisha huu mkataba ambao wamesema *on binding* na uko kwenye *internet* na hata yeye mwenyewe akitaka atautafuta ataukuta mpaka leo umebadilika katika kikao gani baada ya hicho cha cha *Berlin*?

La pili, ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kuwapa hawa wananchi waliolima kahawa *STABEX* yao ambako ndiyo haki yao sio barabara walioimba, wao wanalima kahawa sio barabara kwa nini Serikali hawapi hizo pesa?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ngawaiya kwamba sijaamini wala kufikiria kwamba maswali yanayoulizwa hapa Bungeni yanatushambulia bali anahitaji tu kupata ukweli juu ya mambo yanayotokea humu nchini.

Katika swali lake la kwanza amesema atanipa mkataba ambao ulitiwa saini Berlin, basi nitasubiri nipate mkataba huo na nione unasema nini. Lakini katika kauli tuliyoitoa hapa Bungeni katika Kikao cha 35 cha Mkutano wa 12, tulieleza mazingira yaliyoleteleza mpaka tukafikia hali tuliyonayo sasa hivi, na moja ya matatizo yaliyotokea ni kwamba kutokana na kubadilika kwa mfumo wa biashara ya kahawa nchini ilikuwa ni vigumu kubaini ni nani aliyeuza kahawa kiasi gani na kwa hiyo kumpa zile fedha kama ilivyokuwa imefanyika huko nyuma

Kutokana na ugumu huo wakaitwa wadau wa zao hili wakakutana Moshi kama nilivyoeleza na wakapendekeza kwamba fedha hizi zitumike kwa shughuri ambazo zinamanufaa kwa mkulima na shughuri hizo ni pamoja na kumtengenezea barabara zake na ndivyo ilivyotokea, fedha hizi zikatengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara kwenye maeneo ya kahawa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alipokuwa anatoa hotuba yake hapa Bungeni alieleza barabara zitakazo shughurikiwa kwa kutumia fedha hizi.

Kwa hiyo ni ugumu wa kuwabaini wakulima waliozalisha kahawa ndiyo uliosababisha fedha hizi zitumike kama ambavyo imeelezwa hapa Bungeni.

Na. 202

**Utafiti wa Kilimo cha Pamba Mbeya**

**MHE. ESTHERINA KILAZI (K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitoa tamko la kufanya utafiti wa kina juu ya kilimo cha pamba Mkoa wa Mbeya ikiwemo kutembelea nchi zinazolima pamba Kusini mwa jangwa la Sahara.

(a) Je, nini matokeo ya utafiti huo?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka utafiti huo wazi kwa wananchi?

**WAZIRI WA KILIMO CHA CHAKULA** alijibu:-

Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi sana ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Katika Kikao cha 15 cha Mkutano wa 12 wa Bunge lako tukufu, kilichofanyika tarehe 1 Julai, 2003, niliahidi kwamba Wizara yangu ingeshirikiana na Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kushughulikia hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuzuiliwa kwa kilimo cha pamba katika Mikoa ya kusini kutokana na kuwepo kwa funza mwekundu katika maeneo ya Mikoa hiyo.

Ili kutekeleza ahadi hiyo, tarehe 1 Agosti, 2004 Wizara ilifanya warsha iliyojumuisha Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, Waheshimiwa Wabunge 78 kutoka kwenye Mikoa inayolima pamba kwa wingi na kutoka kwenye vituo vya utafiti vya pamba vya Ukiliguru, Ilonga, Nalyendele *TPRA* na kutoka kwenye Bodi ya Pamba. Warsha hiyo ilijadili hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu karantini ya funza mwekundu katika mikoa ya kusini na kuagiza Wizara ifanye utafiti ili kubaini ukweli wa kuwepo, au kutokuwepo kwa funza mwekundu katika maeneo yaliyo chini ya karantini ya funza mwekundu.

Katika mwezi wa Desemba 2004, watafiti kutoka kwenye vituo vya utafiti vya Wizara walianzisha vishamba vya pamba vya majaribio kwenye Wilaya za Chunya, Nachingwea, Masasi na Newala. Majaribio haya yanatarajiwa kukamilika katika msimu wa 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi sasa naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mpesya, kama ifuatavyo:-

(a) Ukaguzi wa awali wa vishamba vya majaribio uliofanywa katika miezi ya Machi na Aprili, 2005 katika maeneo ya Mikoa ya Mbeya, Lindi na Mtwara ulibaini kwamba funza mwekundu yupo katika vijiji vya Mbala, Galula, Magamba, Chang'ombe, Kanga na Ifumbo vilivyopo katika Wilaya ya Chunya. Rweje na Mpiruka vilivyopo katika Wilaya ya Nachingwea na Mkwera, kilichopo katika Wilaya ya Masasi.

(b) Utafiti umepangwa kukamilika katika msimu wa 2006/2007. Taarifa rasmi ya matokeo ya utafiti huo itatolewa baada ya kukamilishwa kwa utafiti huo.

Na. 203

**Majengo ya *Welfare Centres***

**MHE. JOB NDUGAI ( K.n.y. MHE. HERBERT J. MNTANGI )**aliuliza:-

Kwa kuwa, jengo la Muheza *Welfare* ambalo linamilikiwa na Halmashauri ya Muheza ni miongoni mwa majengo kadhaa ya Welfare centres yaliyokuwa mali ya

ukoloni yaliyortumiwa kama kumbi za starehe baada ya ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia mwaka 1935 – 1945 kwa ajili ya askari wastaafu wa *KAR* na kwa kuwa wastaafu hao wa *KAR* katika Wilaya ya Muheza na katika maeneo mengine nchini Tanzania bado wapo hai na kwa kuwa, wazee hao hawana malipo yoyote ya pensheni wala kipato na kwa kuwa wastaafu wa Muheza wameunda tawi lao chini ya Tanganyika *Legion Club*:-

(a) Je, Serikali haioni ipo haja ya kuwaenzi wazee hao kwa kuwa kuwarudishia majengo ya aina hiyo ambayo walikuwa wakiyatumia wakati huo kwa ulinzi wa taifa letu ili wayatumie kama kitega uchumi chao?

(b) Je, ni katika Wilaya gani nyingine ambako majengo ya aina hiyo yapo na yanamilikiwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hebert Mntangi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia Serikali ya Uingereza ilijenga *Welfare Centres* katika Mikoa yote ili ziwe sehemu za burudani kwa askari wa Tanganyika waliorejea vitani.

Kadharika Serikali ya Uingereza ilianzisha chama cha Tanganyika *Legion* na kujenga makao makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spka, katika miaka ya themanini wakati wa awamu ya kwanza ya madaraka mikoani kulikuwa na ongezeko kubwa la watumishi katika ngazi ya Wilaya na hivyo kujitaji ofisi kwa ajili ya utekerezaji wa mpango huo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa utekereza mpango huo na kwa kutambua kwamba majengo ya *Welfare Centres* hayakuwa yanatumika kwa ukamilifu na walengwa licha ya kuwa sehemu za vijana kuchezea dansi, Serikali ilifanya maamuzi ya kuyachukua majengo hayo na kuyakabidhi kwa Halmashauri za Miji husika na yanatumika kwa shughuri mbalimbali ikiwa ni pamoja na ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukarabati uliofanywa katika majengo ya matumizi yake ya sasa haitakuwa busara kuyarejesha majengo hayo. Kuhusu hali ya maisha ya waliopigana Vita Kuu ya Pili ni kwamba, kupitia chama cha Tanzania *Legion club*, wazee walikuwa wanapata posho ya kujikimu kutoka kwa *British Commonwealth Ex- Services League* mpaka mwezi Septemba 2002 ilipositishwa kutokana na mgogoro wa uongozi ndani ya chama hicho. Serikali kupitia Wizara yangu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kulishughulikia tatizo hili.

**MHE. JOB NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushuru sana kunipa nafsi niulize swali dogo la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Kwa kuwa askari hawa wa *KAR* wapo nchi nzima ikiwa ni pamoja na Muheza, Kongwa na maeneo mengine ya nchi hii, na ni wazee sana na wengi wao wanaamini kabisa kwamba kuna hela ambazo zimeletwa na Serikali ya Uingereza kwa Serikali yetu kwa ajili yao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukawaambia nini wazee hawa kuhusu imani hiyo waliyo nayo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na pesa kutoka Uingereza zilizokuwa zinaletwa Tanzania *Legion Club* kwa ajili ya kusadia wapiganaji hawa wa Vita Kuu ya Pili. Lakini lipofika tarehe 12/11/2000, Serikali ya Uingereza kupitia chama cha *British Commnwealth Ex-Services League* ilizuia kuleta misaada hiyo kutokana na mgogoro uliokithiri ndani ya Tanzania *Legion*. Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi ilijaribu kuwakusanya wazee hawa na tukafanikiwa kupata uongozi wa kuchaguliwa na Mzee Reuben Lyatuu akawa Mwenyekiti. Lakini Mzee Lubala ambaye alitupwa nje kwa kushirikiana na bwana Simon Semfukwe walikwenda chini chini na kumng’oa tena huyu mzee kitu kilichosababisha Uingereza kuendelea kusimamisha mpango ule. Kwa hivyo, tunaendelea kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha kwamba mgogoro huu unafikia tamati ili Uingereza kutoa misaada hii iwasaidie wazee wetu. Kwa hiyo kwa sasa hivi pesa hizo hazipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo.

**WAZIRI WA KAZI MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea tu kidogo kwenye majibu mazuri ambayo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri, na kabla sijafanya hivyo labda nichukue nafasi hii kwanza kuzipongeza timu zetu mbili za Simba na Yanga kwa kuingia fainali katika kombe la Tusker, lakini vile vile pongezi maalum kwa Simba kwa kuchukua ubingwa mara nne mfululizo pamoja na kwamba ilikuwa na wachezaji 10 tu.(*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuongezea ni kwamba, kwa bahati nzuri muda halali wa uongozi uliokuwa madarakani umekwisha. Hivi sasa Serikali inaandaa uchaaguzi mpya, tumeshapeleka matangazo nchi nzima kwa Ma-*DC* wale wazee wajiaandikishe upya ili tujue idadi yao kamili. Wito wa Serikali kwa wazee hawa ni kwamba utakapofika wakati wa kuitisha uchaguzi huu tunaomba wote wafike na Ma- *DC* wawasaidie wahakikishe kwamba wanafika ili tupate viongozi watakao kubalika katika kurejesha imani ya watoa fedha ili waendelee kupata fedha.

Na. 204

**Umeme Unaotokana na Makaa ya Mawe**

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:

Kwa kuwa, taarifa ya Kampuni ya *PB Power* ya Africa Kusini ya mwezi Aprili, 2004 iliyowasilishwa *NDC* na nakala kupelekwa Serikalini imeonyesha kua mpango wa usambazaji wa umeme kwa Tanzania kwa miaka 2 ijayo ambao ni wa bei nafuu na wa uhakika ni wa makaa ya mawe ya Mchuchuma.

(a) Je, ni kitu gani kinachoifanya Serikali kusita kukubali mwelekeo huo?

(b) Je, kuna hazina ya makaa ya mawe kiasi gani katika nchi hii na yanaweza kuzalisha umeme kiasi gani na kwa miaka mingapi ijayo?

(c) Je, inawezekana Tanzania kuwa mzalishaji na muuzaji wa umeme katika nchi za *SADC* na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga lenye, sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuandaa mpango wa kuendeleza sekta ya umeme ni la Wizara ya Nishati na Madini. Kampuni ya *PB Power* ya Afrika Kusini iliagizwa na *NDC* kufanya upembuzi yakinifu wa kuunganisha kituo cha kuzalisha umeme cha Mchuchuma kwenye gridi ya Taifa. Wataalam wa Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO* walipitia ripoti ya mshauri ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa inatofautiana na *Power System Master Plan* ya Serikali kutokana na mshauri kutumia vigezo tofauti pamoja na njia za utafiti ambazo hazikidhi matakwa ya Sekta ya Umeme. Maoni ya Wizara ya Nishati na Madini yakijumuishwa na maoni ya *TANESCO* yalitumwa kwa mshauri tarehe 15 Juni, 2004.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, hazina ya makaa ya mawe hapa Tanzania iko Songwe - Kiwira Mkoani Mbeya na Mchuchuma Katewaka katika Mkoa wa Iringa Wilayani Ludewa. Hazina hiyo inakadiriwa kuwa tani bilioni 2 na iliyothibitishwa kule Mchuchuma pekee ni tani milioni 125. Kiasi cha makaa cha metani milioni 30 kinatosha kuzalisha umeme wa *megawatt* 400 hapo Mchuchuma kwa miaka 20.

Makaa ya mawe yanayotumika kwa sasa ni yale ya Songwe Kiwira ambapo kuna mtambo wa kuzalisha umeme wa *megawatt* 6. Ilikadiriwa kuwa tani 150 zingetumika kwa mwaka, lakini kutokana na hali duni ya uzalishaji wa makaa hayo, uzalishaji umepungua hadi kufikia tani 96,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 1992.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa Tanzania kuwa mzalishaji na muuzaji wa umeme katika nchi za *Southern Africa Power Pool* na *East African Power Pool* baada ya kukamilika mradi wa *Interconnector* kati yetu na nchi za Zambia na Kenya. Ushiriki katika soko la biashara ya umeme ndiyo nguzo ya ushirikiano kati yetu na nchi za Afrika Mashariki pamoja na *SADC*.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Katika jibu lake la msingi amesema kwamba, Tanzania ina hazina ya makaa ya mawe ambayo yanaweza kuzalisha umeme *megawatt 400* kwa miaka 20. Je, kuna tatizo gani, ni kwa nini tusitumie hazina hiyo kuzalisha umeme sasa hivi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina vyanzo vingi sana vya kuzalisha umeme. Maji tunayo na tuna mito mingi sana na kuna miradi ambayo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu wa awali kama *Stigler's Gorge,* Luhuji na kadhalika. Makaa ya mawe kama nilivyosema hapa ni mengi na yanaweza vile vile kuzalisha umeme. Tuna *geothermal,* tuna upepo, tuna jua, vyanzo ni vingi sana, lakini tatizo la kuzalisha umeme ni kwamba unahitaji fedha nyingi sana kwa mradi wowote ule, hata kama ni mradi mdogo.

Fedha hizo aidha zitoke Serikalini mwetu katika Bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaipitisha hapa au tuzipate kwa kukopa, au tuzipate kutoka kwa wafadhili au sasa hivi kuna njia nyingine ya nne ni mwekezaji binafsi.

Kule Mchuchuma kwenye makaa ya mawe tunategemea kwamba wawekezaji binafsi wa *Siemens* kutoka Afrika Kusini, lakini kuna kampuni nyingine vile vile kutoka Japan na India zinaangalia uwezo wa kuzalisha umeme huo kwa sababu sisi wenyewe tumeshindwa kuuzalisha kwa Bajeti yetu wenyewe.

Na. 205

**Kiwanda Cha Nyama Shinyanga**

**MHE. ROBERT K. MASHALLA (K.n.y. MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza: -

Kwa kuwa kipindi kirefu sasa kimepata tangu kiwanda cha nyama Shinyanga kianze kujengwa na bado hakijakamilika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu na kiwanda hicho?

(b) Je, nini hatma ya kiwanda hicho?

(c) Je, yale majengo yaliyopo pale hayawezi kutumika kwa shughuli nyingine za maendeleo ya jamii kama lengo lililokusudiwa limeshindikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga ni kati ya viwanda viwili vilivyokusudiwa kujengwa na Serikali katika miaka ya sabini ili kuongeza uwezo wa iliyokuwa *Tanganyika Packers Limited.* Kiwanda kingine ni kile cha Mbeya. Ujenzi wa Viwanda vya Shinyanga na Mbeya na ukarabati wa kiwanda cha Kawe, Dar es Salaam ulianza kati ya mwaka 1975 na 1978. Shughuli za ujenzi na ukarabati wa mradi huu zilipata ufadhili wa Benki ya Dunia na *SIDA* kwa jumla ya Dola za Marekani milioni 12.

Madhumuni ya kujenga viwanda hivyo na kukarabati kiwanda cha *Tanganyika Packers* kilichokuwa Kawe yalikuwa ni kuongeza idadi ya ng'ombe wa kuchinjwa na pia kuongeza kiasi cha nyama ya kusindika katika kiwanda cha Kawe. Kiwanda hiki kilikuwa na uwezo wa kusindika jumla ya ngo'mbe 200,000 kwa mwaka. Viwanda vya Shinyanga na Mbeya vilipangiwa kuchinja jumla ya ng'ombe 50,000 kwa mwaka.

Madhumuni mengine yalikuwa ni kupanua soko la nyama la hapa ndani na kwa ajili ya kuuza nchi za nje. Hadi ujenzi na ukarabaiti uliposimama kabisa mwanzoni mwa miaka ya themanini, kiwango cha kukamilika kwa kazi ya ujenzi wa majengo, uwekaji wa umeme na ufungaji wa mitambo ulikuwa umefikia karibu asilimia 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa kuendeleza zao la nyama nchini, Wizara yangu bado inaona umuhimu mkubwa wa kuwa na kiwanda cha kusindika nyama ikiwa ni pamoja na kile cha Shinyanga. Mpango uliopo wa Serikali kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ni kumpata mwekezaji kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Juhudi za *PSRC* na kutafuta wawekezaji katika Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kupitia utangazaji wa zabuni ulianza mwaka 2001, lakini mwekezaji huyo hakuweza kutoa *business plan* kama ilivyohitajika na hivyo ikashindikana. Mara ya pili mwaka 2003 *PSRC* walitangaza tena na mpaka hivi leo mazungumzo bado yanaendelea.Majengo yaliyopo pale Kiwanda cha Shinyanga hayakukusudiwa kutumiwa kwa shughuli nyingine za maendeleo ya jamii na kama ilivyopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge kwani hadi sasa dhamira ya kukifufua kiwanda hicho ipo na tunaendelea kumtafuta mwekezaji kama nilivyoeleza hapo awali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa napokea vi-*note* hapa, lakini muda umekwisha kwani tulitumia kupeleka zile hati ambazo walikuwa wanaziwasilisha hapa. Kwa hiyo, tulikuwa tunafidia ule muda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, sasa tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006

**Wizara wa Elimu na Utamaduni**

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi kupitisha makadirio ya matumizi baada ya kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii ya mwanzo kuwapongeza na kuwashukuru; (a) Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa hotuba yake ambayo imetoa tathmini ya mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa Ttaifa kwa jumla; (b) Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba (Mbunge), Waziri wa Fedha kwa hotuba yake iliyowasilisha kwa ufasaha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2005/2006 ambayo imetoa mwelekeo kwa sekta zote zinazohusika katika kukuza uchumi kwa kuzingatia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) ambao pamoja na mambo mengine pia inalenga kuboresha ufanisi wa nguvukazi ya Taifa kwa njia ya elimu; (c) Mheshimiwa Frederick T. Sumaye (Mbunge), Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti iliyofafanua mambo muhimu ya elimu yaliyoamuliwa na Serikali. Natoa shukrani zangu kwa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'; Mbunge wa Babati Mashariki, kwa kutoa ushauri na maelekezo ya kuboresha Bajeti ya Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni baada ya uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Utamaduni imeendelea kuwa na majukumu yafuatayo: -

(a) Kuandaa na kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na Sera ya Utamaduni.

(b) Kupanga na kusimamia mipango yote ya elimu kuanzia Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(c) Kuandaa na kusimamia vigezo vya ufanisi katika kutoa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Watu Wazima na Mafunzo ya Ualimu.

(d) Kuandaa Sheria na Marekebisho ya Sheria ya Elimu na kutoa miongozo mbalimbali ya utekelezaji ili kukidhi mahitaji na mabadiliko katika elimu na utamaduni.

(e) Kutoa miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa vikundi vya sanaa na vyama vinginevyo vya utamaduni.

(f) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia shughuli za Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni: -

(i) Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

(ii) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW).
(iii) Baraza la Mitihani Tanzania *(NECTA).*
(iv) Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA).
(v) Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)
(vi) Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA).
(vii) Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM).*
(viii) Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza.

Katika kutekeleza majukumu hayo Wizara inaongozwa na (a) Sheria ya Elimu Na. 25 ya 1975 na rekebisho Na. 10 la 1995; (b) Taarifa ya Mfumo wa Elimu Tanzania kwa karne ya 21; (c) Sera ya Elimu na Mafunzo; (d) Sera ya Utamaduni; (e) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; (f) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na (g) Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2000 ya Chama Tawala cha CCM. Iili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo katika shule zote nchini, Wizara huendesha ukaguzi wa shule na hutoa mitihani ya kitaifa ya darasa la IV, VII, Kidato cha 2, 4 na 6 na Mitihani ya Cheti na Stashahada ya Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa mwisho wa Serikali ya Awamu ya Tatu inayoongozwa na Rais Benjamin William Mkapa, ningependa kulitaarifu Bunge kuhusu maendeleo makubwa ya elimu na utamaduni katika kipindi hicho miaka kumi (1995 – 2005). Serikali ya Awamu ya Tatu ilichukua hatua muhimu zifuatazo: -

(i) Iliandaa Program ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu *(Education Sector Development Programme – ESDP)* ya 1997 kama hatua muhimu ya kuandaa Utekelezaji wa Taarifa ya Mfumo wa Elimu ya Tanzania Karne ya 21 *(Tanzania Education System for the 21st Century)* iliyozaa Sera ya Elimu na Mafunzo 1995.

(ii) Ilihakikisha inatimiza masharti magumu ya *HIPC* ili iweze tena kukopesheka na kupewa misaada ya maendeleo. MMES na MMES ni matokeo ya hatua hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Elimu ya Msingi ni kama yafuatayo: -

(i)Wanafunzi wa Shule za Msingi (Darasa la I – VII) wameongezeka karibu maradufu kutoka milioni 3.8 mwaka 1995 hadi milioni 7.5 mwaka 2005.

(ii)Shule za Msingi zimeongezeka kutoka 10,927 mwaka 1995 hadi 14,257 mwaka 2005 ambalo ni ongezeko la shule 3,330 sawa na asilimia 30. Shule mpya zilizoongezwa ziko katika maeneo yaliyokuwa mbali na shule au yasiyofikika kwa urahisi.

(iii) Watoto wa rika la elimu ya msingi (miaka 7 – 13) walioko shuleni wameongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 1995 hadi asilimia 95 mwaka 2005. Kwa hiyo, watoto wa rika hilo walio nje ya shule wamepungua kutoka asilimia 45 mwaka 1995 hadi asilimia 5 tu mwaka 2005.

(iv) Watoto wenye umri wa miaka saba wanaoanza darasa la kwanza wameongezeko kutoka asilimia 12.5 mwaka 1995 hadi asilimia 87.4 mwaka 2005. Haya ni mafanikio makubwa kwa sababu mitaala huandaliwa kulingana na umri sahihi kwa kila ngazi ya elimu. Walimu wanajua kuwa wanafunzi darasani wanatakiwa kuwa na umri sawa ili wafundishike vizuri, kwa kasi moja.

(v) Wanafunzi wa umri wa juu kuliko rika la Elimu ya Msingi (miaka 7 – 13) wamepungua kutoka asilimia 22.1 mwaka 1995 hadi asilimia 14.7 mwaka 2005. Haya ni mafanikio mazuri sana yatakayochangia sana kuondoa matatizo ya watoto wa umri mkubwa yaliyokuwa yameshamiri katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Sekondari imepanuliwa ingawaje bado hatujafikia kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya kufuta umaskini na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Lakini mafanikio yafuatayo ni mwanzo mzuri: -

(i) Wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza wameongezeka kutoka 53,698 mwaka 1995 hadi 180,239 mwaka 2005 ambalo ni ongezeko la zaidi ya mara tatu na limesababisha ongezeko la karibu mara tatu la wanafunzi wa ngazi ya Sekondari ya Kawaida (KI – K4) kutoka 183,659 (sawa na asilimia 7.6 ya rika husika la miaka 14 – 17) mwaka 1995 hadi 489,942 (sawa na asilimia 15.9 ya rika husika la miaka 14 – 17) mwaka 2005 wakiwemo wasichana 231,808 sawa na asilimia 47.3.

(ii) Wanafunzi wanaojiunga kidato cha 5 wameongezeka mara 2.7 kutoka 6,875 mwaka 1995 hadi 18,893 mwaka 2005 na kusababisha ongezeko la karibu mara tatu la mwanafunzi wa sekondari ngazi ya juu (K5 na K6) kutoka 12,716 (sawa na asilimia 1.1 ya rika husika la miaka 18 – 19) mwaka 1995 hadi 34,383 (sawa na asilimia 2.4 ya rika husika la miaka 18 – 19) mwaka 2005 wakiwemo wasichana 12,763 sawa na asilimia 37.12.

(iii) Jumla ya wanafunzi wa kidato cha 1 – 6 imeongezeka kutoka 196375 (sawa na asilimia 5.5 ya rika husika la miaka 14 – 19) mwaka 1995 hadi 524325 sawa na asilimia 11.7 ya rika husika la miaka 14 – 19) mwaka 2005 ambalo ni ongezeko la karibu mara tatu wakiwemo wasichana 244,551 sawa na asilimia 44.64.

(iv) Jumla ya shule za sekondari imeongezeka zaidi ya mara tatu kwa asilimia 195 kutoka 595 mwaka 1995 hadi 1755 mwaka 2005 zikiwemo 1206 za Serikali na 549 zisizo na Serikali sawa na asilimia 31.0. (Makofi)

Aidha, huu ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa MMES, mpango ambao utaongeza idadi ya wanafunzi kwenye Shule za Sekondari ngazi ya kawaida hadi 2,000,000 sawa na asilimia 50 ya rika hilo, ifikapo mwaka 2010 na ngazi ya juu hadi 250,000 sawa na asilimia 25 ya rika lengwa.

(v) Kuanzia mwaka huu katika mtaala mpya masomo ya Sekondari yamepunguzwa kutoka 13 hadi 8 kwa kuunganisha Masomo ya Elimu ya Kujitegemea

(Ufundi, Kilimo na Biashara) na masomo ya kawaida. Mtaala mpya umeanza kutumika kidato cha 1 mwaka 2005.

Lengo la hatua hii ni kuongeza ubora wa taaluma inayotolewa katika Shule zetu za Sekondari kwa kuongeza ufundishaji wa masomo sahihi ya ngazi hii ya elimu ambayo ni (a) Hisabati *(Mathematics),* (b) Lugha za Kufundishia (Kiswahili na *English*), (c) Masomo ya Sayansi (*Biology*, *Chemistry* na *Physics*), (d) Sayansi ya Jamii (History, Uraia na *Geography*). Mtaala umerekebishwa ili masomo hayo yawe pia masomo chukuzi ya stadi za kazi na za maisha na masuala mtambuko pamoja na Elimu ya Kujitegemea. Mpangilio huu mpya wa masomo utampatia mwanafunzi elimu bora zaidi ya Sekondari itakayompa msingi mzuri zaidi wa kuendelea na Elimu ya Juu au kumudu vizuri mafunzo ya ufundi na hata mahitaji ya ajira na kujiajiri.

Hatua hii ni utekelezaji wa taarifa maalum ya Mfumo wa Elimu ya Tanzania katika karne ya 21 *(The Tanzania Education System for the 21st Century)* iliyoandaliwa na Tume maalum ya wataalam iliyoteuliwa na Serikali mwaka 1990 na ambayo ilizaa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ambayo mwezi wa nne mwaka 1995 Mheshimiwa Profesa Sarungi, Waziri wa Elimu wa wakati huo aliiwasilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Katika kutekeleza sera hiyo Serikali iliandaa *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Development Programme (ESDP)* ya mwaka 1997 ambayo ninatambua kwamba ilisimamiwa na Waziri niliyempokea, Profesa Juma Kapuya na inatekelezwa kupitia MMEM (2002 – 2006) na MMES (2004 –2009). Aidha, mtaala mpya umezingatia Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025) na haja ya kuendana na dunia ya utandawazi *(globalization)* na soko huria *(liberalization). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio katika Elimu ya Ualimu yamekuwa kama ifuatavyo: -(i)Idadi ya Walimu Tarajali katika Vyuo vya Ualimu imeongezeka kutoka 12,417 mwaka 1995 hadi 29,952 mwaka 2004, ambalo ni ongezeko la walimu 17,535 sawa na asilimia 141.2. Aidha, mafunzo kazini yameimarishwa ili kuboresha ufundishaji.

(ii)Vyuo vya Ualimu vimeongezeka kutoka 34 mwaka 1995 hadi 52 mwaka 2005 vikiwemo 18 visivyo vya Serikali sawa na asilimia 35.

(iii) Ili kuongeza idadi ya walimu wenye Shahada na Stashahada ya Elimu, imeamuliwa kuwa kuanzia mwaka huu 2005, Shule ya Sekondari Mkwawa na Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam, zitabadilishwa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Elimu vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Aidha, mafunzo ya Shahada ya Elimu yanarekebishwa ili yachukue miaka mitatu tu na mwaka wa kwanza utakuwa unatosha kupata Stashahada ya Ualimu ili wahitimu wake baadaye waweze kujiunga moja kwa moja mwaka wa pili na masomo ya shahada. Vyuo vya Ualimu vya Wizara ya Elimu na Utamaduni vinavyotoa mafunzo ya Stashahada ya Elimu, baada ya kufanyiwa marekebisho yanayotakiwa, vitakuwa Vyuo Ambata *(Affiliate Colleges)* vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili viweze kutoa Stashahada ya Elimu kama ile ya mwaka wa kwanza wa shahada ya miaka mitatu.

Kuanzia mwaka huu 2005, Chuo cha Ualimu cha Mtwara kitakuwa Chuo Ambata cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kitaanza kutoa stashahada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, mafunzo ya kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yanaanzishwa katika Vyuo vyote vya Ualimu. Somo hilo litakuwa ni la lazima kwa kila Mwalimu Tarajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko kubwa la shule na wanafunzi limekuwepo pia ongezeko la ubora wa elimu itolewayo katika shule zetu kwa vipimo vya mitihani ya kitaifa inayotungwa na Baraza la Mitihani Tanzania kama ifuatavyo: -

(i) Katika mtihani wa darasa la VII wa kuhitimu Elimu ya Msingi asilimia ya kufaulu *(pass rate)* imeongezeka kutoka 14.6 mwaka 1995 hadi 49 mwaka 2004. *(Makofi)*

(ii) Katika mtihani wa kidato cha 4 wa kuhitimu Elimu ya Sekondari ya Kawaida asilimia ya kufaulu *(pass rate)* katika daraja la I – III imeongezeka kutoka 25mwaka 1995 hadi 39 mwaka 2004 kwa shule zote kwa pamoja na hadi asilimia 55 kwa Sekondari za Serikali zikichukuliwa peke yake.

(iii)Katika mtihani wa kidato cha 6 wa kuhitimu Elimu ya Sekondari ya Juu asilimia ya waliofaulu katika daraja la I – III imeongezeka kutoka 65.5 mwaka 1995 mwaka 1995 hadi 88.4 mwaka 2005. Tatizo kubwa linalotukabili sasa ni wanafunzi wengi waliofaulu vizuri kidato cha 6 kukosa nafasi za elimu ya Chuo Kikuu. Mwaka 1995 tatizo lilikuwa vyuo vikuu kukosa wanafunzi waliofaulu vizuri mitihani ya kidato cha 6 na hata Vyuo Vikuu vikalazimika kuanzisha mitihani yao *(matriculation examination)* na pia mafunzo maalum *(remedial teaching)* ya kuwainua wanafunzi kitaaluma kabla ya kuanza kusomea shahada zao.

Sasa kibao kimegeuka! Tatizo siyo uhaba wa wanafunzi waliofaulu vizuri, bali uhaba wa nafasi za Chuo Kikuu. Hali ya uhaba wa nafasi ya Chuo Kikuu imekuwa mbaya zaidi mwaka huu kutokana na makundi mawili ya kidato cha 6 wa mwaka jana 2004 na mwaka huu 2005 yote mawili kuwania nafasi za chuo kikuu za mwaka huu 2005!

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Utamaduni yamekuwa na mafanikio yafuatayo: -

- Serikali iliandaa Sera ya Utamaduni iliyopitishwa mwaka 1997.

- Vikundi vya burudani vilivyosajiliwa viliongezeka kutoka 133 mwaka 1995 hadi vikundi 634 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 377. *(Makofi)*

- Wanafunzi wa Stashahada ya Sanaa kutoka Chuo cha Sanaa Bagamoyo wameongezeka kutoka 30 mwaka 1995 hadi 84 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, ukurasa 51 – 57, hususan vifungu 54 (i) – (x) na 55 (i) – (iii) yamewekwa malengo mbalimbali ya maendeleo ya elimu ya kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2000 – 2005. Naomba nichukue nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kutekeleza vifungu hivyo kama ifuatavyo: -

(i) Kukamilisha miradi yote ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, madawati, vyoo vya wanafunzi na kuendelea kuhamasisha Wananchi waendelee kujenga Shule mpya za Kutwa za Sekondari kwa kila Tarafa au Kata.

- Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMES) 2002 – 2006 umeandaliwa. Mpango huu unatekeleza ujenzi wa majengo yote ya shule yakiwemo madarasa, nyumba za walimu, maliwato, ofisi na ununuzi wa samani.

- Kuanzia mwaka 2002 – 2005 yamejengwa madarasa 45,000, nyumba 8,527 za walimu, matundu ya vyoo 98,827 na kununuliwa madawati 285,898.

- Shule za Msingi zimeongezeka kutoka 11, 608 mwaka 2000 hadi 14,257 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 22.8.

- Kutokana na juhudi za Wananchi kujenga shule, Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 927 mwaka 2000 hadi kufikia 1,745 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia a88.2/

(ii) Kuzipatia Shule za Sekondari zinazojengwa kwa nguvu za Wananchi usajili bila urasimu, vifaa vya kufundishia, maabara, maktaba, walimu na kuongeza nafasi kwa wasichana.

- Shule mpya 828 za Sekondari zilisajiliwa kati ya mwaka 2000 na 2005. *(Makofi)*
- Idadi ya wasichana katika ngazi ya Sekondari ya kawaida imeongezeka kutoka 112, 303 mwaka 2000 hadi kufikia 231,808 mwaka 2005 sawa na ongezeko la zaidi ya mara mbili.

- Idadi ya wasichana katika ngazi ya Sekondari ya Juu (K5 na K6) imeongezeka kutoka 7,945 mwaka 2000 hadi kufikia 12,763 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 60.6.

- Idadi ya wasichana katika K1 hadi K6 kwa ujumla imeongezeka zaidi ya mara mbili kutoka 120,248 mwaka 2000 hadi kufikia 244,571 mwaka 2005.

(iii) Dola kuelekeza nguvu zaidi katika maandalizi ya walimu ngazi zote

.• Wanafunzi wa Mafunzo ya Ualimu Tarajali Daraja A katika Vyuo vya Ualimu wameongezeka kutoka 3,303 mwaka 2000 hadi kufikia 25,888 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 683.8.

•Wanafunzi wa Mafunzo ya Ualimu Tarajali Stashahada katika Vyuo vya Ualimu wameongezeka kutoka 2,511 mwaka 2000 hadi kufikia 8,024 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 219.6.

(iv)Kuhakikisha kwamba mapengo ya walimu katika baadhi ya Shule za Msingi na Sekondari yanazibwa.

• Walimu wapya 45,451 wakiwemo 37,261 wa Daraja A, 7,152 wa Stashahada walioajiriwa kati ya mwaka 2000 na 2005.

• Kuanzia mwaka 2003 wanafunzi wa Mafunzo ya Ualimu Tarajali wamekuwa wakiajiriwa moja kwa moja baada ya kuhitimu mafunzo.

•Kati ya mwaka 2000 na 2005 vibali vya ajira mbadala viliombwa na kutolewa ili kujaza mapengo ya jumla ya walimu 1,1134 walioacha au kuachishwa kazi kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Elimu ya Awali na ya Msingi, malengo yaliwekwa katika: -

(i) Kufikisha Elimu ya Awali kwa wote wanaostahili haraka kadri iwezekanavyo.

• Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zimeagizwa kufungua madarasa ya Elimu ya Awali katika kila Shule ya Msingi ya Serikali nchini. Aidha, wadau wengine pia wamehamishwa na kuhimizwa kuwekeza katika Elimu ya Awali kote nchini.

• Madarasa ya Elimu ya Awali katika Shule za Msingi za Serikali imeongezeka kutoka 5,234 mwaka 2000 hadi kufikia 21,108 Mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 303.3.

• Watoto wa umri wa miaka 5 – 6 walioandikishwa kwa Elimu ya Awali nchini wameongezeka kutoka 310,933 mwaka 2000 hadi kufikia 638,591 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 105.4.

(ii) Kuongezeka idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule wanaoandikishwa na wanaomaliza Shule za Msingi. Lengo ni kuwa asilimia 85 ya watoto waandikishwe ifikapo 2003.

•Lengo la uandikishaji wa asilimia 85 ya watoto wote lilivukwa kwa kufikia watoto wote walioandikishwa *(Gross Enrolment Ratio-GER)* kuwa asilimia 98.6 ya idadi ya watoto rika lengwa wa mwaka 2002 na wameongezeka hadi *GER* 109.9 mwaka 2005.

•Idadi ya wanafunzi katika Shule ya Msingi imeongezeka kutoka 4,382,410 mwaka 2000 hadi 7,541,208 sawa na asilimia 72.1.

•Asilimia ya watoto wa rika lengwa la Elimu ya Msingi (miaka 7 – 13) walio shuleni *(Net Enrolment Ratio – NER)* imeongezeka kutoka asilimia 58.8 mwaka 2000 hadi kufikia *NER* 94.8 mwaka 2005.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002 – 2006 umeboreshwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuhakikisha kuwepo kwa majengo yote ya shule, walimu, vitabu vya kiada na ziada, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na mkao sawa darasani.

•Asilimia ya watahiniwa wa darasa la VII wanaofaulu imeongezeka kutoka 19.3 mwaka 1999 hadi 48.7 mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato mzima wa ushirikishwaji wa wadau wote wa elimu, malengo yalikuwa: -

(i) Kuhakikisha kwamba Bodi za Shule na Kamati za Shule za Msingi zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria pamoja na kuhakikisha kwamba michango ya ziada inayotozwa na kila shule nchini haiwi kero kwa wazazi na kwamba Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zinasimamia na kudhibiti matumizi ya michango hiyo.

• Wakuu wa Mikoa wamepewa madaraka ya kuteua Bodi za Shule ili ziwajibike kwao ambao ndio wenye mamlaka ya utawala na maendeleo katika Mikoa yao.

• Kanuni ya Uandikishaji na Mahudhurio ya lazima ya mwaka 2002 *(The Compulsory Enrolment and Attendance Rules 2002)* inafanya Elimu ya Msingi kuwa ni ya lazima kwa uandikishaji na mahudhurio na inatoa adhabu ya faini isiyozidi Shilingi 100,000/= au kifungo kisichozidi miezi 9 au adhabu zote mbili kwa atakayevunja kanuni hiyo.

• Wajibu wa kusimamia utekelezaji na kuwapeleka mahakamani wanaokiuka Kanuni ya Uandikishaji na Mahudhurio ya lazima wamepewa Maafisa Watendaji wa Kata. Maafisa Watendaji wa Kata wamepewa wajibu wa kisheria wa kusimamia uandikishaji na mahudhurio ya wanafunzi katika maeneo hayo.

• Kutoa mafunzo kwa Kamati ya Shule za Msingi nchi nzima ili wajumbe wajue wajibu na madaraka yao ya kupitisha na kusimamia mipango yote na matumizi ya fedha za shule.

• Kuifanya Elimu ya Msingi kuwa ni ya bure na lazima kwa kufuta ada na michango mbalimbali ya Shule za Msingi ili isiwe kikwazo kwa watoto wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini kujiunga na shule na kubakia shuleni hadi wahitimu Elimu ya Msingi. *(Makofi)*

(ii) Kuongeza kipaumbele katika Bajeti ya Elimu na pia kuimarisha ushirikiano wa Wahisani, Mashirika ya Dini, Sekta ya Binafsi na kupitia Vyombo na Taasisi zake mbalimbali kama *NGOs,* Jumuiya za Wananchi na kadhalika.

- Serikali ya Awamu ya Tatu imetimiza masharti yote ya Nchi Maskini zenye Madeni Sana *(Highly Indebted Poor Countries (HIPC)* na hivyo kuweza kufutiwa madeni na fedha iliyotolewa kutoka ulipaji wa madeni imetumika kuongeza Bajeti ya Elimu na pia mikopo ya masharti nafuu kutoka Vyombo vya Kifedha vya Kimataifa hususan Benki ya Dunia imepatikana. Aidha, misaada ya wahisani imeweza kupatikana kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Elimu kama MMEM na MMES.

- Bajeti ya Elimu imeongezeka kutoka asilimia 21.8 mwaka 1999/2000 hadi kufikia asilimia 37.3 mwaka 2004.05 na kufikia zaidi ya Shilingi bilioni 500 kwa mwaka kwa ajili ya kupanua na kuboresha elimu, hususan Elimu ya Msingi na Sekondari.

- Ushirikiano na Wadau wa Elimu umeimarishwa kupitia vikao vya pamoja vya Kamati ya Uongozi wa Maendeleo ya Elimu *(ESDP Inter-Ministerial Steering Committee),* Kamati ya Ushauri *(Advisory Committee),* Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(Basic Education Development Committee)* na Vikundi vya Kamati za Kiufundi *(Technical Working Groups).* Mipango imeandaliwa na kutekelezwa kwa ushirikiano na wabia na wadau wote katika maendeleo ya elimu.

(iii)Jitihada za kuwaelimisha wazazi juu ya jukumu lao la kuchangia gharama za elimu ya watoto wao na kuweka utaratibu wa kuwasaidia wale wasiokuwa na uwezo wa kujilipia au wanafunzi waliofaulu vizuri kuingia Sekondari ama Chuo Kikuu ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwagharamia.

- Wananchi wameendelea kuhamasishwa kujenga na kuimarisha Shule za Msingi na Sekondari. Kwa kupitia MMEM na MMES, Serikali imewaunga mkono kwa kutoa Ruzuku ya Maendeleo *(Development Grant)* kwa Shule za Msingi na Sekondari ili kusaidia ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

- Serikali inatoa Ruzuku Maalum kwa ajili ya kulipia gharama za Sekondari kwa watoto wanaotaka katika familia zenye kipato cha chini. Shilingi bilioni 1.1 zilitengwa mwaka 2002, Shilingi bilioni 2.5 mwaka 2003, Shilingi bilioni 4.3 mwaka 2004 na Shilingi bilioni 6.9 mwaka 2005 kwa ajili ya kugharamia Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi wa familia zenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Elimu ya Watu Wazima, Ilani ilielekeza kuwa: -

(i) Suala la kufuta ujinga miongoni mwa watu wazima ambao bado wanakabiliwa na tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu litatazamwa na kupewa msukumo mpya katika maeneo matatu muhimu.

•Kupunguza ongezeko la watoto na vijana wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kuhakikisha kuwa watoto waliokuwa na umri wa miaka 7-10 mwaka wa kwanza na MMEM wanajiunga na Shule za Msingi kwa utaratibu mpya wa Elimu ya Msingi Bure na ya Lazima *(Free and Compulsory Primary Education).*

•Mipango ya Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa MEMKWA umewezesha watoto katika makundi rika mawili (a) watoto wa umri wa miaka 11 – 13 na (b) vijana wa umri wa miaka 14 – 18 wapate Elimu ya Msingi nje ya shule kwa mfumo usio rasmi.

•Kuboresha utoaji wa Elimu ya Watu Wazima kwa kutumia mbinu shirikishi ya reflekti (MUKEJA) ambapo walengwa wanajifunza kusoma, kuandika na kuhesabu kwa namna inayosaidia kujiongezea ujuzi katika shughuli zao za kiuchumi katika maeneo yao. Wanakisomo 260,000 wa mwaka 2003 na 415,000 wa mwaka 2005 wamepatiwa Elimu ya Watu Wazima kwa kutumia mbinu shirikishi ya reflekti Wilaya zinazofaidika na utaratibu huu ni Kinondoni, Ilala, Temeke, Masasi, Newala, Nachingwea, Liwale Tunduru, Songea Vijijini, Moshi Mjini, Lushoto, Sengerema, Biharamulo, Morogoro Vijijini na Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa kuhamasisha uanzishawaji, uendelezaji, utoaji mafunzo na uimarishaji ikiwa ni pamoja na vikundi vya sanaa na burudani nchini, vikundi vya sanaa na burudani vilivyosajiliwa vimeongezeka kutoka 421 mwaka 2000 hadi 634 mwaka 2005 sawa na ongezeko la usajili wa wanafunzi wa stashahada ya sana kutoka 50 mwaka 2000 hadi 84 mwaka 2005 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 68.

Aidha, Mfuko wa Utamaduni umeanzishwa kama chombo cha kutoa misaada ya fedha ili kuendeleza shughuli za Utamaduni za Taasisi na vikundi mbalimbali na pia kama chombo cha kutambua, kuenzi na kutoa tuzo kwa watendaji mahiri katika nyanja za Utamaduni. Miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Utamaduni imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutoka miradi 56 mwaka 2000 hadi 72 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 28.6.

Maamuzi muhimu yaliyofanikisha utekelezaji wa Ilani ni:-

(i) Uamuzi wa Serikali wa kuifanya Elimu ya msingi kuwa ya bure na ya lazima kwa watoto wote wa Tanzania na kupunguza karo ya Sekondari za Kutwa kwa asilimia 50 kutoka Shilingi 40,000 kuwa Shilingi 20,000. *(Makofi)*

(ii)Kuandaa na kutekeleza MMEM 2002 – 2006 na MMES 2004 – 2009 inayotoa Ruzuku ya Maendeleo na Ruzuku ya Uendeshaji ya shule zinazojengwa na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005 na malengo ya mwaka 2005/2006 kwa kila Idara na Taasisi zake ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Msingi 2004/2005, idadi ya watoto katika shule za awali imeongezeka kutoka watoto 554,835 mwaka 2004 hadi 638,591 mwaka 2005. Hili ni ongezeko la watoto 83,756 sawa na ongezeko la asilimia 15.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya Shule za Msingi imeongezeka kutoka 13,689 mwaka 2004 hadi 14,257 mwaka 2005 ambalo ni ongezeko la shule 568 sawa na asilimia 4.1. Wanafunzi katika shule za msingi wameongezeka kwa asilimia 6.5 kutoka 7,083,063 (*NER* 90.5 na *GER* 106.3) mwaka 2004 hadi 7,541,208 (*NER* 94.8 na *GER* 109.9) mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio ya mwaka wa nne wa MMEM 2004/2005, huu ni mwaka wa nne wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM 2002-2006) ambalo lengo lake kuu ni kutoa Elimu Bora ya Msingi kwa wote. Mwaka 2005 tulikuwa na lengo la kuandikisha watoto 1,041,880 darasa la kwanza, lakini walioandikishwa ni 1,348,437 ikiwa ni zaidi ya lengo kwa wanafunzi 326,435 sawa na asilimia 31.3 kutokana na uandikishaji huo.

(a) Wanafunzi wa darasa la I – VII wameongezeka kutoka 7,083,063 hadi 7,541,208.

(b) Wanafunzi wote walioko shuleni kama asilimia ya idadi ya watoto wa rika lengwa *(Gross Enrolment Ratio (GER)* wameongezeka kutoka asilimia 106.3 mwaka 2004 na kufikia asilimia 106.9 mwaka 2005.

(c) Wanafunzi wa rika la Elimu ya Msingi (miaka 7-13) walioko shuleni *(Net Enrolment Ratio (NER)* imeongezeka kutoka asilimia 90.5 mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 94.8 mwaka 2005.

(d) Asilimia ya watoto wa umri mkubwa kuliko rika la Elimu ya Msingi (miaka 7- 13) imepungua kutoka asilimia 15.7 mwaka 2004 hadi asilimia 14.9 mwaka 2005.

(e) Mikoa 19 imefikia *GER* ya asilimia 100 au zaidi. Mikoa miwili tu ya Dodoma na Tabora haijafikia kiwango cha *GER* ya asilimia 100 ambayo ni hatua ya lazima ingawaje haitoshi kufikia Elimu ya Msingi kwa wote.

(f) Walimu 10,563 wameajiriwa hadi Juni , 2005 sawa na asilimia 145 ya lengo la 7,286.

(g) Ruzuku ya maendeleo ya Shilingi bilioni 49.4 ilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, vyoo na utengenezaji madawati.

(h)Ruzuku ya uendeshaji ya Shilingi 31.71 zikiwemo za jumla ya Shilingi bilioni 15.88 za vitabu ili kuinua uwiano kutoka kitabu kimoja kwa watoto watatu hadi kufikia lengo la kitabu kimoja kwa mtoto mmoja na Shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya vivunge vya sayansi na tufe.

(i) Ruzuku ya uwezeshaji ya Shilingi 3,444,160,000 ilitolewa kwa Mikoa, Halmashauri, Kata na Kamati za Shule kwa ajili ya kujenga uwezo, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa MMEM.

(j) Wilaya zilipelekewa Shilingi 689,531,252 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi wa Shule za Msingi pamoja na kuwapima walimu wanafunzi waliokuwa katika mazoezi ya vitendo. Jumla ya magari 24 yaliyogharimu Shilingi bilioni 1.63 yalinunuliwa na kupelekwa katika Wilaya zilizoko katika mazingira magumu. Wilaya 80 zilinunuliwa kompyuta ili kurahisisha utendaji wao wa kazi.

(k) Kiwango cha kufaulu katika mtihani wa Darasa la VII kimeendelea kupanda kutoka asilimia 40.1 mwaka 2003 hadi asilimia 48.7 mwaka 2004 ikilinganishwa na 19.3 mwaka 1999 kabla ya MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Elimu ya Msingi, katika mwaka 2004/2005, Idara ya Elimu ya Msingi ilitekeleza miradi ifuatayo: -

Kwanza, ni lishe shuleni. Mradi huu unaendeshwa kwa ushirikiano na *Program* ya Chakula Duniani (*World Food Programme* (*WFP*) na utaendelea hadi mwaka 2006 katika Wilaya 11 za Mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida na Manyara. Lengo la mpango huu ni kutoa chakula kwa Shule za Msingi zinazowasomesha watoto wa jamii zinazohamahama kama vile wafugaji na wanaoishi kwa kuwinda, kula matunda na kurina asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shule zenye mazingira yanayomjali mtoto yaani *Child Friendly School Project – CFS,* mradi wa shule zenye mazingira yanayomjali mtoto unatekelezwa kwa msaada wa *UNICEF* katika Wilaya 6 za majaribio na utaendelea hadi mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa hali halisi na mpango wa shule yaani *School Mapping and Micro-planning.* Mradi wa utafiti wa hali halisi ya shule *(School Mapping)* umepanuliwa hadi kukamilisha Halmashauri zote 114 kwa mwaka 2004/2005. Aidha, Halmashauri 27 bado hazijafanyiwa *Micro-planning.* Mikakati imeandaliwa ili kufanya zoezi hili katika Halmashuri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Elimu ya Msingi 2005/2006 ni wa tano wa utekelezaji wa MMEM ambao una malengo ya kutoa Elimu Bora ya Msingi kwa wote kama ifuatavyo: -

(a) Kutoa ruzuku ya maendeleo ya Shilingi 5,556,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, kuandikisha Darasa la I Januari 2006 watoto wenye umri wa miaka 7 na waliobakia miaka iliyopita wa miaka 8 na 9.

(b) Kutoa ruzuku ya maendeleo ya Shilingi 3,312,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za vijijini.

(c) Halmashauri zimeruhusiwa kutenga fedha toka ruzuku hizo kwa ajili ya ujenzi wa matangi ya maji na vyoo na utengenezaji wa madawati ili kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu.

(d) Kuajiri walimu wapya 7,286 ili kukidhi ongezeko lkubwa la watoto wanaoandikishwa darasa la I.

(e) Kutoa nafasi za mafunzo tarajali kwa walimu 9,000 wa Daraja la A.

(f) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) nje ya mfumo rasmi wa elimu na kuimarisha Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA)

(g) Kutoa ruzuku ya uendeshaji wa shule ya Shilingi 62,145,000,000 kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili hatimaye kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). *(Makofi)*

(h) Kuimarisha ubora wa elimu kwa kutekeleza Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi uliorekebishwa na kuboresha mfumo wa mitihani na upimaji katika Elimu ya Msingi na Ualimu ngazi ya cheti.

(i) Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa MMEM ngazi za Mikoa, Halmashauri, Shule, Vyuo vya Ualimu na kuratibu ukaguzi wa hesabu za MMEM katika ngazi hizo na asasi za Wizara za *TET* na *NECTA*.

(j) Kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 zimetengwa jumla ya Shilingi 384,188,546,534. Kati ya fedha hizo, Shilingi 44,998,760,000 ziko katika fungu 56 ambalo limeombwa na Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Fedha zitakazopelekwa kwenye Halmashauri moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kugharamia Elimu ya Msingi ni Shilingi 301,321,699,834. Aidha, Shilingi 31,868,086,700 zinaombwa na Wizara yangu kwa ajili ya MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Idara ya Elimu ya Sekondari, malengo ya Elimu ya Sekondari ni kama ifuatavyo:

(a) Kuongeza nafasi ya utoaji Elimu ya Sekondari kwa rika la Elimu ya Sekondari (miaka 14 – 17) kutoka asilimia 7 ya mwaka 2003 hadi kufikia asilimia 50 ifikapo 2010.

(b)

Kupanua Elimu ya Sekondari kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kwa kuongeza nafasi za kidato cha I kutoka kupokea asilimia 23 ya watahiniwa wa Darasa la VII mwaka 2003 hadi asilimia 50 ifikapo mwaka 2010.

(c) Kuboresha Elimu ya Sekondari kwa kuongeza asilimia ya wanaofaulu mitihani ya kitaifa ya Kidato cha 4 katika madaraja I, II, III kutoka asilimia 39.1 mwaka 2003 hadi asilimia 60 ifikapo mwaka 2010.

(d) Kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa kwa jinsia zote na kwa Wilaya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Elimu ya Sekondari mwaka 2004/2005, kwa kuzingatia malengo ya Elimu ya Sekondari, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 nililitaarifu Bunge lako juu ya kuanza kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 – 2009.

Lengo la kuu la Mpango Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 – 2009 ni kuongeza idadi ya vijana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu Elimu ya Sekondari wakiwa na matokeo mazuri ya kujifunza kutoka 345,000 mwaka 2003 hadi 2,000,000 mwaka 2010. Aidha, nilitaja malengo matano ya MMES kuwa ni: -

(a) Kuongeza idadi ya wanaojiunga na Elimu ya Sekondari (*improvement of access)* kufikia asilimia 50 ya rika lengwa (Miaka 14-17) na asilimia 50 ya wahitimu wa Darasa la VII; pia asilimia 50 ya wahitimu wa Kidato cha Nne kujiungana Kidato cha Tano kila mwaka.

(b) Kuinua Usawa *(Improvement of Equity)* kwa jinsi zote, Wilaya zote, wenye ulemavu wa aina zote na makundi yenye tofauti ya mapato.

(c) Kuinua ubora *(Quality Improvement)* wa elimu ili wanaofaulu Kidato cha Nne katika Madaraja I-III waongezeke kutoka asilimia 36 mwaka 2003 hadi asilimia 70 mwaka 2009.

(d) Kupeleka madaraka Mikoani, Wilayani na shuleni ili kuboresha usimamiaji na uendeshaji wa Shule za Sekondari, madaraka ya uamuzi na usimamizi wa shule utahamishwa kutoka Wizara kwenda ngazi za Mkoa, Wilaya hadi Bodi za Shule baada ya kujengewa uwezo.

(e) Kuinua ubora wa Usimamiaji wa Elimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake ya msingi ya kuandaa sera, kufuatilia na kutathmini, kutunga kanuni, kuainisha na kuhakiki utumiaji wa rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuanza kwa MMES, mwaka 2004/2005 Idara ya Sekondari imepata mafanikio yafuatayo: -

(a) Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 1,291 mwaka 2004 hadi 1,745 Mei 2005. Hili ni ongezeko la shule 454 sawa na asilimia 35.2. Aidha, shule 10 zimeongezeka katika kipindi cha mwezi Juni 2005 na kufanya jumla ya shule 1,755 ambazo ni ongezeko la asilimia 35.9.

(b) Idadi ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 147,490 mwaka 2004 hadi wananfunzi 180,239 mwaka 2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.3.

(c) Wanafunzi wa Kidato cha kwanza hadi cha nne wameongezeka kutoka 401,598 mwaka 2004 hadi 489,942 mwaka 2005. Hili ni ongezeko la wanafunzi 88,344 au asilimia 22.

(d) Shule za Sekondari zisizo za Serikali zimeongezeka kutoka 463 mwaka 2004 hadi 549 mwaka 2005. Hili ni ongezeko la shule 86, au sawa na ongezeko la asilimia 18.6

(e) Jumla ya madarasa 667 yamejengwa katika shule zilizokuwepo 2004/2005 (kwa lengo la kuzipanua) pamoja na shule 386 zilizofunguliwa 2005. *(Makofi)*

(f) Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoingia Kidato cha Tano katika Shule za Serikali; shule 15 zimebadilishwa kuwa Sekondari za ngazi ya juu tupu *(A- level).*

Shule mpya 17 zimefungua mikondo ya ngazi ya juu tangu Agosti 2004 ambayo haikuwepo katika shule hizo. Shule 84 za Ngazi ya Juu zilizokuwepo zimeongeza mikondo ya ngazi ya juu na kufanya ongezeko la wanafunzi 4,901 zaidi ya mwaka uliopita sawa na asilimia 43.

Shule zilizofanywa Sekondari za Ngazi ya Juu Tupu ni Weruweru, Loleza, Songea Wasichana, Nganza, Ruvu, Kondoa, Shycom, Tanga, Milambo, Mwenge, Ndanda, Njombe, Musoma, Karatu na Minaki.

Vile vile, Shule za Sekondari za Ngazi ya Juu zilizoanza Agosti 2004 ni Songea, Ifunda Wasichana, Changarawe, Tumaini, Ruvu, J. J. Mungai, Ulayasi, *Nyerere High School*, Mpanda, Mahiwa, Kifaru, Ngudu, Nangwa, Rungwe, Iyunga, Lufilyo na Engutoto.

(g) Shilingi 4,619,120,000 zimepelekea shuleni kwa ajili ya ruzuku ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia na Shilingi 4,939,000,000 zimefidia ada kwa wanafunzi 264,950 wa kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kupeleka fedha za ukarabati katika shule za sekondari 30 ambazo ni Mpwapwa, Malangali, Rungwe, Engutoto, Mwika, Bukoba, Same, Iyunga, Tarakea, Tunduru, Mkuu, *Tanga Technical*, Weruweru, Karatu, Bwiru Wavulana, Pugu, Mtwara Ufundi, Chato, Songea Wavulana, Bagamoyo, Kibondo, Kondoa, *Usangi Day*, Vudoi, Songea Wasichana, Dakawa, Mzumbe, Kabuku, Balangdalalu na Endasaki. Idadi ya

Shule za Sekondari za Serikali zinazotoa Elimu ya Kidato cha Tano na Sita imeongezeka kutoka 84 mwaka 2004 hadi 101 mwaka 2005. Shule zisizo za Serikali zinazotoa Elimu ya Kidato cha Tano na Sita ni 127. Kwa hiyo jumla ya Shule za Sekondari zenye Kidato cha Tano na Sita mwaka 2005 ni 228.

Mikondo mipya ya Kidato cha Tano imeongezwa katika Shule 78 za Sekondari na kufanya wanafunzi waliochaguliwa kuingia Kidato cha Tano kuongezeka kutoka 12,253 mwaka 2004 hadi 16,059 mwaka 2005. Hili ni ongezeko la wanafunzi 3,806 sawa na asilimia 31.1

Jumla ya wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita imeongezeka kutoka 31,001 mwaka 2004 hadi 34,383 mwaka 2005. Jumla ya wanafunzi wote wa Shule za Sekondari Kidato cha Kwanza hadi cha Sita imeongezeka kutoka 432,599 mwaka 2004 hadi kufikia 524,325 mwaka 2005.Katika kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa, Serikali imeendelea: -

(a) Kuhakikisha kuwa idadi sawa ya wasichana na wavulana wanachaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza kila Mwaka.

(b) Kulipia gharama za elimu kwa wanafunzi 12,000 wa Kidato cha Kwanza kutoka familia zenye kipato cha chini kwa kutumia fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Wanafunzi 12,000 wa Kidato wa Kidato cha Pili hadi cha Tatu hugharamiwa kwa fedha za matumizi ya kawaida na wasichana 1,481 wa Kidato cha Nne hadi cha Sita hugharamiwa chini ya mradi wa *Girls Secondary Education Support (GSES).*

(c) Kuhamasisha ufunguzi wa Shule za Sekondari za Kutwa hususan kwenye maeneo ambayo hayana shule za kutosha ambapo Shule mpya 378 za Serikali zimefunguliwa. Mikoa yote, kupitia Wilaya na Halmashauri zao imefungua jumla ya madarasa mapya 1,802 ya Kidato cha Kwanza mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuendelea kuinua ubora wa Elimu ya Sekondari ndani ya MMES yafuatayo pia yamefanyika: -

(a) Shule za Sekondari za Serikali 644 zilipewa kiasi cha Shilingi 490,152,400 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya Sayansi na Hisabati.

(b) Walimu 461 walipatiwa mafunzo kazini, 327 mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati, 75 Programu Maalum ya Shahada ya Hisabati katika Chuo Kikuu cha Tumaini, 15 mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 5 mafunzo ya Shahada ya Juu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na 3 mafunzo ya Kompyuta katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha.

(c) Walimu 1,650 wameajirwa.(d) Ruzuku ya Maendeleo ya Shilingi 5,138,000,000 imetolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 734 katika shule mbalimbali zilizojengwa na Wananchi.

(e) Katika kuimarisha uongozi na usimazimi wa Elimu, Wizara ilifanikiwa kuwapatia Mafunzo ya Uongozi ya mwezi mmoja Wakuu wa Shule za Sekondari 60 za Serikali na zisizo za Serikali.

Aidha, iliendesha mafunzo kwa ajili ya Watekelezaji Wakuu wa MMES yaani, Wakuu wa Shule 1,038, Wahandisi wa Wilaya 120, Wahandisi wa Mikoa 20 na Wajumbe wa Kamati za Shule za Ujenzi 1,038 ili waweze kujua wanachohitajika kufanya katika kutekeleza MMES na kuweza kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu mpango huo.

(f) Ufaulu katika mitihani ya Kidato cha Nne Daraja la I hadi III umeongezeka kutoka asilimia 37.6 mwaka 2002 hadi asilimia 38.8 mwaka 2004 kwa shule zote na kutoka asilimia 45.2 mwaka 2002 hadi 53 mwaka 2004 kwa Shule za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotumwa kwenye shule zote za Sekondari zilizingatia vigezo vya mahitaji yaliyopo na idadi ya watoto wanaojiunga Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi waliomaliza darasa la Saba katika eneo husika na Wilaya zilizokuwa chini ya *Transition rate* ya asilimia 35. Kiasi cha Shilingi bilioni 43.1 zilitumwa shuleni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli ya kujenga madarasa 1,499 zilipelekwa Shilingi bilioni 10.5, kujenga nyumba za walimu 842 Shilingi bilioni 7.6, kukarabati shule 30 Shilingi bilioni 2.7, upanuzi wa shule 84 kuwa *A level* na 15 kuwa *A level* tu Shilingi bilioni 3.0, kununua vifaa vya kufundishia Shilingi bilioni 4.3, kununua chakula cha wanafunzi Shilingi bilioni 4.1, kuimarisha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) Shilingi bilioni 0.8, kuimarisha Elimu ya Ualimu Shilingi bilioni 4.0, kuimarisha Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)* Shilingi bilioni 1.0, kutoa ruzuku kwa watoto toka familia maskini Shilingi bilioni 1.6, kutoa ruzuku ya punguzo ya ada Shilingi bilioni 3.5 na kurekebisha Mitaala ya Elimu ya Sekondari *(TET)* Shilingi bilioni 0.2, jumla Shilingi bilioni 43.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Elimu ya Sekondari 2004/2005, miradi miwili ifuatayo ilitekelezwa na Wizara yangu sambamba na MMES kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari.

Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sayansi *(Science Education for Secondary Schools (SESS): -*

Mradi huu unalenga kuboresha ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati *(Science Education for Secondary Schools* (SESS) na kutoa Elimu dhidi ya UKIMWI, *(Prevention and Awareness in Schools of HIV and AIDS (PASHA)* ambao ulianza rasmi Julai, 2003. Kazi zilizotekelezwa na mradi huo katika kipindi hili ni: -

(a)Kuwapatia Mafunzo ya Uwezeshaji ya wiki tano nchini Kenya walimu 7 wa Masomo ya *Physics, Mathematics, Biology* na *Chemistry.*

(b)Kuwapatia mafunzo kazini ya wiki moja walimu 210 wa masomo ya *Physics, Biology, Chemistry* na *Mathematics* katika Mikoa ya Dodoma, Pwani na Iringa.

(c)Kutoa Mafunzo ya Ufuatiliaji (*Monitoring*) katika shule ya wiki moja Kwa Wakuu wa Shule, Wakuu wa Shule Wasaidizi na Walimu Waandamizi Taaluma.

(d)Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo katika mada za Kuzuia Maambukizo ya Virusi vya UKIMWI kwa walimu 84 katika Mkoa wa Tanga.

(e)Walimu 57 wa somo la *Biology* walipatiwa Mafunzo ya Mbinu Shirikishi za Ufundishaji wa mada za UKIMWI na 114 wamepata mafunzo ya ushauri nasaha.

(f)Kuendesha Kambi ya Sayansi kwa wasichana 270 wa Kidato cha Kwanza kutoa Mikoa 9 ya Arusha, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro na Singida. Kambi hiyo ilishirikisha pia vijana 10 kutoka nchi za Kenya na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Pili wa Elimu *(Education II Project),* katika mwaka 2004/2005 huo ulifanya yafuatayo: -

(a)Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa mafunzo kazini kwa walimu wapatao 900 kwa masomo ya Sayansi na Hisabati, Wakufunzi 180 wa masomo ya Sayansi na Hisabati, Wakaguzi wa Shule 60 wa masomo ya Sayansi na Hisabati na Wakuu wa Shule za Sekondari 306.

(b) Samani za maabara kwa shule zote 36 zimekamilika. Shule 26 zimepelekewa samani hizo na shule 10 ambazo ni Zingibari, Mnyambe, Igunga, King'ori, Mitole, Lukuledi, Kaliua, Chalao, Mogabiri na Manga zitapelekewa samani mara baada ya ujenzi wa maabara utakapokamilika.Shule 26 ambazo zimejengewa maabara na kupelekewa samani ni Mwaya, Galapo, Kijota, Oldonyosambu, Meatu, Runzewe, Nangwanda, Mbinga, Matola, Mangaka, Makiba, Matekwe, Mbekenyera, Bwisya, Kyela, Mahiwa, Kongwa, Kilangalanga, Mambwe, Kizwite, Kitomondo, Mkonge, Bumangi, Malagalasi, Inyonga na Chalo.

(c) Vitabu 35,600 vya masomo ya Sayansi na Hisabati vimepelekwa katika Shule 81 za Sekondari katika Halmashauri 30.

Halmashauri 30 zilizopatiwa vitabu vya Hisabati na Sayansi ni Igunga, Tabora Vijijini, Urambo, Bariadi, Geita, Kwimba, Misungwi, Musoma Vijijini, Musoma Mjini, Muleba, Korogwe, Muheza, Babati, Mwanga, Mbulu, Rombo, Kibaha, Kigoma Vijijini, Sikonge, Kasulu, Dodoma Vijijini, Singida Vijijini, Tandahimba, Kilwa, Newala, Ruangwa, Mbinga, Serengeti, Nkasi na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Malengo ya Elimu ya Sekondari 2005/2006, katika kipindi cha cha mwaka 2005/2006 chini ya MMES, Wizara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo: -

(a)Kujenga madarasa mapya 427 kwenye Shule za Sekondari zilizopo, madarasa 1,210 kwenye shule mpya za ngazi ya kawaida zinazojengwa na Wananchi na mengine 128 katika Shule za Ngazi ya Juu zilizopo.

(b)Kujenga nyumba za walimu 427 kwenye Shule za Sekondari zilizopo na nyumba 573 katika shule mpya za kawaida.

(c)Kujenga jumla ya maabara 88 katika shule zilizopo za ngazi za kawaida na juu.

(d)Kujenga majengo mengineyo ya shule kama vyoo, hosteli, mabweni, maktaba na kumbi za mikutano.(e)Kufanya ukarabati wa shule za zamani.

(f)Kukarabati miundombinu kwenye shule 6 za wanafunzi wenye ulemavu.

(g)Kugharamia Elimu ya Sekondari kwa wanafunzi 24,000 wa kidato cha Kwanza na Pili wa familia zenye kipato cha chini ndani ya MMES. Kuhusu Idara ya Elimu ya Ualimu, katika mwaka 2004/2005 ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Kuandaa walimu bora ili kukidhi mahitaji ya Shule za Awali 250, Msingi 25,888, Sekondari na Vyuo vya Ualimu 8,024. Walimu hawa ni wa ngazi ya cheti Daraja A na Stashahada Tarajali.

(b) Kuboresha taaluma na utaalam wa ufundishaji wa masomo ya Shule za Msingi kwa walimu wa Daraja A na B/C 50,000 wanapatiwa mafunzo kazini kwa utaratibu maalumu. Awamu ya kwanza ya walimu hawa (25,000) watafanya mtihani wa Daraja A ifikapo Mei, 2006.

(c) Kuboresha mazingira ya kutolea mafunzo katika Vyuo vya Ualimu 32 kwa kuvipatia vifaa vora vya kutosha kufundishia na kujifunzia.

(d) Kuhakikisha mafunzo ya ualimu yanakidhi mahitaji ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

(e) Kujenga uwezo wa Vituo vya Walimu 123 vya Wilaya (*Teachers' Resources Centres* – TRCs) kwa kuviwezesha kutoa mafunzo kazini kwa walimu hususan wa Shule za Msingi.

(f) Kutoa Mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa wakufunzi 230 ili kuboresha Mbinu za Kufundisha na Kujifunza.(g) Kuboresha uwezo wa wakufunzi 350 katika kuandaa walimu

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mafanikio ya Utekelezaji, Idara ya Elimu ya Ualimu iliendelea kutoa mafunzo kwa Walimu Tarajali wa Daraja A na Stashahada pamoja na Mafunzo ya Ualimu Kazini. Aidha, mafunzo ya Ualimu Kazini, Sayansi Kimu na Elimu Maalum ngazi ya cheti yameanza kutahiniwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Wizara imeanzisha utaratibu rasmi na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika kuboresha kozi ya wakufunzi iliyokuwa ikiendeshwa katika Chuo cha Ualimu Morogoro na kutahiniwa na Taasisi ya Elimu ya Stockhom – Sweden kama sehemu ya mafunzo ya Shahada ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanachuo/Walimu katika Vyuo vya Ualimu mwaka 2004/2005 ni kama ifuatavyo: -

(a) Walimu tarajali wa Daraja A waliohitimu baada ya kufaulu mazoezi ya kufundisha kwa vitendo shuleni ni 14,800.

(b) Wanachuo walioandikishwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Daraja A Tarajali Januari 2005 ni 6,489.

(c) Walimu wanafunzi waliofanya mazoezishuleni (Mwaka wa Pili) ni 10,792.

(d) Wanachuo Stashahada mwaka wa kwanza ni 3,624. (e)Walimu wa Daraja la B/C waliojiandikisha kwa mafunzo maalum Daraja B/C kufikia A ni 50,000.

(f) Walimu wa Daraja B/C ambao tayari wamefanya mitihani ya Wizara ya kutathmini mafunzo haya ni 25,000.

(g) Walimu wa Shule za Msingi waliopata mafunzo ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mbinu shirikishi kupitia vituo vya walimu ngazi ya Wilaya ni 41,927.

(h) Walimu wa Shule inayomjali Mtoto S/M – katika Wilaya za Masasi, Kisarawe, Songea, Vijijini, Musoma Vijijini na Ngara waliopatiwa mafunzo kuhusu ufundishaji wa Madarasa Mseto kwa kutumia njia shirikishi kwa ushirikiano wa *UNICEF* ni 260.

(i) Wakufunzi waliojiunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mafunzo ya Shahada ya Ualimu ni 280.

(j) Moduli zilizochapishwa kwa ajili ya walimu wa B/C ni 765,721.

(k) Moduli zilizochapishwa awamu ya pili kwa ajili ya walimu wa B/C ni 325,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu itaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(a) Kuanzisha miundombinu na mtandao wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Vyuo vya Ualimu vyote kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

(b)Kutenganisha Vyuo vya Stashahada na daraja A. Vyuo vya stashahada vitakuwa 14 na daraja la A vitakuwa 18. Aidha, vyuo vyenye uwezo mdogo vitapanuliwa kufikia uwezo wa kuchukua wanachuo 600.

(c)Kufuatilia uandaaji wa muhtasari wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu.

(d) Kuandaa Mkakati wa Kuboresha Menejimenti na Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanachuo wapya Tarajali kwa mwaka 2005/2006 ni kama ifuatavyo: -

(a) Wanachuo Tarajali Daraja A mwaka wa kwanza (Chuoni) ni 4,599.

(b) Wanachuo Tarajali Daraja A mwaka wa pili Shuleni ni 7,500.

(c)Wanachuo Tarajali Stashahada waliopo mwaka wa pili ni 3,624.

(d) Wanachuo Tarajali Stashahada mwaka wa kwanza ni 4,400.

Jumla ya ndogo ya walimu wapya Tarajali ni 20,123.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanachuo wapya wa Mafunzo Kazini kwa mwaka 2005/2006 ni kama ifuatavyo: -

**(**a)Walimu wa Daraja B/C watakaofanya mitihani ya Baraza la Mitihani Tanzania mwaka 2006 ni 26,000. Mafunzo kazini kwa walimu Daraja A ngazi ya cheti ni kama ifuatavyo: -

(i) Elimu Maalum ni 90.

(ii) Elimu ya Awali ni 250.

(iii) Sayansi Kimu ni 100.

Mafunzo kazini kwa walimu Daraja A ngazi ya Stashahada ni kama ifuatavyo: -

(i) Elimu Maalum ni 30.
(ii) Sayansi Kimu ni 40.
(iii) Fani za Sanaa Maonyesho na Ufundi, Michezo na Muziki ni 60.

(b) Walimu wa Shule za Msingi watakaopatiwa mafunzo ya ufundishaji na kujifunza kwa njia shirikishi ni 45,000. Jumla ndogo mafunzo kazini ni 71,570.

Jumla ya Wanachuo Wapya Tarajali na Mafunzo Kazini ni 91,693.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Idara ya Ukaguzi wa Shule ilikagua jumla ya Asasi za Elimu 17,148 sawa na asilimia 89 ya lengo la mwaka. Katika

kuboresha kazi ya ukaguzi wa shule, Wizara imenunua magari 12, kwa ajili ya ukaguzi wa shule na imeendesha mafunzo ya awali ya ukaguzi wa shule kwa Wakaguzi wa Shule wapya.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na: -

(a) Kufanya utafiti kuhusu ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi katika Shule za Msingi na Vyuo vya Ualimu Daraja la A.

(b) Kuandika Jarida la Fahamu Elimu kuhusu hali ya ufundishaji wa somo la *Civics* katika Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara imepanga kufanya ukaguzi wa asasi mbalimbali za Elimu 19,905. Aidha, idara itanunua magari 18 na kutoa mafunzo ya awali 8 ya Ukaguzi wa Shule kwa Wakaguzi wa Shule wapya 127. Idara pia itaendesha mafunzo ya Mbinu Shirikishi za Ufundishaji kwa Wakaguzi wa masomo ya *English*, Kiswahili, *Physics, Chemistry, Biology* na Ualimu.

Malengo ya Ukaguzi wa Shule mwaka 2005/2006 ni kukagua Shule za Awali 5,041, Shule za Msingi 7,018, Vituo vya Ufundi Stadi 130, Vituo vya Elimu Maalum 85, Vituo vya Elimu ya Watu Wazima 6,780, Shule za Sekondari 805 na Vyuo vya Elimu ya Ualimu 46. Jumla ni 19,905.

Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na:-

(a) Kupitia na kuboresha Mwongozo wa Mafunzo na Kiongizi cha Mkaguzi wa Shule.

(b) Kuboresha mazingira ya kazi kwa Wakaguzi wa Wilaya.

(c) Kuendesha mafunzo ya Menejimenti kwa Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Maendeleo ya utamaduni 2004/2005 ni: -

(a) Kupanua kiwango cha Ushiriki wa Wananchi katika shughuli za Utamaduni.

(b) Kuboresha Usimamizi na Uendeshaji wa shughuli za Utamaduni.

(c) Kuimarisha Elimu na Mafunzo ya Fani za Utamaduni.

(d) Kuimarisha na Kukuza Tasnia na Miundombinu ya Utamaduni.

(e) Kulinda na Kuimarisha Maadili na Utambulisho wa Taifa.

(f) Kuimarisha Ushirikiano wa Kimataifa katika Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ikishirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza mambo yafuatayo:- (a)Kukamilisha Uteuzi wa Vazi la Taifa kufuatia Mashindano ya Taifa ya Wabunifu yaliyofanyika Dodoma mwezi Juni 2003.

(b)Kwa kushirikiana na Mfuko wa Utamaduni, Idara iliendesha mafunzo ya ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa mbalimbali za utamaduni. Mafunzo haya yalitolewa kwa Maafisa Utamaduni wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji katika Mikoa 20 ya Tanzania Bara na Visiwani. Halmashauri ambazo hazikupatiwa mafunzo hayo ni zile zilizomo katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Maafisa Utamaduni walio katika Halmashauri hizo watapewa mafunzo haya katika mwaka wa fedha wa 2005/2006.

(c) Kuendesha Mkutano wa mwaka wa Sekta ya Utamaduni Mjini Morogoro tarehe 22 hadi 26 Novemba 2004. Jumla ya Wajumbe 187 walihudhuria Mkutano huo wakiwemo Maafisa Utamaduni wa Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Wawakilishi wa Wizara mbalimbali, Mashirika ya Umma, Mashirika yasiyo ya Serikali na Vyama vya Hiari.

(d) Kuendesha Tamasha la Utamaduni la Taifa ambalo lilifanyika Mjini Morogoro tarehe 24 – 26 Novemba, 2004. Lililohudhuriwa na wasanii 300 toka sehemu mbalimbali za nchi na Tamasha la Sanaa la Kitaifa lililofanyika katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo Septemba 2004.

(e) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Sanaa kwa wanafunzi 90 na ya muda mfupi kwa wanafunzi 70 katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

(f) Kutuma msaada uliotoka Mfuko wa Utamaduni Tanzania kwa miradi 70 iliyopo sehemu mbalimbali nchini. Msaada huu ulikuwa wa Shilingi 416,806,707 kwa miradi yote.

(g)Kuendesha mafunzo kwa wasanii kwa ajili ya kuwapatia mbinu sahihi za kuelimisha umma kuhusu *VVU* na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni itaendelea kukuza utamaduni kwa kutekeleza yafuatayo: -

(a) Kuandaa na kuendesha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Utamaduni.

(b) Kuendesha Tamasha maalumu la Utamaduni lenye lengo la kuimarisha umoja, amani, mshikamano na upendo miongoni mwa Watanzania.

(c) Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 90 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii 120 walio kazini katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo.

(d) Kuandaa na kuendesha Tamasha la Sanaa la Kimataifa.

(e) Kuendesha mafunzo ya mbinu za utawala na uendeshaji wa shughuli za Utamaduni kwa Maafisa Utamaduni 60 wa Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji.

(f) Kuendesha utafiti katika Mikoa 10 wa kubaini mila na desturi nzuri zinazoweza kuimarisha ufanisi katika vita dhidi ya UKIMWI, umaskini, rushwa na ubaguzi wa kijinsia. Aidha, mila na desturi ambazo ni kikwazo katika vita hivi zitabainishwa ili kuwatanabaisha Wananchi kuachana nazo

(g) Kukuza matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha katika Wizara, Idara, Mashirika na Vyombo vya Habari.

(h) Kuimarisha vikundi mbalimbali vya utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Idara ya Utawala na Utumishi ilishughulikia:-

(a) Ajira ya walimu wapya 1,744 wa Shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na watumishi wasio walimu 49.

(b) Masuala mbalimbali mengine ya ajira kama vielelezo Na.44.1 na 44.2 vinavyoonyesha.

Walimu wa Stashahada (Ajira mpya) ni 1,500, Walimu wa Shahada wa Sekondari (Ajira mpya) ni 150, Walimu mbadala wa Sekondari ni 67, Walimu Daraja A mbadala ni 27. Jumla ya Walimu wa Sekondari ni 1,744.

Watumishi wasio Walimu walimu walikuwa Walinzi 3, Maafisa Maghala Wasaidizi 17, Wachumi 1, Wakutubi 2, Msaidizi wa Hesabu 1, Madereva 13, Katibu Mahsusi 5, Afisa Habari 1, Wapishi 2, Fundi 1, Wasaidizi wa Ofisi 2 na Wauguzi. Jumla ya Watumishi wasio walimu 49.

Shughuli nyingine za Ajira 2004/2005 ni waliothibitishwa kazini 120, marekebisho ya mishahara 5,500, malipo ya mirathi 40, malipo ya kustaafu 240 na waliofukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali 17 - Jumla ni 5,917.

(c) Aidha, jumla ya watumishi 157 walipata mafunzo mbalimballi ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

Mafunzo kwa Wafanyakazi 2004/2005 ni kama ifuatavyo: - Mafunzo ya Shahada ya kwanza 81, Mafunzo ya Shahada ya Pili 21, Mafunzo ya Muda Mfupi kwa fani mchanganyiko 30, Mafunzo ya Stashahada za Uzamili 15, Mafunzo ya Cheti 10. Jumla157.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo: -

(a) Kuomba kibali cha ajira mpya ya watumishi 795 wa kada mbalimbali na Walimu wa Shule za sSekondari wapatao 3,094.

(b) Kupeleka Watumishi 100 kwenye mafunzo ya muda mrefu na 50 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

(c) Kuhakikisha kuwa Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma inatekelezwa kikamilifu kwa kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma za usafi, ulinzi na mapokezi.

(d) Kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Tathmini ya Utendaji Kazi wa Watumishi kwa utaratibu mpya unaolenga kuweka malengo na matokeo katika utendaji kazi *(Performance Management System)* kwa watumishi wa Makao Makuu ya Wizara, Shule na Vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, walitoa Mafunzo ya Menejimenti na Utawala kwa Viongozi Watendaji wa Wlimu 431 wa ngazi mbalimbali.

Mafunzo ya Menejimenti - *ADEM* kwa mwaka 2004/2005 ni kama ifuatavyo: - Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi wa Idara mbalimbali za Elimu walengwa 164, Mafunzo Mafupi ya mwezi mmoja ya Wakuu wa Shule na Wakuu wa Shule Wasaidizi wa Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali walengwa 124, Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (mwezi mmoja) walengwa 40, Walimu Wakuu wa Shule za Msingi walengwa 103. Jumla ni 431. *(Makofi)*

Aidha, ADEM imewezesha Vyuo vya Ualimu 37 kuunganishwa na mtandao wa Tovuti kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, *ADEM* itatoa mafunzo mbalimbali kwa Viongozi Watendaji wa Elimu 21,294 pamoja na Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanachuo 100.

Mafunzo ya Wafanyakazi 2005/2006 ni kama ifuatavyo: - Stashahada ya Uongozi wa Elimu 100, Cheti ya Uongozi na Uendeshaji kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 2,520, Mafunzo Mafupi kwa Waratibu wa Elimu Kata 2,800, Uongozi kwa Wakaguzi wa Shule 200, Uongozi wa Shule za Sekondari 200, Mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi za Shule za Sekondari 15,574. Jumla 21,394.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Idara ya Sera na Mipango iliendelea kushirikiana na Idara nyingine katika kutekeleza majukumu ya: -

(a) Kupanga, kuratibu na kutekeleza mipango ya elimu kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na Sera ya Utamaduni.

(b) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya kazi.

(c) Kusimamia ukarabati wa majengo ya Shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(d) Kuwa kiungo kati ya Wizara yangu na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha, Wahisani na Wadau mbalimbali.

(e) Kutayarisha mipango na *program* ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya sekta ndogo ya *Basic Education* (Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu ya Watu Wazima).

(f) Kuandaa na kuratibu rasimu za maandiko mbalimbali zikiwemo Hotuba za Bajeti. Aidha, Idara imeweza kutafsiri Sera ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka 1995 kutoka Kiingereza kuwa Kiswahili.

(g) Kuandaa Tovuti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

(h) Kuandaa mwongozo wa ufuatiliaji wa shughuli za elimu.

(i) Kukiwezesha Kitengo kipya cha Mawasiliano na Habari kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Idara ya Sera na Mipango itashughulikia masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Kufanya utafiti, ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha.

(b) Kufanya mapitio na kuziba mapengo yaliyobainishwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo.

(c) Kufuatilia mwenendo wa utoaji wa huduma za Elimu na Utamaduni na kutoa ushauri wa kitaalam.

(d) Kuandaa na kuratibu rasimu na maandiko mbalimbali ya kitaalam yanayohusu miradi na mipango, sera, takwimu, hotuba ya bajeti rasimu za nyaraka za Baraza la Mawaziri na makala mbalimbali.

(e) Kuandaa mapitio ya matumizi ya fedha za umma *(Public Expenditure Review PER*) na (*Medium Term Expenditure Framework – (MTEF)* za Wizara na Sekta ya Elimu kwa jumla kwa kushirikiana na sekta ndogo nyingine za elimu.

(f) Kusimamia na kuratibu ukarabati wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Ualimu.

(g) Kutoa mafunzo kwa Jumuiya za Shule na Vyuo kuhusu matengenezo madogo madogo na dhana utunzaji wa majengo na mazingira yake.

(h) Kuratibu misaada ya wahisani.

(i) Kuimarisha Mfumo wa Menejimenti na Mawasiliano ya Kielimu (*Education Management Information System 'EMIS*).

(j) Kuendelea kuwa Sekretarieti ya uthibiti wa ubora wa vitabu vya kielimu na zana za kufundishia zinazotumika shuleni na vyuoni.

(k) Kutoa miongozo ya ujenzi kwa wadau mbalimbali wanaojenga shule.

(l)Kutoa ushauri wa kiufundi kwa ujenzi wa Shule za Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza Utawala Bora, Uwazi na Uwajibikaji, Wizara ya Elimu na Utamaduni imeanzisha Kitengo cha Mawasiliano na Habari, ambacho ni Kitovu cha Mawasiliano kati ya Wizara na Wadau mbalimbali wa Elimu nchini wakiwemo Wanahabari na Wananchi kwa jumla. Katika mwaka 2004/2005 kitengo hiki kilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kuandaa na kusambaza nyaraka mbalimbali za elimu na utamaduni kwa wadau wa elimu.

(b) Kuratibu utoaji wa habari kwa Vyombo vya Habari.

(c) Kuitangaza Wizara na program zinazotekelezwa katika Sekta ya Elimu na Utamaduni.

(d) Kusambaza kwa wadau nyaraka zinazohusu mabadiliko yanayojitokeza katika Sekta ya Elimu na Utamaduni.

(e) Kuratibu maandalizi ya mada zilizowasilishwa kwenye semina, makongamano na mikutano katika Wizara.

(f) Kuhuisha habari zinazohusu Wizara katika Tovuti ya Wizara na ya Taifa.

(g) Kushauri Idara, Vitengo, Mabaraza na Taasisi zilizo chini ya Wizara katika kuandaa nyaraka na taarifa (*press release*) mbalimbali kwa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/2006, kitengo kitaandaa Mkakati wa Mawasiliano ambao utaainisha namna ya kuwasilisha mambo yote muhimu

yanayofanywa na Wizara yangu kwa Wananchi na wadau wote, yakiwemo masuala yote muhimu ya *program* za MMEM na MMES. Malengo maalumu ya kitengo hiki ni:-

(a) Kuandaa na kusambaza nyaraka mbalimballi za elimu na utamaduni kwa wadau wa elimu.

(b) Kusambaza kwa wadau nyaraka zinazohusu mabadiliko yanayojitokeza katika Sekta ya Elimu na Utamaduni.

(c) Kuratibu utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa majarida mbali mbali katika Wizara.

(d) Kushauri Idara, Vitengo, Mabaraza na Taasisi zilizo chini ya Wizara katika kuandaa nyaraka na taarifa (*press release*) mbalimbali kwa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Elimu Kiongozi pamoja na kuratibu utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo na Sera ya Utamaduni na kutoa miongozo ya kuboresha Elimu na Utamaduni, huongoza vitengo maalumu vilivyo katika ofisi yake.

Afisa Elimu Kiongozi pia husimamia na kuimarisha uongozi katika kutoa Elimu. Aidha, Afisa Elimu Kiongozi husimamia shughuli za uhusiano wa elimu Kimataifa ikiwa ni pamoja na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika **(***SADC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kilitekeleza yafuatayo: -

- Kuendesha mafunzo ya kupanga usimamizi wa *program* za Elimu ya Watu Wazima na kuwaandaa Maafisa Elimu hao waweze kuwa wakufunzi wawezeshaji wa Elimu ya Watu Wazima.

- Kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 73 wa EWW katika Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke na wawezeshaji 15,534 wa MEMKWA – (Kundi Rika la Pili) katika Halmashauri zote nchini.

- Kununua na kusambaza seti za moduli 360,000 na nakala 1,600 za miongozo ya EWW katika Halmashauri zote nchini

- Kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa MEMKWA (Kundi Rika la Pili) mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kitatekeleza yafuatayo: -

- Kufuatilia utoaji wa mafunzo kwa wawezeshaji wa vikundi vya Elimu ya Watu Wazima na MUKEJA katika Halmashauri, madarasa ya MEMKWA (Kundi Rika la Pili) na kutathmini maendeleo ya EWW/MUKEJA.

- Kutoa miongozo ya uendeshaji wa MEMKWA na MUKEJA.

- Kupanua MUKEJA kufikia vituo 1,140 na kusimamia utekelezaji wake katika Halmashauri zote.

- Kuchapa na kusambaza moduli 2,280 za kufundishia na kujifunzia EWW katika Halmashauri zote.Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, CHEWATA ilitekeleza yafuatayo:-

- Kuendesha semina za kuhimiza uhai wa Chama cha CHEWATA kwa Waratibu Elimu Kata kwa Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni.

- Kuandaa warsha kwa ajili ya kuhamasisha Chama cha Midahalo ya Elimu ya Watu Wazima katika Wilaya za Mbeya Mjini, Mbeya Vijijini na Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, CHEWATA itaendesha semina kwa Walimu wa Elimu ya Watu Wazima ili kufufua CHEWATA katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Pwani na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Kitengo kilitekeleza yafuatayo: -

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 576 wasio wataalam wa Elimu Maalumu kuhusu Elimu Jumuishi.

- Kuchapisha na kusambaza jumla ya nakala 1,500 za vitabu vya masomo mbalimbali ya Shule za Msingi kwa wanafunzi wasioona.

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Breli na Lugha ya Alama na Stadi za Maisha ya kila siku kwa Walimu Wataalam 180.•Kuandaa visawidi vya miongozo ya kufundishia Walimu Wataalam wa wasioona, viziwi na wenye ulemavu wa akili na michoro mguso (*Brail*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Kitengo kitatekeleza yafuatayo:

- Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi wa Elimu Maalum.

- Kuchapa aina 30 za vitabu vinavyohusu mtaala katika Breli nakala 24,000 kwa ajili ya wanafunzi wasioona.

- Kuandaa kisawidi cha pili cha mwongozo wa mafunzo kwa Walimu Wataalam wa Elimu Maalum.

- Kuendesha mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa walimu wasio na fani ya Elimu Maalum, 1,000 na Viongozi wa Elimu ngazi ya Wilaya.

- Kuendesha mafunzo mafupi kwa Walimu Wataalam 300.

- Kufanya tathmini katika Wilaya 56 ili kubainisha takwimu za wanafunzi wenye ulemavu, mahitaji ya kielimu kwa wanafunzi na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Kitengo cha Usajili wa Shule kilitekeleza yafuatayo: -

- Kilisajili Shule zisizo za Serikali 166 na Shule za Sekondari za Kutwa 379.

- Kilithibitisha wenye Shule na Mameneja wa Shule 101 zisizo za Serikali.

- Kilitoa leseni za kufundisha kwa waombaji 909 waliothibitishwa kuwa na sifa zinazostahili.

- Kiliratibu masuala ya Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Kusini mwa Afrika.

- Kilishiriki katika utafiti wa ubora wa elimu katika nchi 15 za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006-Kitengo cha Usajili kimepanga yafuatayo: -

- Kusajili shule zisizo za Serikali 150 na shule za Wananchi za Sekondari za kutwa 170.

- Kuthibitisha wenye Shule na Meneja wa Shule 100 zisizo za Serikali.

- Kuendesha warsha kwa Waratibu wa Elimu wa Kata, Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Maafisa Elimu 200 wa Wilaya kuhusu taratibu za usajili wa shule.

- Kutoa leseni ya kufundisha kwa waombaji 400.

- Kuchapa nakala 400,000 za vyeti vya usajili wa walimu.

- Kusajili walimu walio kazini.

- Kuratibu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) iliandaa na kutangaza vipindi 246 kama ifuatavyo: -

- Vipindi 52 vya ufundishaji.
- Vipindi 52 vya Boresha Elimu.
- Vipindi 144 vya masomo ya *English* na Maarifa ya Jamii kwa Darasa la V, VI na VII.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Kitengo kitashirikiana na *RTD* kutangaza vipindi 320 kama ifuatavyo: -

- Vipindi 52 vya redio Boresha Elimu ili kuhamasisha jamii juu ya utekelezaji wa MMEM na MMES.

- Vipindi 52 vya redio "Ufundishaji."

- Vipindi 216 vya masomo ya *English*, Maarifa ya Jamii na Kiswahili kwa Darasa la V, VI na VII.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, sehemu ya Elimu dhidi ya UKIMWI ilitekeleza yafuatayo: -

- Kukamilisha mada za Elimu ya UKIMWI ili kuziingiza kwenye mihtasari ya masomo chukuzi katika Shule za Sekondari.

- Kuchapisha na kusambaza maandiko ya mafunzo ya elimu ya kujikinga na UKIMWI shuleni na vyuoni.

- Kutoa mafunzo kwa Walimu wa Sekondari na kutekeleza *program* ya Elimu dhidi ya UKIMWI shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006 sehemu ya Elimu ya UKIMWI itatekeleza mambo yafuatayo: -

- Kukamilisha mada za Elimu dhidi ya UKIMWI kwa ajili ya kuingizwa kwenye masomo chukuzi ya Elimu na Ualimu.

- Kuchapisha na kusambaza maandiko ya mafunzo ya Elimu dhidi ya UKIMWI shuleni na katika Vyuo vya Ualimu.

- Kuendesha mafunzo kwa Walimu wa Shule za Msingi.

- Kutayarisha vifaa vya elimu ya UKIMWI kwa ajili ya mafunzo ya elimu maalum (Wasioona na Viziwi).

- Kutoa mafunzo ya Unasihi kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004/2005, Sehemu ya Elimu ya Familia ilitekeleza yafuatayo: -

- Kutoa mafunzo kwa walimu 829 wa masomo chukuzi ya Elimu ya Familia kutoka Shule za Sekondari za Kanda ya Kati, Kaskazini na Kusini.

- Kutoa mafunzo ya ufuatiliaji wa Elimu ya Familia kwa walimu 262 wa Shule za Sekondari za Kanda ya Kati, Kaskazini na Kusini.

- Kuhariri, kuboresha na kuchapisha vitabu vya masomo chukuzi ya Elimu ya Familia.
- Kuendesha midahalo kuhusu afya ya vijana iliyowajumuisha wanafunzi 40 wa Shule za Sekondari za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/2006, katika Elimu ya Familia shuleni, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa: -

- Walimu 850 wa Kanda ya Kaskazini, Kusini na Nyanda za Juu KUsini na Wakuu wa Shule za Sekondari kutoka shule 350 za Kanda za Kaskazini, Kusini na Nyanda za Juu Kusini.

- Mafunzo ya Uelimishaji Rika kwa wanafunzi rika 120 kutoka Shule za Sekondari.

Aidha, Wizara ya Elimu na Utamaduni, ilitekeleza yafuatayo:-

- Kuhakiki, kurekebisha na kuhariri visawidi vya vitabu vya masomo chukuzi ya Elimu ya Familia kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari.

- Kuchapa aina nne za vitabu vya masomo chukuzi ya Elimu ya Familia kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari na kutoa jumla ya nakala 20,000.

- Kufuatilia utekelezaji wa Elimu ya Familia katika Shule za Sekondari.

- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Mradi wa Elimu ya Familia ili kuwawezesha wafanye kazi kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 sehemu ya Elimu ya Mazingira ilitekeleza yafuatayo: -

- Kukamilisha na kuchapa Mwongozo wa Kufundishia Elimu ya Mazingira na kuusambaza nchi nzima, katika Shule za Msingi.

- Kuandaa mipango na utoaji wa Elimu ya Mazingira kwa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.

- Kushirikiana na asasi nyingine katika kuelimisha Wakaguzi wa Shule, Maafisa Elimu Wilaya (Taaluma) na Waratibu wa Vituo vya Ualimu *(TRCs)* kuhusu umuhimu wa Elimu ya Mazingira na Utumiaji wa Mwongozo wa Ufundishaji wa Elimu ya Mazingira.
- Kufanya tathmini ya utekelezaji wa ufundishaji wa Elimu ya Mazingira.

- Kutayarisha vitini kutokana na mada ngumu za mazingira zilizoko kwenye mtaala wa Elimu ya Msingi na Sekondari ili kusaidia utumiaji wa Mwongozo wa Kufundishia na Kujifunzia Elimu ya Mazingira katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006 Sehemu ya Elimu ya Mazingira itatekeleza malengo yafuatayo: -

- Kukamilisha kutafsiri na kuhariri mwongozo wa kufundisha Elimu ya Mazingira kwa Shule za Msingi na kuchapisha nakala 90 za mwongozo huo.

- Kujenga uwezo na utumiaji wa mwongozo kuhusu Elimu ya Mazingira katika ufundishaji miongoni mwa Wakuu wa Shule za Sekondari wapya.

- Kuelimisha utumiaji wa Mwongozo wa Elimu ya Mazingira katika Shule za Msingi kwa Wakaguzi wa Shule 240 Kikanda.

- Kutayarisha Mkakati kabambe wa Elimu ya Mazingira wa Wizara.

- Kukamilisha Uhariri wa Vitini vya kufundishia Elimu ya Mazingira kulingana na Mwongozo na muhtasari.

- Kufanya tathmini na ufuatiliaji kwa kutembelea shule 20 za Kanda ya Kati na Tanga Mjini kuona hali ya ufundishaji na kujifunza Elimu ya Mazingira.

- Kushirikiana katika Mikutano, Kongamano na Warsha za *Globe*, Siku ya Mazingira Duniani na nyinginezo ili kukuza ushirikiano na wadau wa Elimu ya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)* iliendelea na ukuzaji mitaala kwa ngazi mbalimbali kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhariri Andiko la Muundo wa Taifa wa Ukuzaji Mitaala na kuliwasilisha andiko hilo Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa idhini.

(b) Kutafiti na kurekebisha mtaala wa Elimu ya Msingi na mihtasari ya masomo.

(c) Kutayarisha na kuchapisha kijarida cha *TIE Newsletter* na jarida la *Tanzania Educational Journal (TEJ).*

(d) Kuingiza maudhui ya elimu ya *VVU* na UKIMWI, Stadi za Maisha na Jinsia katika mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari.

(e) Kuendesha mkutano wa paneli ya somo la Stadi za Kazi.

(f) Kuandaa andiko na zana za tathmini ya utekelezaji wa mtaala wa MEMKWA katika Wilaya ya Makete.

(g) Kurekebisha mihtasari na vitabu vya masomo ya MEMKWA.

(h) Kufanya tathmini ya ufuatiliaji (*tracer study*) ya wahitimu na wawezeshaji wa MEMKWA katika Halmashauri za Ngara, Songea Vijijini, Masasi, Kisarawe, Makete na Musoma Vijijini.

(i) Kuingiza maudhui ya ajira mbaya kwa watoto kwenye mihtasari ya MEMKWA.

(j) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji na waratibu 326 wa MEMKWA katika Halmashauri za Ngara, Songea Vijijini, Masasi, Kisarawe, Makete na Musoma Vijijini.

(k) Kuanzisha mradi wa Elimu ya Maji (*Value Based Water Education*) kwa kushirikiana na *UNHABITAT* na kuendesha semina kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kuandika makala za kufundishia.

(l) Kuandika moduli za Elimu ya Usalama Barabarani na kuendesha semina kwa Walimu na Wakufunzi kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

(m) Kuendesha semina kwa Walimu 246 wanaofundisha masomo ya Sekondari ya *Geography, Biology* na *Mathematics* katika Mkoa wa Kagera na Kanda ya Magharibi.

(n) Kuandika mihtasari na moduli za kufundishia Elimu ya Ugonjwa wa Vikope (*Trachoma*) katika Wilaya za Dodoma na Singida.

(o) Kufanya utafiti na kurekebisha mtaala wa Elimu ya Sekondari na mihtasari ya Kidato cha 1 – 4.

(p) Kubuni na kutengeneza seti ya vifaa vya ubaoni vya kufundishia Hisabati.

(q) Kuendesha semina ya kuwahamasisha Wafanyakazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na athari zake.

(r) Kutafsiri mihtasari ya masomo 5 ya MEMKWA kutoka Kiswahili kuwa Kiingereza

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, TET itatekeleza mambo Makuu yafuatayo: -

(a) Kuchapisha na kusambaza Mfumo wa Taifa wa Ukuzaji Mitaala.

(b) Kuifanyia mapitio mihtasari sita ya Ualimu ngazi ya Cheti.

(c) Kuandika miongozo mitatu ya kufundishia kwa ajili ya Shule za Msingi.

(d) Kuandika miongozo ya kufundishia katika Shule za Awali na Elimu Maalumu.

(e) Kuifanyia mapitio mihtasari ya Sekondari ngazi ya Juu na Ualimu ngazi ya Stashahada.

(f) Kufuatilia utekelezaji wa mitaala iliyorekebishwa kwa Shule za Msingi na Sekondari.

(g) Kutayarisha moduli tatu za masomo ya Stadi za Kazi, Sayansi na Maarifa ya Jamii kwa ajili ya Darasa la V-VII.

(h) Kufaragua vivunge vitatu vya masomo ya *English*, Kiswahili na Haiba/Michezo na kuandika miongozo yake.

(i) Kuandaa vipindi vinne na kuvirekodi katika redio na televisheni kwa masomo mawili ya Shule za Msingi.

(j) Kuandika miongozo miwili ya kufaragua zana za kufundishia na kjifunzia katika Shule za Awali.

(k) Kufanya tathmini ya ufundishaji wa masomo sita ya MEMKWA katika Halmashauri sita za majaribio za Ngara, Kisarawe, Musoma Vijijini, Makete, Songea Vijijini na Masasi.

(l) Kufanya mapitio kwenye vitabu vyote vya kielimu, pamoja na Miongozo na mihtasari ya MEMKWA.

(m) Kufanya semina tatu za kitaaluma kwa wakuza mitaala kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Intaneti na Tovuti.

(n) Kufanya utafiti na tathmini ya njia za kufundishia na kujifunzia zinazotumika Shuleni.

(o) Kutoa mafunzo kwa Walimu wa Shule ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kuhusu ufundishaji wa masomo yaliyomo katika mitaala iliyorekebishwa.

(p) Kuchapisha maandiko kuhusu ugonjwa wa *VVU* na UKIMWI na madhara yake kwa ajili ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(q) Kuandaa muhtasari wa TEHAMA kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ilitekeleza mambo yafuatayo: -

(a) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima kwa Watendaji 202.

(b) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Wakufunzi na Walimu 87 ili kuinua viwango vya elimu na ujuzi kazini.

(c) Kuendesha warsha ya kupitia na kurekebisha masomo ya *Biology, Physics* na *Chemistry* yanayoendeshwa kwa njia ya Posta.

(d) Kuchapa majarida 500 ya *Studies in Adult Education*" na 500 ya *Journal of Adult Education* .

(e) Kutoa mafunzo ya sheria ngazi ya cheti kwa walengwa 188.

(f) Kukarabati Vituo vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Mikoa ya Iringa na Tabora.

(g) Kununua majengo ambayo yanatumiwa kama madarasa katika Mkoa wa Morogoro.

(h) Kuajiri Wakufunzi 12 kati ya 20 waliotarajiwa.

(i) Kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa TEWW 41 na wanafunzi 202 wa Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima.

(j) Kutoa Elimu kwa njia ya Posta/Masafa ya kujiendeleza kwa walengwa 11,378 wakiwemo vijana 7,090 walio nje ya shule

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima kwa utaratibu wa masomo ya jioni katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(b) Kutoa masomo ya Elimu Masafa kwa walengwa 15,000.

(c) Kuandika na kurekebisha masomo ya Elimu Masafa matano mapya hatua ya tatu katika mfumo wa Moduli kwa masomo ya Kiingereza, Kiswahili, Jiografia, Historia na Hisabati

(d) Kuandaa na kuchapisha majarida ya *Studies in Adult Education (SAED)* na 62, *Journal of Adult Education (JAET)* Na. 14 na Sauti ya Wanawake Na. 6.

(e) Kutoa elimu dhidi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa Taasisi Mikoani na kuendesha kampeni dhidi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa Sekta ya Elimu nchini.

(f) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Cheti cha Sheria toka 188 hadi 250.

(g) Kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 162 wa Taasisi.

(h) Kufanya ukarabati wa majengo ya Taasisi katika vituo vya Mikoa ya Mbeya, Tabora na Dar es Salaam.

(i) Kununua magari 5 kwa ajili ya kufuatilia Mikoani *Program* ya Elimu ya Masafa.

(j) Kutoa ajira ya watumishi wapya 33 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) ilitekeleza mambo yafuatayo: -

(a) Kuongeza vitabu 30,032 na majarida 20,650 katika makataba.

(b) Kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Maktaba ya Mkoa wa Dodoma.

(c) Kuanza ujenzi wa majengo ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo.

(d) Kuendesha Tamasha la Vitabu pamoja na hema za kusomea watoto katika vituo 10 vya Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Tanga, Arusha, Mara, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Morogoro na Ruvuma.

(e) Kuendesha semina na kambi za kusomea kuhusu UKIMWI katika Mikoa Iringa, Tanga Kilimanjaro, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Wananchi wote kwa ushiriki na michango yao ya hali na mali katika kuchangia utekelezaji wa mipango ya Elimu na Utamaduni. Aidha, nawapongeza viongozi wote wa ngazi mbalimbali pamoja

na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kwa kushiriki kwao katika kufanikisha utoaji na uendeshaji wa Elimu na Utamaduni:-

(a) Kuimarisha na kuboresha huduma kwa kuongeza machapisho 40,000 katika Mikoa 18.

(b) Kutoa makala 2 za *Tanzania National Bibliography (TNB)*.

(c) Kuendeleza ujenzi wa Maktaba ya Mkoa wa Dodoma.

(d) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo.

(e) Kuweka mfumo wa kisasa wa kutumia teknolojia katika kutoa huduma.

(f) Kutoa mafunzo ya ukutubi katika ngazi ya Cheti, Stashahada na mafunzo ya muda mfupi.

(g) Kuendesha semina, warsha na hema za kusomea kuhusu UKIMWI kwa watumishi na wanajumuiya.

(h) Kuendesha Tamasha la Wiki ya Vitabu katika vituo 10 na kambi za kujisomea katika vituo 4 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/05, Baraza la Mitihani *(NECTA):-*

(a) Liliendesha mitihani ya Kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi ya Darasa la VII Tanzania Bara; Elimu ya Sekondari ya Kidato cha 4 na 6; Ufundi na Ualimu. Matokeo ya mitihani hiyo imeoneshwa kwenye vielelezo vilivyoambatishwa.

(b) Liliendelea kujenga kituo cha kusahihishia mitihani cha Mbezi Wani.

(c) Liliendesha mafunzo kwa wafanyakazi 183 kwa lengo la kupunguza maambukizi ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Kisukari, Ukoma na Malaria.

(d) Lilishughulikia Rufaa 245 za wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/06, Baraza la Mitihani la Tanzania. Litaendelea kutekekeza wajibu wake wa kutunga na kuendesha mitihani yote ya Kitaifa kwa ufanisi pamoja na kuendesha na kusimamia mitihani itolewayo na Bodi 9 za Mitihani ya nje kama ifuatavyo: -

(a) Kufanya utafiti, tathmini, usanifu na kuinua ubora wa mitihani mbalimbali ya Kitaifa.

(b) Kuendesha mitihani ya Elimu ya Msingi, Maarifa (*Qualifying Test),* Kidato cha 4 na 6, kuhitimu Elimu ya Ualimu Daraja la A na Stashahada ya Ualimu.

(c) Kuendesha mitihani ya Cheti cha Ufundi Sanifu (*Full Technician Certificate (FTC);* na Stashahada ya Juu ya Uhandisi (*Advanced Diploma in Engineering* (*ADE)* kwa niaba ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)*.

(d) Kusimamia mitihani ya nje inayofanywa na watahiniwa binafsi hapa nchini.

(e) Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Kusahihishia Mitihani cha Mbezi Wani.

(f) Kuendeleza *program* ya kompyuta itakayowezesha utoaji wa matokeo ya kufaulu mtihani wa Kidato cha 4 na Uchaguzi wa wanafunzi wa kuingia Kidato cha 5 kwa pamoja ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitekeleza yafuatayo: -

(a) Kukuza ujuzi wa sanaa kwa kutoa elimu kwa wasanii 580 wa muziki kwa kuendesha mafunzo ya siku 5 kwa kila Mkoa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Tanga, Arusha na Tabora.

(b) Kuelimisha wasanii 608 kuhusu Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki katika Mikoa ya Tabora, Arusha, Tanga, Iringa na Mbeya.

(c) Kuhimiza jamii kuthamini na kuboresha sanaa kwa kuanzisha na kuimarisha matamasha, halaiki na mashindano katika Mikoa ya Rukwa, Singida na Dar es Salaam.

(d) Kuratibu utoaji wa tuzo kwa wasanii bora wa mwaka 2004 katika tuzo za *Tanzania Music Awards* na *Tanzania Gospel Music Awards*. Wasanii 18 walipata tuzo hizo.

(e) Kwa kushirikiana na OKOA *Arts Group* ya Dar es Salaam kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya siku 5 kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu ufinyanzi na ususi bora na masoko kwa wasanii 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, BASATA litatekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kutoa Elimu ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii 650.

(b) Kutoa mafunzo ya uboreshaji sanaa ya muziki, sanaa za ufundi wa mikono, ngoma, sarakasi na tamthilia kwa wasanii 540.

(c) Kutoa mafunzo ya uongozi bora kwa vikundi 30 na Vyama 5 vya Sanaa.

(d) Kuratibu utoaji wa tuzo kwa Wasanii Bora wa mwaka 2005 katika tuzo za *Tanzania Music Awards* na *Tanzania Gospel Music Awards.*

(e) Kuandaa maonyesho ya Kitaifa ya sanaa za ufundi katika Mikoa minne.

(f) Kutoa elimu ya jinsi ya kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI kwa wasanii wagharibishaji 160.

(g) Kufanya utafiti wa sarakasi ya asili yenye miondoko ya ngoma za jadi katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kukagua na kutoa ushauri wa kitaalam; kupanga katika madaraja na kutoa vibali kwa filamu na mikanda ya *video* 417.

(b) Kukagua, kutoa ushauri wa kitaalamu na kupanga katika madaraja kumbi 40 za Sanaa za Maonyesho na jumba moja la sinema "*The New World Entertainment Cinema"* katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/06, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza itatekeleza kazi zifuatazo: -

(a) Kukagua, kutoa ushauri wa kitaalamu na kupanga filamu 2,000 katika madaraja mikanda ya video 5,000 na programu mbalimbali za televisheni 1,000 kabla ya kuonyeshwa kwa hadhira ya watazamaji.

(b) Kuendesha warsha kwa waratibu 21 wa Mikoa kuhusu mbinu na ujuzi wa kisasa wa kutoa huduma kwenye Ofisi za Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza katika Mikoa na Wilaya kwa kuzingatia maadili mema ya utamaduni wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005, Baraza la Kiswahili la Taifa lilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kusimamia Maadhimisho ya Nane ya Kiswahili.

(b) Kuhamasisha matumizi ya Kiswahili katika Sekta ya Biashara.

(c) Kuendesha semina kwa Waandishi wa Habari kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili.

(d) Kuendesha warsha ya kusanifu istilahi mchanganyiko 275.

(e) Kutayarisha na kurusha hewani kupitia redio na televisheni vipindi 156 vya kuhamasisha lugha ya Kiswahili kwa Wananchi.

(f) Kupokea, kusoma na kutoa ithibati ya lugha kwa miswada 30.
(g) Kukusanya makosa 100 katika Vyombo vya Habari katika jitihada za kufuatilia kwa karibu na kusahihisha makosa ya ufasaha wa lugha.
(h) Kuchapisha jarida la "Lugha Yetu Na. 39" Kiswahili na Utandawazi na 'Tafsiri Sanifu Na. 6'.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza mambo yafuatayo: -

(a) Kusimamia maadhimisho ya Tisa ya Siku ya Kiswahili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Kiswahili, kwa kuzingatia kaulimbiu ya Kiswahili Mhimili wa Kuleta Amani.

(b) Kuchapisha jarida la Lugha yetu Na. 40.

(c) Kuandaa warsha ya lugha kwa wataalamu 10 wa BAKITA na 5 wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) ili kuwianisha matumizi ya maneno ya Kiswahili.

(d) Kuandaa warsha ya kusanifisha istilahi katika uwanja wa uhusiano wa Kimataifa.

(e) Kuandaa semina kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari ili kudhibiti matumizi yasiyokuwa fasaha.

(f) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya Lugha ya Taifa vipindi 52 vya Kumepambazuka na 52 vya 'Ulimwengu wa Kiswahili' katika televisheni.

(g) Kuchapisha kamusi ya istilahi za UKIMWI.

(h) Kusoma miswada ya vitabu vya Kiswahili vya taaluma na kuipa ithibati ya Baraza.

(i) Kuratibu na kutoa huduma ya Ukalimali katika mikutano ya Kimataifa na katika shughuli za mashirika, kampuni na watu binafsi.
(j) Kuchunguza makosa mbalimbali yanayofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili na kuyasahihisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo ya jumla yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa elimu kwa kuzingatia programu za MMEM na MMES: -

(a) Kutokusomwa na kutotafasiriwa kwa usahihi miongozo na maelekezo ya *program* hizi ambako kumesababisha baadhi ya wadau, wasimamizi na Watendaji wasiweze kutekeleza majukumu yanayotakiwa na programu hizi kwa kiwango kilichokusudiwa.

(b) Kuwepo kwa pengo kubwa la kifedha katika program ya MMES kutokana na kuwa na chanzo kimoja tu cha fedha ambacho ni mkopo nafuu wa Benki ya Dunia, wakati bado tunasubiri ahadi za wabia na wadau wetu.

(c) Kuchelewa kuzibwa pengo la fedha la MMEM kutokana na kumalizika kwa mkataba wa miaka mitatu wa kupata fedha kutoka Benki ya Dunia na wahisani wengine kuwa katika mchakato wa badiliko kutoka *Pooled Fund* kuingia *Budget Support* ambao haijakamilika.

(d) Kuwepo kwa tatizo la uelewa juu ya uendelevu wa programu ya MMEM. Baadhi ya Wadau na Watendaji wanadhani kuwa utekelezaji wa MMEM mwisho wake ni mwaka 2006 na hivyo kupunguza kasi ya kusimamia utekelezaji wa shughuli zilizoamuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mdau, msimamizi na mtekelezaji ni vema akaelewa kwamba program ya MMEM ni endelevu ili kuwawezesha wale watoto walioanza Darasa la 1 chini ya mpango huu mwaka 2002 waweze kuikamilisha mzunguko kamili wa Darasa 7 ifikapo mwaka 2008 na wale wanaoanza Darasa la 1 mwaka 2006 wakamilishe mzunguko kamili mwaka 2012.

Kipindi cha miaka mitano cha MMEM (2002 – 2006) ni kipindi cha mpango kwa lengo la kufikia Elimu ya Msingi kwa wote. Kwa hiyo ilihitajika kujenga majengo mengi ya shule kukidhi ongezeko kubwa la wanafunzi na walimu. Baada ya mpango kukamilika ongezeko la miundo mbinu ya shule litakuwa la kawaida linaloendana na ongezeko la idadi ya watu na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itatekeleza maamuzi yafuatayo: -

(a) Kuimarisha MMEM kwa kuandaa Awamu ya Pili ya MMEM 2007 – 2015 kwa madhumuni ya kuwa na mpango endelevu ili kufikia malengo ya *EFA* na *Millenium Development Goals (MDGs).*

(b) Kuimarisha utekelezaji wa *Program* ya MMES 2004 – 2009 kwa kuzijengea Shule za Sekondari uwezo mzuri wa kupokea, kutunza na kutumia fedha za Ruzuku ya Uendeshaji na Ruzuku ya Maendeleo kwenye akaunti zao za shule.

(c) Kuendelea kuimarisha mitaala ya Elimu ya Sekondari ili kukidhi haja ya mabadiliko yanayoendelea ya utandawazi, ushindani wa kiuchumi na uboreshaji wa elimu.

(d) Kuendelea kutoa ruzuku zote husika kwa stahili yake kwa Shule za Serikali na Zisizo za Serikali.

(e) Kuimarisha ufuatiliaji, tathmini na uwezeshaji wa MMEM na MMES ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Wananchi wote kwa ushiriki na michango yao ya hali na mali katika kuchangia utekelezaji wa mipango ya Elimu na Utamaduni. Aidha, nawapongeza viongozi wote wa ngazi mbalimbali pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kwa kushiriki kwao katika kufanikisha utoaji na uendeshaji wa Elimu na Utamaduni.itatekeleza maamuzi yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani za pekee kwa wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Utamaduni. Wahisani hao ni Uswidi, Uingereza, Ufaransa, Ireland, Japan, Norway, Finland, Canada, Uholanzi, Ujerumani, China, Korea ya Kusini, Ubelgiji na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU).* Aidha, Mashirika yaliyochangia Elimu na Utamaduni ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB), SIDA, NORAD, WFP, UNICEF, UNESCO, UNFPA, UNDP, ILO, EU, USAID, JOVC, VSO, CELTEL, CBP, Peace Corps, Book Aid International Aga Khan Education Foundation, Plan International, World Vision, Ireland Aid, Care International* na Mashirika mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na misaada hiyo ya kifedha, utekelezaji wa mipango ya elimu na utamaduni kwa mwaka 2004/2005 isingefanikiwa na kukamilika katika kiwango nilichoelezea bila jitihada, ushirikiano na uongozi wa pamoja katika Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku K. P. Sakila, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kwa ushirikiano, uaminifu na uadilifu wake. (amekuwa ni mjukuu wangu mzuri sana pale wizarani. *(Makofi)*

Namshukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu ya Utamaduni Dr. Naomi B. Katunzi kwa ushauri wa kitaalam na kitaaluma, pamoja na wasaidizi wake akiwemo Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wa Idara zote, Wakuu wa Taasisi za Elimu na Utamaduni katika ngazi mbalimbali, walimu na wafanyakazi wengine wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na katika maandalizi ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu pia kwa Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na Wajumbe wa Mabarza na Taasisi zote Zilizo chini ya Wizara yangu na wafanyakazi wengine wote katika ngazi mbalimbali kwa

kazi nzuri waliyoifanya ya kuimarisha na kuendeleza Elimu ya Utamaduni. Aidha, naushukuru uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa ushirikiano wao. Napenda kuwashukuru viongozi wa tawi la TUGHE la Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao unaoepusha migogoro kazini katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ndio mwaka wa mwisho wa Serikali ya Awamu ya Tatu na wa Bunge hili, nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: -

Kwanza, kwa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa kwa kuniteua na kunipa fursa ya kuitumikia nchi yangu kama Waziri wa Elimu na Utamaduni wa kipindi hiki cha mwanzoni mwa karne ya 21 yenye changamoto za dunia ya utandawazi na soko huria na kunipa jukumu la kutekeleza Taarifa ya Mfumo wa Elimu ya Tanzania katika karne ya 21 (*The Tanzania Education for the 21 century)* iliyozaa Sera ya Elimu na Matunzo ya 1995 (*The Education and Training Policy 1995)* na *ESDP.*

Pili, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushiriki wake wa kikatiba katika uteuzi wangu na kwa uongozi wake mzuri na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wenu mzuri sana. Ahsanteni sana. (*Makofi)*

Pia, namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanallah Taala* kwa kunijaalia kuwa katika timu nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tatu iliyofunga mabao mengi ya maendeleo. *(Makofi)*

Tatu, nawashukuru sana Wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kunichagua kuwa Mjumbe wao katika Bunge hili na nawaomba waendeleze kufanya hivyo katika Bunge hili na nawaomba waendeleze kufanya hivyo katika Uchaguzi Mkuu ulio mbele yetu; nami endapo watanipa tena ridhaa yao nitaendelea kuwatumika kama Mbunge wao *Luhala* na *Upifu;* Kwa busara na Ushujaa kama isemavyo *motto* ya *Hehe Council* iliyobuniwa na Hayati Mtwa Adam Sapi Mkwawa: ‘*Lidege Lingi Siliwhana amayago’. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia kwako namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake uliotulizana wa *Nyumba ya Malumbano* kama wanavyoliita Bunge kule Malawi. Kwa uongozi wake uliotulizana tumelumbana kwa utulivu sana katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa na jukumu la kusimamia na kuongoza Maendeleo ya elimu kwa miaka hii mitano ya mwisho ya Serikali ya Awamu ya Tatu natoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali ya Awamu ya nne: -

(i) Inafaa na inahitajika kuikamilisha bila kuchelewa uandaaji wa:-

(a) Mpango wa Maendeleo wa Mafunzo ya Ufundi (*Vocational Education Development Plan (VEDP)* wa kupanua mafunzo ya ufundi kwa ajili ya wanafunzi ambao hawataendelea ngazi inayofuata ya elimu ya kawaida.

(b) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu *(Higher Education Development Plan (HEDP)* ili kumudu ongezeko kubwa la wahitimu wa K6 kutokana na upanuaji wa Elimu ya Sekondari ya Juu unaoendelea. Wakati mwaka huu wanafunzi wa Sekondari ni 524,325; ifikapo mwaka 2010 wanaohitimu K4 na K 6 watakuwa zaidi ya 600,000 kwa mwaka.

(ii) Inahitajika mapema iwezekanavyo kuanza kuandaa Awamu ya Pili ya MMES kwa lengo la kufikia Elimu ya Sekondari kwa Wote (*Universal Secondary Education (USE)* ifikapo mwaka 2015.

Hatua hizo mbili zitakuwa ni kichocheo muhimu cha kusukuma gurudumu la maendeleo 'kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya.'

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza yote hayo, ninaomba sasa Bunge lako baada ya kuijadili hoja yangu pamoja na kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, lipitishe Makadirio ya Matumizi ya Shilingi 175,434,506,800 ili kuwezeshwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kutekeleza mipango ya mwaka 2005/2006. Kati ya fedha hizo: -

(a) Shilingi 66,070,411,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Elimu na Utamaduni; na

(b) Shilingi 109,364,095,800 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru wewe binafsi, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati yangu, ningependa kutumia nafasi hii, kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati yangu, nitoe pole na rambirambi kwa familia na Wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa, kwa kuondokewa na Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Margareth J. Bwana, aliyefariki dunia hivi karibuni. Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni katika maeneo yafuatayo: Taarifa ya Utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005; Taarifa ya Utekelezaji wa maagizo ya Kamati iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mwaka wa Fedha 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa nia ya kuboresha utendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2004/2005 hasa katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM, unaohusu ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na ununuzi wa samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Vilevile kwa mafanikio yaliyofikiwa katika kuandikisha wanafunzi katika Shule za Msingi hasa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambayo kwa kweli ina takwimu, vielelezo na majedwali ya kutosha kwa kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu ajira na maslahi ya walimu. Ili kuboresha hali ya walimu, Kamati inatoa mapendekezo ambayo yanalenga kufanikisha utekelezaji katika kushughulikia madai na kero mbalimbali za Walimu kama ifuatavyo: Kwa kuwa Serikali iko katika programu mbalimbali za kuboresha elimu ya msingi nchini, Kamati inashauri uandaliwe Mpango Maalum wa kuhakikisha kuwa inapata walimu walio bora kuanzia vigezo vya kuwadahili na mafunzo wanayopewa wakiwa vyuoni. Aidha, kadri mitaala mipya inavyoanzishwa, vivyo hivyo walimu wawe wanapewa mafunzo *(Refresher Courses),* ili kuwawezesha kumudu ufundishaji wa mitaala hiyo mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali vilevile iangalie kwa kina, upatikanaji wa mishahara kwa walimu waishio vijijini kwani inaonekana wanatumia muda mwingi na gharama kubwa katika kufuatilia mishahara yao Wilayani. Kamati inashauri Serikali iangalie utaratibu wa kuweza kuwapatia walimu posho ya safari *(Per Diem),* kila mwisho wa mwezi wanapokwenda Wilayani kufuatilia mishahara ili waweze kufidia gharama za kufuatilia mishahara hiyo. Vinginevyo Serikali ifanye utaratibu wa kuwafikishia mishahara yao kwa mikataba maalum kati yake na Mabenki kwa utaratibu wa *Mobile Banks.* Serikali vilevile ihakikishe kuwa, walimu wote wanaofundisha wanafunzi walio katika Mpango wa Elimu Kwa Walioikosa (MEMKWA), wanalipwa. Mpaka sasa kuna baadhi ya walimu katika Halmashauri mbalimbali walio katika mpango huu hawajalipwa, hali ambayo inakatisha tamaa na kurudisha nyuma maendeleo ya vituo vya MEMKWA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni zinazotawala fedha za Serikali zizuie kabisa uhamishaji wa fedha za elimu kwenda vifungu vingine au kutumika vinginevyo. Vilevile

maagizo yote ya Serikali ambayo utekelezaji wake unahitaji fedha, yazingatie bajeti iliyoidhinishwa au ziombwe fedha maalum kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zote zitenge fedha za kutosha katika vifungu vinavyohusu stahili za walimu na kusimamia kikamilifu matumizi yake.

Madiwani vilevile wajengewe uwezo ili waweze kuwa na stadi za kuchambua na kufuatilia fedha za matumizi ya kawaida *(Other Charges),* zinazohusu Walimu na Idara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hazina iwe inatoa maelekezo ya matumizi ya fedha za matumizi ya kawaida *(OC)* zinazopelekwa kwenye Halmashauri kulingana na vifungu vilivyopo kwenye Bajeti.

Mfumo wa usimamizi wa fedha za ruzuku zinazotolewa na Serikali Kuu kwa mamlaka za Serikali za Mitaa, uangaliwe upya ili sheria na kanuni ziruhusu pia Wakuu wa Wilaya na Mikoa kupata taarifa za fedha zinazotolewa kwa mamlaka zilizo katika maeneo yao. Kamati inaamini taarifa hizo zitawawezesha Wakuu hao kuzisaidia Halmashauri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa mara kwa mara ufanywe ili kuona fedha za ruzuku ya elimu zinatumika kama ilivyokusudiwa na kutoa taarifa haraka kwa Serikali kuhusu Halmashauri ambazo zinatumia ruzuku ya elimu kinyume na ilivyokusudiwa ili hatua sahihi zichukuliwe dhidi ya Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iziagize Halmashauri zote, kila robo mwaka zitayarishe taarifa sahihi ya mapokezi na matumizi ya fedha za elimu na kuziwasilisha kwenye vikao vya kila robo mwaka vya Kamati ya Mkoa ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, ili viongozi wa Mkoa na Wilaya waweze kufuatilia utumiaji wa fedha hizo. Serikali vilevile iweke utaratibu wa kufanya tathmini kila mwaka ili kuona madai na kero za walimu zimetatuliwa kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione umuhimu wa kurekebisha Sheria ya Elimu Na.25 ya 1978 na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002. Aidha, Kamati inaona kuwa ni vema kuzipitia Sheria za Serikali za Mitaa Na 7, 8 na 9 za 1982 ili ziwe na vifungu vinavyozitaka Halmashauri kuwajibika kwa kutoa taarifa za vipindi maalum za mapato na matumizi ya fedha za ruzuku ya elimu kwa viongozi wa Wilaya na Mikoa ili viongozi hao wajue kinachoendelea kwa madhumuni ya kuimarisha ufuatiliaji wa Halmashauri ili kuboresha utendaji. Watendaji wakuu katika Halmashauri ambao wamekuwa wakishindwa kutekeleza wajibu wao mahali walipo, wachukuliwe hatua za kisheria na sio kuwahamishia katika vituo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yote yaliyopo kwenye Mpango wa Maendeleo ya Elimu yaliyokusudiwa kuwaendeleza walimu, yatolewe kwa walimu hao badala ya kutumika kwa Warsha na Makongamano kwa watumishi wengine

Mheshimiwa Naibu Spika, Lugha ya Kiswahili imekuwa ni mhimili mkubwa katika kuleta umoja miongoni mwa Watanzania. Ni lugha pekee ya asili katika Bara la Afrika, ambayo sasa imekubaliwa kutumika katika Mikutano ya Umoja wa Afrika *(AU)*. Hivyo, ni vema Serikali ikawa na Mipango thabiti ya kuikuza na kuieneza lugha hii ndani na nje ya nchi. Aidha, tunashauri utaratibu wa sasa wa baadhi ya mada za makongamano, warsha na semina, kuandikwa kwa Kiingereza na hatimaye kutolewa kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza, ni vema uachwe na kuwe na utaratibu wa kutumia lugha moja tu ya Kiswahili au Kiingereza. Aidha, Serikali ijenge na kuboresha Ofisi za Makao Makuu ya Baraza la Kiswahili Tanzania ili ziendane na hadhi ya lugha hii Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa mafanikio yaliyopatikana katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu, kuongezeka kwa ajira ya walimu, kuongeza ushiriki wa Wananchi katika kufanya maamuzi kuhusu maendeleo ya shule zao kupitia kamati za shule na kuhakikisha kuwa kila shule ina akaunti yake ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana katika mpango huo, bado kuna upungufu kama ifuatavyo:-

- Idadi ya watoto wenye ulemavu wanaoandikishwa shule kutoridhisha. Kamati inashauri kuwa malengo na njia madhubuti zichukuliwe kuhakikisha kwamba, watoto wote wenye ulemavu wanaandikishwa shule ili kila Mtanzania anufaike na Mpango huu. Pia Serikali iwe na takwimu sahihi kati ya watoto wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaomaliza darasa la saba ikiwa ni pamoja na kufuatilia mahudhurio yao darasani kuliko kuhimiza uandikishaji peke yake;

- Idadi ya walimu wanaopangwa katika wilaya bado ni tatizo. Walimu wenye sifa zinazostahili wanapatikana zaidi mijini na pembezoni mwa miji. Uwiano kati ya walimu wa kike na wa kiume waliopo vijijini bado ni mdogo;

- Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iunde kitengo cha kufuatilia matumizi ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya Mpango wa MMEM. Aidha, kuwe na udhibiti wa ubora wa majengo yanayojengwa chini ya mpango huu ili yaweze kudumu kama inavyotakiwa;

- Ujenzi wa madarasa uende sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu na kuboresha vitendea kazi ili kuboresha elimu. Aidha, miundombinu katika shule ijengwe kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi na walimu walemavu ikiwemo upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo vinakidhi mahitaji ya walemavu wa aina zote na kuwafanya wafurahie mazingira ya shule zao.

- Kwa kuwa Mradi wa MMEM unatarajia kukamilika mwaka 2006, Serikali iwaandae Wananchi ili waweze kuuendeleza hususan katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya shule. Hata hivyo, tunashauri Serikali ianze kujadiliana na wafadhili ili kuona

uwezekano wa kuwa na awamu ya pili ya kuimarisha Elimu ya Msingi, ambao utalenga zaidi kwenye ujenzi wa nyumba za walimu na kuendeleza walimu; na

- Kiasi cha Dola 10 za Kimarekani ambazo zilipangwa kutolewa kwa kila mwanafunzi katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM, hazifiki zote kwa walengwa kama ilivyokusudiwa kwa kuwa zinatumiwa kwa shughuli nyingine zinapofika ngazi ya Halmashauri za Wilaya. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za kinidhamu kwa Wilaya zinazotumia fedha hizi kinyume na ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa sasa wa utawala wa Shule za Sekondari unahitaji urekebishwe ili kusogeza madaraka kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya, kwa sababu kwa hali ilivyo sasa, walimu na wakuu wa Shule za Sekondari, wanapata matatizo kutokana na utawala wa shule hizo kuwa moja kwa moja chini ya Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaohudumiwa na ruzuku ya MMES kutoka familia zenye kipato duni kufikia 24,000. Kamati inashauri kuwa, kwa vile tatizo la watoto yatima ni kubwa na linazidi kuongezeka, idadi ya watoto wanaohudumiwa na ruzuku hii iongezwe au Serikali ibuni mikakati mipya ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano (2004 - 2009), Bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa Elimu ya Sekondari inatazamiwa pengine kufikia shilingi trilioni 1.3. Kamati inashauri kuwa ni vema Wananchi wakaeleweshwa vizuri vyanzo vya fedha hizo, kama ni msaada au mkopo na wajibu wao ni nini. Pia Serikali ihakikishe kuwa kuna mtiririko mzuri katika upatikanaji wa fedha hizo na Wananchi wafahamu matumizi ya fedha hizo kupitia Bodi za Shule, Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya.

Serikali bado inaendelea kudaiwa madeni na wazabuni wanaotoa huduma za chakula katika Shule za Sekondari, hivyo ni vema fedha hizo zilipwe ili wazabuni hao waendelee kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mitihani kufika kwa mtahiniwa, ambaye ndiye mlengwa, kwa muda na siku iliyopangwa na Baraza la Mitihani la Taifa, inakuwa imepitia katika michakato mbalimbali ikiwemo utungaji, uchapaji, usafirishaji , uhifadhi na usambazaji wa mitihani hiyo katika vituo vya mitihani. Katika hatua zote hizi wadau mbalimbali wanahusika katika kutunza usiri wa mitihani hii. Ni vema kila mdau atimize wajibu wake. Katika matukio ya kupatikana kwa baadhi ya mitihani kabla ya wakati mnamo mwaka 2004 kulikotokana na kuibiwa kwa mitihani hiyo wakati ikiwa imehifadhiwa kama ilivyotokea kwenye Shule ya Ngateu Mkoani Arusha. Inaonesha kuwa Serikali haikutimiza wajibu wake sawa sawa kwani suala la ulinzi wa mitihani ni jukumu la polisi na siyo la Baraza la Mitihani. Kamati inashauri wadau wote wawe waangalifu ili kuhakikisha kuwa mitihani haivuji, haiibiwi, wala kuporwa na kuingia katika mikono ya wasiohusika kabla ya wakati uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, Taasisi ya Elimu Tanzania, ishirikiane na Taasisi inayoshughulika na ukuzaji mitaala ya Zanzibar ili kuwa na

viwango sawa vya elimu katika Jamhuri ya Muungano. Aidha, vipengele vya kisheria na Kikatiba vinavyozuia ushirikiano huu, viangaliwe upya ili kuondoa tofauti za kielimu ndani ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taasisi ya Elimu Tanzania ndiyo inayojishughulisha na ukuzaji mitaala kwa ajili ya Shule za Misingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ni vema Taasisi hiyo ikapewa uwezo na uamuzi wa mwisho wa jukumu la kutathmini na kuhakiki ubora wa vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia kwa kina na kwa makini, mpango mzima wa kubadilisha mitaala ya Shule za Sekondari nchini, Kamati ya Huduma za Jamii inakubaliana na mabadiliko hayo na kubaini kuwa chimbuko la marekebisho ni utekelezaji wa maamuzi na malengo ya Kitaifa yaliyomo katika maandiko muhimu yafuatayo, ambayo nina uhakika na Mheshimiwa Waziri naye ameyasema:-

Kwanza, Taarifa iitwayo, *The Tanzania Education System for the 21st Century,* iliyoandaliwa na Tume Maalum ya Wataalam, iliyoteuliwa na Serikali mwaka 1990. Taarifa hiyo ilipelekwa Serikalini na kupitishwa Novemba, 1992. Mapendekezo ya taarifa hiyo ndiyo yaliyotumiwa kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 *(The Tanzania Education and Training Policy of 1995),* yakiwemo mapendekezo ya kupunguza masomo ya Sekondari, kuunganisha masomo ya michepuo ya ufundi, kilimo, biashara, sayansikimu na masomo ya kawaida, kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari ya Kawaida.

Pili, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 iliyopitishwa na Baraza la Mawaziri, Februari mwaka 1995 na Bunge la Tanzania likaarifiwa na kuijadili hapo Aprili, 1995, inafafanua kuwa Taasisi ya Elimu Tanzania ndiyo yenye wajibu wa kurekebisha mitaala na pia inadhihirisha haja ya kupunguza masomo ya Elimu ya Sekondari na kuunganisha masomo ya michepuo ya ufundi, kilimo, biashara, sayansikimu na masomo ya kawaida ili kuimarisha ufundishaji wa hisabati, lugha na masomo ya sayansi.

Tatu, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu *(Education Sector Development Programme - ESDP),* iliyopitishwa na Serikali mwaka 1996, baada ya mchakato uliohusisha sekta nzima ya elimu na wadau wote wa elimu pamoja na wabia wote wa maendeleo ya kielimu.

Nne, Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia 2025 *(Tanzania Development Vision 2025),* iliyotolewa na Serikali mwaka 1999 na inayolenga ifikapo mwaka wa 2025 Tanzania iwe nchi iliyosheheni wasomi wanaoweza kuhimili ushindani wa kikanda na Kimataifa na wanaoweza kumudu changamoto za Soko Huria *(liberalization)* na dunia ya utandawazi *(globalization).*

Tano, chimbuko linatokana na Mpango wa Hatua za Kupunguza Umaskini *(Poverty Reduction Plan of Action 2000 - 2010).*

Sita, Mkakati wa Kupunguza Umaskini *( Poverty Reduction Strategy - PRS)* iliyopitishwa na Baraza la Mawaziri kabla ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mawazo kuwa, shule ni mahali ambapo wanafunzi wanapewa taaluma katika masomo ya msingi *(academics)* na chuo ni mahali ambapo wanachuo wanapewa utaalam *(profession),* kwa fani/mchepuo fulani ili wawe wataalam kama vile walimu, mafundi, maafisa kilimo, maafisa biashara na kadhalika. Kwa hiyo, kufundisha masomo ya fani na michepuo katika shule ni kutoa taaluma na utaalam kwa wakati mmoja, jambo ambalo kutokana na utafiti, limeonekana linawachanganya wanafunzi. Taaluma ni msingi wa kupatia utaalamu, kwa hiyo ni lazima kwanza mwanafunzi apewe taaluma ya kutosha akiwa shuleni kabla ya kuanza kumfundisha chuoni utaalam anaoupenda yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inakubaliana na mapendekezo ya wataalam, washauri na matokeo ya utafiti, ambayo yalibainisha kuwa mtaala wa sasa ulikuwa na udhaifu ufuatao:-

- Masomo yalikuwa mengi mno yakiwemo ya mchepuo ambayo yalichukua nafasi kubwa ya ratiba kwa gharama ya muda wa masomo mengine;

- Masomo ya lazima yalikuwa mengi mno, masomo 13 hasa Vidato vya Kwanza na Pili na yalikuwa yakiwaelemea wanafunzi;

- Msisitizo ulilenga mno maarifa bila kujali stadi muhimu za kufikiri, za maisha, ujuzi, vitendo na ubunifu;

- Michepuo ya kujaribu kujenga utaalamu iliingizwa mapema mno na kwa uzito mkubwa kabla misingi ya kutosha ya kitaaluma na maarifa haijaimarika kwa mwanafunzi. Misingi hiyo hupatikana katika masomo ya Hisabati, Lugha za Kufundishia, Masomo ya Sayansi na Maarifa ya Jamii yakiwa yamebebeshwa Elimu ya Kujitegemea;

- Michepuo huhitaji fedha nyingi na muda mrefu kuiendesha kikamilifu;

- Waliosoma michepuo baada ya kuhitimu wamekutwa hawako kwenye ajira zinazoendana na michepuo hiyo kama vile Kilimo, Ufundi, Uhasibu na Biashara. Hata Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, hakiwapi unafuu wowote waliosoma mchepuo wa kilimo kwa miaka sita, Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita;

- Mtaala wa sasa ulifaa wakati chini ya asilimia 20 ya wanafunzi waliohitimu Elimu ya Sekondari ndio walioendelea na Elimu ya Juu. Tunapoboresha Piramidi la Elimu kwa ngazi ya Elimu ya Juu kufikia asilimia 50 ya wahitimu kwa Kidato cha Sita ifikapo mwaka 2009, inalazimu mtaala urekebishwe ili uwafae walengwa wenye muachano mpana zaidi wa uwezo wakiwemo watakaoishia ngazi husika ya elimu na watakaosonga kwenda ngazi ya juu yake;

- Mtaala wa sasa hauzingatii vya kutosha masuala mtambuko *(Cross - cutting Issues);* na

- Mtaala wa sasa haukidhi mahitaji ya soko hasa katika vidato vya tano na sita na hautoshi kumudu changamoto za soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kuwa, hakuna kinachodumu isipokuwa mabadiliko. Hata hivyo, Serikali haikufanya matayarisho ya kutosha kukidhi haja ya mabadiliko. Hivyo, tunashauri sasa Serikali itumie muda huu wa mpito, kutoa ufafanuzi wa kutosha kwa Wananchi na wadau wote wa elimu. Vilevile Serikali iimarishe Vyuo vya Kilimo, Biashara na Ufundi, ili kupokea wanafunzi watakaomaliza Kidato cha Nne na Sita ambao watakuwa wamepata taaluma ya msingi na kwamba watakuwa tayari kupokea utaalamu. Pia tunashauri kuwa, walimu waliokuwa wanafundisha masomo ya mchepuo, waendelee kufundisha masomo mengine kwa sababu ni wahitimu wa Stashahada za Ualimu na Shahada ya Elimu

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nichukue fursa hii, nimpongeze Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph J. Mungai na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Bujiku K. Sakila, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa Mwaka uliopita, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006. Aidha, nawapongeza wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dr. Naomi Katunzi, kwa ushirikiano walioutoa Kamati ilipokuwa inajadili Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa umakini na ushirikiano wao wakati wa kujadili Taarifa ya Utelekezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha uliopita na kufikiria Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2005 /2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni Fungu 46 kwa kuwataja majina. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Halimenshi K. Mayonga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba na mimi, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda nichukue fursa hii, nikishukuru Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), kwa ushirikiano wao mkubwa

walioutoa wakati wa kufuatilia madai na maslahi ya walimu Tanzania katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii. *(Makofi)*

Nampongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Theonist K. Ruhilabake, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika. Mwisho, naomba nichukue fursa hii, nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri katika kipindi chote cha miaka mitano na tunawatakia afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM (k.n.y. MHE. KHAMIS ALI SALEH - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda nichukue nafasi hii, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1), Toleo la 2004.

Napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba wapigakura wa Jimbo langu la Mtambile, niwape pole Wananchi wa Jimbo la Kilombero, kwa kumpoteza mwakilishi wao, Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kwa kumpoteza Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Baada ya salamu hizi za rambirambi, napenda nichukue nafasi hii, niipongeze Kamati ya Uongozi ya Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote cha uhai wa Kambi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii, nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi *(CUF)* Taifa, kwa kuteuliwa na chama kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa Chama, anayegombea nafasi ya Urais, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pia Mheshimiwa Juma Duni Haji, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika nchini Oktoba, 2005. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na vyama vyao kugombea nafasi ya Urais kwenye Uchaguzi mkuu huo: Kwanza kabisa, Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema na Mheshimiwa Rukia Kiota wa Chama cha *TLP,* Mheshimiwa John M. Cheyo wa Chama cha *UDP,* Mheshimiwa Edmund S. Mvungi, Naila Jidawi wa *NCCR-Mageuzi,* Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM) na wengine ambao wameshapitia mchakato huo. Kwa wale ambao bado, niwatakie kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na timu nzima ya wataalam wake, kwa kazi ya kuiandaa Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ingelipenda kuelekeza maoni yake katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukua kwa uchumi wa kisasa wenye uwezo wa kuboresha maisha ya Wananchi, kunategemea wafanyakazi wenye ujuzi na maarifa. Kwa hakika utafiti unaonesha kuwa, kukua kwa uchumi wa Taifa lolote, kunashabihiana kwa karibu na kiwango cha kuwekeza katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Dunia inashuhudia mapinduzi ya teknolojia ya mawasiliano ya habari *(Communication and Information Technology),* ambayo yanaleta mageuzi makubwa ya uchumi na biashara ya Kimataifa. Ni dhahiri hatutaweza kushindana kiuchumi na kibiashara katika ulimwengu tulionao leo, iwapo hatutachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa, watu wetu wengi kadri inavyowezekana, wanapata fursa ya kujifunza taaluma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba elimu yetu kwa ujumla imeendelea kukumbwa na matatizo mengi, lakini hali ni afadhali kidogo hivi sasa kuliko ilivyokuwa mwaka 2000. Mwaka 2000 kulikuwa na wastani wa watoto 8,070,000 waliokuwa wanapaswa kuwa katika shule za msingi, lakini kati ya hao ilikuwa ni watoto 4,370,500 tu ndio waliokuwa wanasoma katika shule zilizokuwepo na waliobaki 3,699,500 walikuwa hawasomi kwa sababu mbalimbali. Aidha, inakadiriwa kuwa mwaka 2000 kulikuwa na watoto yatima 800,000 kutokana na wazazi wao kufariki kwa ugonjwa wa Ukimwi na hivyo kuzidisha uwezekano wa ongezeko la watoto ambao wangekosa shule ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, Kambi ya Upinzani, ililivalia njuga tatizo hili na kuifanya Serikali ije juu na kudai kuwa, vyama shindani vilikuwa vinasema uongo. Hata hivyo, pamoja na kuja juu, baada ya chama hicho kurudi madarakani, kilizikubali hoja za vyama shindani, ikiwemo ya kufuta ada na michango yote mashuleni na kuanzisha operesheni kubwa ya kupunguza idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule ambao walikuwa mitaani. Hivi sasa watoto wenye umri wa kwenda shule lakini hawako mashuleni imepungua kutoka watoto 3,699,500 iliyokuwepo mwaka 2000 hadi kufikia watoto 986,937. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya kiasi yaliyokwisha patikana, sehemu kubwa ya watoto ambao wako mashuleni wanasoma katika mazingira magumu. Mazingira haya ni pamoja na msongamano kwenye madarasa, uchakavu mkubwa wa majengo, njaa na uhaba mkubwa wa walimu na vifaa vya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matatizo haya na mengine, uwezo wa darasani wa wanafunzi umeendelea kuwa wa chini. Ili kufanya marekebisho yanayohitajika kumfanya kila mtoto anayepaswa kuwa shule ya msingi asome tena, ni vema asome kwenye mazingira bora, hivyo wastani wa madarasa mapya 28,198 yanahitajika. Hali kadhalika walimu wapya 41,122 inabidi waajiriwe na wastani wa madawati mapya 328,979 yatengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Tanzania ilianza kuingia matatani mnamo mwaka 1974, ilipoamuliwa kwamba, kufikia mwaka 1977 kila mtoto mwenye umri kati ya miaka saba hadi 13, awe ameanza shule ya msingi. Mfumo huu wa elimu uliitwa *Universal Primary Education (UPE).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni mfumo ulionesha mafanikio makubwa hasa kwa wingi wa idadi ya watoto wa kuanza shule ya msingi. Katika ya mwaka 1974 hadi 1978, idadi ya watoto wa kuanza darasa la kwanza iliongezeka kwa kiasi cha asilimia 71.76, kutoka watoto 248,000 hadi watoto 878,321. Idadi ya watoto waliokuwa katika shule ya msingi ilipanda kutoka watoto 1,228,886 mwaka 1974 na kufikia kilele cha watoto 3,553,144 kwa mwaka 1983. Wakati huo Tanzania ilifikia asilimia 98 ya kuandikisha watoto wa kuanza darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana waliomaliza darasa la saba walichukuliwa haraka katika vyuo vya ualimu. Walipewa mafunzo ya haraka na kurudi kufundisha. Walimu hawa wa *UPE* walichangia kiasi kikubwa kwa kujituma kukuza elimu lakini kutokana na kiwango chao kidogo cha elimu, walimu hao walifanikisha kiasi kidogo na pia walipelekea kuzorota kwa elimu katika Taifa letu. Sasa baada ya zaidi ya miaka 20 tangu mfumo huo ulipoanzishwa, walimu watatu kati ya kumi ndio waliofuata mafunzo halisi ya ualimu. Walimu wa *UPE* ni zaidi ya asilima 47 ya walimu wote wa Tanzania. Ingawa sasa hivi wanajiendeleza lakini hawafanikiwi kushinda mitihani kwa kiwango kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kosa la kuwaandaa walimu aina ya *UPE,* limefanyika tena. Vyuo vya ualimu hivi sasa vimejaa vijana ambao wengine wamegushi vyeti, matokeo yake ni kuzalisha walimu wengi wasio na uwezo wa kufundisha. Elimu yetu itaendelea kushuka. Watoto wanamaliza darasa la saba bila kujua kitu. Wengine hawawezi kuandika hata majina yao. Ni ndoto kwamba, hali ilivyo sasa hivi, mtoto aweze kujiajiri baada ya kumaliza darasa la saba na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya wanafunzi hao kupelekwa vyuoni, bado muda wanaokaa vyuoni ni mdogo mno kwa wao kuweza kuielewa vizuri taaluma hiyo ya ualimu. Hali halisi ilivyo ni kuwa umri wa vijana wanaoingia katika taaluma hiyo ni kati ya miaka 20 - 22, kumbuka kuwa wakiwa na *poor performance academically.* Hivyo, walimu hao ambao ni dhaifu, hapo hapo Serikali haina pesa za kuwapeleka kwenye mafunzo ya mara kwa mara wawapo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kigezo nilichokitaja hapo juu, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, kwa kipindi cha miaka 20 hadi 30 ijayo, Serikali na Taifa kwa ujumla, itaendelea kuzalisha wanafunzi walio dhaifu kuweza kushindana na wenzao toka Mataifa jirani au kuonesha kuwa kweli wana ujuzi na maarifa. Tumelazimika kusema

haya kutokana na *trend* inayofanywa na Serikali kuwa, wale wanafunzi ambao matokeo yao katika mitihani hayakuwa yanaridhisha, basi wanapelekwa kozi ya ualimu. Hivyo, Serikali haina budi kuchukua hatua muafaka, kwa wakati muafaka, ambapo kutokana na kutojali kwa muda mrefu hivi sasa, Taifa limejikuta likihitaji kufanya marekebisho makubwa katika elimu ya msingi ili kurejesha hali ya kawaida katika ngazi hiyo ya elimu.

Gharama za kuleta marekebisho haya pekee, achilia mbali gharama za kuendesha elimu ya msingi kwa ujumla, zinakisiwa kufikia shilingi bilioni 60 kwa mwaka, kama kuna nia ya kukamilisha marekebisho hayo katika kipindi cha miaka mitano. Pia bado kiwango cha ubora elimu ya msingi inayotolewa nchini ni cha chini mno, kwa wastani kila mwaka, katika kila wanafunzi 100 wanaofanya mtihani wa darasa la saba, 70 hawapati alama za kufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ualimu ni ya kitaalam. Mbali ya mwalimu kufundisha darasa zima katika ujumla wake, anatakiwa pia kumfuatilia kwa karibu mwanafunzi mmoja mmoja ili aweze kutoa msaada wa ziada kwa wale wenye kasi ndogo ya kujifunza. Vilevile maslahi duni kwa walimu yamesababisha walimu wengi walazimike kujikita zaidi katika kuhangaika kujikimu kuliko kuzingatia kanuni za ufundishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya Wananchi Oktoba 30, 2005, *inshallah* itafanya yafuatayo: Kwanza, Serikali itatumia kiasi cha asilimia 25 ya bajeti yake kila mwaka, kuboresha sekta ya elimu kwa ujumla. Asilimia 50 ya bajeti yote ya elimu itaelekezwa kwenye kupanua na kuboresha elimu ya msingi. Hali hii itasaidia kukamilisha marekebisho yanayotakiwa katika ngazi hii ya elimu katika muda wa miaka mitano. *(Makofi)*

Hatua nyingine muhimu ambazo zitachukuliwa na Serikali ili kupanua na kuboresha Elimu ya Msingi ni pamoja na kuhamasisha ujenzi wa shule zisizomilikiwa na Serikali, ambapo Serikali itafanya juhudi kubwa kuwahamasisha watu binafsi, mashirika ya dini na mengine yasiyokuwa ya Serikali na makampuni ya biashara, kujenga shule zaidi za msingi. Pia ili Wananchi walio wengi, waweze kumudu gharama za kusomesha watoto wao kwenye shule hizi, Serikali haitatoza kodi yoyote. Aidha, Serikali itavifanyia marekebisho makubwa viwango vya kodi zote zinatozwa kwenye vifaa vya elimu ili sekta ya elimu kwa ujumla, inufaike na punguzo la gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mitaala, Serikali itafanya marekebisho ya mitaala kwa kuzingatia zaidi umuhimu wa maudhui, muda wa kila somo, uwezo wa wanafunzi na faida ya somo lenyewe ambapo mitaala italenga kukuza lugha ya Kiingereza na hivyo kuwaongezea wanafunzi uwezo wa kumudu vizuri masomo ya sekondari na kufuta dhana kwamba, kiingereza ni lugha katika shule maalum *(International Schools).* Lugha ya Kiingereza ni muhimu katika kuchota hazina ya elimu iliyomo katika mtandao wa *internet,* ambapo asilimia 90 ya tovuti zote zinatumia lugha ya kiingereza. Pia shule zisizomilikiwa na Serikali zitakuwa na uhuru wa kufundisha masomo ya ziada kama itakavyokubaliwa na bodi za shule zinazohusika. Vilevile

itakuwa ni marufuku kwa wanafunzi wa shule za msingi kutumiwa kwa ajili ya maandamano ya aina yoyote, zaidi ya yale yanayohusu siku ya mtoto duniani. Hii ina maana kwamba, watoto wa shule za msingi, hawatahusishwa na vitu kama mbio za mwenge, mapokezi ya wanasiasa au kutumika katika shughuli za kuwachezea ngoma na kuwatumbuiza wanasiasa hao. Itakuwa ni marufuku kwa wanafunzi kujihusisha na aina yoyote ile ya biashara kwenye maeneo ya shule. Pia mashindano baina ya shule na shule kwa michezo mbalimbali yataendelezwa na kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti unaonesha kuwa watoto wenye njaa hawafundishiki na huu ndio msimamo na mtazamo wa Serikali mbadala siku zote. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Kamati za Shule, itahakikisha kwamba, watoto wote wa shule za msingi wanapata walau mlo mmoja kamili wa chakula kikuu kinachopatikana katika eneo husika, wakati wanapokuwa shuleni. Pia shule zitakuwa vituo vya kuboresha afya ya watoto. Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, kama vile *UNICEF,* itaweka utaratibu wa kuwagawia watoto virutubisho muhimu kama vile vitamin A, inayoongeza kinga ya mwili na kuboresha uwezo wa macho, dawa za kuua minyoo, elimu ya afya bora na kinga dhidi ya maambukizo ya maradhi hatari ya Ukimwi, Malaria na Kifua Kikuu. *(Makofi)*

Ada na michango ni eneo ambalo limekuwa likilalamikiwa sana na wazazi. Michango ambayo haitabiriki imekuwa ni mingi na inavyoonekana siyo yote ambayo inachangishwa kwa nia njema. Serikali itahakikisha kuwa, huduma zote zinazotakiwa katika elimu ya msingi, zitakuwa ni jukumu la Serikali na kwa hiyo basi, zitakuwa zinatolewa bure. Pia katika huduma za ukaguzi ambapo hivi sasa zimedorora kwa kiasi fulani, zitahuishwa na kuimarishwa. Kila shule ni lazima ikaguliwe angalau mara moja kwa muhula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya chekechea kwa kiasi kikubwa imeachiwa taasisi binafsi na watu binafsi kuiendesha. Serikali kwa upande wake, imejaribu kuandaa mitaala kwa ajili ya ngazi hiyo ya elimu. Aidha, Serikali imejaribu kuweka sera kuwa watoto ambao hawajapitia shule za chekechea wasiandikishwe katika shule za msingi, ingawa utekelezaji wa sera hii ni wa kinadharia, ukizingatiwa kuwa Serikali yenyewe haijawekeza chochote kuhakikisha kuwa shule za chekechea zinasambaa katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa ya Wananchi hapo Oktoba 30, 2005 itahakikisha yafuatayo yanafanyika: Serikali haitajihusisha moja kwa moja na utoaji wa elimu hii. Hata hivyo, Serikali itawahamasisha Wananchi, ikiwa ni pamoja na watu binafsi, taasisi za kidini na mashirika yasiyo ya Kiserikali, kuwekeza kwenye nyanja hii chini ya utaratibu ufuatao: Serikali itashughulika na kuweka viwango vinavyotakiwa na usajili; itawasaidia Wananchi wenye nia ya kuanzisha shule za chekechea kwa kuwapatia viwanja vinavyotosheleza mahitaji kwa ajili ya kuzingatia viwango wakati wa ujenzi na kwa kuwa hivi sasa hakuna utaratibu wa kuwaandaa walimu wa chekechea kwenye vyuo vyetu, Serikali itauanzisha ili watakaowekeza kwenye shule za chekechea, wasiwe na shida ya kupata walimu wenye sifa. Vilevile shule za chekechea hazitatozwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani si sahihi kwa wahitimu wa Kidato cha Sita, tena wale wenye *weak perfomance,* kwenda mafunzo ya wiki nne na kuhitimu kuwa walimu wa Sekondari. Hili linathibitishwa na jinsi wazazi wanavyoacha kuwapeleka watoto wao katika Shule za Serikali na badala yake kuwapeleka kwenye shule za binafsi, nadhani Mheshimiwa Waziri, anayo mifano mingi kuliko ambavyo tungetoa sisi. Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa Serikali inapima ubora wa elimu ya Msingi na Sekondari kwa kigezo cha wanafunzi kufaulu na kufeli. Hili ni kosa linaloendelea hadi elimu ya juu, kwani Wahadhiri na Wakuu wa Vitivo kwenye vyuo vya elimu ya juu, wamekuwa wanalaumiwa kwa wanachuo kushindwa mitihani chuoni, hii inatokana na mpango huu wa uajili wa walimu wanaofundisha shule za sekondari na sio kosa la wahadhiri ila ni uwezo wa wanafunzi wanojiunga katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linatokana na kuwa wanafunzi hao walifaulu kwa *standardization* ya Baraza la Mitihani. Kambi ya Upinzani inasema, ubora wa elimu unapimwa na *skills and knowledge acquired* na siyo *performance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaipongeza Serikali kwa kutoa mara kwa mara, takwimu za idadi ya wanafunzi ambao wameingizwa shuleni darasa la kwanza, lakini cha kuuliza ni kwamba, je, wale wote wanaoandikishwa wanafanikiwa kumaliza elimu ya msingi, ni wangapi wanakwamia darasa la nne na ni wangapi hawafiki hadi darasa la saba? Hivyo basi, ni kwa nini takwimu hizo Serikali haiziweki wazi ili Wananchi wenyewe wapime na watafute njia mbadala ya kupunguza tatizo hilo kulingana na takwimu hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongozi mwa nchi zilizo nyuma katika nchi nyingi ulimwenguni kwa maendeleo ya elimu ya sekondari. Katika kila vijana 100 wenye umri wa kuwa shule za sekondari ni sita tu ndio wanaosoma sekondari, ukilinganisha na wastani wa 27 katika nchi za Kiafrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Taifa letu kuwa nyuma mno katika elimu ya sekondari linaanzia katikati ya miaka ya sitini, pale Serikali ilipotangaza kuwa elimu ya sekondari sio muhimu na kusisitiza elimu ya msingi, kwa kuwa nchi yetu ni ya wakulima waishio vijijini ambapo elimu haikuonekana tena kuwa ni haki kwa kila mwenye uwezo wa kujiendeleza hadi mwisho wa upeo wake; dhana ya kuelewa na kupata ujuzi kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari ilipotea na sehemu yake ikapandikizwa dhana ya kuchaguliwa; watu na taasisi binafsi, hata waliokuwa na uwezo, walikatazwa kuwekeza kwenye elimu ya sekondari na Serikali haikujenga shule nyingi mpya za sekondari, ukiondoa mbili, tatu, za mchepuo wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tuingiapo madarakani, tunategemea kufanya yafuatayo katika kuinua na kuboresha elimu hii: Kama ilivyo kwa elimu ya msingi, elimu ya sekondari nayo inahitaji kupanuliwa na kuboreshwa. Ongezeko la bajeti ya elimu kwa ujumla litatupa uwezo wa kufanya marekebisho yanayohitajika. Serikali inakusudia kutumia asilimia 25 ya bajeti ya elimu, kuimarisha na kuboresha elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusudio hili, Serikali itachukua hatua zifuatazo ili kuyafikia malengo haya:-

- Kupanua nafasi za elimu ya sekondari. Serikali itahakikisha kuwa ada na michango yote katika ngazi ya sekondari vinafutwa na nafasi za kutosha zinapatikana ili kila kijana aliyepata alama za kufaulu katika mtihani wa darasa la saba, aweze kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari, bila kikwazo chochote; *(Makofi)*

- Kuhamasisha ujenzi wa shule zisizomilikiwa na Serikali ambapo Serikali itafanya juhudi kubwa, kuwahamasisha watu binafsi, mashirika ya dini na mengine yasiyokuwa ya Kiserikali na makampuni ya biashara, kujenga shule zaidi za sekondari. Aidha, Serikali itatoa kila aina ya msaada unaohitajika ili kufanikisha lengo hili, ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo visivyo na sababu katika usajili wa shule hizi. Ili Wananchi walio wengi, waweze kumudu gharama za kuwasomeshea watoto wao kwenye shule hizi, Serikali haitatoza kodi yeyote; na *(Makofi)*

- Serikali itafanya marekebisho kwenye mitaala inayotumiwa na shule za sekondari ili pamoja na mambo mengine, kuingiza elimu zaidi ya vitendo kuliko nadharia; kuingiza somo la kompyuta na matumizi ya mtandao wa *internet,* kwa utaratibu ambao umeshaelezwa vizuri, Serikali itakapokuwa madarakani miezi michache inayofuata; somo la uraia litaboreshwa ili kuwajenga vijana katika utamaduni wa kuthamini haki za binadamu na kwa hiyo, kuwa mstari wa mbele katika kutetea haki hizo na kuendeleza michezo na mazoezi ya viungo

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya baadhi ya watoto wetu nchini ni walemavu na wanahitaji elimu maalum ili nao waweze kujiendeleza. Kwa kawaida watoto hawa wana gharama kubwa zaidi katika kuwahudumia kutokana na mahitaji yao kuwa chini ya uangalizi maalum. Kasoro zilizojitokeza ni kukosekana kwa Sera ya Elimu, inayojumuisha mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu, kumesababisha idadi kubwa ya vijana wenye ulemavu kukosa fursa ya kupata elimu na huduma zilizoko katika taasisi mbalimbali za elimu kuanzia ngazi ya msingi, sekondari na vyuo, hazijazingatia mahitaji maalum ya walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, ikipata ridhaa hapo Oktoba 30, 2005, kwa kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwaendeleza watoto hawa na kuwapunguzia wazazi mzigo wa ziada katika kuwahudumia, Serikali itachukua hatua zifuatazo:-

- Itazindua Sera Mpya ya Elimu, ambayo itakuwa imeyajumuisha kwa ukamilifu mahitaji maalum ya wanafunzi wenye ulemavu;

- Itafanya marekebisho mbalimbali ya kiufundi kwenye taasisi mbalimbali za elimu ili kuondoa vikwazo dhidi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma katika taasisi hizo; na

- Mahitaji maalum ya kielimu kwa watoto wenye ulemavu yatajumuishwa katika mitaala ya vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa inakisiwa kuwa, kuna Watanzania wenye umri wa miaka 18 na kuendelea wapatao milioni 5.5 ambao hawajui kusoma na kuandika. Idadi hii ni kubwa mno katika nguvu kazi ya watu wasiozidi milioni 16. Kasoro zilizojitokeza ni:-

- Kuupuza kwa muda mrefu, umuhimu wa kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule wameandikishwa shule, kumechangia sana katika kuongeza idadi ya vijana wanaoingia katika utu uzima ilihali hawajui kusoma na kuandika;

- Kuanguka kwa ubora wa taaluma inayotolewa katika shule za msingi, kumesababisha kundi kubwa la watoto kumaliza darasa la saba wakiwa na uwezo mdogo sana wa kusoma na kuandika. Wengi wa hawa hupoteza ujuzi huu baada ya miaka michache huko mitaani kwa sababu ya kutoweka kwa kiasi kikubwa, kwa utamaduni wa kujisomea miongoni mwa Wananchi;

- Hivi sasa maktaba mbalimbali za Serikali zinatoza ada kwa wanaotaka huduma ya kujisomea. Hali hii inazidi kufifiisha hamu ya Wananchi kujifunza na kujiendeleza kielimu; na

- Mkazo uliokuwepo katika miaka ya 70 kuhusu elimu ya watu wazima, uliachiwa taratibu kufifia hadi hatimaye ukatoweka kabisa. Kwa hivi sasa fedha za bajeti ya elimu ya watu wazima zinatolewa lakini haziwanufaishi walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani iingiapo madarakani, Serikali inatarajia kufanya yafuatayo ili kurekebisha kasoro zilizopo ili kuleta mafanikio:-

- Serikali itahuisha upya madarasa ya elimu ya watu wazima, ambapo itaandaa utaratibu utakaowezesha kila shule ya msingi iliyoko nchini, kuendesha madarasa ya elimu ya watu wazima kila siku jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Kwa hali hii, fedha za bajeti ya elimu ya watu wazima, zitatumika ipasavyo na hivyo kuwanufaisha walengwa;

- Serikali itafuta ada zote zinazotozwa na Maktaba za Serikali hivi sasa na kuhakikisha kuwa huduma katika maktaba hizi zinaboreshwa kwa kiwango cha juu ili kukidhi haja ya Wananchi kujiendeleza kielimu; na *(Makofi)*

- Serikali Itaanzisha mpango wa muda mrefu wa kuziunganisha maktaba na mtandao wa *internet* ili Wananchi waweze kunufaika na huduma hiyo kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwalimu ni mtu ambaye anapaswa kupewa heshima kubwa katika jamii. Hali za walimu wetu zinazidi kuwa mbaya siku hadi siku na malalamiko yao yote yamekuwa yakipuuzwa, kukabiliwa na vitisho na kusimangwa kwa kisingizio kuwa, ualimu ni kazi ya wito hivyo, hawapaswi kulalamika. Kasoro zilizopo ni kushuka kwa ubora wa taaluma katika taasisi zetu za elimu pamoja na mambo mengine

kunachangiwa pia na maslahi madogo ya walimu. Walimu wamepoteza ari ya kufundisha kikamilifu na muda mwingi wanalazimika kujiingiza katika shughuli nyingine za kutafuta maslahi binafsi katika kujikimu. Pia, maslahi ya walimu yamekuwa ni fimbo ya kuwachapia walimu wafanye kile ambacho Serikali inakitaka. Hivyo basi, kutokana na maslahi madogo fani hii inashindwa kuhamasisha *intellectuals* kuweza kuingia katika fani hii kama ilivyo kwenye uhasibu. Vilevile, malimbikizo ya madai ya walimu mara nyingi yamekuwa yakilipwa si kwa wakati walimu wanapoyahitaji, ila pale ambapo Serikali inahitaji msaada wa walimu hao katika kufanikisha malengo yake fulani fulani, mathalan, wakati wa kuandikisha wapiga kura, sensa, chaguzi, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ualimu ni fani inayotaka utulivu, tofauti na fani nyingine ambazo muda wa usiku ni kupumzika, hivyo basi, nyumba za kuishi kwa walimu ni muhimu sana. Kutokana na takwimu zinaonesha kuwa, kuna upungufu wa nyumba 129,302, kati ya nyumba 161,396 zinazohitajika Tanzania nzima. Upungufu wa walimu katika mashule usipoangaliwa unaweza kuwa jambo la kudumu. Utafiti uliofanywa mwanzoni mwa miaka ya 90 ulionesha kuwa, kila mwezi wastani wa walimu 25 walikuwa wakiacha kazi kutokana na kutoridhishwa na mazingira ya kazi.
Vilevile kigezo kinachotumika katika kuonesha idadi ya walimu kwa shule cha mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 siyo cha kufundishia bali ni cha kiutawala. Vigezo vya kujuana wakati wa kupandisha watumishi vyeo, vimetawala. Pia uboreshaji wa elimu ni kwenye *physical resource instead of human resource,* kitu ambacho ni makosa, kisa, wafadhili hakuna, bajeti ni ndogo. Hivyo, kutokana na shule zilizopo, kuna upungufu wa vyoo 180,021 kati ya 280,791 vinavyohitajika Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tuingiapo madarakani, Serikali inategemea kufanya yafuatayo: Itahakikisha kuwa inaboresha maslahi hayo ili angalau yawe na uwiano mzuri na yale ya wafanyakazi wa sekta hiyo katika nchi jirani; pamoja na kuchukua hatua nyingine kulifanikisha hili, Serikali itapunguza kwa kiasi kikubwa, idadi ya watendaji wa sekta hiyo walioko maofisini kwa kuwatafutia ajira nyingine na fedha zitakazookolewa kutokana na zoezi hili, zitaelekezwa kuboresha zaidi maslahi ya walimu, wakufunzi na watafiti na kuondoa mtindo na utaratibu wa *PTR,* unaotumika kupanga walimu kwenye mashule na badala yake utaratibu utakaowekwa, utategemea idadi ya vipindi kila mwalimu anavyoweza kufundisha kwa siku *(Work Load per Teacher). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika, kwani toka hapo nyuma Shule za Seminari zilikuwepo, lakini ubora wa wahitimu wake haukutofautiana na wanafunzi waliohitimu katika Shule za Serikali na si hilo hata matokeo shule kama Mazengo, Azania, Tambaza, Ndanda, Ihungo, Usagara, Bwiru, *Kilimanjaro Boys,* Jangwani, Zanaki na kadhalika. Zilikuwa ni shule zilizoongoza lakini kwa sasa tatizo ni walimu wazuri, wenye taaluma nzuri ya ualimu, wamechukuliwa na shule binafsi, kwa kuwa wanathaminiwa na maslahi yanawaridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza wale wasemaji wakuu, sasa kwenye orodha hii ninao wachangiaji 16, ambao kwa vyovyote hatuwezi kumaliza. Lakini jambo ambalo nimesimama kujaribu kulieleza ni kwamba, kama tutajipa muda wa kutosha kwenye Kamati, basi wachangiaji watakuwa wachache. Kama tunaweza kuongeza kwenye Kamati ili tusichukue muda mrefu, basi tunaweza kuongeza wachangiaji. Lakini hilo tukubaliane kwamba, wakati wa Kamati itabidi vifungu vingine tuvipitishe kwa *guillotine.* Kwa hiyo, mimi nitaendesha ninavyoona ni muafaka kwa wote. *(Makofi)*

Sasa na wale ambao hawajachangia kabisa, ambao kwa orodha hii ninao watatu, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Agnes Mkanga na Mheshimiwa Nimrod Mkono. Kwa hiyo, tutaanza na hao halafu wengine nitakuwa nawataja kadri tunavyokwenda.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa, kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kabla sijaendelea, naomba nitumie nafasi hii, nitoe salamu zangu rambirambi kwa wenzetu waliotutangulia, kwanza ni Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na kwa Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, aliyekuwa anawakilisha Mkoa wa Rukwa, Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo za rambirambi, sasa naomba niendelee na pongezi. Kwanza kabisa, naomba naomba nitoe pongezi kwa wawakilishi wetu wa Chama cha Mapinduzi, waliochaguliwa na Chama katika uchaguzi wa mwezi Aprili, kule Chimwaga nikianza na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye anachukua bendera ya CCM katika kuwania nafasi ya Urais. Pili, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye aliteuliwa kuwa Mgombea Mwenza na tatu, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ambaye anachukua bendera kuwania nafasi ya Urais wa Zanzibar. Nilikwisha waandikia barua za kuwapongeza, lakini kupitia Bunge lako Tukufu, ninapenda niwatakie afya njema. Vilevile naomba niwapongeze bila kuwasahau, Wana-CCM wale wengine 10 ambao nao walijitokeza kuchukua fomu kutaka kuwania nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi, nao pia wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu, Dr. Katunzi, Afisa Elimu Kiongozi na Wataalam wengine wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya. Kwa kweli kwa kumwezesha Mheshimiwa Waziri, kuja hapa na hotuba nzuri kabisa, yenye ufasaha mkubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa kweli bila unafiki, umeiongoza Wizara ya Elimu na Utamaduni vizuri sana. Mimi mwalimu kwa kusomea na nimekuwa nikifuatilia sana maendeleo ya elimu hapa nchini. Kwa kweli napenda kuthibitisha wazi kabisa kwamba, umekuwa kinara mzuri kuliko hata sisi wenyewe walimu, umefanya kazi nzuri sana na hivyo naona wapiga kura wa Mufindi Kaskazini wananisikia, wanajua kazi

watakayofanya tarehe 30 Octoba, 2005 itakapofika. Nafikiri unastahili kura zote. Nakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Ninawapongeza vilevile Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kutoa hotuba zao za bajeti, zenye mielekeo mzuri ili kuweza kupunguza umaskini hapa nchini. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo, sasa naomba nitumie nafasi fupi, nichangie machache ili kuboresha au kutoa ushauri katika maendeleo ya elimu hapa nchini. Moja kwa moja nianze na Mpango wa MMEM na Mpango wa MMES, kwa kweli imeleta mafanikio makubwa sana ya elimu hapa nchini. Hakuna ambaye ana shaka. Ukiangalia Mpango wa MMES sasa hivi, utaona kuwa idadi kubwa ya wanaojiunga na Kidato cha Tano, imeweza kuongezeka na hivyo malalamiko yale tuliyokuwa tunayasikia huko nyuma kwamba, watoto wanafika darasa la saba hawaendi sekondari, sasa yamepungua kabisa na tunaona na kushuhudia kabisa kwamba, sasa watoto wetu ambao walikuwa wanasomeshwa katika shule za msingi, wanapata elimu ya sekondari.

Tungependa kuboresha elimu ya sekondari kwa kiwango kikubwa sana lakini kila mmoja anajua kabisa kwamba, hali yetu ya nchi kama nchi inayoendelea bado ni maskini. Tuna mambo mengi sana ambayo tungeweza kuyafanya, lakini tunakwamishwa na mambo ya Bajeti. Labda nigusie hili suala la upungufu wa walimu, kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana, kiasi ambacho hizi shule nzuri, ambazo Waheshimiwa Wabunge hapa wamehamasisha sana kwa bidii kubwa, hakuna Mbunge ambaye amenyamaza bila kuhamasisha ujenzi wa shule za sekondari. Hivi leo katika kila Wilaya au kila Jimbo, kila Mbunge atakapokwenda kujieleza atasema jinsi alivyojitahidi kuboresha elimu ya sekondari na kuhamasisha ujenzi wa sekondari, lakini Walimu bado ni tatizo.

Hivi sasa viongozi wa elimu wanachofanya ni kujaribu kuchukua Waratibu wa Elimu wa Kata ambao wamesoma vizuri na kuwaweka huko kufundisha kwa muda au wale ambao wanamaliza *form six* na wanasubiri kwenda labda Chuo Kikuu na Taasisi nyingine za juu, wanachukuliwa kufundisha kwa muda. Wengine ni wale ambao wanamaliza *SUA,* kwa mfano, wanangoja ajira, wengine wanatafuta ajira watachukuliwa watapelekwa huko kufundisha. Sasa hapo bado tutakuwa tumeleta mashaka ya hii *quality education,* tunayoizungumzia ambayo ni kweli ipo. Tume-*improve* kabisa katika quality, lakini kama hatutaamua kwa makusudi kabisa kuweza kufundisha walimu wa kutosha, kupata walimu tarajali wengi, kwa kweli tutarudisha nyuma ari hiyo ambayo Wananchi wameiweka. Sasa ni vizuri upanuzi huu uende sambamba na mafunzo ya ualimu.

Nashukuru kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, amefanya baadhi ya shule kuwa vyuo vikuu vishiriki vya chuo kikuu, ambavyo ni Mtwara Chuo cha Ufundi, Mkwawa Sekondari, pamoja na Chuo cha Ualimu Chang'ombe - Dar es Salaam. Lakini hivi kwa kweli havitoshi na ningeomba kwa bidii kabisa, kamshauri Mheshimiwa Waziri, aweze kuongeza baadhi ya vyuo vifuatavyo, kwa mfano, Chuo cha Ualimu cha Tukuyu kule Mkoa wa Mbeya ni chuo cha siku nyingi, kina walimu wazoefu, kwa hiyo, kingeweza kuingia katika mpango huo. Lakini vile vile

angeweza kushirikiana na kuzungumza na madhehebu ya KKKT, wanacho chuo kizuri cha Ualimu cha Uyole pale Mbeya, nacho pia kingeweza kufikiriwa kuingizwa katika mpango huu wa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki na pale Kilimanjaro kuna chuo fulani kinaitwa Marangu, ni Chuo cha siku nyingi na kustahili kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri maeneo haya yatatakiwa kuangaliwa vizuri. Wakati nikiendelea kuzungumzia upungufu wa walimu katika shule za sekondari, hivi karibuni nilikuwa natembelea Mkoa wa Mbeya, ambapo ndiko nawawakilisha wanawake, niliweza kufika katika shujle moja inaitwa Lufiriyo katika Wilaya ya Rungwe. Ni shule nzuri ambayo mimi mwenyewe nilikuwa mmoja wa washiriki walioijenga ile shule, inapendeza na tumeweza kuchangia katika nguvu ya Serikali kujenga madarasa mazuri na nyumba za walimu. Tumejenga maabara na maktaba, kwa njia ya kujitegemea na wafadhili wengine.

Kwa hiyo, naomba shule ile ipewe *Headmaster,* mpaka sasa haina, kwa hiyo, naomba sana hili liangaliwe kwa hali ya juu kabisa. Katika shule hiyo vilevile tungeomba suala la kuipatia vifaa vya maabara na nataka kuthibitishe kabisa tena kwamba, mimi nilikuwa mmoja kati ya wajenzi wa maabara hiyo. Ni maabara nzuri kabisa, ambayo ilijengwa kwa nguvu za Wananchi, kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali na wahisani, lakini mpaka sasa haina vifaa. Kwa hiyo, naomba tusizivunje hizi nguvu za Wananchi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, uiangalie shule ile kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kurudia, nafurahi tena kusikia Wizara au Serikali yenyewe itasimamia suala zima la ujenzi wa maabara. Ni kweli hii ni hatua ambayo Waheshimiwa Wabunge ni lazima tupige makofi kwa nguvu zetu zote. Ujenzi wa maabara siyo kazi ndogo, si sawa na ujenzi wa darasa, si sawa hata kidogo. Mimi nashangaa wakati mwingine ninapopita katika mashule mbalimbali yanayojengwa, utaambiwa hii ni maabara, wakati ni darasa tu, ile si maabara, maabara ina *standard* zake za kujenga. Ni jengo ambalo linahitaji fedha nyingi, sasa leo tunaposikia Wizara yenyewe itasimamia, ni jambo la kupongezwa kabisa. Kwa kweli tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Sasa kuna maabara nyingine kama hizo nilizozitaja, zinahitaji vifaa. Kuna maabara nyingine ambayo mimi mwenyewe niliisimamia katika shule ya *Tukuyu Day,* ni maabara nzuri kabisa, imara kabisa, imejengwa kwa *standard* nzuri, tunaomba ipatiwe vifaa. Kuna maabara kule Tarakea imejengwa na Wananchi wenyewe kule mpakani na Kenya, nzuri kabisa na ni imara, tena ya kupendeza. Ninaomba na yenyewe ifikiriwe kupewa vifaa katika mpango huu tutakaouzungumzia hivi sasa.

Jambo lingine ni nyumba za walimu, kwa kweli ni kigezo ambacho naomba Wizara msisitize sana. Kazi hii nzuri tuliyoifanya au tunayoendelea kuifanya Waheshimiwa Wabunge ya kuhamasisha kujenga sekondari, wazazi wamejielekeza zaidi kwenye madarasa tu, wanasahau kabisa hapo lazima aje *Headmaster* na kusimamia ile shule na kusimamia maendeleo ya shule hiyo mpaka ikamilike. Kwa hiyo, ninaomba sharti hili la kusisitiza kwamba, walau nyumba ya *Headmaster* na nyingine mbili au tatu

zijengwe pale shuleni. Hiyo ni lazima kwa sababu ni kweli walimu wanafika pale hakuna nyumba. Watakachosema wazazi, ooh, tumempangia kwa jirani. Kule Kilimanjaro kwa mfano, watasema hapana hawa wamejenga nyumba nzuri wanakuja tu wakati wa *Xmas,* kwa hiyo, tumewaambia watoe hiyo nyumba wampe *Headmaster,* hiyo siyo sahihi. Mwalimu anahitaji kukaa mahali ambapo ana uhakika atakaa kwa muda wa kudumu. Naamini hiyo siyo kengele yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninarudia kuunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuanza kwa kutoa rambi rambi kwa vifo vya wenzetu waliotutangulia mbele ya haki, hasa hawa wawili wa mwishoni, Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na mpendwa wa jina wangu, Marehemu Mheshimiwa Margareth J. Bwana. Kiasi kwamba, naamini Mheshimiwa Naibu Spika, leo hukutaka kutumia neno Margareth, lakini ni jina langu hilo, ukaona uweke Agness kwamba, labda nitasahau. Kwa kweli kiliniuma kwa sababu ilikuwa ghafla na Ijumaa yake tulizungumza mazuri tu kama wajina, lakini hatuna jinsi kwa sababu Mungu aliamua na yeye anajua kwa nini aliamua hivyo, iliyobaki ni kuwaombea tu Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, ambao baada ya mchakato wa kutafuta nani atakayeweza kutufaa kushika bendera, tuliwapata Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwamba, ndiye atakayekuwa Rais, atachukua bendera lakini atakuwa Rais tu. Siyo kwamba mshika bendera hapana, ndiyo Rais mwenyewe huyo huyo. Hiyo iko wazi, mgombea mwenza, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, naye lazima tu ataendelea na bila kumsahau Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Ninaloomba tu Wana-CCM na Wananchi, tuwe makini Oktoba 30, 2005, katika kujua pumba, mchele na chuya ni kitu gani ili tusije tukajiingiza kwenye matatizo ambayo hayana msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara, chini ya uaskari wa mwavuli wa Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu, Dr. Naomi Katunzi, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi na Watendaji wote kwamba, kwa kweli kwa miaka mitano wamefanya kazi nzuri, wameitekeleza Ilani ya Uchaguzi, pamoja na Wananchi, wao wakitoa miongozo na Wananchi wakiwasikiliza na kuweza kuyafanya hayo yote ambayo wameyafanya.

Ni ukweli usiofichika, elimu imekuwa na progress kubwa, kwa kweli matatizo hayawezi kwisha kwa sababu kwisha kwa matatizo ni kufa kwa dunia na dunia kamwe haitaweza kufa. Kwa hiyo, mengi wameyafanya mazuri na matokeo yake mengi tunayaona, lakini bado naaamini matatizo yataendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nina machache au mengi ya kuyazungumzia, si lengo langu kukosoa, lakini kuendelea kushauri. Huu ni mwaka wangu wa tano kuwepo ndani ya Bunge hili, kwa bendera ya wanawake, kuwawakilisha watu wenye ulemavu nchini, wakubwa, wadogo, wanafunzi, wazee na wa aina zote tu za ulemavu. Lakini kwa upande wa elimu, bado ninaondoka nikiwa na masikitiko kidogo kama siyo mengi, pamoja na MMEM na MMES, pamoja na *highness,* vyote vitakavyokuja huko mbele kwa sababu kuna programu hapa tumeelezwa, bado watu wenye ulemavu wamefaidika kidogo. Niungane na yaliyosemwa na Kamati ya Huduma za Jamii, kweli uandikishaji ni mdogo, kama wapo ni wachache sana. Kweli miundombinu ni hafifu ama hakuna kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka miaka miwili ya nyuma, Serikali iliahidi kwamba, kwa upande wa miundombinu, watajitahidi kutoa ramani na miongozo ili madarasa yanayojengwa, vyoo na kadhalika, yawe katika *standard* inayostahili. Lakini la kusikitisha, nimetembea tembea hata mwaka huu kwenye maeneo ya shule, miongozo hiyo inaelekea kwamba, haijafika katika ngazi husika ili kweli wahusika waweze kutekeleza masuala haya, sasa hapo sijui wa kulaumiwa ni nani. Lakini kwa kweli haijafika kwa sababu wanashangaa, ingekuwa imefika hawakutekeleza, hilo lingekuwa ni tatizo lingine. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara isichoke, ihakikishe kwamba, miongozo inayoitoa inafika sehemu husika kusudi watoto wenye ulemavu tangu ngazi ya awali, msingi na kunakoendelea, ambako wao wana dhamana nako, mambo haya yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu wengi hawajasoma, hasa watoto. Tumefurahishwa sana na mpango wa MEMKWA kwamba, itaokoa hao wengi waliokosa kwenda kusoma. Lakini napo kwa upande huu wa MEMKWA, maandalizi ya kuwa-*accommodate* hawa hayako kabisa, achilia mbali kwamba, hata walio na nafasi ya kusoma MEMKWA walimu hawapo. Matatizo mengi yapo lakini kwa watoto wenye ulemavu, sikushuhudia kuwaona katika mikoa 14 niliyoitembelea na mashule pia hawapo. Sasa hapo napo pana mambo ambayo yanapaswa kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kingine cha watoto wenye ulemavu kuweza kumudu au kutomudu shule au masomo ni ukosefu wa vifaa, huo umeelezwa. Lakini nchi yetu nafahamu kuna mtambo kwa mfano, kwa kutumia vifaa, vitabu au *cassettes* zilizokuwa *recorded* za mafundisho kwa upande wa watoto wenye ulemavu wasioona.

Kulikuwa na mtambo pale Shule ya Uhuru Mchanganyiko, ambao uliwekwa na wafadhili sijui wa Ujerumani miaka ya nyuma, ulikuwa unasaidia sana kutengeneza *tape recorders* ambazo zilikuwa zinatumika mashuleni, kuhariri vitabu kwa kutumia *braille* na vitu kama hivyo. Lakini mitambo ile kwa sasa hivi imekufa kabisa, kama siyo kuacha kufanya kazi. Wataalam wapo, tatizo ni kwamba, vitendea kazi na vile vitu ambavyo vinahitajika ili suala hili liweze kutekeleza havipo. Kwa hiyo, hapo naiomba Wizara ifufue mtambo angalau baadhi ya vifaa vya *braille papers* na yale ambayo yalikuwa yanaweza kufanyika na mtambo huu, basi viweze kufanyika. Walikuwa hata wanahariri vitabu vya shule za sekondari kwa kutumia wataalam wale tulionao.

Kwa hiyo, wale wataalam wasikae bure pale. Kinachotakiwa ni kufufua tu ili angalau tuweze kupunguza hata gharama ya kuagiza nje vifaa hivi. Pamoja na kwamba, Serikali nayo sasa hivi inaachia vitu vingine vitendeke na watu binafsi, lakini kuna vitu vya msingi kama hivi kwa sababu kama wengine walivyozungumzia, elimu ya watu wenye ulemavu ni ghali. Kwa hiyo, Serikali ikubali wakati mwingine kubeba jukumu badala ya kila kitu kuwaachia watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango mzuri kabisa wa kuboresha elimu kwa watu wenye ulemavu kwa dhana ya elimu ya mjumuisho *(Inclusive Education),* lakini nina wasiwasi endapo maandalizi ya mpango huu hayatakuwa kamili, ninachelea kusema kwamba, huenda hapa hakuna ambacho watoto wenye ulemavu wataambulia. Sidhani kama wataweza kuambulia kama maandalizi hayatafanyika kikamilifu. Kama mpango wa MMEM ambao huu mjumuisho naona ni ndani humo humo, kama kule awali bado kuna matatizo mengi, sembuse kwenye mjumuisho. Kwa sababu kwenye mjumuisho mimi ninafikiria kwamba, sijui hawa watoto watawekwa kwenye darasa moja na wasio na ulemavu.

Kwa mfano, tuchukulie watoto viziwi wawekwe darasa moja na wengine wote wanaosikia. Sijui walimu mle ndani ya darasa watakuwa wawili, yule wa viziwi ambaye atamsaidia kwenye lugha ya alama, sijui atakuwa mwalimu yule yule mmoja. Hapo kwa kweli nina wasiwasi, kwa sababu sasa itakuwaje, ili huyu kiziwi aweze kupata hicho kinachozungumzwa kwa umakini zaidi.

Kwa hiyo, ninaomba hapa kama kweli dhana hii itatekelezeka, pamoja na kwamba ni dhana iliyoshauriwa kutoka Umoja wa Mataifa na sisi Taifa tumelibeba hivyo. Kwa kweli tusilifanyie pupa, tufanye maandalizi ya kutosha kabisa na kujizatiti la sivyo kama nilivyosema, nina wasiwasi hapa badala ya kujumuisha ndiyo itakuwa inawatenga kabisa.

Ninashauri pamoja na wazo hili, bado tuwe na msisitizo wa kuwa na shule maalum, tena za *boarding,* ambapo watoto hawa watakaa bwenini waweze kupata elimu kiutoshelevu, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Lakini Serikali kwa bahati mbaya, haya mambo yote yameachiwa sasa taasisi za dini ambazo sasa zinalalamika. Ruzuku inayotolewa ni kwa wale walimu waliopo pale, lakini uendeshaji zinaachiwa taasisi hizi. Shule za *boarding* kwa watoto wenye ulemavu hasa viziwi na wasioona ni muhimu sana kuliko kuwachanganya, hawataambulia chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mchepuo, nashukuru sana kwa jitihada za kuboresha elimu, lakini nalo hili kidogo labda ningependa baadaye nieleweshwe, kwa watoto wasioona, hesabu kama somo nadhani walikuwa hawachukui kutokana na *complications* zilizopo humo na kwa sasa hivi masomo yatakuwa saba. Sasa kama hesabu kweli walikuwa hawachukui na sasa masomo ya biashara na kilimo hawatachukua, yametolewa, je, hii haitawaathiri watakapomaliza Kidato cha Nne na masomo labda matatu hayamo, watapewa gredi gani hawa ya kufaulu? Hilo ninaomba tu nisaidiwe kuelimishwa, si kwamba nina matatizo hata ya kuweza kupinga hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wenye ulemavu wana matatizo mengi tu kama wafanyakazi, nashauri wawe karibu na shule, wapatiwe nyumba karibu na maeneo ya shule wanazofundisha. Licha ya nyumba wapewe *hardship allowance.* Wengine siku ya Jumamosi wanapokwenda kulima waka-*substitute* mshahara wao, kupanda maharage hawa hawawezi. Walimu wengine wanahitaji watu wa kuwasaidia kusoma makala, kwa mfano, wale wasioona, asome makala, aitafsiri, ndipo aandaye kipindi. Yule msomaji sasa watu wanadai hakuna hata chochote cha kumsaidia, mishahara tunaifahamu, sawa inaendelea kuboreshwa, lakini kwa hawa ningeomba kabisa pawe na upendeleo maalum, wapewe *hardship allowance* kwa sababu wana matumizi ya ziada ambayo ni ya lazima itakayowawezesha kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, hilo ningependa kulikazia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa lugha, bado naomba kusisitiza kuwa lugha ya alama ni muhimu, ifundishwe mashuleni. Niliwahi kutoa ushauri hapa kwamba, walimu tarajali wafundishwe elimu maalum katika vyuo vyote vya ualimu ili wanapokwenda mashuleni wasibabaike, waweze kumudu kufundisha na kuwasaidia watoto wenye ulemavu watakaowakuta. Hii inaendana na hiyo elimu mjumuisho. Itarahisisha kuliko ukisema wachache wameenda, wote wawe na *basics.*

Wale ambao wana nia sasa ndiyo waende ku-*specialize* zaidi. Hiyo itasaidia kwa sababu kama nilivyosema, elimu ya watu wenye ulemavu ni ngumu na ina kazi sana kuitekeleza kwake. Kuna mawazo kwamba, katika vyuo vyetu, tutaanzisha sasa elimu ya kompyuta na mtandao wa mawasiliano; je, Wizara imeandaa vipi kuwaelimisha walimu tarajali ambao watakuwa hawaoni kwenye haya masomo ya kompyuta? Hilo naomba pia nisaidiwe. Kwa kweli baada ya ufafanuzi au baada ya haya niliyoyazungumzia, sina mengi. Naishukuru Wizara lakini waendelee kwa kweli kuyafanya haya kikamilifu. Kile Kitengo cha Elimu Maalum, kifanye kazi ya kuendelea kushauri vizuri na kukagua kama haya mambo tunayoshauriana kweli yanatekelezwa?

Naomba nimjibu mpinzani hapa aliyesema kwamba, kwa bahati mbaya watoto wengi ni walemavu. Ulemavu siyo bahati mbaya, ni mipango ya dunia kwamba, lazima pawe na pande mbili za binadamu, siyo bahati mbaya hata kidogo. Ndiyo maana walemavu wapo na wataendelea kuwepo, kwa sababu ndiyo hali ya *balance* ya maisha. Kwa kutumia dhana kama hizo kwamba, ni bahati mbaya, ndiyo maana watu wenye ulemavu wanachukuliwa kwamba ni watu dhalili, wanachukuliwa tu kwamba ni watu wa kusaidiwa saidiwa tu, huruma huruma, hapana. Wanapaswa kuwa na haki za kimsingi kama binadamu wengine wowote wale. Kwa hiyo, ulemavu siyo bahati mbaya. *(Makofi)*

Mimi sikupata bahati mbaya kuwa nilivyo, unafurahia tu na kuna maana kwa nini umekuwa hivi. Ili ulimwengu ujue, ili ulimwengu uhangaike kutushughulikia kama hivi sasa ninavyosema Wizara hamjafanya, muifanye kazi, inaleta changamoto ya maisha ndani ya binadamu. Kwa hiyo, hilo nilikuwa ninaomba kabisa lituondoke na sisi tuwe walimu wa kuelimisha wengine. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, mimi ninapenda kushukuru kwa ushirikiano nilioupata kwa Wizara, haya ni ya kukumbushana na Mungu akijalia, tutaendelea kuja kukumbushana kama akitusaidia kupita tena. Ahsante sana, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii ya muhimu sana kuhusu elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami ninaungana na wenzangu walionitangulia, kutoa rambirambi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wawili waliotutoka kwa kipindi hiki; Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Rukwa. Naomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao pema Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa kazi nzuri sana aliyoifanya na kuleta bajeti hii ya Wizara yake. Naiunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa upande wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakayoyasema ni nyongeza tu, lakini la msingi sina tatizo na hii bajeti, kuna mapungufu yaliyojitokeza ukiangalia bajeti hii. Kwanza, ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa na Serikali kushughulikia suala la elimu. Serikali inapata fedha ama Bunge linapitisha bajeti hapa kuipa Wizara itumie kiasi fulani cha fedha, *whether* kwa kutokana na makusanyo ya kodi. Sasa nimeangalia, nimemwuliza Mheshimiwa Waziri, hii *GDP* tukichukua asilimia tunaitumia kwa elimu leo ni kama asilimia 4.3 ya *GDP* ndiyo inatumika kuboresha elimu. Mimi nadhani hili ni tatizo kubwa kweli, tusipoliangalia hatutakuwa na nchi ya wasomi. Huko nyuma miaka ya 70 Taifa lilikuwa linatumia kiasi cha *GDP* isiyopungua asilimia 15 kwa mambo ya elimu. Narudia, tulikuwa tunatumia *GDP* isiyopungua asilimia 15 kwa elimu, ndiyo maana tukafikia lengo la *UPE* wakati huo. Kama leo tumeteremka mpaka asilimia 4.3, nadhani tunafanya utani katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba, hali ya uchumi si nzuri lakini itakuwaje, tutenge kiasi kikubwa kwenda kwa Wizara nyingine kama vile barabara, jeshi na mambo mengine tukaisahau elimu, ambayo ndiyo msingi wa Taifa letu. Nchi zote zinazoendelea tukiacha Afrika, zinatumia kiasi kikubwa, lakini siyo sisi tunaosema tumeingia kwenye utandawazi au *globalization.* Natoa mfano wa Ireland, wanatumia kiasi kikubwa sana cha fedha kuweza kusomesha watoto wao. Kwa nini hatufanyi hivyo, wenzetu Kenya na Uganda watoto wao wengi kuliko sisi maana wanatumia asilimia kubwa ya *GDP* wanasoma na sehemu nyingine.

Hakuna vita, hapa mahali pametulia kwa nini tusitenge fedha za kutosha kuweka kwa elimu badala ya kungojea wahisani? Kwa nini tusifanye mpango unaoendelea kule Wizara ya Ujenzi wanakotumia kiasi fulani cha mapato yao wenyewe ndio baadaye wanaongeza zile za wafadhili? Nadhani lingekuwa jambo la busara, vinginevyo nchi hii itakuwa ya watu ambao si wasomi ni mbumbumbu.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, suala lingine linajitokeza, naona kuna ujenzi wa majengo chini ya MMEM, tumeboresha majengo mengi ya *primary schools*. Sasa najiuliza elimu inatokana na majengo tu ama na walimu; kwa nini tusitumie hizo fedha kusomesha walimu wengi kuliko kujenga majengo ambayo hayawezi ku-*produce* mtoto. Majengo ya *primary schools* yanaweza kutumika wakati wa asubuhi kusomesha watoto wa shule ya msingi na hayo hayo yakatumika kusomesha watoto wa sekondari wakati wa jioni bila matatizo tukaokoa fedha, huo ni ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda Venezuela, nimeona wanafanya hivyo, jengo moja linatumika kwa ajili ya wanafunzi wa shule ya msingi asubuhi na jioni wanatumia wa sekondari. Hizo fedha tungezitumia tungeweza kuwalipa walimu wengi wanaofaa wakaenda kufanya kazi hiyo na mnaweza ku-*share*. Walimu wanaweza kuwa na uwezo wa kufundisha shule za msingi, pia wana uwezo wa kufundisha shule za sekondari, ukawatumia wale wale na mimi nadhani kwa mahesabu yangu ya haraka haraka, tunaweza kuokoa nusu ya bajeti tuliyopanga kuboresha elimu.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naona sasa kuna jambo lingine linajitokeza, kila Kata inajenga sekondari, sasa nadhani inaanza kuwa kama ile inayoitwa *zero-grazing,* eti kila ng'ombe achungwe kwenye zizi. Kuna madhara makubwa ukifanya hivyo, sisi tulikwenda mashule mengine mbali na tulikotoka, mimi nilikwenda *Tabora School,* wengine Minaki na kadhalika. Unapowasambaza ndio unapata mbegu bora, ukiwaweka pale pale kwenye Kata ndio *zero-grazing,* una-*produce inferior students.* Mimi nadhani tungefanya mkakati wa kuwabadilisha kuhakikisha kwamba, mtoto wa pale pale asisomee pale pale aende pengine akajifunze mambo mengine mazuri. Tukisema wabaki pale pale, kuna matatizo yanayojitokeza na sioni kwa nini tuendeleze hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwe na sekondari nzuri za Wilaya ambazo zinaweza kutumika na Kata kadhaa au tusiwe na shule moja bora mkoani. Wakati huu ni wa utandawazi, wakati huu ni wa *globalization,* elimu lazima ifanane na wenzetu popote. Elimu yetu sio tofauti na ya Malawi, Kenya, Uganda na kadhalika, lazima ifanane. Ni mchango wangu kwamba, tukiboresha haya mapungufu niliyoyaeleza kwa kifupi, tunaweza kuwa tumepiga hatua kubwa kuboresha elimu kwa ujumla.

Baada ya kusema haya yote, naunga mkono tena hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa tena nafasi hii ili na mimi niweze kusaidia kuchagia kidogo katika elimu. Kwanza, namsifu sana Waziri kwa jinsi alivyoweza kuiandaa bajeti hii, pamoja na mtumishi wa chini yake, kwa kweli ni changamoto nzuri na sina cha kuzungumzia zaidi ya yale aliyoyasema. Mimi kilichonifanya hata nikazungumza ni kero ambazo nazipata katika jimbo langu, ambazo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, *a-take note* ili arekebishe kwa sababu kwa kweli ni kero na sijui zinakuja kwa sababu gani, kwa sababu elimu haina itikadi wala upendeleo, ni haki ya kila raia wa Tanzania.

Nataka kutoa mfano mmoja wa shule ya sekondari tuliyokuwa tunaijenga sehemu moja inaitwa Kiboriloni katika Kata ya Moshi Mjini, kwenye Jimbo langu la uchaguzi.

Shule ile niliweza kusaidia kuijenga nikishirikiana na Diwani wangu mpaka tukafika 99%. Halmashauri ya Moshi na hapa ni lazima nimlaumu sana Mkurugenzi kwa sababu alileta mabati ya kupaua badala ya kupeleka shuleni akapeleka nyumbani kwa Diwani akaenda akayaweka uani bila hata kuyahesabu wala kusaini kama amepokea nini.

Katika makisio yetu ya Halmashauri, tulipokuwa tunapitia mabati yale pamoja na rangi, alikuwa ametoa haifiki shilingi milioni tano, lakini kwenye bajeti tukakuta ametoa shilingi milioni 26. Mimi naona huo ni wizi na hakuna mtu aliyechuguza japokuwa nimepiga kelele nyingi sana juu ya jambo hili na linakatisha tamaa hata nguvu za Wananchi waliochangia, pamoja na wale wafadhili waliosaidia kujenga ile shule. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, ulitupie macho hilo na tunaomba tuhakikishiwe ya kuwa, *auditing proper* inafanyika na hizi pesa ambazo tunahakika zimeliwa, waliozila wachukuliwe hatua na pesa zile zirudishwe angalau ziongeze madarasa mengine. Si hivyo tu, Mkurugenzi alituruhusu twende tukakope mbao za kupaua ili ile shule iweze kutumika kwa haraka iwezekanavyo. Ni miaka mitatu sasa hajalipa ile pesa aliyotuambia tukakope, imekuwa ni shule ya matatizo tangu wakati tukiomba kujenga kiwanja, ilichukua miaka miwili kabla hawajaturuhusu kujenga na mimi naona ni kuzorotesha elimu katika Jimbo langu.

Jambo lingine katika Kata ya Msalanga, tulikuwa na sera ya Halmashauri yetu ya kwamba, watumie nguvu zao wajenge wakishafika kwenye lenta Halmashauri inapaua. Jambo la kushangaza, zile Kata ambazo zina Madiwani ambao wanatoka Upinzani, wamemaliza kuzijenga lakini hazipauliwi, unakuja kukuta Kata yenye shule imejengwa kwenye Diwani wa CCM inamaliziwa. Ninatoa mfano wa Kata ya Rau, ambayo mimi nimechangia matofali yote ya kujenga ile shule, Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja, Diwani alisema yeye ndiye aliyejenga na mimi nilikuwepo lakini sikujali kwa sababu hainidhulu chochote.

Tukimwambia hebu tuletee mahesabu ya ujenzi ni mwaka sasa hatoi, sasa hii inatukatisha tamaa, ni mtu ambaye napenda kujitolea kwa nguvu zangu na uwezo wangu kusaidia na kujenga lakini mambo kama haya yanapotokea, nilikwenda mpaka kwa Mkuu wa Mkoa nikalalamika kwake na yupo hapa ndani, nikamwambia matatizo haya pesa za MMEM na MMES hasa za MMES zilipokuja sisi tulikuwa na mpango wetu wa kusema Wananchi wajitolee katika Kata ili wajenge hizo shule. Pesa za MMES zilipokuja ziliweza kupelekwa katika shule ambayo ilikwisha malizika na kupauliwa na kila kitu badala ya kujenga darasa jipya wakasema wanaanza kuweka sakafu katika lile darasa na ni karibu shilingi milioni 16, nashangaa pesa zinaliwa hivi hivi. Hii ni hujuma, mimi naiona kama ni hujuma na wanafanya hivyo kwa makusudi kwa sababu mimi Mbunge wa Moshi Mjini ninatoka Chama cha Upinzani, kwa sababu watu wataona kuna maendeleo na maendeleo kweli nimeyaleta na hata wafanye nini hawataweza kufuta ule ukweli ambao Wananchi wameuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunapata tabu nyingi wakati tunapotaka kuleta maendeleo katika Kata zetu, inatia kinyaa wakati umefanya kazi, umejenga shule kwa pesa zako, halafu anakuja mwingine anasema ni mimi nimejenga. Nakumbuka Mheshimiwa Pius Ng'wandu, alipokuja Moshi aliitisha mkutano pale tukakutanika wote,

tukasema yeyote anayechangia katika ujenzi wa shule itakuwa *appreciated* na nyingine hata jina lake litatumika unakuja kukuta shule hata senti tano mtu hajachanga anapewa jina na mwingine ndiye aliyechanga pesa zile za kujenga, hii ni hatari, inawavunja moyo wote wale wenye nia njema na nchi hii. Mimi sikusema kuwa nitasema mengi sana, maana nimetoa hayo ambayo yananiudhi na ubaguzi wa kishenzi ambao unatumika, mimi nauita wa kishenzi, kwa sababu sio wa kistaarabu, yeyote anayetenda mema anategemea na yeye arudishiwe mema, hata Mungu ndivyo anavyosema. Kuna kitu kimoja kidogo ambacho naiomba Wizara iangalie kwa makini, unakuta vijana hawa walimu wa miaka thelathini mpaka labda arobaini, hawa bado damu yao ni mbichi na inachemka, unamkuta mke anaweza kukaa Dodoma miaka mitano na mume anakaa Dar es Salaam miaka mitano hawakutani, hatuchochei UKIMWI?

Hawa ni binadamu na binadamu yeyote hawezi kukubali kuwa atakaa hivyo hivyo, ni lazima Wizara ijaribu kutafuta njia ya kuwasidia hawa ili waweze kukaa na familia zao na itapunguza matatizo mengi hata katika bajeti ya chakula, familia inapokaa sehemu mbili inakuwa ni matatizo kuhimili maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kwa kifupi juu ya pesa za MMES na MMEM, pesa za MMEM zilipoletwa, maagizo yalikuwa ziende katika Kamati za Shule ili shule iweze kutumia Kamati zake na nguvu za Wananchi, waweze kujenga zile shule. Ilipokuja katika Jimbo langu la Moshi, utaratibu ule ulivunjwa kwa makusudi, Halmashauri ikaandika *cheque* ili iweze kumridhisha Waziri, ikapelekwa kwenye shule na kesho yake ikaambiwa andika *cheque* mara ya pili irudi kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi akaweka *contractor.* Sasa hiyo kama si *corruption* ilikuwa hapo, tuseme ni nini na nguvu za Wananchi hazikutumika kabisa katika kuendeleza, ilikuwa ni *contractor* amewekwa pale wakati *directive* ya Serikali ilikuwa ni Kamati za shule zijenge, lakini kauli, yaani wanageuka tu hivi hivi na hali ni hii, maana yake ni kula rushwa tu. Kwa nini umpendelee *contractor* badala ya kuwaacha wale wanaohusika wafanye kazi ile na tumeona madhara yake kule Moshi na nilipiga kelele sana juu ya jambo hili lakini wapi, hakuna anayesikiliza na mimi nalalamika hapa kwako Waziri, wale waliohusika wachukuliwe hatua na hili tuone haki inatendeka.

Mhehsimiwa Naibu Spika, sina mengi zaidi ya hayo, naomba kukomea hapo na Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja yako nikiwa na matumaini haya niliyokwambia hapa, utayafanyia kazi, asante. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri, pamoja na wataalam wake, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika muda wa miaka hii kumi ambayo tunakaribia kumaliza awamu ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa dhati kwa sababu kama kumetokea mageuzi katika nchi hii, ambayo watu wanaweza kuyaona na kuweza kufikiri kwamba wamepata mabadiliko ni katika eneo la elimu. Sio siri ukiangalia shule zetu za msingi kabla ya utaratibu wa MMEM hazikuwa shule ambazo unaweza kujivunia mtu kwamba, leo tuna shule za msingi. Lakini leo pita mahali popote ndani ya nchi ya Tanzania,

utaoana kabisa hii ni shule kwa mafanikio ya ubora wa shule ya msingi watoto kufanikiwa kufaulu vizuri ni matokeo ya mahali mazingira watoto ambayo wanasomea. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri na wengine waliosema kwamba, tukisema kwamba mafanikio ya awamu ya tatu hayajaenda kwa Wananchi, kwa kweli nadhani tunazungumza mambo mengine.

Kwa sababu shule za msingi ni za Wananchi na halafu imekuwa kama ni kichocheo, watu sasa wameona umuhimu wa kupeleka watoto wao shule. Kwanza ni mazingira ya shule halafu kufuta ada za shule za msingi, sasa unakuta Wananchi waliowengi wanaona umuhimu wa kupeleka watoto wao shule. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa kabisa, kwamba ni faida ya kukua kwa uchumi, ni mojawapo ya eneo ambalo liko wazi kabisa na kila kitu chema hakiwezi kukosa kasoro na hasa kwa mradi mkubwa ambao umetekelezwa nchi nzima. Lazima kasoro zitakuwepo na nadhani kasoro hizo kila mtu mwenye busara yake, alizitegemea. Usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha zile za MMEM mahali pengine haukufanyika vizuri, kwa hiyo, ni suala la Halmashauri zinazohusika kwa kweli kwenda kukagua kila shule kuona fedha zilifanya kazi iliyokusudiwa na pia ni wakati muafaka kwamba, hili tatizo la walimu kweli bado lipo na shule nyingine hawatoshi.

Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo najua Wizara inayafahamu na katika matatizo ya utekelezaji, Waziri ameyasema vizuri sana, lakini pia tuingie katika suala zima la ujenzi/ukarabati au suala zima la elimu ya sekondari. Nalo hilo ni matokeo ya shule zile za msingi sasa watu wameona lazima watoto wao waende sekondari na ndio hiki kilichofumuka cha ujenzi wa shule za sekondari kila mahali. Naomba nishukuru binafsi, Wizara imenisaidia sana kuhakikisha shule tulizoweza kujenga katika mwaka huu zote zimesajiliwa na watoto wameanza kusoma. *(Makofi)*

Haidhulu tumeanza kwa kuchelewa kwa hiyo kuna watu wengine watoto wao wameshaenda walikokwenda, lakini asilimia kubwa ya watoto wameweza kuanza shule tarehe 25 Aprili, 2005. Kwa hiyo, shule zote tulizojenga kwa kweli zimefunguliwa na wazazi na Wananchi wote wanafurahia matunda ya jasho lao. Wamefanya kazi kubwa na watoto wao wamewaona wako shuleni na tunaendelea kufanya kazi nyingi za kuweza kuzikamilisha vizuri zaidi shule hizo. Ningeomba hapa kwamba, shule ambazo tulizitoa kwenye Shirika la Elimu la Wilaya na kuzikabidhi Serikalini, zilikuwa kama shule tatu, nimeona katika Kitabu cha Waziri shule moja ya Matola kulikuwa na maabara ilijengwa kwa muda ilichelewa, sasa hivi Serikali nadhani imekamilisha shule, tunashukuru.

Pia kuna shule hizi nyingine tulizochukua kama Shule ya Mpechi, Shule ya Uwemba na Shule ya Kifanya, kwa kweli majengo yake yapo katika hali ngumu sana. Shule ya Mpechi wamewasilisha Wizarani makadirio yao ya kuweza kuwasaidia waweze kukarabati. Naamini Mheshimiwa Waziri, ataangalia uwezekanao wa kuwapa zile fedha waweze kukarabati. Shule ya Njombe ni ya Serikali toka siku za nyuma lakini wakati utaratibu wa MMES haujaanza, Wananchi wa Mji wa Njombe tulijenga mojawapo ya *form five* na *six,* kwa kujitegemea wenyewe.

Sasa naiona Serikali imeamua kuichukua ile shule yote iwe inafundisha *form five* na *six,* majengo ya awali tulijenga sisi, sasa nilifikiria Wizara ingewasaidia wale Wananchi thamani ya majengo yale mawili wakatupa fedha sisi tukarabati shule ile ya Mpechi. Tungefanya hivyo tungekuwa hatudai hela nyingine, kwa sababu tulijenga kwa kweli wenyewe kabisa bila msaada wa Serikali katika shule ambayo inahudumia nchi nzima. Sasa nilifikiri Waziri angeweza kutufanyia utaratibu wakayatathmini yale majengo mawili ya *form five* na *six* sasa wakatupa thamani ya fedha inayolingana kusudi tukakarabati ile ya Mpechi ambayo iko karibu pale pale, zote ni za Wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni ombi rasmi na nimetumwa na Wananchi kusema hivyo, lingine ningependa kusema kwamba, wakati kuna mafanikio ya shule ya msingi na sekondari, sasa inaelekea huku juu kwenye vyuo vikuu wanafunzi wanajazana na wengine wanakosa nafasi na kuwekwa kwenye *waiting list,* ambayo haijulikani. Sasa nafikiri hawa wanaoshughulikia elimu ya juu na elimu hii ya sekondari, wakae pamoja waone namna gani wataweza kulitatua hili tatizo.

Kwa sababu tunakuwa kama tunawafanya watoto wakifika kule juu wachanganyikiwe kweli kweli. Lakini hiyo ni sifa ya mafanikiko, ambayo yanatupa matatizo haya. Lakini haya ni matatizo ya mafanikio, naamini kabisa vichwa vilivyoko katika Wizara hizi mbili, vitaweza kupata ufumbuzi wa hili pia kusudi tuwe na utaratibu watoto waende kusoma bila matatizo yoyote.

Lingine ambalo ningependa kusema ni mawazo yangu, hakuna mtu aliyesema lakini mimi naona niseme tu na Waziri ataniambia hivi tunavyohangaika na walimu wa sekondari na kuwachukua wale waliomaliza *form six* kuanza kufundisha hizi sekondari nyingi tulizozijenga, hivi kweli hatuwezi kuchukua walimu kwa mkataba kama miaka mitatu kutoka nchi za jirani hapa wakatusaidia kufundisha wakati sisi tunafundisha wa kwetu ili wajazie nafasi hizi wakati sisi tunaendelea kufundisha walimu wengine katika vyuo ulivyosema Mheshimiwa Waziri, kusudi tusipate elimu iliyokuwa dhaifu sana.

Hili litakuwa tena kundi ambalo tumelifundisha lakini halikupata faida ya kusoma vizuri. Nadhani tusipate aibu, tuingie Mkataba na nchi jirani kwa miaka angalau mitatu tunapofundisha wa kwetu wenyewe wajazie nafasi wakifaulu hawa wa kwetu, wale wageni waondoke. Mimi sijui nafikiri kwa sauti lakini kila siku nimeamini kwamba, hatuwezi kuwaacha watoto wasiende sekondari itakuwa ni kosa. *(Makofi)*

Pia hatuwezi kuwafundisha kienyeji, tutafanya makosa, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kweli tunaweza kuwachukua walimu nchi za jirani wakafundishe miaka mitatu halafu wawe wanakuwa *replaced* na hawa wanaomaliza. La mwisho ningependa niseme, naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii, kwa kuweza kuwaeleza Watanzania kwa uwazi, umuhimu wa kuingiza mtaala mpya kwa sekondari, kwa sababu kila alipokuwa anasema Waziri, ilionekana ni tatizo lake mwenyewe binafsi.

Ninaishukuru Kamati ambayo imekwenda kwa undani na kujifunza hili wazo lilitoka wapi na kwa nini limefikishwa hapa. Kwa hiyo, naomba Watanzania tusiingie kwenye malumbano ya kisiasa wakati tunazungumzia mambo ya taaluma. Kwa hiyo,

naipongeza sana Kamati kwa sababu imekwenda kwa undani na kufuatilia hili suala limetoka wapi, kumbe linaonekana lipo ndani ya maamuzi ya kitaalamu ya Serikali. Kwa hiyo, sio suala la Mheshimiwa Joseph Mungai peke yake, maana amefika mahali anapigwa vita kama mtu binafsi, kumbe suala lenyewe zima liko ndani ya Serikali. Kwa hiyo, naishukuru sana Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kuweza kuliweka bayana na nilikuwa namshawishi Mwenyekiti wa Kamati, akaongee na waandishi wa habari pia haya aliyoweza kuyafanyia utafiti kuliko ku-*personalize* suala ambalo ni la Kiserikali. Kwa hiyo, naomba niipongeze sana Kamati kwa hilo na kuwaomba Watanzania tusichezee masuala ya kitaaluma kama tunavyochezeana katika siasa. Tutaharibu vizazi vinavyokuja kwa ajili ya tabia zetu za kuona mambo yote ni ya kisiasa. Sijawahi kuona mtu aliyesomea mtaala wa kilimo toka *form one* mpaka *six* akawa afisa kilimo. Sijawahi kumwona mtoto aliyejifunza useremala akawa ni seremala baada ya kumaliza. Kwa hiyo, ni mambo ambayo tunafikiri kwa kweli yalikuwa yanawapotezea watoto wakati na kuacha kusisitiza umuhimu wa elimu ambayo inatumika duniani kote na inayomwezesha mtu ku-s*pecialize* baada ya kumaliza. Kwa hiyo, naomba niipongeze sana Kamati hii kwa kuona umuhimu wa kusema ukweli wakati watu wanataka kufanya mambo haya yawe ya siasa wakati ni mambo ya taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii na kuwapongeza wataalam wote.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuzungumza katika hoja hii ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kwanza kabisa, ningependa kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kalenga, nitoe rambirambi kwa kifo cha mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, ambaye imempendeza Mwenyezi Mungu, kumchukua ghafla, kwa hiyo, natoa rambirambi kwa familia yake na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na namwomba Mwenyezi Mungu, amrehemu na kumjalia uzima wa milele mbinguni, *amina*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ningependa kusema kabisa kwamba, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Elimu na Utamaduni bila matatizo yoyote na nampongeza yeye, pamoja na wataalam, kwa kuandaa hotuba hii ambayo ni nzuri sana, ina mpangilio mzuri wa mipango ya elimu, Kitaifa. Kwa hiyo, nachukua kitabu hiki cha hotuba yake kama *reference book* ya mipango ya elimu Kitaifa na nitakihifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, kumetokea mapinduzi makubwa katika elimu Kitaifa na wakati wa hoja ya Waziri wa Fedha, nilizungumzia kwamba, hata kwangu katika Jimbo la Kalenga, ambako nilipo ingia kama Mbunge mwaka 2000, kulikuwa na shule za sekondari mbili walizojenga Wananchi, sasa hivi tumeweza kuongeza shule tisa na kufikia shule kumi na moja katika Jimbo hilo na ni shule ambazo ni muhimu kwa sababu Jimbo ni kubwa na watu ni wengi sana kwa kila Kata. Kwa hiyo, wanahitaji shule hizo na pengine tunaweza tukahitaji zaidi ya hapo kulingana na wingi wa watu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitaifa, Mheshimiwa Waziri lazima tuseme wazi kwamba amekuwa ni kichocheo kikubwa cha mafanikio haya kutokana na juhudi, ubunifu, msukumo wake wa kujitolea, pamoja na Watendaji Wakuu wake na Watendaji wote ambao kwa kweli wametekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2000. Ningependa kufananisha ili ieleweke vyema, nimnukuu mwandishi mmoja anaitwa John Maxwell. Anasema: *"A leader is someone who knows the way, goes the way and shows the way."* Hii naona Mheshimiwa Joseph Mungai amethibitisha katika Uongozi wake wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ujenzi wa Shule zetu, kama nilivyosema, kwa upande wangu ni Shule tisa. Tumepata msukumo mkubwa kutoka katika mpango wetu huu wa MMES. Lakini kulikuwa pia na matatizo ya upatikanaji wa fedha hizo za MMES na Mheshimiwa Waziri analifahamu vizuri suala hili. Tulikuwa kwenye mawasiliano mara nyingi, kwamba kwa upande wangu Shule tatu ilichukua muda mrefu sana kupata fedha. Shule ya Sekondari ya Lumuli, Shule ya Sekondari ya Liandembera, Ifunda na Shule ya Sekondari ya Luhota au Maguliwa zilichelewa sana.

Kwa hiyo, zilipunguza sana ari ya wananchi ambao walikuwa wanajenga Shule hizo. Sasa matatizo yanaweza kuwepo na kadhalika, lakini ni muhimu Watendaji kueleza ukweli kunapokuwa na matatizo ya *disbursement* fedha hizo. Si vyema kutoa taarifa ambazo si za kweli kwamba fedha tumetuma mna-*check NMB* hakuna fedha, mnauliza mnaambiwa tumetuma, mpaka pengine mara tano mnaambiwa tumetuma na hakuna fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni wazi wale wanaotuma fedha wanajua kwamba hawajatuma. Au mara nyingine kama kuna tatizo la kupatikana fedha, sio vyema kutumia lugha ambazo hazieleweki, kwa mfano kusema matatizo yaliyopo ni *technical*. Sasa sisi watu wote ni waelewa tumekwenda Shule, unaeleza tatizo ni nini ili tuweze kuwaeleza wananchi kwamba kuna tatizo hili. Lakini nikienda kwa wananchi nikawaambia nimeambiwa tatizo ni *technical*, si naonekana kama vile hata ninachozungumza hakina maana!

Kwa hiyo, ningeomba Watendaji, kunapokuwa na matatizo, tushirikiane tuwe tunaelezana halafu na wananchi tunaelezana, kwa hiyo, wanajua wanakuwa na matumaini. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri alinisaidia sana katika kutatua matatizo haya. Kwa hiyo, fedha ziliweza kupatikana. Lakini ningependa vile vile kuwasilisha maombi kwamba Shule hizi, Mheshimiwa Waziri alikuwa ameahidi kwamba tutapata Shilingi milioni 14 kwa kila Shule kwa ajili ya madarasa na Shilingi milioni tisa kwa ajili ya nyumba za Walimu. Lakini Shule zifuatazo zimepata Shilingi milioni 14 peke yake bila ile Shilingi milioni tisa ya nyumba za Walimu, nazo ni Shule ya Lumuli, Shule ya Liandembera, Shule ya Mseke, Shule ya Zihi na Shule ya Maguliwa. Iliyopata ni Shule ya Kiwele peke yake ambayo imepata zote kwa hiyo jumla ya Shilingi milioni 23, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeomba katika awamu hii tunayokwenda, basi kwanza tujaziwe hizi ambazo hazikulipwa safari iliyopita ili waweze

kuendelea na ujenzi wa nyumba za Walimu. Halafu kuna Shule mpya ambayo ilikuwa haipo katika mpango wa kupewa msaada wa MMES kwa wakati huo. Lakini tayari inajengwa imeshafikia hatua kubwa, nayo ni Shule ya Mgama nayo tungeomba ipewe fedha zote hizo, yaani za Shilingi milioni 14 na Shilingi milioni tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna Shule zile za zamani kwa mfano kama Kalenga, Isimila ambazo sasa ni za Serikali, zinapaswa ziongezewe fedha za MMES kwa sababu idadi kubwa sana ya wanafunzi imeongezeka katika Shule hizo. Kwa hiyo, wanafunzi ni wengi kupita uwezo wa ku-*accommodate* watoto hao. Ni jambo zuri, lakini basi tuendelee kurekebisha tuongezee madarasa na nyumba za Walimu. Vile vile na Shule ya Kiponzero nayo imekwishakuwa ya Serikali imepata tu Shilingi milioni tisa kwa ajili ya nyumba za Walimu. Lakini napo pana ongezeko kubwa la wanafunzi, Shule ya Wasa hiyo ambayo imepata Shilingi milioni 23, tunashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumza na Mheshimiwa Waziri na kukubaliana kimsingi kwamba zile Shule ambazo zilijengwa kama Shule za Tarafa, kwa mfano kama Shule ya Kalenga ambazo ni za Serikali sasa zijengwe ziongezewe Kidato cha Tano na cha Sita. Ningependa nilikumbushe hili ili tulikamilishe na vile vile Shule nyingine ambazo ni za Tarafa kama Shule ya Isimila ambayo ni ya Tarafa ya Mlolo na Shule ya Kiponzero Tarafa ya Kiponzero nazo zipate hadhi hiyo ili iwezekane kabisa kwamba wanafunzi wanaosoma katika Shule hizi za Kata na zote waweze kupenya kupata Elimu ya *High School* na hivyo hivyo baadaye kuweza kufika kwenye Vyuo Vikuu na kupata taaluma muhimu zinazohitajiwa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza juu ya mradi wa uboreshaji wa Elimu ya Sayansi, *Science Education for Secondary Schools (SESS).* Ningependa nipendekeze zaidi ya hilo alilopendekeza kwamba Shule za Sekondari nyingi sasa ziko Vijijini kwenye Kata. Huko bakia ya kwamba amekubali kwamba Serikali itachukua jukumu la kujenga Maabara, lakini vile vile Maabara hizo au Shule hizo zinahitaji umeme ili kufanya *science experiment,* kwa masomo kama *Physics, Chemistry, Biology* na kadhalika.

Sasa kama wanafunzi wetu katika Shule hizi tunazojenga watasoma masomo ya *science* na kupata elimu ya viwango vya juu kama wengine ni muhimu sana kupeleka umeme. Kwa hiyo, tubuni mpango mkubwa Kitaifa wa kupeleka umeme uwe ni umeme wa *solar* au ni wa *generator* ingawa *diesel* gharama yake ni kubwa sana. Lakini tupeleke umeme ili nao wasome masomo ya *science* vyema. Bila umeme hawawezi kusoma *science* ipasavyo. Vile vile, ningependa Mheshimiwa Waziri katika mpango huu wa MESS, Shule zinazojengwa huko Vijijini, Shule binafsi ambazo watoto wetu wanasoma nazo zingepata mgao wa kiwango fulani cha MMES. Kama katika Jimbo langu kuna Shule ya Sekondari ya Sagamiko iko Kijiji cha Wenda Kata ya Mseke, Shule nzuri kabisa tungeomba juhudi za wenye Shule hii tuwasaidie ili Shule hii iweze kukua na kuwa imara.

Vile vile, katika Kijiji cha Maguliwa kuna Shirika la Dini la Kilutheri huko Florida kupitia kijana mmoja anasoma huko, wameamua kutusaidia kujenga Shule lakini

pamoja na wananchi. Sasa baadaye itakapofika hata kuiendesha tungeomba vile vile nao wapewe mgao wa MMES ili kuimarisha Shule kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa haraka kidogo ili nimalize kwa muda uliopangwa na niweze kuwasilisha maoni yangu ambayo kwa kweli ni ushauri tu, sina kitu chochote ambacho ni cha kuweza kumbishia Mheshimiwa Waziri. Ningependa nimpongeze tena kwa juhudi zake kubwa sana, tunajivunia sana juhudi zake. Pia, ningependa ninapomaliza nimnukuu mwandishi mwingine anaitwa Emil Bisel ambaye anasema *great thoughts speak only to the thoughts great minds, but great actions speak to all man kind.* Mambo yote haya mawili Mheshimiwa Joseph Mungai ,Waziri wetu wa Elimu na Utamaduni, umeyafanya nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kwa furaha kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya ndugu Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kabla ya kuendelea, niungane na yale maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', mawazo aliyosema na Mheshimiwa Anne Makinda na wengine ili kufupisha mchango wangu. Kwa sababu muda hauruhusu, basi nitakwenda kwenye shughuli zenyewe, ambapo moja ni kuipongeza Wizara kwa kazi ngumu na nzuri wanayofanya.

Mambo mengi yamefanywa na ni makubwa, ya kimapinduzi na tunatumaini awamu mpya itatumia ngazi hii kwenda mbele zaidi. Isaac Neutron wakati fulani aliwahi kusema kwamba: "Kama mimi nimefanya mambo mazuri zaidi kuliko wenzangu walionitangulia, basi ni kwa sababu nimesimama katika mabega ya wenzangu walionitangulia." Lakini kwa sababu sisi tuko kwenye utawala na wenzetu, Upizani wanasubiri awamu nyingine, basi kazi yetu kubwa hapa ni kutetea, kuboresha hoja zetu ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni haya, nilikuwa na mapendekezo ya kimsingi. Moja ni kule kuhangaika. Mtu unaweza ukawa kwenye Wizara ukawa unakaa tu mradi mambo yanakwenda, lakini kule kuhangaika nadhani ndiko huku unakotakiwa kusifu. Mheshimiwa Joseph Mungai amehangaika sana kufanya kazi katika Wizara hii. Sio kufurafura, yaani kuhangaika kwa maana ile ya kufanya kazi vizuri. Mheshimiwa Joseph Mungai anaelewa maana yake, kuna kufurafura kwa Kibena kuna maana yake na kwa Wahehe kuna maana yake. Umehangaika kujenga misingi ambayo tutajivunia baadaye. Nilikuwa nina mapendekezo yafuatayo ili kuboresha mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, napendekeza kwamba pamoja na mapinduzi haya ni vizuri somo la Hisabati liwekewe mkakati maalum ili lifundishwe kutoka *Form One* mpaka ngazi ya *degree*. Ili kuweka msingi imara wa *science,* huwezi kuboresha kuendeleza *science* bila kuboresha au kuimarisha watu wako katika somo la *science*. Kwa sasa hivi limekufa, kwa hiyo, ni lazima tuazime kutoka nje mabingwa wa *science* na kuweka *special program* na motisha kwa wanaofundisha Hisabati. Kwa kweli

wakati ni huu, vinginevyo tutakuwa na watu wanaojua Historia bila hesabu na sasa hivi kila somo linahitaji Hisabati. Hilo pendekezo naomba lichuliwe maanani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa sasa wanajengwa Shule nyingi za Sekondari katika kila Wilaya, haiwezekani zisimamiwe kutoka Makao Makuu Dar es Salaam. Tuongeze madaraka ya *REO* kwa maana ya *manpower* na madaraka zaidi kusudi aweze kusimamia elimu katika ngazi ya Mkoa. Haiwezekani isimamiwe kutoka Dar es Salaam, hatua hii ichukuliwe haraka na kwa faida ya nchi ya hii. Vinginevyo, mambo ni mazito. Sasa hivi nimwachia *DO* anahangaika na Shule za Msingi zinaathirika kwa sababu ya mtu huyo ambaye hakuandaliwa na hana *manpower* ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kwa sababu ya mapinduzi haya ambayo yanakwenda kwa kasi kubwa ya kujenga Shule za Sekondari zinaota kama uyoga na kuna siasa ndani yake, sio rahisi kuzuia. Anne Makinda pale amesema labda uazime, lakini hata ungeazima, maadamu hu-*control production* ya mambo yako, ujenzi wa Shule za Sekondari itakuwa ni kazi ngumu sana.

Nilidhani hili labda tungeliwekea mkakati sasa tukubaliane, maadam wote wanajenga, lakini sasa tuweke utaratibu kusudi tuwe tunajenga kuoanisha na *production* ya Walimu kusudi tukidhi mahitaji hayo. Vinginevyo, yatakuwa ni majengo tu. Tuelewe Shule siyo majengo tu, wala sio vitabu tu, ni mchanganyiko wa sifa na mambo mengi ya lazima, vinginevyo tutazidi kugawa Walimu hawa hawa na vifaa hivi hivi na baadaye tutakuwa tuna *Extended Primary School* na elimu itakayokuwa *diluted* na *as a Nation,* tutajikuta hatuwezi tukashindana na wenzetu.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hapa, kwa kweli itabidi lazima wanasiasa hasa Wabunge tukubali kwamba itabidi kuwe na *control* kwamba Mkoa fulani mwaka kesho mnafungua Shule kadhaa kwa sababu ya Walimu kadhaa. Vinginevyo tutapata tatizo la kugawana hiki kidogo na baadaye tutakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, nilikuwa napendekeza kwamba madaraka ya kupeleka Walimu kununua vitabu, uamuzi huo ni mzuri, lakini nadhani tutasambaza kadi. Napendekeza kwamba mambo mengine yaende kwa Walimu mpaka Walimu wa Shule za Msingi waweze kuamua lakini ununuzi wa vitabu uwe chini ya yule Mtaalam wa takwimu ndani ya Wilaya chini ya *DO* ili aweze kuwajibika kwamba vitabu vingapi vimekwenda wapi?

Kwa sasa hivi kuna matatizo mengi sana. Wale Walimu wa Vijijini wanapata matatizo na wanachukua vitabu ambavyo ni *paper back* na vingine vimepatikana kwa mfano vitabu vya Kongwa hapa vinauzwa Kagera. Shuleni hakuna vitabu, takwimu zinaonyesha wamenunua, lakini usimamizi ni mgumu sana na *DO* hawezi kuwajibika kwa sababu anasema mimi nilikwishapeleka fedha kwa jambo kama hili lisimamiwe na *DO* na yule mtaalam wake kusudi aweze kuwajibika kwamba anasimamia elimu. Ni wazo zuri la kuwapeleka kule, lakini nadhani *we are biting more than we can choose.* Tumsimamie *DO* na yule wa *logistics* yule asimamie vitabu ili uweze kumwuliza vingapi

vimekwenda wapi na aweze kukueleza. Hata kama kuna madhambi hapa angalau *cancer* hii iko kwa watu wachache kuliko kusambaza kwa Walimu wote wa *Primary School.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa napendekeza kwamba lile suala la kuhakiki madeni ya Walimu wa Sekondari, Wakaguzi lile zoezi limefikia wapi? Kwa sababu wale wa Shule za Msingi tumefanikiwa na wameanza kuwalipa. Lakini hawa wanadai zaidi ya Shilingi bilioni moja na wengine wale Wakaguzi zaidi ya laki nane na bado hili zoezi halijakamilika tulikuwa tunapendekeza kwamba hatua zichukuliwe ili kuongeza motisha kwa Walimu hawa ambao wamekuwa wakidai muda mrefu. Sisi tunapongeza kwa hatua zile zilizochukuliwa, lakini hii hatua nadhani inaathiri sana kasi za Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika ukurasa wa kwanza wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri, mimi nakubaliana sana na ile *quotation* ya Rais wetu aliposema kwamba inabidi kuwa na vipaumbele miongoni mwa vipaumbele. Katika kujenga hizi Shule za Sekondari kwa sababu ya matatizo tuliyonayo, napendekeza kwamba tuwe na *Secondary School* katika ngazi ile *Territorial or Nation Secondary Schools, Regional Secondary Schools, District Secondary Schools* na hizi za kawaida. Hizi za kawaida na hizi ambazo tunajenga hizi za siasa siasa hizi, tunapeleka Walimu wanne, siyo *absorbers* kwa sababu tu ya *pressure* unazijenga, basi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukitaka tusambaze hii nguvu *scenery* kwa watu wote tutakwama kabisa. Tubaki na Shule kama za Ilbolu za Mzumbe na kuwe na Maabara zote nzuri na kila kitu kusudi uwapate watu ambao watashindana Duniani. Ukitaka usambaze kwa Shule zote 2000 hutaweza kwa sababu uwezo huna. Sasa ukitaka kuondoa hata Ilbolu nayo uiuwe na Mzumbe uuwe maadam ni *Nation*, sioni sababu kwa nini isiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba Shule kama Ilbolu zinakuwa ndio *Territory National, then* unakuwa ile *the best brains* na kwa faida ya nchi yetu, wale ambao wanaweza kuendesha nchi kwa maana kwamba wana-*cope* na mabadiliko ya sasa, basi watakwenda katika Shule hizo. Hata kule Uchina kuna *Universities* ambazo wanafundisha Kichina tu, zile ni kwa ajili ya *local consumption,* zile za Kimataifa ni kwa ajili ya wale wanaokwenda kushindana na dunia nyingine. Kwa hiyo, nasi hapa tuwe na Shule zile, maadam hazibagui ni kwa nchi nzima, tuendelee nazo tukiamua kwa ghafla na kwa kisiasa tukasambaza hii nguvu tutauwa nchi kabisa, zote zitakuwa hivi hivi, watabaki *Division Four* na nchi itakuwa haina mabingwa.

Hata kwa mfano *computer* hizi huwezi kusambaza kila mahali, mahali pengine hapana umeme, hapana vifaa vyote vya lazima. Sasa ukitaka wafanye siasa, kwa kweli mamlaka shughuli zake zote ziwe na Walimu wote, haiwezekani. Hizi nyingine siyo kwa *absorbers* za kisiasa, hizi nyingine kwa ajili ya ku-*solve a problem* la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza hilo kwamba, Wizara isivunje Ilbolu wala Mzumbe badala yake iimarishe na iende hatua kwa hatua ku-grade Shule kwa madhumini hayo. Elimu siyo kama *holy communion, Padre* katika utaratibu wa *Roman*

*Catholic* akiona kipande cha mkate kimekwisha akigawa anavunja lakini kila kipande kinakuwa kama ni mkate kamili. Katika hili *we need a complete dose. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napendekeza kwamba pamoja na kwamba siyo mahali pake, hii *program ya Taken off Colleges* mbona haina mtu? Kuna *MESS* kuna MMEM lakini hii *Taken off Colleges* ni *dead,* hizi zilizopo zibatizwa ziwe *University*. Mbeya inabatizwa *University, Dar Tech.* imekwisha kwenye hadhi ya *University,* labda inabaki Arusha nayo hivyo hivyo. Hakuna hapa katikakati *program* ya kupandisha au kujenga *Technical Colleges,* kama siyo mahali pake maadam anayekaimu, Waziri Mkuu yupo hapa, basi anahusika vile vile, nadhani atusadie. Napendekeza kwamba tu-*revive* lile wazo la kuwa na *National Educational Advance or Council.* Katika Wizara ya Elimu kulikuwa na kitu kama hicho, nadhani *Board*, wakati umefika sasa kutokana na mapinduzi haya kwa kweli tuwe na kitu kama hicho.

Katika hili, labda tungezidi kwenda zaidi hivi kwenye ngazi ya Wilaya *DO* na Shule za Msingi zote zile, halafu asimamie na Sekondari sijua labda pale kungekuwa na *agent* wa *REO* kwa mawazo yale kusudi amsadie huyu *DO* ku-*monitor* na ku-*cordinate* mambo ya *Secondary School.* Kama Njombe peke yake itakuwa ni Shule 40, halafu isimamiwe na yule *REO* halafu *multiply by eight district,* kuna Shule sijui 400. Nadhani twende na mapinduzi. Mambo yanabadilika kwa kasi kiasi kwamba tusipoangali mambo yatatupita kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, si vizuri kuunda ile Tume ya Elimu tena kuangalia mambo yanavyokwenda katika dunia hii? Katika ukurasa Na.1 Waziri amem-*quote* Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, anasema hivi: "Maana ya shabaha yetu siyo kutoa elimu hafifu kuliko ile inayotolewa sasa, shabaha yetu ni kutoa elimu ya aina fulani."

Nadhani kama angekuwa hai, Hayati angesema katika mazingira ya utandawazi. Maana alikuwa anazungumzia elimu inayofaa kwa Mtanzania. Katika mazingira ya sasa, haiwezekani kuwa na kitu cha namna hiyo labda Kijiji cha sasa unazungumzia katika mazingira haya ambayo kuna *pollution*, kuna *interference* kuna madudu mengi yanaingiliana pamoja. Kwa hiyo, elimu ipi itamfaa Mtanzania, basi ni elimu ambayo ina-*cope* na mazingira ambayo tunayo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumalizia mchango wangu tena kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na kumwomba kwamba, yale mapendekezo yangu kuhusu kuboresha ngazi ya Mkoa na cheo cha *REO* hata kama ni kubadili na kumwongezea *manpower* ili aweze kusimamia mabadiliko haya ni muhimu sana. Vinginevyo mambo kama haya tutakwama tutabaki pale pale. Nia ni nzuri, lakini inawezekana isiambatane na utekelezaji mzuri. Tumefanikiwa na mafanikio haya tusipoyasimamia vizuri yanaweza tena yakaanguka maana hakuna watu wawili wanaofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba lile wazo la Hisabati kama msingi wa *science* ni lazima litiliwe mkazo. Hivi sasa Walimu wote

wanakimbia, wote wanafundisha Kiswahili, Siasa na Historia wote wanakimbia na dunia ya sasa huwezi kusomea masomo hayo bila kuwa na Hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niweze kuchangia mawazo haya na ninamtakia tena mafaniko ndugu yangu huyu na kumshauri kwamba katika dunia ya sasa ubora wa Taifa lolote lile unategemea aina ya elimu inayotolewa kwa raia wake. Tukipuuza ubora wa elimu tunajipuuza wenyewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naona kwa asubuhi hii tuishie hapo. Nina mawili tu. Moja, ni wale watakaochangia mchana waweze kujiandaa, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Janet Kahama.

La pili, wakati Mheshimiwa Philemon Ndesamburo anachangia, katika maelezo yake alisema, watu waliokuwa wanahujumu kule, akasema huu ni ushenzi. Sasa nimepata vi-*note* vinasema sasa mbona anatumia lugha inayoudhi? Sasa sijui Waswahili wanasemaje! Lakini mimi nilipojifunza Kiswahili niliambiwa kwamba ushenzi maana yake ni mtu asiyestaarabika, nilidhani sijui. Lakini ni vizuri tukakubaliana kwamba lugha hizi si nzuri sana wakati mwingine, zinaleta tatizo kidogo kanuni ya 50 kifungu kidogo cha 8(a) kinasema kwamba: “Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi.”

Sasa tatizo la hiyo unaweza ukaachiwa, lakini mwingine atakapojibu anaweza akasema kutumia neno lile ni ushenzi, sasa mkabadilishana maneno ambayo hayatakuwa mazuri sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani katika kujibu hutatumbukia kwenye hili katika kulieleza hilo. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba asubuhi Mheshimiwa Naibu Spika aliwaambia wachangiaji walikuwa 16 na kwa utaratibu wetu kipindi cha asubuhi kinaweza kuchukua watu 11 tu. Kwa hiyo, ameongeza wanne. Maana yake tutakuwa na dakika 45 tu za kuweza kupitia Kamati ya Matumizi. Kwa sababu tukimpa Waziri saa moja, inabakia dakika 45. Kwa hiyo, mjue nyie mnaochangia sasa. Kwa hiyo, nitaanza kuwaita wale walioitwa asubuhi. Mheshimiwa Bernadine Ndaboine atafuatiliwa na Mheshimiwa Milton Mahanga, atafuatiwa na Diana Chilolo na atamalizia Mheshimiwa Janet Kahama.

**MHE. BERNADINA R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mfupi, naona sitarudia yale ambayo yameshasemwa na wenzangu. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuchangia bajeti hii wakati huu wa mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nishirikiane na wenzangu kwa kumshukuru sana Waziri wa Elimu na Utamaduni na kumpongeza kwa kazi nzuri aliyoifanya kuboresha elimu nchini. Vile vile, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, namwombea Mwenyezi Mungu amrudishie afya yake ili aweze kuendelea na kazi ya kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Dr. Naomi Katunzi, ambaye ni rafiki yangu na tumefanya naye kazi pamoja. Sitawasahau Watendaji wote wa Wizara ambao wamefanikisha kuleta hotuba hii ya Wizara ya Elimu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wengi wameshauri na mimi naomba niingie moja kwa moja katika ushauri. Kwanza ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata naomba uendane na ujenzi wa hosteli hasa kwa watoto wa kike. Kwa sababu watoto wa kike ambao wanaingia katika hizi Sekondari za Kata wanatoka mbali sana na Shule hizi na hivyo kulazimika kupanga katika nyumba za Wenyeji ambazo ziko karibu. Kutokana na tatizo hili, watoto wa kike wanapambana na matatizo kama ya kubakwa, mimba zisizotarajiwa na vile vile kukosa muda wa kujisomea. Watoto wa kiume nao wanajihusisha na madawa ya kulevya na vile vile hujihusisha na ujambazi. Kwa hiyo, ujenzi wa hosteli katika Shule hizi utasaidia kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wa kumaliza Shule ya Msingi ni mdogo sana miaka 13 hadi 14. Kutokana na umri kuwa mdogo sana, watoto wanapatwa na matatizo yafuatayo:- Kwanza hasa watoto wa kike kuolewa na umri mdogo, kuzaa katika umri mdogo, kuzaa watoto wengi na mwisho hawa watoto wanapokuwa watu wazima wanapatwa na matatizo ya kiafya. Kwa hiyo, ningetoa ushauri kwamba umri wa kumaliza Shule ya Msingi uongezwe kwa kuongeza muda wa kukaa Shuleni katika Shule ya Msingi badala ya kuwa miaka saba iwe miaka tisa na umri wa Sekondari iwe miaka minne. Kwa hiyo, watoto wamalizapo Elimu ya Msingi watakuwa angalau wamekuwa kidogo kuweza kuhimili matatizo hayo ambayo nilikuwa nimeyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Walimu waishio kwenye mazingira magumu, yameshaelezwa na wenzangu, kwa hiyo na mimi ningeshauri hawa Walimu wanaoishi Vijijini waongezewe posho ili iwe motisha kwa Walimu wengine waweze kukubali wanapopangiwa kwenda Vijijini lakini Vile vile iwasaidie hao Walimu wanapokuwa wanafuatilia mishahara yao Wilayani waweze kupata fedha za kuweza kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa Walimu Vijijini ni tatizo kubwa. Nashauri kuwe na mpango maalum wa kuwasomesha watoto ambao wanatoka sehemu hizi za Vijijini kwa Mkataba kusudi wanapomaliza Ualimu waweze kufundisha katika Shule za huko Vijijini ambapo Walimu walio wengi wanashindwa kwenda kwa visingizio mbalimbali. Kuna visingizio vya imani za kishirikina hasa kule kwetu Kigoma ambapo Walimu wa kike wanaopelekwa Vijijini wanasema kwamba huwa wanashtukia usiku wamelazwa nje. Sijui kama kuna ukweli, ama sio kweli, lakini ni matatizo ambayo yanawapata Walimu ambao wanakuwa Vijijini.

Kwa hiyo, nashauri kwamba badala ya Walimu hawa kupanga katika nyumba za kienyeji, basi juhudi zifanywe kusudi waweze kujengewa nyumba za Walimu pale Shuleni. Ingawa suala hili liko katika mpango lakini kwa Vijijini iwe ni mpango wa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kugushi vyeti kwa Walimu wanaojiunga na Vyuo vya Ualimu, ni ukweli usiopingika kwamba wale wanaojiunga na Ualimu, kwa kuwa ajira ni adimu, basi wengi wanagushi vyeti kusudi waweze kusoma katika Vyuo vya Ualimu. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kuwepo na usaili kusudi hawa wanapokuwa Vyuoni waweze kufanya *interview* kuona kweli kama Vyeti ambavyo wametoa ni vya kweli.

Nakumbuka ilishafanywa Musoma ambapo kuna kijana mmoja aliulizwa alisomea Shule gani, akasema alisomea Rugambwa Sekondari. Akaulizwa Rugambwa Sekondari iko wapi? Akasema iko Mkoa wa Iringa na unakwendaje huko Rugambwa Sekondari? Akasema anakwenda kwa treni. Hii inaonyesha mara moja na inaonyesha wazi kwamba huyu mtoto hakusoma katika hiyo Shule ya Rugambwa Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine alikuwa amepata "A" katika somo la Biolojia, alipoulizwa Mwalimu Mkuu wa Shule yako alikuwa anaitwa nani? Alikuwa hamjui. Akaulizwa Mwalimu wa somo la Biolojia, akasema nimemsahau. Akaulizwa: Je, mimea inapumua kwa njia gani? Akasema *by photosynthesis.* Kwa hiyo, ilikuwa inaonekana wazi kwamba huyu Cheti kilikuwa sio chake kilikuwa ni cheti cha kugushi. Kwa hiyo, naomba usaili ufanywe kusudi kubaini wale ambao wanagushi vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa MEMKWA bado haujaanza katika sehemu nyingi hapa nchini. Nashauri kwamba kwa kuwa mpango huo haujaanza, Waziri atakuwa ni shahidi kabisa, alipokuja Mkoa wa Kigoma, kuna watoto wa miaka 14 ambao walikuwa Darasa la Tatu na Darasa la Nne lakini ni watoto ambao walikuwa wamedumaa kimwili. Kwa hiyo, walikuwa wana-*fit* kabisa katika madarasa waliyokuwemo. Kwa hiyo, kama hili linakuwepo, nashauri watoto ambao wamedumaa kimwili kwa sababu vile vile watakuwa wamedumaa kiakili waweze kuruhushwa kujiunga na Shule za Msingi pamoja na watoto wengine ambao wanaonekana wanalingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Watu Wazima kwa mpango wa MKEJA bado vile vile haujaanza hasa kule kwetu. Hivyo, tunashauri Walimu wapewe motisha ili uweze kuanzishwa mpango huo kwa sababu mpango huu wa MKEJA ndio mpango wa Elimu ya Watu Wazima ambao unawasaidia watu wazima hasa wanawake, waweze kujua kusoma na kuandika na hivyo kuweza kutatua matatizo ambayo yanawapata kimsingi kama matatizo ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia *TV,* kuna matangazo ya Hakielimu ambapo tunawaona watoto walemavu wawili wakisaidiana wao peke yao. Baadaye Mwalimu anawaambia watoto kwamba tusiwabague wale wenye ulemavu. Lakini hii haionyeshi mantiki yenyewe ya kutowabagua watoto, kwa sababu nadhani kingeongezwa kipande cha kuonyesha Mwalimu baada ya kuona kwamba watoto wenye ulemavu

wanahangaika, angeongeza kipande cha kuonyesha kwamba, Mwalimu anawachanganya na watoto wengine wanasaidiwa.

Lakini katika kile kipindi inaonyesha watoto wako peke yao tu wanahangaika, halafu tunasema “Tafakari”. Naomba kiongezwe kisehemu ambacho kitaonyesha kwamba tunawasaidia. *(Makofi)*

Vile vile kuna sehemu ambayo inaonyesha tusiwabague watoto wa kike. Mwalimu anamtuma Karani amfukuze yule mtoto mwenye mimba. Haijaonyeshwa katika elimu, tunawasaidije hawa watoto wa kike ambao wanapata mimba wakiwa mashuleni? Wengine inakuwa sio kwa sababu zao binafsi, ni kwa sababu wanabakwa na wakati mwingine wanakuwa wamebakwa na Walimu ambao wanawafundisha. Sasa naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwasaidia hawa watoto ambao wanapata mimba Shuleni waweze kupimwa *DNA* na ikionekana ni Walimu au watu wazima ambao wamewapa mimba, basi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mashuleni tulikuwa na vitu ambavyo vinamsaidia mwanafunzi kielimu kwa mfano *clubs* michezo, elimu ya afya, ngoma za utamaduni. Naomba vitu hivi vitafutiwe nafasi katika ratiba ya elimu kusudi viweze kuwasaidia wanafunzi pindi wawapo mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Lakini kwanza na mimi nichukue nafasi hii kutoa pole nyingi sana kwa ndugu, marafiki na wananchi wa Rukwa kwa kuondokewa na mpenzi wao Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Wizara ya Elimu na Utamadui kwa ujumla, kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika katika kukuza hii Sekta ya Elimu hapa nchini. Hii inaonekana zaidi katika upanuaji wa Elimu ya Msingi kwa kupitia mpango wa MMEM na vile vile *MMES* kwa kiasi fulani. Sisi watu wa Ukonga ni mashahidi wa mpango huu wa Serikali ambao kwa kweli umesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwaka 2000 tulikuwa na Shule za Msingi 26 pale Jimboni, lakini sasa kwa miaka mitano hii tumeongeza Shule 48 na sasa tuna Shule 74 katika Jimbo. Sasa hili ni ongezeko la asilimia 185 na kwa kweli kuna mengi mengine ambayo yamefanyika. *(Makofi)*

Vile vile, niipongeze Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuboresha na kulipa haki za Walimu ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kwa muda mrefu hasa Walimu Shule

za Msingi. Lakini ni vyema Serikali basi ikaangalia malalamiko yaliyopo kwa Walimu wa Shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu pamoja na Wakaguzi kama ambavyo tumeelezwa na wadau hapa ili na wenyewe matatizo yao yaweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nilitaka nizungumzie zaidi Kitengo cha Utamaduni au suala la utamaduni katika Wizara hii. Wizara hii inaitwa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Huu Utamaduni ninaozungumzia tunauelewaje? Tunautumiaje na kwa kweli maana yake ni nini hasa? Kwa sababu tunaweza tukawa tunasema tu ili kurefusha labda jina la Wizara ili liwe refu kidogo Wizara ya Elimu na Utamaduni. Lakini kwa kweli utamaduni wenyewe ambao tunauzungumzia hatuuelewi vizuri au hatuutumii. Kwa sababu utamaduni inatakiwa uwe ni utamaduni wa kuleta maendeleo ya wananchi. Je, hilo ndilo linalotokea kweli kwa sasa hivi au bado hatujathamini utamaduni katika suala zima la kuleta maendeleo katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo sera ya utamaduni ya mwaka 1997. Je, ile sera tunaitumiaje katika kuboresha hali yetu ya maendeleo ya Watanzania? Sasa hivi tunayo hata Siku ya Utamaduni tarehe 21 Mei. Tulisherehekea Siku ya Utamaduni kwa ngoma na vifijo. Je, baada ya pale ndiyo tumeshafurahi, tumekunywa tunangojea mwaka kesho tupate tena siku nyingine ya Utamaduni tusherehekee tena au tunachukua ile kama changamoto ya kuangalia na ku-*re-assess* ule umuhimu wa utamaduni katika kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni unaweza kuuchukua kwa haraka kwamba ni utambulisho wa kitaifa kwamba sisi kama wananchi tunajitambuaje. Lakini unaweza vile vile ukasema labda utamaduni ni ngoma hizi ambazo tunazicheza, michezo, maigizo, maonyesho ya asili au michoro na vinyago tunavyochonga na vitu kama hivyo ndio utamaduni huo kweli peke yake! Mimi nakubali kwamba huo ni utamaduni. Lakini twende mbele zaidi tuangalie nini hasa umuhimu wa utamaduni katika maendeleo ya nchi.

Nakubali kwamba katika suala la kukuza maadili, lazima tuangalie utamaduni wetu ili Taifa hili lisije likajiingiza katika suala zima la utandawazi na tukapotea katika kuangalia sisi tuna utamaduni gani kama Watanzania. Kwa sababu tunaangalia kwamba utandawazi kama tusipokuwa makini unaweza ukatupotezea utamaduni wetu ambao tunauzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitofautishe hapa utamaduni na hizi mila, desturi au jadi za kiasili ambazo kwa Kiingereza tunaziita *Traditions* na utamaduni ambao ni *Culture*. Kwa sababu wakati ambapo hizi *tradition,* mila, desturi au jadi ni vitu ambavyo viko *static.* *Culture* au utamaduni ni *dynamic* ni kitu ambacho kinatakiwa kiendelezwe kiboreshwe kulingana na wakati ili kuleta maendeleo. Kwa kweli utamaduni na maendeleo ni vitu ambavyo vinakwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuelewe kwamba ni vipi basi utamaduni wetu unaweza ukaendelezwa, ukaboreshwa au ukageuzwa, ukabadilishwa kwa manufaa ya maendeleo ya wananchi wetu na kuondoa umaskini. Je, katika sera zetu za maendeleo

katika nchi hii na kuondoa umaskini suala la utamaduni tunalichukuaje? Katika MKUKUTA nafasi ya utamaduni ikoje? Imeelezwaje? Tutafanya nini kwenye Sekta ya Utamaduni ili kuondoa umaskini wa wananchi? Kwa hiyo, kwa upana wake lazima tuangalie kwamba utamaduni unatusaidiaje, tumeweka mikakati gani ya kuendeleza utamaduni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wakoloni ambao walitutawala na kwa kweli hata Wakoloni Mamboleo wa sasa hivi wameshiriki sana katika kudidimiza utamaduni wa Kiafrika na utamaduni wa Kitanzania. Kwa kweli katika mipango ambayo wanatupangia sisi wa nchi zinazoendelea wamekuwa hawatilii maanani utamaduni wa Mwafrika na kwa maana hiyo wamekuwa wakipotosha ile mipango yao ya maendeleo ambayo wanataka kutuletea.

Mipango mingi ambayo inatengenezwa na hawa Wahisani na Wafadhili kwa ajili yetu inashindwa kufanya kazi kwa sababu wakati wa kutayarisha mipango hiyo hawakuzingatia utamaduni wa Waafrika au utamaduni wa Kitanzania. Kwa bahati, wao wamekuwa wakisema kwamba utamaduni wa Kiafrika ni chanzo cha umaskini. Lakini hii si kweli. Ni kwa sababu hawatumii tu huu utamaduni na sisi wenyewe hatutumii utamaduni katika kuendeleza maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba lazima tuchukue utamaduni kutoka ile *traditional culture* kwenda kwenye *modern culture*. Kwa sababu kama nilivyosema utamaduni ni kitu kinachoendelea. Tuangalie ni maeneo gani ambayo utamaduni unaweza ukaleta maendeleo kwa wananchi wetu. Nimezungumzia suala la maadili ya wananchi wetu na sasa hivi tunaangalia mambo ya *internet, TV* na kadhalika ambayo yanaweza kuharibu utamaduni wetu. Lakini kuna masuala mengine ya kimaendeleo. Chukulia kwa mfano kilimo ambacho tunasema tunataka tukikuze au Miji yetu inayozidi kukua kwa wingi, watu wanahamia Mijini, utamaduni unacheza kitu gani katika suala hilo?

Sasa tunao utamaduni kwa mfano suala la kilimo ambapo akinamama ndio walizoea kuwa wakulima, akina baba wao wanakunywa pombe, vijana wao wanacheza. Tunabadilishaje huo utamaduni wa kwamba mkulima wa Kijijini ni mwanamke na mwanamume kazi yake ni kunywa pombe na vijana kazi yao ni kucheza. Baadaye huu utamaduni wa kutofanya kazi unawafanya vijana sasa wanahamia Mijini. Miji yetu inakua: Je, ni changamoto gani tunayoipata sasa kwa sababu ya kutozingatia utamaduni huo katika kukua kwa Miji yetu ambayo inakua kuliko hata Miji mingi duniani.

Kwa hiyo, tuna changamoto hapa kwamba tunaboreshaje kilimo kwa kubadilisha utamaduni wa Mwafrika kwa wanaume kutofanya kazi au vijana kutofanya kazi? Tunabadilishaje utamaduni huu wa *extended family* ambapo vijana wengi sasa wanakimbilia Mijini kukaa kwa ndugu zao na watu wengine? Kwa hiyo, unakuta Mjini umekwenda mtu mmoja lakini watu wamekuja kumi kutoka Vijijini. Ni utamaduni wa *extended family,* tunauchukuaje na tunaufanyiaje kazi ili kutuletea maendeleo au kuleta mambo ambayo yanaweza kusaidia?

Tunao utamaduni kwenye suala la akinamama, maendeleo ya akinamama na usawa. Tumeona kwamba tuna utamaduni wa kurithi wanawake wajane, tuna utamaduni wa kuwanyima akinamama urithi wa mali, tunao utamaduni wa kuwapiga wanawake na kuwatumia kama pembejeo ya kuleta maendeleo yetu. Sasa tuna mkakati gani wa kubadilisha utamaduni wa aina hiyo ili tuweze kupata maendeleo ya akinamama na usawa wa jinsia? Je, katika sera yetu ya utamaduni hilo limezingatiwa au hapana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo suala la kusimamia haki na uwajibikaji. Hapo zamani tulikuwa na Mabaraza ya Vijiji, Mabaraza ya Wazee ya Watemi au Wakuu wa Kaya, Wakuu wa Ukoo. Je, utamaduni huu umetusaidiaje? Sasa hivi tumekwenda mpaka tumepanua kidogo tumefika kwenye Mabaraza ya Vijiji, Mabaraza ya Vitongoji au ya Kata. Ni katika kuendeleza huo utamaduni kwamba yale Mabaraza ya kiukoo yalikuwa yanasaidia kuliko hata hizi Mahakama za sasa hivi. Sasa hivi ndio tunapanua hiyo, tunakwenda kwenye Mabaraza ya Kata. Hawa Askari Sungusungu ni katika kuendeleza utamaduni wetu wa kujilinda wenyewe. Je, tunaiboreshaje hiyo ili tuweze kupata maendeleo endelevu zaidi? Hata utamaduni wa kuchangiana kidogo kidogo, umaskini wetu tunachangiana. Tunao huo utamaduni toka mwanzoni, tunauendelezaje?

Watu waliokuwa wanakunywa pombe kwa kutumia ile *calabash* au kibuyu sijui inaitwa mboko, kwetu Wajaluo Profesa Sarungi atanisaidia wanatia "Agwata", mnatumia ile mna-*share* ile kidogo kidogo, sasa: Je, tunautumiaji huu utamaduni ambao ni wa kusaidiana? Lakini ndio huo tunauendeleza sasa hivi. Kuna vocha ya *vodacom* ya Sh.1,000/= unamgawia mwenzako Sh. 500/=, ndio utamaduni huo! Je, tunaiendelezaje hiyo katika kuhakikisha kwamba umaskini wetu tunashirikiana kwa pamoja?

Lakini utamaduni wa kupenda kazi. Tumekuwa na utamaduni ambao kuna watu hawapendi kazi. Sasa hivi tunapiga kelele humu Bungeni kwamba kuna maeneo ambayo sijui Mtwara, Kigoma, Lindi maendeleo ni hafifu tuongeze bajeti. Sawa!! Tunaweza tukaongeza bajeti, lakini je na sisi kwenye maeneo hayo, utamaduni wa kufanya kazi tumeutiliaje maanani? Tunasema Wachaga wao ni wafanyakazi wazuri, wana moyo wa kufanya kazi, kwa hiyo, wanaendelea. Sisi wengine je? Tunajifunza nini kutoka kwa Wachaga na kutoka kwa Wakinga?

Sasa Wanyakyusa pale Mbeya wanajifunzaje kwa majirani zao Wakinga? Pale Segerea kuna kijana mchoma nyama kwa miaka 12 yeye anatoka Mbeya. Miaka 12 anachoma nyama, mishikaki mitamu kuliko mahali popote Dar es Salaam. Lakini kwa miaka 12 hajajenga na wanasema angekuwa Mchaga ndio mchoma nyama pale angekuwa sasa hivi ana ghorofa tatu. Sasa je, utamaduni huu wa Kichaga, Kikinga tunajifunzaje? Tumewekaje kwenye sera ya kujifunza? Sasa unaona kwamba hawa Wachaga wana mwamko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye siasa, sasa hivi pale Dar es Salaam naambiwa kuna Wachaga kama sita au watano wanagombea Ubunge pale Dar es Salaam. Sasa wanao kumbe mwamko wa kisiasa na biashara. Sasa je tunaigaje? Hata kwenye lugha tunatumiaje lugha katika kukuza utamaduni wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yote na ya dini, kwa mfano kwenye dini utakuta tunao utamaduni wa kuamini kwamba ukichangia kwenye dini au kwenye ukoo, harusi na nini unapenda, unaona kwamba ni vizuri zaidi kuliko kuchangia Serikali.

Unakuta kwamba labda kama Kanisa au Msikiti unajenga Shule waumini watachangia zaidi pale kwa moyo kuliko unavyochangia Serikalini, kujenga Shule hivyo hivyo. Je, ni kwa sababu gani? Ni imani waliyonayo pale. Je, tunajengaje hii ili wananchi vile vile wapende kuchangia hata Serikalini kama wanavyochangia kwenye dini? Ni kubadilisha ule utamaduni uweze kufika mahali ambapo hata Serikali unaona kwamba unasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kutumia uganga wa kienyeji, kutibu ni utamaduni. Kwa hiyo, nataka kusema, tuangalie Sera ya Utamaduni, lakini tuhusishe wadau wote toka juu mpaka chini. *NGOs,* watu kwenye *level* ya kaya ili tuweze kuangalia mambo gani ya kiutamaduni ya Kitanzania ambayo tunaweza tukaendeleza na tukawa na maendeleo endelevu. Ninachotaka kusema, sera ya utamaduni bado haijaangaliwa vizuri, tuiangalie itusaidie kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DIANNA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mmoja wa wachangiaji katika Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi ya awali kabisa kwa masikitiko makubwa kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Marehemu Margareth Bwana. Naomba rambirambi hizi ziwafikie wazazi, watoto, kaka zake, ndugu na marafiki pamoja na Wapigakura wake. Mungu aiweke mahali pema roho ya Marehemu Margareth. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya rambirambi hizo, nitumie nafasi hii kwa kuipongeza bajeti. Kwa kweli bajeti ni nzuri. Mheshimiwa Waziri kazi zake zinajulikana ni nzuri kwa kipindi chote cha miaka mitano ambayo nimekuwa naye hapa Bungeni na a-*appreciate* kazi yake. *(Makofi)*

Vile vile, niipongeze bajeti iliyosomwa leo hapa, ni nzuri na ina mwelekeo mzuri kabisa kwamba mtazamo wa mwaka huu sasa utakuwa ni mzuri katika kuinua elimu na mambo yote ya elimu kwa ujumla. Baada ya pongezi hizo ambazo walengwa wake hasa ni Waziri Mheshimiwa Mungai, Naibu Waziri, Ndugu yangu Mheshimiwa Sakila, Katibu Mkuu mwanamke mwenzangu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo za bajeti, sasa nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali, kwani ilishawahi kuteua wataalamu kwenda kuhakiki madeni ya Walimu Shule za Msingi. Baada ya kuhakiki madeni hayo, ni vizuri zaidi Serikali pia

ikatoa Tume ambayo iliongozwa na Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwenda kuhakiki madeni hayo pamoja na kero nyingine za Walimu.

Nashukuru kazi iliyofanywa na Tume hii imeleta matunda makubwa kabisa kwa Walimu wa Shule za Msingi kwa sababu madeni mbalimbali yamelipwa na bado yanaendelea kulipwa na ninaomba madeni hayo basi yaendelee kulipwa mpaka ifike hapo madeni yaishe labda ifike wakati waende na wakati, maana yake wawe na madeni mapya sio madeni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuongea juu ya kero za Walimu wa Shule za Sekondari, Walimu wa Vyuo vya Elimu, pamoja na Wakaguzi wa Shule. Hawa wenzetu wamesahaulika katika kulipwa mapunjo yao. Wanadai fedha za matibabu, wanadai fedha za likizo, fedha za safari na madai mbalimbali mengi tu. Lakini nashangaa Serikali haijaona umuhimu wa kuwalipa Walimu hawa madeni hayo.

Madeni haya yanahakikiwa Ofisini, ni lini Mwenyekiti ukaona kazi ya kuhakiki madeni kwenye mafaili? Naiomba Serikali iteue Kamati iende Mashuleni ihakiki madeni ya Walimu katika Shule za Sekondari, Walimu wa Vyuo na Wakaguzi wetu.

Chama cha Walimu kishirikishwe kama kilivyoshirikishwa kwenye madeni ya Shule za Msingi. Nakipongeza pia Chama cha Walimu, kinafanya kazi nzuri, kimekuwa karibu na Walimu wao na kimekuwa kikiwasimamia kwa hali zote.

Lakini nashangaa Serikali inaziba masikio kwa hili. Hatuwezi kufanya kazi kwa kutumia mafaili. Kamati iende, ihakiki madeni Waalimu walipwe, tusiwakatishe tamaa Waalimu wetu kwa sababu ni haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kwa kuipongeza Serikali kuhusu mpango wa MMEM. Mpango huu kwa kweli ulikuwa ni mzuri sana, pamoja na kwamba palikuwa na mapungufu madogo madogo. Sasa unakuja mpango wa MMES, naiomba Serikali mapungufu yaliyojitokeza kwenye mpango wa MMEM kwenye MMES yasijitokeze. Kuwe na *transparency* ya pesa zinazokwenda mashuleni, Kamati za Shule zipewe elimu. Hawawezi kukagua matumizi ya pesa watu wasiokuwa na taaluma waelimishwe, wapewe hata Semina za wiki mbili kama walivyofanyiwa Waheshimiwa Madiwani, wakawa na uwezo wa kuhakiki pesa za Halmashauri zao. Nina hakika hata Kamati za Shule zikipewa elimu zitaweza kufuatilia pesa zinazokwenda mashuleni na mpango wa MMES utakuwa na mafanikio makubwa kwa nchi yetu kama tulivyopata mafanikio katika mpango wa MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie muda huu pia kuikumbusha Serikali katika Waalimu hao hao wa Sekondari, wa Vyuo pamoja na Wakaguzi, wapo ambao wanaidai Serikali, walipandishwa vyeo, wamepanda madaraja, lakini wana malimbikizo ya madai ya mishahara yao kutoka mwaka 2000 mpaka leo 2005. Kwanini Serikali isione

hili? Walimu wanakata tamaa, Waalimu na taaluma zao wananyanyasika, wanakuwa wanyonge, wanavunjika mioyo kwa sababu ya kutokukumbukwa katika haki zao za msingi. *(Makofi)*

Nina hakika kupitia Bunge hili, leo Waalimu wa shule za Sekondari na Vyuo na Wakaguzi watasikia wataambiwa nini hapa. Nataka tusikie wanaambiwa nini? Kwa sababu habari ya kuulizauliza Wabunge huko, sasa tumechoka, tena Bunge lenyewe linavunjwa keshokutwa, ni bora mkasema hapa hapa wakajisikilizia wenyewe kwamba haki zao za msingi watazipataje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kwa kuikumbusha Tume ya Utumishi wa Waalimu *TSD*, Tume hii nayo imekuwa ni kero kwa Waalimu. Wastaafu wengi, wengine wanaofuatilia mirathi ya Waalimu waliofariki wanakwenda mpaka kwenye Tume hii, wanaambiwa kumbukumbu zimepotea, kumbukumbu zinapotelea wapi? Mwalimu mhusika alishafariki, leo msimamizi wa mirathi atazipata hizo kumbukumbu, kama sio kutaka kuwanyima haki za msingi warithi wa Marehemu ama Waalimu wastaafu? Hivi ni wangapi wenye uwezo wa kufuatilia mambo haya mpaka Dar es Salaam? Naiomba sana Serikali ifuatilie Tume hii iwatendee Waalimu haki, wahakikishe kumbukumbu zinawekwa bayana mapema kabla ya muda wa Mwalimu wa kustaafu haujafika. *(Makofi)*

Kama Mwalimu anapewa taarifa ya kustaafu mwaka mmoja kabla, kwanini kumbukumbu zake zisiwekwe kwa muda huo wote ili anapostaafu tu, haki yake ya msingi aipate? Tunakaa tunapiga kelele tunailaumu Hazina hapa, lakini vile vile na Tume yetu inachangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kuomba Walimu waheshimiwe, wathaminiwe na watambuliwe. Ni kweli wapo Maafisa wengi wanaowathamini Walimu, wanawaheshimu, wanaongea nao lugha nzuri za mapenzi za kuelekezana. Lakini vile vile wapo wenye lugha mbaya. Mwalimu ni binadamu, anahitaji aheshimiwe, kama kuna lolote aelezwe kwa utaratibu unaofaa. Kuna Walimu wanaokemewa kama watoto, hata watoto sasa hivi wanakataa kukemewa na wazazi.

Wanakubali kukemewa pale wanapoona wamekosa. Naomba Waalimu waheshimiwe watambuliwe, itumike lugha ya kistaarabu katika kuwaelekeza na vile vile Waalimu niwakumbushe kupitia hadhara hii, tumieni chombo chenu cha kujadiliana na Mwajiri, mnapoona hamtendewi haki, mna chombo chenu. Habari ya kulalamika pembeni imeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie pia nafasi hii kuikumbusha Serikali, kwamba mimi mwenyewe hapa nilikuwa Mwalimu. Hapo nyuma tulikuwa na kitu kinaitwa *Teaching Allowance*. Hiyo *Teaching Allowance* ilikuwa inawasaidia Walimu kwa sababu Mwalimu anafanya kazi katika mazingira magumu. Ile chaki peke yake ni ugonjwa kwa Mwalimu. Ni Walimu wengi wanastaafu wameathirika na chaki, Waalimu wanakaa Vijijini wengi wanashindwa wanaacha kazi kwa sababu hawapati hata pesa ya mazingira magumu. Hivi Mwalimu na Daktari wana tofauti gani? Ninaomba Walimu

wafikiriwe kupewa kifuta jasho, yaani *Teaching Allowance.* Ni haki yao ya msingi kabisa, ili kuwatia moyo waweze kufanya kazi vizuri kama mwajiriwa mwingine wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali sasa imetambua Shule yetu ya Walemavu ya Singida Mjini, inaitwa Tumaini Shule ya Msingi. Ni Shule ambayo tayari sasa imeshaanza kupata mgao wa Serikali, naishukuru sana Serikali. Lakini mgao huo hautoshi. Naomba Serikali itambue kwamba Shule hiyo ni mpya, inahitaji vifaa vingi kwa sababu ni mpya. Naomba basi, Serikali itoe fedha za ziada kuhakikisha kwamba Shule hiyo inakuwa na vifaa vya kutosha ili iweze kufanana na hadhi ya Shule hiyo. Wanafunzi walemavu hawawezi wakafundishwa vilivyo bila vifaa. Wale wanahitaji vifaa kwa sababu ni walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Serikali kwa hili itakuwa imenisikia na itaona umuhimu wa kutoa fedha za ziada kwa ajili ya Shule ya Tumaini iliyopo Singida Mjini ili iweze kufanana na Shule nyingine za Walemavu na ili iweze kufanya kazi yake kama ilivyotarajiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naiomba Serikali ianze kutoa mafunzo kazini kwa Walimu wa miaka mingi kwa sababu, kuna hii mitaala mipya, Waalimu wengine hawaielewi, Waalimu wameshakuwa miaka mingi kazini kwa hiyo, semina, warsha na mafunzo yatolewe kwa ajili ya Walimu hawa ili waweze kwenda na *syllabus* hizi mpya. Taaluma zinaanza kutolewa bila utaratibu kwa sababu ya Walimu kutokuzielewa *syllabus* hizi vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niongee kuhusu ruzuku ianayotolewa na Serikali kuhusu watoto wasiokuwa na wazazi na watoto wenye wazazi wasiokuwa na uwezo. Naishukuru Serikali kwamba inasomesha baadhi ya watoto katika Halmshauri zetu ambao wazazi wao walishafariki ama wazazi wao hawana uwezo. Lakini si watoto wote wanaosemeshwa na Serikali, naomba Serikali ibebe mzigo huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Tunawagawa watoto, wote hawa wanahaki sawa, wote wamefiwa na wazazi wao, wote wazazi wao hawana uwezo, hii habari ya kusema kwamba hawa wanasomeshwa na Halmashauri, kuna Halmashuri nyingine hazina uwezo, zina mapato duni. Kwa hiyo, watoto wao hawapati stahili yao na watoto wanaendelea kuwa wengi waliofiwa na wazazi ama wenye wazazi wasio kuwa na uwezo. Kwa hiyo, Serikali hapa naomba isijikanganye, ukiyavulia maji nguo, yaoge*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sitaki nigongewe kengele ya pili, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia nafasi. Samahani kidogo sauti yangu ni ya kikohozi. Baada ya hapo mimi naomba nianze kabisa moja kwa moja kuunga mkono Bajeti hii na ipite moja kwa moja. *(Makofi)*

Naomba nimpongeze Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi chote hiki, pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambaye hayupo sasa hivi, ninamtakia Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema. Naomba pia nimpongeze Katibu Mkuu, Bibi Naomi Katunzi, Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri walizofanya, maana yake kwa kipindi hiki nadhani sasa Watanzania wamekwishajua MMEM ni nini, MMES ni nini, MEMKWA ni nini na kadhalika. Wamefahamu kwa sababu wamekwishaona kazi nzuri iliyofanyika katika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kidogo nieleze tu mambo mengi ambayo nilitaka kuzungumza, yamezungumzwa na wengine na sitaki kupoteza wakati isipokuwa tunaelewa elimu ni kitu cha msingi hasa Elimu ya Msingi, ni kitu cha msingi na kikubwa sana kwa ajili ya watoto wetu wa Shule hizi za watoto wadogo.Katika mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini (MKUKUTA), nguzo mojawapo iliyowekwa ni kuboresha hali ya kuishi kwa wananchi na huduma za jamii ikiwemo elimu yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa *PEDP*, mimi ningeomba kwanza kabisa tegemeo letu limekuwa katika zile Dola 10 ambazo zilikuwa zimepangiwa tunaomba sana pesa hizi zote zifike mapema kabisa kabla ya wakati wa kuanza mihula ya Shule ili kusudi Bajeti hii ifanyiwe kazi vizuri na Wakufunzi na Kamati za Shule zinapochelewa ndipo mambo yanapochelewa. Tunaomba sana tujitahidi tujifunze kupeleke pesa hizi mapema na kufanya hivyo ni kupunguza lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa rasmi nyingine ambayo imejitokeza ni kuwa matumizi ya fedha ya elimu mara nyingi, kwanza wamesema 40 *percent* inaonyesha kuwa bado haijawafikia walengwa, haijafika mashuleni. Sasa jambo hili mimi ninaona ni jambo la muhimu sana na pia litaturudisha nyuma iwapo kutakuwa na matatizo yakijitokeza hapo katikati, naomba sana Mheshimiwa Waziri na ninaamini atarudi hapo hapo aendelee na mpango wake na alisimamie jambo hili ili kuhakikisha watoto wetu wanasoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mishahara ya Walimu. Mimi naomba kwa ufupi tu kuwa, Walimu kwa kweli wamesota sana na wameteseka sana na pia kwa kuwa mshahara wao sio mkubwa kiasi hicho, basi angalau hicho kidogo wanachokipata kiwafikie mapema kabisa ili kiwawezeshe na wao kuwa na motisha ya kufanya kazi na kufundisha watoto wetu vizuri.

Kingine ambacho ningeomba tu kwa ufupi, tumejenga Shule nyingi nzuri lakini bado naendelea kusema, ubora wa majengo ya Shule hizi naona ni kitu muhimu sana. Tafadhali sana Wahandisi wanaopewa kazi hii wafanye kazi vizuri pamoja na wananchi wafanye kazi vizuri, vinginevyo tunaweza kujenga nyumba nzuri, majengo mazuri ya Shule halafu yakashindwa kuhimili yakapotea mara moja na kuanza kubomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Elimu ya Sekondari, kuna umuhimu kabisa wa kufikiria kuziongeza Sekondari kwa haraka sana, kwa sababu ninaona tumefanya kazi nzuri ya kujenga Shule za Msingi, matokeo yake tusije tukakwamisha watoto wengi

kama nilivyosoma kwenye gazeti kwamba Kilimanjaro imekwama sana kupata Shule kwa ajili ya watoto kuingia Sekondari. Hili ni jambo lazima tulitilie mkazo sana. Bajeti ya *SEDP* imetuonyesha kuwa Shilingi trioni 1.3 zimekwishatengwa kwa kipindi cha miaka mitano, sasa katika hii mimi hapo nimesimama leo kuzungumza tu kuhusu eneo la Shule za zamani katika kujenga majengo mapya na katika kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi siku ya Jumapili, ilinikuta niko Tabora na nikapata moyo wa kwenda kutembelea Shule yangu ya zamani ya Tabora *Girls Secondary School* na Tabora *Boys Secondary School. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda vile kwa matumaini kuwa nitaona ni Tabora niliyoijua mimi zamani au itakuwa imekuwa nzuri zaidi. Kwa masikitiko makubwa na wala si uongo nilijikuta ninatoa machozi badala ya kuwa na furaha. Tulipokuwa tumeanza katika Shule ya Sekondari ya Wavulana, tulikuwa na Mwalimu Mkuu, alikuwa ni mtu mzuri ametuzungusha. Kwa kweli katika sehemu ya *lower school, it was perfect*. Tulipoingia *hall* ambalo sasa wanalifanya la *dining room* tulikuta meza chache za kulia chakula, mafomu wanayokalia wanapokula watoto yameraruka na kupasuka kiasi kuwa mtu ukikaa hata nguo yako inararuka. Kulikuwa na uchafu, hazijapakwa rangi kabisa.

Lakini kitu kilichonigusa zaidikwa kweli kikanihuzunisha pembeni ni *storage area.* Ndiyo, imetengwa kwa ajili ya malazi ya Walimu waliokosa nyumba za kukaa. Hiyo imenisikitisha sana na ni mlango ambao unaingilia kutoka *the main dining area*, ndiyo wanaingilia Walimu kwenda kulala na hizo ndiyo nyumba zao.

Kwa kweli ninakuomba sana Mheshimiwa Mungai chonde chonde wewe ni *Taborian,* umesoma pale, nakuomba sana jambo hili uliangalie vizuri sana lilituhuzunisha wote na Mwalimu alisema walikwishaomba hapo zamani Shilingi milioni 600 miaka michache iliyopita, lakini ilikuwa hawajapelekewa. Lakini hata mandhari nje, nyumba za Walimu ambazo zilikuwa zikikaliwa na *Headmaster* na Walimu wa zamani Wazungu, zile zote kwa kweli zinahitaji ukarabati wa hali ya juu. Ile nyumba ya *Mr*. Creb inasikitisha katika hali yake na ndiyo alikuwa *Headmaster* mashuhuri aliyetoa vigogo wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nikaendelea na safari yangu kwenda katika Shule ya Tabora *Girls*, hapo ndiyo ilinisikitisha sana. Kuna nyumba tano ambazo zilikuwa za Walimu wa zamani wakiwepo akina Mwalimu Mary Makeja, dada yangu na nikaenda *specifically* kuingia ndani, zimepasuka zote na zenyewe Mwalimu anasema hizo wameziweka ni nyumba za makumbusho. Sasa utawekaje nyumba ya makumbusho na huikarabati? Ni nyumba ambazo zimejengwa kwa mawe na ni ndogondogo sana. Tumetoka hapo, kitu kilichotuhuzunisha sana tena sana, ni kuwa maeneo tuliyokuwa tukisomea *science laborator*y za *chemistry* na *physics*, nusu imefungwa kabisa haitumiki kwa sababu haiwezekani hata binadamu kukaa mle. Ni kitu cha kuhuzunisha mno.

Kwa maana hiyo watoto wanakosa sehemu ya kwenda kusomea na masomo ya *science* ndiyo tunayaomba sasa hivi. Msemaji mwenzangu hapa Mheshimiwa Makwetta amezungumzia *science* kuwa ni muhimu, lakini hapa tumeshindwa.

Baada ya hapo, tukakuta sehemu ya chakula na yenyewe hali mbaya, ma-*domitory* hayatoshi na ma-*domitory* mengi yamekwishakuwa mabovu, nyumba za Walimu ni mbovu, majani ni marefu sana. Sasa sitaki kugongewa kengele ya pili. Mimi nimesimama leo kuzungumza kwa uchungu tu wa Shule hizi mbili. Nilichokuwa nikiomba sana ni kuwa Kamati ya Huduma za Jamii bado iko hapa, kuchukua kiberenge au ki-*motor trolley* ni *six hours* mpaka kufika Tabora na kinachukua watu tisa. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri katika wiki hii au ijayo tupandisheni sisi katika Kamati yetu twende kwa muda wa siku moja tukaangalie hali yenyewe tutoe ripoti nzuri kabla wenzetu hawajaja kuchukua majukumu haya amasivyo watatulaumu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tena sana *this is not a joke is something that is very serious.* Lakini kinachonisikitisha, *two days ago* katika Redio Afrika imesema kuwa Shule ya Tabora imekuwa ya mwisho katika mitihani. Ndiyo wa mwisho kufanya mitihani, tunategemea nini Mheshimiwa Waziri? Hawawezi kusoma vizuri katika mazingira niliyoyaona mimi, hawawezi kusoma vizuri. Nyuso za wasichana zilikunjika, ngua zao hazikupendeza halafu walishika vibakuli vidogo wala sio vizuri vya kwenda kuchukulia chakula. Kwa kweli niliona uchungu kwa sababu na mimi ni mama niliona uchungu sana.

Mimi naomba, sitaki mambo ya kuja kushika Shilingi hapa, lakini naomba tafadhari mtupeleke siku moja tukatoe ripoti nzuri halafu utuambie na leo kama ni hela ngapi utakazozitoa uzipange katika Shule hii yenye heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule hii imetoa watu wakubwa sana akiwemo mwenyewe Waziri Mungai, akiwemo Kahama, Mheshimiwa Mramba yupo hapo, Mheshimiwa Kapuya mwenyewe tena anatoka Tabora yupo hapo na Rais wa Bunge la Afrika ninayekaa naye hapa Mheshimiwa Mongella ametoka Shule ile na mimi mwenyewe na wengine wengi mmetoka pale Tabora na Mzee mwenyewe Kingunge yuko hapa. Sasa leo mnataka kuwaambiaje wananchi na walio nje hata hao Waingereza waliotuachia ile Shule watahuzunika kusikia wale wanafunzi mliowaacha ndiyo walishika madaraka ya nchi, lakini ile Shule imekufa kabisa.

Mimi naomba wana *Taborians* waliotoka pamoja na Wabunge wote wa Tabora wajikusanye waweke nguvu moja kuhakikisha Mheshimiwa Waziri unafanya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niishie hapo lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri alifikirie hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote kwa kazi nzuri Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu shule za wananchi za Sekondari zinazojengwa Vijijini ziko katika mazingira magumu. Walimu hukataa kufundisha katika shule hizi pale ambapo kwa sababu za kipekee Walimu wachache kuchagua/kukubali kufundisha katika shule hizo Kurugenzi ya Sekondari imekuwa kizingiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimefika Ofisi za Mkurugenzi wa Sekondari zaidi ya mara 10, kuelezea hali hii, bila mafanikio pamoja na na kupewa ahadi. Ili kufuatilia suala hili siku za usoni nimeona sasa suala sasa kuwa katika *Hansard.* Shule za sekondari zilizojengwa na wananchi katika Wilaya ya Mbulu nyingi zina maabara ya kisasa kabisa. Hii ni juhudi za wananchi na wafadhili mbalimbali. Serikali haina shule yake Wilayani Mbulu, lakini pia haijafikiria kusaidia angalau maabara moja kwa moja ya shule ya Sekondari zinazojengwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa katika maabara zitakazojengwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 angalau moja itajengwa Wilayani Mbulu na napendekeza maabara hiyo ijengwe katika Shule ya Sekondari ya Murray ambayo ina umri wa miaka 10 sasa na haina maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa Mkoa wa Manyara ni Mkoa pekee ambao hauna shule hata moja ya sekondari yenye kiwango cha *High School* wanaohusika na MMES wangeliona hili kama tatizo la pekee ili mkoa huu nao uwe na shule yenye maabara ya *A- Level.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shule ya Sekondari ya Murray, Mbulu hali ya shule hii ni mbaya. Uongozi wa Wizara unafahamu kutokana na taarifa za Bodi kuwa mwalimu mkuu mwaka jana wote amefika maeneo ya shule yake mara chache zaidi kuliko muda aliotumia kuishi Mjini Mbulu umbali wa kilometa 25. Hakuna tatizo la nyumba wakaguzi wa kanda wanafahamu kuwa mwalimu huyu ana tabia ya kupokea fedha za karo bila stakabadhi na pia ameanza kutumia vibaya fedha za MMES. Wananchi wamenituma kuwa mwalimu mkuu huyu ni vema aondolewa hata bila *(replacement)* iwapo hilo ni tatizo katika Wizara.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri, Katiba Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. Baada ya maneno hayo ya utangulizi ninaomba nichangie maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu. Kutokana na upanuzi wa Elimu ya Sekondari na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza, madarasa mapya mengi yamefunguliwa na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa walimu katika shule zote za Sekondari na Msingi. Upungufu huu usipodhibitiwa utaathiri sana ubora wa elimu nchini. Hali hii imeanza kujitolesha katika Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 Wilaya ya Kondoa ilipewa kibali cha kufungua shule sita za sekondari lakini mpaka ilipofika mwezi Mei, 2005 ilikuwa bado shule hizo hazijapatiwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba shule mpya za Mrijo, Farkwa, Msakwalo, Bukulu, Busi na Ulla zipatiwe Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za MMES, Wilaya ya Kondoa ilipangiwa kupatiwa fedha za kuboresha majengo na kujenga majengo mapya ya sekondari kama ifuatavyo:-

(a) Madarasa 54 kila moja 7 milioni sawa na shilingi 378 milioni.
(b) Nyumba 8 kila moja milioni sawa na shilingi 72 milioni na jumla ya gharama zote ni shilingi milioni 450.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri wa Elimu na Utamaduni kutamka wakati alipokuwa akijibu swali langu namba 37 kuwa Wizara imetuma fedha hii kwenda Wilaya ya Kondoa lakini mpaka sasa fedha iliyopokelewa ni kama ifuatavyo:-

(a) Madarasa 26 kila moja shilingi 7 milioni sawa na 182 milioni;
(b) Nyumba 8 kila mija shilingi 9 milioni sawa na shilingi 72 milioni na jumla ya gharama zote kuwa ni shilingi milioni 254.

Kwa mahesabu haya ni dhahiri kuwa bado fedha kiasi cha milioni 196 za madarasa 28 hazijapokelewa Wilayani Kondoa. Namwomba Waziri anifahamishe shilingi 196 milioni zilitumwa kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu mdogo naomba kutamka kuwa naunga mkono hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Moshi Mjini, nahujumiwa sana katika ujenzi wa shule na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu sehemu nyingi katika nchi hii, hutumia matofali ya kuchoma. Katika ujenzi wa shule katika Jimbo langu ni marufuku kutumia matofali ya kuchoma, ni lazima tutumie matofali ya *cement.* Nilimuuliza *Mayor* wangu kwa nini mnakataza matumizi ya matofali ya udongo, akaniambia, siyo yeye bali ni *Regional Engineer,* nilimwandikia barua lakini sasa ni mwaka mzima hataki kunipa sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa matofali ya kuchoma ni nafuu sana na wananchi wana uwezo huo. Nakuomba Waziri wakati ukifunga mjadala wako utoe ufafanuzi au msimamo wa Wizara katika utumiaji wa matofali ya kuchoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huu ufafanuzi kwani ujenzi wa shule Moshi Mjini unahujumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalamu wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika suala zima la kupambana na ujinga katika nchi yetu. Kwa kweli nchi yetu kielimu tunaendelea kupiga hatua kubwa sana. Juhudi hizi zinaonyesha stahili za wazi za kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa pamoja na juhudi kubwa inayofanywa na Wizara hii yapo mambo ya msingi ambayo ningependa kushauri ili elimu yetu iweze kupanda zaidi, kwanza, elimu inayotakiwa kutolewa isiwe bora elimu, bali iwe elimu bora. Baadhi ya watoto wetu wanaomailiza darasa la saba na kidato cha nne hadi cha sita hawajui kuandika vizuri na kusoma, uelewa wao wa mambo ni mdogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, walimu wanaofaulu toka katika Vyuo vya Ualimu wapatiwe mafunzo mengi ya vitendo *(Teaching Practice),* baadhi ya walimu ndiyo chanzo cha wanafunzi wengi kutofaulu kutokana na udhaifu wa walimu, hii inamaanisha walimu hao wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni suala la upungufu wa walimu katika nchi yetu lipangiwe mkakati sasa wa kulimaliza. Napongeza juhudi zinazofanyika lakini tulimalize kabisa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni maslahi ya walimu yatazamwe upya. Kazi ya ualimu ni ngumu sana. Muda wote unamalizika kumuandaa mtoto. Kwa maana hiyo, mwalimu hana muda wa kufanya mambo mengine yanayompatia kipato. Kwa hiyo, nashauri na kuomba yafuatayo yarudishwe, kwanza ni *teaching allowance,* pili, *house allowance,* tatu, *transport allowance* na mengine mengi ya kumpatia mwalimu motisha ili aipende kazi yake na kumfanya mwalimu ajiandae vizuri kumfundisha mtoto.

Tano, ni kuhusu elimu ya awali. Bado hadi leo hii shule nyingi za msingi hazina Shule za Awali. Elimu ya awali ndiyo msingi. Suala hili bado Wizara haijalipa uzito unaostahili. Ninasisitiza liwe ni la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhusu nidhamu mashuleni. Hali ya nidhamu kwa baadhi ya shule imeshuka sana. Hali hii inatokana na baadhi ya walimu kuwa na tabia za ovyo, uongozi mbaya, kutoelewana kati ya Mwalimu Mkuu, Walimu na Wafanyakazi. Wanaopewa ualimu mkuu wachujwe kwa makini sana uongozi legelege shule inakosa nidhamu na matokeo yake ni utoro, kupeana mimba na kadhalika.

Saba ni Mpango wa MMES. Naomba sana kuwe na kitengo maalum kutoka Wizarani kinachokagua juhudi za wananchi ndipo Serikali itoe msaada. Kutegemea viongozi wa Wilaya na Mkoa peke yao si sahihi. Yapo matatizo yanayojitokeza baadhi ya shule kutopewa majengo waliyostahili kupewa mfano shule ya Hale Sekondari imejengwa madarasa manne, madarasa hayo yalitakiwa kupauliwa na bati tu lakini wakati wa mgao wa MMES shule hiyo imepewa nyumba ya mwalimu. Shule hiyo imejitahidi kujenga nyumba tatu za walimu. Walichotaka ni madarasa. Suala hili ninaomba sana lizingatiwe shule ipewe majengo kulingana na shida yake ya wakati ule suala hilo lisipozingatiwa litakatisha tamaa wananchi.

Nane, kuwepo na bajeti maalum ya kuweka umeme shule zetu za Sekondari hasa shule zile ambazo ziko karibu na umeme wa grid kama vile Semkiwa Shule ya Sekondari, *Old Korogwe Secondary School* na Hale Shule ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa ni kuhusu idara ya Ukaguzi. Idara hii ndiyo roho ya elimu iimarishwe. Shule kama hazikaguliwi elimu itakufa. Hawana usafiri, wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitumia fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji, Maafisa, Walimu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kusimamia majukumu yake vizuri na mafanikio makubwa yanayojenga misingi imara kwa maendeleo ya wananchi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake hii nzuri yenye mwelekeo mzuri wa kimaendeleo kwa nchi yetu na wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni asilimia mia kwa mia na ninaitakia kila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo chimbuko la msingi kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake wote kwa hivyo sisi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla hatuna budi kuunga mkono na kuipitisha vizuri ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kuweza kwenda kufanya kazi na majukumu mbalimbali yaliyopangwa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mara tu bajeti hii itakapopitishwa Wizara iendelee kufanya kazi na majukumu yake yaliyopangiwa kwa mafanikio makubwa na pia kurekebisha yale mapungufu ambayo yamejitokeza huko siku za nyuma. Nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya suala lililohusu Elimu ya Msingi anasema kuwa; “Wanafunzi wa shule za msingi (Darasa la I mpaka la VII) wameongezeka karibu maradufu kutoka milioni 3.8 mwaka 1995 hadi milioni 7.5 mwaka 2005.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naipongeza sana Wizara yetu hii kwa ongezeko kubwa na lenye kupiga hatua thabiti za kimaendeleo kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara na Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania kuyathamini vizuri sana mafanikio haya kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanapata elimu iliyo bora na nzuri kwa kiwango kinachokidhi Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya mtu yeyote na nchi au Taifa na dunia kwa ujumla. Kwa hiyo, tuongeze juhudi zetu na nguvu zote katika elimu na katika fani zote za kimaisha, kiuchumi na kimaendeleo. Taaluma ndiyo msingi sahihi kwa maendeleo yoyote na kwa pahali popote au eneo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakulima na wafanyakazi wanahitaji kuwa na kwango chochote kile kinachohusiana na shughuli hiyo na wala siyo jambo sahihi kuwa elimu inahusika zaidi katika sehemu za viwanda na Taasisi zingine za Kiserikali na Kimataifa kwa kuelewa mambo fulani na yanayohusiana na Elimu ya Juu Kiufundi, Kisayansi na Teknolojia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulichangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni juu ya kuzuia ajira ya watoto nikimnukuu ukurasa wa 35 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri juu ya suala hili la kuzuia ajira mbaya ya watoto anasema kuwa; “Mradi wa kuzuia ajira mbaya ya watoto MEMKWA unaendeshwa kwa mahusiano kati ya Shirika la Kazi Duniani, Halmashauri husika na Wizara yangu.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naipongeza sana Wizara na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwepo mradi huu ambao unazuia ajira mbaya kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nautakia mafanikio mazuri na makubwa katika kufanikisha malengo yake yaliyokusudiwa. Watoto wanahitaji malezi, mafunzo, kupatiwa elimu na huduma nyingine za msingi ambazo zitawajengea misingi iliyo bora kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watoto hawa walioko katika ajira mbaya na watoto wenzao waliozagaa na kuzurura mitaani kama watashughulikiwa na kutunzwa ipasavyo na Wizara husika pamoja na Serikali yetu kwa ujumla, itatupelekea nchi yetu kuwa katika mazingira mazuri ya kiusalama, umoja, amani na mshikamano hivi sasa na siku zinazokuja. Amani na Umoja wa nchi zinapatikana kutokana na misingi imara na ya awali inayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutafanikiwa kuwaondoa watoto walioko katika ajira mbaya na wale wa mitaani na tukaweza kuwarejesha shuleni na kupewa elimu, tutajenga Taifa letu katika maendeleo makubwa ya kiuchumi na umoja na amani kuanzia sasa na huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulifanyie kazi kwa usahihi na mafaniko kama yalivyopangwa na mradi huu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulichangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ni kuwa nikinukuu Gazeti la Mwananchi la Ijumaa tarehe 01/07/2005 liliandika kuwa shilingi bilioni 30 kuboresha Sayansi Sekondari. Tunaelezwa kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni imefikia hatua hiyo kwa kutumia mabilioni ya fedha kutokana na wanafunzi wa Shule za Sekondari nchini kufanya vibaya katika masomo hayo katika mitihani yao ya kidato cha nne kwa muda mrefu. Tunaelezwa kuwa pesa hizi ambazo zinakusudiwa kuboresha Sayansi Sekondari asilimia 90 zitakotokana na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na asilimia 10 zitatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui fedha zitatumika na Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umakini mkubwa kwa msingi huo naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nichangie kwa lengo la kuboresha katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa elimu ya msingi. Licha ya kuwa kazi nzuri imefanyika, lakini bado shule nyingi hazijaanza kunufaika na mpango huo na hata zile ambazo zimenufaika bado upo upungufu wa madarasa na nyumba za walimu. Nashauri Serikali ifanye tathmini huru ya kupitia hali halisi ya utekelezaji ili kubaini maeneo ambayo hayajanufaika na mpango huo na hatimaye kutafuta fedha na kutoa kipaumbele kwenye maeneo hayo. Mfano ni Wilaya ya Mbinga ambayo ina shule 284 na baadhi ya kata zilikua hazijapata fedha hadi tarehe 30 Juni, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya awali ni mizizi ya elimu katika jamii yoyote ile. Hapa nchini na hasa maeneo ya vijijini elimu ya awali bado inapewa hadhi ya chini ukilinganisha na msisimko uliojitokeza katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM. Moja ya kero zinazojitokeza ni tozo mbalimbali za fedha wanazotozwa wazazi au walezi wa watoto wanaosoma shule za elimu ya awali wazazi wanashindwa kulipa fedha hizo na hivyo kuwafanya watoto kukosa elimu hiyo. Naishauri Serikali iondoe kero hizo na kutoa ruzuku kwa shule zote za Chekechea zinazomilikiwa na watu binafsi au mashirika ya dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanuliwa kwa mpango wa MMES hakutaleta mafanikio yanayokusudiwa endapo idara ya ukaguzi haitaimarishwa kwa kupewa vitendea kazi hasa usafiri wa kuaminika. Ofisi za Kanda za Ukaguzi haziwezi kukidhi mahitaji ya ukaguzi ukizingatia ongezeko kubwa la shule za sekondari.

Nashauri Serikali ipanue wigo wa ukaguzi kwa kufungua ofisi hizo Mikoani na hata Wilayani kwa kuzingatia idadi ya Sekondari zilizojengwa. Utaratibu wa kupeleka Ukaguzi wa Shule za Sekondari karibu utaongeza tija katika ukuzaji wa elimu ya Sekondari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha mchango wangu kwa kuishauri Wizara kutoa agizo la kuanzishwa kwa mabaraza ya kujadili na kudhibiti UKIMWI kwenye shule za msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu kufanya hivyo kwa kushirikiana na *TACAIDS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote za kudhibiti UKIMWI bado UKIMWI umewaandama sana wanafunzi na walimu kwa hiyo kuokoa kizazi kijacho lisiwe jambo la hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine tena naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa jinsi anavyoendelea kuiongoza Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa ufanisi wa hali ya juu.

Katika Wilaya ya Ruangwa ambayo ilikuwa nyuma sana kimkoa ikiwa na shule chache za msingi, jumla ya shule 31, hivi sasa imeweza kuongeza idadi hiyo mpaka kufikia shule 68. Ingawa kazi hii ilianzishwa na wananchi wenyewe kwa kuanza ukarabati wa madarasa mwaka 1996, uanzishwaji wa MMEM uliongeza nguvu ya wananchi ambayo siyo walimaliza ukarabati wa madarasa bali waliongeza pia idadi ya shule za msingi kama ilivyo hapo juu.

Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka zaidi ya mara mbili katika kipindi hili. Kilio kikubwa sasa hivi ni uhaba wa walimu. Kwa niaba ya wananchi wa Ruangwa namwomba tena Waziri atusaidie kupata walimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumpongeza Waziri kwa kuanzisha mpango wa MMES katika kuongeza idadi ya shule za Sekondari nchini. Wilaya ya Ruangwa ambayo ilikuwa na shule za Sekondari mbili tu mpaka mwaka jana hivi sasa chini ya mpango wa MMES wananchi wa Ruangwa wamejenga jumla ya shule 14 za kutwa. Kati ya hizo mbili zinafunguliwa mwaka huu.

Ni mategemeo yetu kuwa ujenzi huu utamalizika ifikapo mwaka 2007 na hivyo kuifanya Wilaya kuwa na shule za Sekondari 16. Tunaiomba Wizara ya Elimu iendelee kuunga mkono kwa juhudi hizi za wananchi. Uamuzi wa Waziri wa kuchukua jukumu la ujenzi wa madarasa utaibua tatizo la ukosefu wa kupata mazingira muafaka ya

kufundishia masomo ya Sayansi na hivyo kuongeza kasi ya Watanzania kuingia katika teknolojia ya kisasa.

Pamoja na pongezi hizi, nachukua fursa hii tena kumwomba Waziri kufanya mabadiliko kwa baadhi ya maofisa wa elimu Wilayani kama nilivyomwomba, naye akaahidi kufanya hivyo. Naamini mabadiliko hayo niliyoyaomba yatatekelezwa kabla Mheshimiwa Joseph Mungai hajamaliza kipindi chake cha Uwaziri wa Elimu.

Aidha, kwa muda mrefu tangu Wilaya kuanzishwa mwaka 1995 mpaka leo haijapata mwenye taaluma katika nyanja ya utamaduni. Tatizo hili limeifanya Wilaya kudumaa katika eneo hili. Ingawa hili siyo jukumu lake moja kwa moja, namwomba ashauriane na TAMISEMI ili kukidhi matakwa haya ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Joseph Mungai katika kipindi kinachokuja.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa huduma zenu mlizozitoa kwangu na Bunge zima kwa muda wote niliokuwa Bungeni. Vile vile naomba Mwenyezi Mungu atujalie tufanikiwe tena ili tuweze kuja tena Bungeni na kushirikiana tena. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili tangu lilipoanza, Wabunge wenzetu wengi wamefariki na kwenda mbele ya haki. Namwomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema mbele ya haki na awape subira wafiwa wote, tukielewa kuwa sisi sote ni waja wake Mungu na hatuna budi kwake kurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ukiwa ni mkutano wangu wa mwisho katika Bunge hili, nawashukuru sana wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa ushirikiano tuliokuwa nao katika muda wote tuliokuwa pamoja na kuwaombea kila la kheri na baraka katika kazi zao na Mwenyezi Mungu atujalie tufanikiwe tena katika Bunge lijalo ili tuendeleze ushirikiano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo hapo juu naomba kumpongeza sana Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi zao walizozichukua katika kazi zao na kufanya Tanzania kufikia kiwango cha juu kabisa cha kuandikisha watoto waliofikia umri wa kujiunga na shule kwa kuanza kupanga mikakati mazuri ya mpango wa Elimu ya Msingi inayojulikana kama MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze Wizara kuwa baada ya mafanikio ya MMEM hivi sasa wameendelea na mpango wa kuendeleza Mpango wa Elimu ya Sekondari inayojulikana kama MMES.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii si jambo la masihara na linahitaji imani, moyo na kuwajibika kwa hali ya juu jambo ambalo Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wameliendeleza kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi hizi zilizoonyeshwa na watendaji wa Wizara hii, ipo kila haja na haki ya kuwapongeza watendaji hawa kwa kila hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya maendeleo yote haya mbali na juhudi za Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote ni lazima ili kufanikiwa kunategemea ushirikiano wao na wafanyakazi wengine hasa walimu ambao ndiyo wanaokaa na kuwafundisha watoto wanapokuwa shuleni na wazee ambao wana jukumu la maangalizi na ulezi wa watoto nyumbani pamoja na kufuatilia ipasavyo mafanikio ya mipango yote hii ya MMEM na MMES. Jambo hili limetendeka vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote haya lakini ili kufanikiwa na mipango hii lazima kuwa na nyenzo ambazo ni fedha za kuendesha shughuli zao hivyo kutokana na hotuba ya bajeti iliyowasilishwa mbele yetu hii leo kuna kila sababu ya kuiunga mkono hotuba hii na kwa imani kabisa na kuitaka Serikali bila ya kikwazo kuipatia Wizara hii fedha zote zilizoombwa bila ya kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Wizara imeomba fedha zake kulingana na pato la Serikali, ipo haja ya kuona umuhimu wa elimu kwa nchi yetu ya Tanzania ili kuwa na maendeleo, tukizingatia kuwa kuwekeza katika elimu ndiyo njia pekee ya kuiendeleza nchi katika ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hii naona kuwa katika miaka ijayo, Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kuwa inaipatia Wizara hii fedha zaidi ili iwe na uwezo zaidi ya kuwatayarisha vijana wetu na Maendeleo ya Elimu na matayarisho ya kuendelezwa kwa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moyo wa binadamu una wivu, wivu ni uchoyo lakini vitu hivi vikiambatana na mafanikio ni faraja na vikiambatana na husuda na ufisadi huwa karaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaona wivu wangu ni wa mafanikio kwa hivyo ninachokiomba ni kuona kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni ya Tanzania Bara, ishirikiane na Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar katika mipango yao ili Tanzania yote tuwe na mwelekeo mmoja wa kuwatayarisha vijana wetu kwa Elimu ya Juu licha ya kuwa na Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri katika suala zima la elimu, kwa muda mrefu Mheshimiwa Waziri amemudu kazi katika Wizara hiyo ngumu lakini

kwa ufanisi sana ameshirikiana na Wabunge vizuri kila tatizo lenye kutakiwa ufafanuzi alitusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wakurugenzi wake Elimu ya Sekondari na Elimu ya Msingi wamefanya vizuri sana katika kufanikisha mipango ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu ujenzi wa hosteli katika shule ya Maposeni na Mapilimbi, Songea Vijijini. Tunashukuru sana Ubalozi wa Japan kujenga Hosteli ya Wasichana *Maposeni Secondary School* ingawa mkataba wa ujenzi huo unahusu pia Serikali kuweka vitanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana ni mwaka wa tatu bweni limeisha lakini bado Serikali haijaweka vitanda katika bweni hilo, inasikitisha. Naomba Waziri atuambie ni lini sasa Serikali itaweka vitanda kwani Ubalozi wanataka kufungua bweni na bado Serikali haijatimiza ahadi. Vile vile kwa muda mrefu sasa Sekondari ya Mpilimbi imejengwa kwa nguvu za wananchi na sasa wameshajenga bweni, wanashindwa kumalizia mambo madogo madogo Serikali inasemaje? Shule hizo zote ziko katika Wilaya ya Songea Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *vote 1001 sub vote 4325 Improvement Perf of Girls in Secondary School,* tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kufahamu kifungu hicho chenye shilingi 458,178,400/= zinatumikaje katika ku-*improve performance of Girls in Secondary School* na mgawanyo kimkoa ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mimba kwa watoto wa kike, wako watoto wadogo wanaopata mimba wakiwa *Primary School,* hawa angalau wanaweza kuendelea hata kwa MEMKWA lakini Serikali inasemaje kwa wale wanaopata balaa hilo wakiwa Sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja na naipongeza sana Wizara kwa kusimamia vizuri Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na imeandaliwa vizuri sana. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake wote. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mgao wa fedha za MMES, kuna shule moja katika Jimbo langu inaitwa Kashishi. Hii ilipangiwa fedha za madarasa mawili na nyumba ya mwalimu moja. Tunashukuru tumepata za madarasa mawili bado fedha zile za nyumba moja ya mwalimu yaani shilingi milioni tisa. Tunaomba nazo zitumwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kujenga viwanja vya kisasa vya michezo Kijiji cha Michezo na pia *Sport College,* ni muhimu michezo shuleni

ikaimarishwa ikiwemo pamoja na kurejesha mashindano ya michezo ya shule na vyuo katika ngazi zake mbalimbali. Ni muhimu tutambue kuwa michezo sasa hivi ni ajira na ni uchumi zingatia Tony Blair, Chirac na kadhalika sasa hivi wako Singapore kuomba *Olympics.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kwa njia ya maandishi kuiomba Serikali kutoa ufafanuzi juu ya wanachuo waliorudishwa mwaka jana ambao tayari walishajiunga na mafunzo na sifa walikuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule nyingi za msingi hususani za vijijini bado zina shida ya walimu, wapelekwe wanachuo wengi vyuoni ili upungufu huo uishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba niishauri Serikali juu ya mafunzo ya walimu wa shule za sekondari ya wiki tatu. Ukweli mafunzo haya hayatoshi, ni kupotosha elimu ya sekondari kama ni uhaba basi elimu itolewe hata ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya na kukuza elimu nchini na kuboresha mazingira ya Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi yafuatayo:-

Malipo ya walimu ambayo yamelimbikizwa kwa muda mrefu bado hayajafanywa vizuri ingawa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kulipa kwa kiwango kikubwa. Wilaya ya Mbarali kuna walimu walioorodheshwa katika kulipwa posho za nauli (usafiri), likizo na uhamisho wamejikuta majina yao hayarudi na hawakupewa sababu za kutokulipwa mpaka sasa hawajajua hatma yao.

Mazingira ya kazi kwa wakaguzi wa shule bado ni mabaya sana, kuanzia ofisini hasa usafiri ambao ungewafanya wafanye kazi zao mapema. Mazingira ya Mbarali ni magumu sana yanahitaji usafiri wa gari ili wafanye kazi yao vizuri. Naomba Wizara ifikirie angalau Mbarali ipate usafiri wa gari kwa ajili ya Wakaguzi wa Shule (Elimu ya Msingi).

Kuhusu majengo ya MMEM Wilaya ya Mbarali, Wilaya ilianza na maombi ya Idadi ndogo ya Madarasa (vyumba 61), awamu ya pili wananchi walipata mwamko mkubwa na kujenga majengo mengi. Sasa yamebaki bila kuezekwa vyumba vinavyozidi 160. Naomba kujua hatma ya madarasa haya itakuwaje kwani zinazoletwa zinakuwa ni kiasi kisichotosheleza.

Nashauri Serikali au Wizara ifanye tathmini ya majengo yote haya ili pesa ziweze kupelekwa kwa kufuata mahitaji ya kila Wilaya ili kukuza mwamko huu wa kuchangia kwa wananchi.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa leo. Kwanza naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake. Pili, naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Elimu na Utamaduni.

Katika bajeti hii nataka kuchangia mambo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu uwiano wa walimu vijijini na mijini. Pamoja na juhudi za Serikali kuongeza walimu lakini bado kuna tatizo la uwiano usioridhisha wa walimu kwa shule za mijini na vijijini. Walimu wengi wanaopangwa vijijini hutafuta sababu mbalimbali za kurudi Mijini, hivyo shule za vijijini zinaendelea kuwa na walimu wachache sababu kubwa ya kufanya hivyo ni mazingira yasiyoridhisha ya kukosa nyumba na kuwa na ugumu wa kupata mahitaji muhimu.

Pili, ni mishahara inayolingana na wale wa Mijini. Wakati mwalimu anayeishi Mjini haingii gharama yoyote kufuata mshahara wake, mwalimu toka kijijini anakabiliwa na gharama zifuatazo katika kufuata mshahara wake ambazo ni nauli, fedha ya kujikimu kwa mfano chakula hata kama ni kwa siku moja na upotezaji wa muda kwani hana uhakika wa kupata mshahara siku ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya matatizo ya gharama, nashauri Wizara iwe na mishahara ya walimu wa vijijini na yenye kuzingatia kurejeshewa gharama nilizozitaja au la sivyo warudishiwe nauli zao pamoja na kulipwa malazi. Hii itatoa motisha kwa walimu kubaki Vijijini.

Tatu ni mazingira ya upatikanaji wa nyumba kwa walimu hata zile za kupanga. Natambua mpango wa MMEM ambao umejenga nyumba chache lakini kiwango kikubwa cha upungufu wa nyumba vijijini mpango huu hauwezi kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa kwa nini Serikali isibuni mpango wa kuwalipa posho ya mazingira magumu vijijini ili tusiendelee kuwa na upungufu wa walimu shuleni? Karibu shule nyingi za vijijini hazifaulishi kama shule za mijini kitu ambacho ni athari ya muda mrefu. Kwa tabia hii ni lini tutarekebisha tatizo hili bila kurekebisha matatizo ya walimu?

Nne ni kuhusu upotevu wa muda kwa walimu kufuata mishahara. Mpaka sasa sioni ni vipi Serikali inapunguza tatizo hili ili walimu vijijini wasiendelee kupoteza muda wao wa kuwa darasani. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ufumbuzi wa matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Kwanza, nashauri kuwa ili kuboresha elimu kuwe na mpango kabambe wa kufundisha walimu kikamilifu badala ya majuma matatu, mtindo huu wa sasa utaathiri ubora wa elimu nchini.

Pili, kasi ya ujenzi wa shule za sekondari nchini iambatane na mahitaji megine ya shule hizi. Wizara iandae utaratibu kwa madhumuni hayo. Kasi hii itazua matatizo mengi na magumu.

Tatu, shule maalum zilizopo mfano, Ilboru ya hapa nchini zisivunjwe kwani kufanya hivyo kutaua kabisa ubora wa elimu ya sekondari nchini. Zibaki za Kitaifa ila badala yake pole pole tuwe na shule za Serikali za aina nne, ambazo ni *Territorial or National* mfano, Mzumbe, Ilboru na kadhalika, *Regional, District* na *Ordinary.*

Nne, ili kukuza sayansi kwa makusudi Wizara iwe na programu ya kujenga maabara za kisasa katika shule zake zote, kufundisha watunza wa maabara. Hii ndiyo njia ya kufufua sayansi.

Tano, somo la hisabati linakufa nchini. Bila hisabati hakuna mafanikio. Katika sayansi somo la hisabati liwe ni somo la lazima hadi Vyuo Vikuu, *special* programu iandaliwe kupata walimu wa hisabati.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na pongezi kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na naomba iwekwe wazi kwenye *Internet* ya Bunge ili tuweze kuisoma duniani hata tukiwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya madai ya walimu. Bado baadhi ya walimu hawajapata madai yao naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa MMES naomba Wizara hii itupatie kiasi cha fedha zilizopelekwa kila Wilaya tupewe Waheshimiwa Wabunge wote fedha za MMES zilizopokelewa Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi ingawa pongezi haziombwi lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni bila ya aibu wala nongwa Bungeni hapa atoe pongezi kwa wafuatao, moja, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, *WEO, VEO* na Madiwani kwa kutoa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu adhabu ya viboko sheria inasemaje kuondoa kabisa viboko mashuleni au kupiga viboko kwa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyeo vya walimu. Walimu wanacheleweshwa sana kupanda madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walimu wanawake, natoa hoja kuwe na upendeleo maalum kwa walimu wanawake kuhusu malipo, vyeo, ulinzi na usalama kuepukana na wanaume wanaowafuata fuata na kuwaharibia maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wasichana wanaopata mimba, suala hili liangaliwe kwa makini sana na uamuzi uwe wa haraka. Kwanza wanafunzi wote nchini kuanzia shule za msingi hadi sekondari hakuna kutumia neno wanawake na wanaume yaani wanaume na wanawake piga marufuku leo hii kwa kimo chao ni wasichana na wavulana kwani mke huolewa, mume huoa, wasichana na wavulana hii sisitiza kweli kweli.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango niliyoutoa kwa kuzungumzia Bungeni, nimeona mchango ufuatao niutoe kimaandishi.

Kuna ubia wa kutoa *refresher course* kwa walimu wasioona kati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Chama cha Wasioona Nchini *(TLB)* ambapo shule husika zilielezwa kuwawezesha walimu kwenda kuhudhuria semeina hizo.

Kwa mfano, kwa sasa semina hiyo iko *Dodoma Inn* hapa Dodoma lakini malalamiko ni kuwa baadhi ya wakuu wa shule wamekataa kabisa kuwawezeha walimu husika. Naiomba Wizara ifuatilie juu ya agizo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ajira za sasa ni kupitia usaili hata daraja la Ukuu wa shule za msingi, sekondari na kadhalika, naomba kuishauri Wizara kuwa katika usaili suala la kuwaelekeza masuala ya wanafunzi, walimu na kadhalika wenye ulemavu lipewe kipaumbele. Hii ni kwa sababu wanapaswa angalau kuandaliwa na hali halisi watakayokumbana nayo huko kwenye maeneo yao. Vinginevyo sehemu zingine walimu wenye ulemavu wananyanyaswa bila sababu kwa vile hawaelimishwi kuhusu masuala yanayowahusu.

Hata hivyo, nafahamu kuwa kuna baadhi ya walimu wenye ulemavu ambao nao wana matatizo ya kukiuka kanuni za kazi na masingi ni kwa Wizara kutochoka kutoa miongozo na maelekezo ya jinsi wanajamii (walimu) wanavyopaswa kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara yangu Mikoani niligundua kuwa baadhi ya shule za msingi zenye vitengo maalum vya watoto wenye ulemavu wa akili, hawahesabiwi wakati wa kutoa idadi ya wanafunzi ili kuweza kupata hesabu za ruzuku ya Serikali ya *capitation fees.* Kwa msingi huo vitengo hivyo madarasa yao hayajakarabatiwa na hawapati huduma za uji, wala vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama mipira, kalamu za rangi, mwanasesere na kadhalika. Hivyo naomba maelekezo utaratibu wa kupata *capitation fees* na matumizi yake ina maana walengwa hawajui au ni mapungufu tu ya wahusika wachache?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyokumbuka Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mtwara Vijijini ni moja ya Wilaya ambayo katika shule ya sekondari tulikuwa nyuma na yeye alisisitiza mara zote tuhamasishe wananchi kujenga shule za sekondari na Serikali itawaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya hivyo na nina Kata 18 na kila Kata wamejenga sekondari toka shule moja tu mwaka 1995, wakati naanza hadi leo tuna shule 18, 7 wanasoma vijana hivi sasa na 11 zina majengo, zingine ziko kwenye kozi ya 10, zingine ziko kwenye kozi ya 7 na kadhalika.

Ninachoiomba Serikali tusaidiwe fedha za madarasa na nyumba za walimu kwa shule hizi kwa kila Kata. Fedha tulizopata karibu milioni 42 za madarasa ni chache mno na tuligawa kwa shule 4 tu kati ya shule 18 na fedha hizo hazina nyumba za walimu ni madarasa 2 tu kila shule kwa hizo 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto karibu 450 kati 1,300 tuliowafundisha tumeshindwa kuwapeleka darasani. Tunaomba tupewe fedha za kutosha kukamilisha shule zetu tunazojenga za kutosha kila Kata moja.

Pili, waruhusiwe vijana hao 450 tuwajumuishe na watakaofaulu mwaka kesho, ili mradi tuongezee fedha, tuwaingize mwakani na wenzao ili tuwatendee haki, najua hilo halipo lakini tunaomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, michezo katika shule za msingi na sekondari. Tunajitahidi kujenga shule nyingi hivi sasa, Wizara iendelee kusisitiza kufanyika mashandano ya shule mbalimbali.

Pili, utamaduni tunaomba jengo la utamaduni Busokelo lipewe utaalamu na Mkurugenzi anayehusika atembelee kituo hicho. Tunashukuru mfuko wa Utamaduni kusaidia ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, vazi la Taifa litangazwe na Wizara ihamasishe wananchi kulivaa vazi hilo. Ni jambo la kujivunia Tanzania kuwa na vazi lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naiomba Serikali iongeze bidii kwa haya yafuatayo:-

Moja, kuongeza ruzuku kwa ujenzi wa shule na nyumba za walimu wa sekondari. Walimu wana taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba ruzuku itolewe kujenga mabweni ya wasichana katika sekondari ya Urugero, Ngimu na Kijota katika Jimbo la Singida Kaskazini.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na natoa ushauri.

Moja, marekebisho ya fedha za MMES yawe kwa maamuzi ya Kamati za Ujenzi za Kata ili Kamati iwe na uhuru wa matumizi hayo. Kwa sasa walimu wakuu walezi wana maamuzi na sauti ya fedha hizo. Usumbufu wa kupewa fedha kwa mafungu madogo madogo kwa kufuata Mikoani.

Pili, kuna majengo mengi ya madarasa ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi yanahitaji kupata fedha za MMEM katika Wilaya ya Nzega. Je, tufanye nini ili fedha hizo zitumwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa utendaji mzuri wenye mfano wa kuigwa. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzito na yenye kina kirefu na maelezo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa zote za utendaji mzuri wa Wizara hii. Kero ya uhaba wa walimu ni kipingamizi kikubwa cha kutoa elimu nzuri. Suala hili lipewe kipaumbele ili tusije tukarejea tena kwenye elimu ya UPE ambayo ubora wake ulikuwa duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa upo uhaba mkubwa wa walimu katika shule za sekondari katika Jimbo langu la Lushoto. Naomba nipatiwe walimu katika sekondari za Mlongwema, Malibwi na Ubiri. Sekondari mpya ya Ngwelo haina kabisa walimu. *Headmaster* hadi hii leo hajateuliwa. Naomba hatua za dharura zichukuliwe ili shule ya Ngwelo ipate uongozi na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sekondari ya Magamba inahitaji usafiri, gari walilonalo sasa ni la mwaka 1969 naomba wasaidiwe usafiri maana shule ni ya *boarding* na iko mbali na huduma za hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Joseph Mungai, Naibu Waziri Mheshimiwa Bujiku Sakila, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya kusimamia majukumu ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kuchangia hoja yangu ambayo ni kero kubwa kwa wanafunzi na walimu wa shule ya *Tabora Girls,* shule ya wasichana ambayo iko katika mazingira magumu yanayowafanya wasome kwa wasi wasi kwa kutokuwa na usalama wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo yaliyopo yamechakaa na ni ya muda mrefu hayajafanyiwa ukarabati wa kina, kwa mfano, mpaka sasa hali ya mabweni, vyoo, vitanda, jiko na maji ni tatizo katika shule hiyo, kwani ikikumbukwa ni shule ya zamani na yenye kumbukumbu ya historia kwa Tanzania. Kwa kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya kwa kila Kata, ningeshauri pia shule zilizopo zipewe fedha kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo naomba niiombe Serikali iangalie pia suala zima la wazabuni wanaohudumia shule hizo kwa kuandaa malipo yao kwa wakati muafaka kuliko wamekuwa wakitoa huduma kwa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Serikali ijenge uzio wa shule ya wasichana angalau kwa awamu, kuliko ilivyo sasa ambapo mara kwa mara huvamiwa na wahalifu na kuibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Wizara iangalie motisha kwa walimu wanaofundisha shule za sekondari hapa nchini na kuboresha mazingira ya nyumba zao ziko katika hali mbaya. Hali hiyo inasababisha wao kuvunjika moyo wa kufundisha na kujiunga na shule za binafsi hasa wanapoona walimu wa shule za msingi wanatetewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa awamu inayokuja ningeshauri Serikali iangalie na kuweka mikakati ya makusudi kumaliza tatizo la nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari kwa kushauri *TASAF* izame katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeshauri Serikali na kuomba suala la maji ni vyema vikachimbwa visima kwenye shule za sekondari na msingi hasa vijijini, kutokana na uwezo mdogo wa wananchi ambao hawawezi kumudu gharama za uchimbaji wa visima hivyo vya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iangalie upya tatizo la wanafunzi wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni ili waweze kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Serikali kuanzisha shule za awali hapa nchini ili watoto waweze kuandaliwa vizuri.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri ambayo imejidhihirisha katika hotuba ambayo ameitoa

asubuhi ya leo. Nampongeza sana kwa hotuba hiyo na kutamka waziwazi kuwa naunga hoja mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa moyo wa upendo na ushirikiano alioutoa kwangu kwa kukubali kulitembelea Jimbo langu la Siha na kuweka msukumo mkubwa katika elimu hasa kwa shule ya Sekondari ya Sanya Juu. Kitendo cha Mheshimiwa Waziri kukubali kutumia siku nzima kuwa nasi na kushiriki katika *harambee* ya kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kinathibitisha kuwa yeye kweli ni mpiganaji ambaye amekusudia kuleta mapinduzi katika elimu nchini Tanzania. Kwa niaba ya watu wangu wa Siha naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Joseph Mungai, nasema ahsante sana.

Mwisho, napenda kuipongeza sana Wizara kwa namna ilivyosimamia miradi yote miwili yaani MMEM na MMES, ni maoni ya watu wa Siha kuwa Wizara imefanya kazi nzuri na tunaipongeza sana kwa juhudi hizo. Kupitia MMES shule za sekondari 10 mpya zimeanzishwa katika Jimbo la Siha jambo ambalo lingekuwa ni ndogo kama si mpango mzuri wa Wizara. Pongezi sana Wizara ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za kutwa ni kweli kuwa wananchi katika maeneo mengi wamehamasika kujenga shule za sekondari za kutwa.

Pamoja na nia hii njema, moja, hali ya watoto katika shule hizi ni mbaya kwa sehemu nyingi. Watoto wanaishi kwenye nyumba wanazoita *gheto.* Hali ya *gheto* ni mbaya sana na nimetembelea *gheto* kadhaa na kujionea hali ilivyo. Tusipotibu hii hali tunatengeneza bomu huko mbele, siyo kwa maana ya mimba tu lakini hasa tabia inayojengeka. Shule siyo masomo ya nadharia tu lakini lazima kuwe na malezi. Nashauri kabla shule haijaandikishwa iwe lazima wajenge hosteli kwanza kwa watoto wanaotoka pembeni mwa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, shule hizi ni nyingi lakini bila walimu wa kutosha na wenye sifa tunatia hasara kubwa kwa watoto. Kazi hii nzuri na maandalizi yapo, lakini kuwe na mkakati maalum wa muda mrefu na siyo wa *crash programme* kama ilivyokuwa sasa. Tujifunze kutoka *UPE.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Karatu High School* ina matatizo ya muda mrefu ya uongozi. Wanafunzi wameandamana mara nyingi hasa wakilalamikia uongozi mbovu na kutokuwepo kwa walimu hasa wa *Form V* na *VI.* Naomba Serikali ichukue hatua ya haraka kuokoa shule hii. Tukichelewa tunaweza kupata madhara zaidi. Nashukuru.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri wa

Elimu na Utamaduni, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam wote wa Wizara ya Elimu kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli Wizara hii imefanya kazi nyingi, asiyetaka kukubali kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii, basi lazima awe na kasoro kwenye ubongo wake. Wizara hii imefanya kazi nzuri nzuri sana hongereni na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu dogo naomba nisaidiwe walimu kwa ajili ya shule za sekondari Buziku, Katende, Chato, Buzilayombo na *Buseresere Secondary School.*

Mwisho, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, hongereni kwa kubadilisha maisha ya Watanzania kielimu. Naunga mkono hoja.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara wote kwa jumla kwa kazi yao nzuri na nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2004/2005 nilitoa kero zinazosumbua Mkoa wa Mtwara na sijui Wizara imetatuaje? Nayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, uhaba wa walimu kwenye shule za sekondari na za msingi. Pili, kukosa masomo ya sayansi, hisabati na hakuna maabara katika baadhi ya shule. Shule za Sekondari kukosa simu, umeme, maji kama Mnyambe na kadhalika. Nne, Serikali ilitamka itatoa kipaumbele kwa walimu wa Mikoa ya Kusini iwapatie motisha ya usafiri, nyumba au posho na kadhalika, je, ni motisha gani imetolewa?

Tano, walimu wasioripoti kwa maana ya kukataa kwenda Mikoa ya Kusini, Serikali ilitamka huko nyuma kwamba mfanyakazi kwa jumla ambaye hatakwenda Kusini ataadhibiwa, je, wameadhibiwa wangapi? Sita, shule za sekondari hazina usafiri wa gari na pikipiki na zina umbali wa maili 35 -45. Huruma zipi zinafanyika za kuwapatia usafiri shule zilizo mbali na Makao Makuu ya Wilaya?

Saba, watoto wa kike bado wananyanyaswa na kukosa elimu kutokana na kukatishwa elimu kwa kupata mimba na sheria zilizopo hazijasimamiwa ipasavyo kukomesha tabia hizo, hatma yake mtoto wa kike hukosa elimu stahili na hatimaye hubakia kulea mtoto na kukosa elimu na vipaji vya mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa liwe na mafanikio mbalimbali, nashauri Serikali kutilia maanani elimu ya mtoto wa kike, ana vipaji vingi ambavyo tunavipoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uendeshaji wa shule za sekondari za binafsi ziendane na sera ya Taifa na zifuatiliwe pia uendeshaji unapotetereka Serikali iweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nipongeze tena Wizara kwa mipango mizuri ya kusimamia elimu kuanzia shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi kubwa zilizofanywa na Wizara katika kuboresha elimu nchini. Hata hivyo, nina yafuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuvuja mitihani ni kubwa bado. Hili hupelekea wale wasiostahili kuendelea na masomo kwa kuwa wanaopata nafasi ya kupata mitihani kabla ni wenye uwezo na nafasi katika nchi yetu, watoto wa kabwela ambao wangefaulu na kuendelea kwa akili yao huachwa na hivi kuonekana elimu ni ya watu wenye nafasi tu! Pia hii itapelekea kupata wataalamu wasio na uwezo na hii ni hatari kwa Taifa. Pia wahitimu wetu na mfumo mzima wa elimu nchini utadharauliwa. Wizara ichukue hatua za ziada kudhibiti tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguzi wa shule mpya za sekondari hauendani na upatikanaji wa walimu. Hili husababisha watoto kwenda shuleni kucheza na si kusoma. Kwa mfano, shule ya sekondari ya Gwampu katika Jimbo la Buyungu, kuna mwalimu mmoja tu na hivi hawezi kufanya lolote. Shule ya Muhange ina walimu watatu tu na hivyo kusababisha watoto wengi kufeli mtihani wa kidato cha pili! Ingawa ni sera kwamba kila shule ya msingi iwe na darasa la awali, hili halijafanikiwa kote na pale darasa hilo lilipo uendeshaji wake haueleweki na hutegemea hisani ya mwalimu mkuu tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba walimu ni asilimia 52 ya watumishi wa Serikali, bado kipato chao ni asilimia 49 ya mishahara ya watumishi hao. Wizara ione umuhimu wao na waongezewe mishahara na marupurupu ili wapate motisha tosha kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa ujumla wake ione ukweli wa kuweka huduma za walimu wote chini ya Wizara moja badala hivi sasa ambapo huhudumiwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni, Menejimenti ya Utumishi na Umma, TAMISEMI na Wizara ya Fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za makusudi zichukuliwe ili walimu wa kufundisha masomo ya jamii - *Civics, History and Geography* waandaliwe ipasavyo kwani wengi waliopo walikuwa wamechukua somo moja tu kama somo la kufundishia, kwa hiyo, si rahisi kupata mwalimu wa mtaala mpya anayeweza kufundisha masomo hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana na pia wananchi wote kwa Mkoa wa Rukwa aliokuwa anawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze uongozi wa Wizara kwa kazi kubwa ya kuendeleza sekta ya elimu nchini. Kazi kubwa na jitihada za kutosha zimefanyika na zinaonekana kwa dhati! Pamoja na jitihada zote ambazo zimechukuliwa naomba nishauri machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza makazi ya walimu. Mazingira ambayo walimu wanaishi hususan walimu wa shule za msingi vijijini bado ni tatizo ambalo linahitaji ufumbuzi wa haraka kama kweli tunakusudia kupambana na umaskini vijijini. Tusipojenga mazingira ya kuvutia vijijini itakuwa ni vigumu walimu kwenda kufundisha vijijini na hivyo kupelekea shule nyingi kukosa walimu na hatimaye kupelekea kushuka kwa viwango vya elimu katika shule za vijijini.

La pili, ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Hivi sasa moja ya sababu inayopelekea wazazi kupeleka watoto kwenye nchi za jirani kama vile Kenya na Uganda na shule chache za binafsi ufundishaji kwa lugha ya Kiingereza katika shule za msingi. Huo ndio msingi muhimu wa kumjenga mwanafunzi anayejiunga na elimu ya sekondari kwa sababu huko lugha ya kufundishia ni Kiingereza. Tatizo hili limesababisha vijana wetu wengi waliohitimu Chuo Kikuu kutokuwa mahiri katika lugha ya Kiingereza ambayo ni muhimu katika dunia hii ya utandawazi. Kwenye ushindani wa ajira hawawezi kushindana na vijana wa nchi za Kenya na Uganda. Serikali iangalie uwezekano wa kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza katika shule zetu za msingi.

Tatu, madai ya walimu wa sekondari. Hivi karibuni Serikali iliunda Tume kufuatilia madai mbalimbali ya walimu wa shule za msingi ambayo ilikuwa kero kubwa. Tume imefanya kazi nzuri na walimu wa shule za msingi wamelipwa. Tatizo hili lipo pia kwa walimu wa shule za sekondari nchini. Ni vyema sasa Serikali ikachukua hatua ya kuunda Tume itakayoshughulikia madai mbalimbali ya walimu wa shule zote za sekondari ili nao watendewe haki kama ilivyokuwa kwa walimu wa msingi.

Nne, Serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya mpango wa MMEM na mpango wa MMES. Hata hivyo, kumekuwepo na taarifa za ukiukwaji mkubwa wa taratibu za fedha za Serikali na pia ukiukwaji wa taratibu/sheria ya manunuzi na hivyo kutoa mwanya kwa fedha za umma kutumika ovyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni matumizi ya fedha za *fumigation* kwa shule ya Sekondari Mara, Musoma Sekondari na Tarime Sekondari ambako taratibu hazikufuatwa na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa wahusika kwa vile ulaji uliwashirikisha Maofisa wa Wizara. Naomba kupata maelezo wakati Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni atakapokuwa akihitimisha hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni hoja ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi ya Jimbo la Mchinga, kuwapa pole wafiwa wote wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao katika kipindi hiki wametangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajielekeza katika maeneo mawili tu. La kwanza ni la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, alimwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa lugha yake mwenyewe a-*take note* juu ya mambo ambayo anayaona anafanyiwa njama na Mkurugenzi wake wa Halmashauri. Kwa sababu ombi lake lilimtaka Waziri kuzingatia hayo, Mheshimiwa Waziri ameyazingatia na kwa sababu tuhuma hizi ni nzito, Waziri ameona ni busara akalifanyie kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wasikie na upande wa pili unasemaje kabla ya kuweza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ningependa nijielekeze katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara hii ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, kuhusu hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wanadamu tumeumbwa kwa namna tofauti. Tupo tunaoangalia kwa macho tukayaamini tunayoyaona, lakini wapo wanaoangalia kwa nafsi wakayaona wanayoyaamini. Ndiyo maana hotuba hii ya Msemaji Mkuu imesemea zaidi mambo ambayo hayaonekani na ameshindwa kabisa kuyaona yale ambayo yapo yanaonekana ambayo kwa kweli ndiyo mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa mfano, amesema Serikali haijachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watu wengi kadri iwezekanavyo wawe wanapata fursa ya kujifunza taaluma ya Teknolojia ya Habari. Kama amesikia vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, ukurasa wa 52, somo hili sasa la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na ni la lazima kwa wakufunzi ili kuboresha mbinu za kufundishia. Ni somo vile vile la lazima kuanzia sasa kwa wanachuo wote Tarajali wa Daraja la A, maana huwezi kumwandaa mwanafunzi juu ya somo hili bila ya kuanza kwanza kwa Wakufunzi wa walimu hao Tarajali. Hili limewekwa kwenye ukurasa wa 52, lakini kwa bahati mbaya nalo hakuliona vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, amesema vile vile kwamba mafanikio katika Elimu ya Msingi eti yametokana na shinikizo la Kambi ya Upinzani katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000. Hii ni habari ya kuzua kweli kweli. Kwa sababu mafanikio haya tunayoyaona leo ya MMEM na MMES yalianzishwa wakati Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, akiwa Waziri mwaka 1990, hata Vyama vya Upinzani havijazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake ilikuja kuandaliwa wakati Waziri akiwa ni Profesa Juma Athuman Kapuya, mwaka 1995 na kuzaa programu iliyojulikana kama *ESDP* ya mwaka 1997. Lakini hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, ukurasa wa 55, ibara ya 54 kifungu kidogo cha sita inasema kuongeza idadi ya watoto wenye umri wa kwenda Shule wanaoandikishwa na wanaomaliza Shule za Msingi, malengo ya Serikali ni kuwa asilimia 85 ya watoto waandikishwe Shule ifikapo mwaka 2002, kwamba mpango huu umezaliwa na shinikizo la upinzani, shinikizo lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la msongamano kwenye madarasa ambalo Mheshimiwa amelizungumzia lipo katika ibara ya 54, ibara ndogo ya kwanza, kukamilisha miradi yote ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, madawati, vyoo vya wanafunzi na kuendelea kuwahamasisha wananchi waendelee kujenga Shule mpya za kutwa za Sekondari kwa kila Tarafa na Kata. Hili shinikizo la Kambi ya Upinzani katika mafanikio haya limetokea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza vile vile kwamba asilimia 47 ya Walimu wa Shule za Msingi ni Walimu wa *UPE,* Waalimu hawa hawajaendelezwa. Hili ni jambo la kuchekesha vile vile, kwa sababu asilimia 50 ya Walimu wa Daraja la B na C hivi sasa wako katika mafunzo maalum ya kuendelezwa kuwa Daraja la A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni tuliamua Walimu hawa wasome kutoka *grade B* na *C* kwenda Kidato cha Nne. Lakini hata wale waliofaulu tumeona hawakuwa na manufaa makubwa kwa elimu ile ya Kidato cha Nne. Tumeanzisha mpango huu wa kuwatoa *grade B* na *C* kwenda *grade A* na tunaona mafanikio yao yameanza kuleta ufanisi hata kabla programu yenyewe haijakamilika na kwa kweli sio vyema sana kudharau mpango huu wa *UPE,* kwa sababu kwa wakati ule ulisaidia sana, maana ndiyo tulikuwa tuna- *operation* Vijiji. Kwa hiyo, watoto kila mmoja alipata Elimu ya Msingi ambayo ni haki yake na ni bure kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuuchezea chezea tu, kuudhihaki mpango huu wa *UPE* wakati mwingine unatutia mashaka kama huyu ni Mtanzania mwenzetu kweli au anazungumza kwa niaba ya mtu mwingine! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge pia anasema Walimu wanaojiunga na mafunzo tarajali Daraja la A, hawana sifa na wanapata maandalizi hafifu na kwa maneno yake mwenyewe alitumia neno *trend* nafikiri alikusudia ule mwelekeo unawapa wasi wasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema ni kwamba Walimu wanaochaguliwa kujiunga na mafunzo haya ni Walimu waliofaulu Kidato cha Nne, tena kwa kiwango cha Daraja la Tatu ndiyo maana Walimu hawa hawaombi kwenda kusomea *grade A* maana wanachaguliwa kama wale wanaochaguliwa kuendelea na *Form Five* na *Six* baada ya mtihani. Ukiwa na sifa pungufu haumo, ukiwa na Vyeti bandia, haumo na tukikufuma unachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile unapimwa kama una uelekeo wa Ualimu, maana unaweza ukawa *academically* mzuri lakini uelekeo wa Ualimu ni mbovu, huendi. Marekebisho ya Mitaala hayazingatii umuhimu wa maudhui, muda wa kila somo na uwezo wa mwanafunzi. Mambo ambayo yametajwa na Mheshimiwa Mbunge kuhusu marekebisho ya Mitaala yamekuwa yakizingatiwa na kama akipata nafasi akakisoma kitabu hiki, ataona aliyoyazungumza yote yamo humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutojishughulisha na uendeshaji wa shule za chekechea na badala yake kuwaachia watu binafsi. Sera ya Elimu na mafunzo imeweka bayana suala la uendeshaji wa elimu ya awali na kwa mwaka 2004/2005 tuliomaliza juzi tarehe 30 Juni, 2005. Wizara hii iliandaa walimu bora, siyo bora walimu ili kukidhi mahitaji ya shule za awali 250 na mpango huu ni mpango endelevu, na hili limo katika hotuba ya Waziri wa Elimu aliyoitoa leo. Bahati mbaya hatuna muda wa kusoma, inaonekana.

Kuhusu wahitimu wa kidato cha sita wenye matokeo hafifu kujiunga na mafunzo ya muda mfupi ya walimu, kiwango cha kufaulu katika mtihani wa kidato cha sita kwa wanaochaguliwa kujiunga na mafunzo haya ni *principal passes* mbili katika masomo yanayofundishwa shuleni. Mafunzo haya ni ya awali ya kumwandaa ili wajiunge na mafunzo kamili ya ualimu. Kwa hivyo, wala hatubahatishi wala hatufanyi mchezo katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza hawamalizi elimu ya Msingi. Aidha, takwimu haziwekwi wazi.

Mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge afanye rejea katika kitabu cha takwimu kinachoitwa *BEST* ambacho tumegaiwa leo, atakuta hili limewekwa bayana kabisa. Hili suala la wanafunzi kuishia njiani, kwa kweli ni letu sote, wazazi, taasisi za dini na sisi Waheshimiwa Wabunge. Maana sababu nyingine wanazoishia njiani ni maadili mabaya tu ya kifamilia. Mtoto anakuja, anaposwa nyumbani kwa wazazi wake, mambo yameisha. Mimba watu wanazungumza, wanamaliza wazazi wakati sheria zipo tumepitisha katika Bunge hili. Kwa hivyo, hayo mengine ni yetu sote, lakini kwa suala la kuweka bayana, yako bayana kwenye kitabu hiki. Ningeomba akipitie kitabu hiki tena atayakuta mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wahitimu wa elimu ya msingi wanaojiunga na elimu ya sekondari ni ndogo. Idadi ya wanafunzi kwa kweli wanaojiunga na elimu ya Sekondari imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Chini ya MMES inategemewa kuwa idadi hii itaongezeka hadi kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 na kwa asilimia 100 kwa mpango wa MMEM.

Kuhusu Bajeti ndogo ya elimu, wao wakiingia madarakani watafanya asilimia 25, hivi nchi yoyote duniani inapopanga Bajeti inakuwa na mambo mawili, moja mfuko unaoitwa *Consolidated Fund,* wa madeni na nini unawekwa kando, unaobakia ambao unaitwa *National Discreational Budget* hii inakuwa ni kwa ajili ya *recurrent* kwa Wizara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa akiangalia hii kwenye kitabu hiki, ukurasa wa 85, *table 8.2,* ataona kwamba kwa hii Bajeti ukishatoa ile *Consolidated Fund,* 2004/2005, Wizara yetu ya Elimu imetengewa asilimia 37.3, yeye anataka akiingia madarakani akaturudishe nyuma kabisa kwenye asilimia 25. Sasa katika mazingira hayo wewe watu hawakurudishi madarakani hata kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema wao wakiingia madarakani wanafunzi hawatoandamana katika maandamano yoyote ila Siku ya Mtoto Duniani, sasa mimi hapa ningependa niulize, hivi mwenye mtindo huo wa kushirikisha watoto kuandamana kwenye mambo yasiyokuwa na msingi nani? CCM au wao? Maana wamefikisha mpaka uchaguzi mdogo, mtoto ambaye hajafikia hata miaka 18, amepigwa na amezikwa kwa bendera kwamba ni mwanachama wao. Mwanachama gani hajafikisha hata miaka 18? Sasa hili jambo la kwao wanawarushia CCM. Labda wanajaribu kutuambia kwamba wakiingia madarakani ndiyo sasa wataongeza kasi ya kuwashirikisha watoto. *(Makofi/Kicheko)*

La mwisho kabisa, anasema Serikali kutojali maslahi ya walimu, kutoa vitisho, kuwasimanga, kuwapuuza kwa kisingizio kuwa ualimu ni kazi ya wito na kwamba walimu tunawajali tu katika matukio maalum kama vile ikija Sensa na Uchaguzi. Haya ni maneno ya kufitinisha. Serikali imekuwa ikishughulikia maslahi ya walimu toka kuwapandisha vyeo, kulipa malimbikizo yao ya madeni na masuala ya Sensa yanapoingia wale hawatumwi tu hivi bure na yenyewe nayo wanalipwa posho zao wanazostahili kama watumishi wengine wa Serikali. Hata inapofikia kwamba ni Uchaguzi kwenda kusimamia bado wanalipwa kama watumishi wa sehemu nyingine. Lakini kwa bahati mbaya Msemaji Mkuu anafikiria kazi hii ya Sensa na uandikishaji, wanaotumiwa ni walimu peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kukamilisha hoja yangu.

Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeelo ya Vijana na Michezo, kwa kunipunguzia kwa haya aliyoyaeleza kutokana na hoja zilizochangiwa. *(Makofi)*

Katika hoja hii tukijumlisha kwa pamoja wote waliochangia mambo yanayohusu Elimu katika Bajeti mbali mbali tumepata wachangiaji 82. Katika hoja yangu peke yake wamechangia wachangiaji 40, wakiwemo 13 waliochangia humu Bungeni na 27 waliochangia kwa maandishi. Lakini katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo yanayohusu Wizara yangu yalichangiwa na Waheshimwa Wabunge 11 na katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, walichangia Waheshimiwa Wabunge 17.

Katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mambo ya elimu yalichangiwa na Waheshimiwa Wabunge 14. Kwa hiyo,

ukijumlisha wote hao ndiyo ile jumla ya 82. Wote hao napenda kuwashukuru sana kwa michango yao kwa sababu hata wakati wa Wizara hizo nyingine, Maafisa wa Wizara yangu walikuwepo hapa Bungeni, wakati mwingine mimi mwenyewe na wakati mwingine Mheshimiwa Naibu Waziri. Tumeyachukua masuala mengi ya ushauri waliyoyatoa tuweze kuyafanyia kazi. Kutokana na wingi huo haiwezekani niweze kuyajibu katika muda ulipo hapa ndani Bungeni.

Napenda basi niwashukuru waliochangia kwa kuongea humu Bungeni kwa kuwataja. Wale wengine walikwishatajwa na Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri waliokuwa wanatoa hoja hizo. Hapa napenda niwashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw'.

Ninamshukuru pia Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim wa Kambi ya Upinzani, nimshukuru Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa mwana Tabora mwenzangu Janeth Bina Kahama.

Niwashukuru pia waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa Semindu Pawa ambaye ametuletea mchango wake kwa *fax* kutoka huko aliko. *(Makofi/Kicheko)*

Pia Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa John Magufuli, Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Lydia Thecla Boma na Mheshimiwa Waziri mwenzangu niliyempokea Wizara hii Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. Wote nawashukuru sana kwa michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, napenda nigusie baadhi ya mambo muhimu ambayo nayaona yanahitaji ufafanuzi.

Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Omar Kwaangw', ambaye kwa ufasaha mkubwa sana alifafanua jambo hili la mtaala mpya ambalo limekuwa na utata na watu wakidhania ni mimi tu Waziri wa elimu wa sasa naibua mambo yangu. Lakini yeye alizama kabisa katika *record* na maamuzi sahihi yaliyotufikisha hapo. Namshukuru kwa ufafanuzi mzuri alivyotoa historia ya jambo hili. Lakini pia nimshukuru sana kwa namna

alivyofafanua vizuri sana tofauti iliyopo kati ya shule na chuo, kwamba shule inafundisha taaluma na Chuo kinafundisha ufundi, vitu hivi viwili vinabebana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma inamwandaa mwanafunzi kwa mambo yote mawili, kwanza kusonga mbele kitaaluma kutoka ngazi moja kwenda ngazi nyingine. Lakini pia inamwandaa kijana wetu kuweza kupokea ufundi vizuri zaidi. Kwa hiyo, lazima tuyatambue mambo yote mawili na kwamba katika mazingira fulani inabidi uweke uzito katika mojawapo ya hayo mambo mawili na ndio pale katika kitabu cha Bajeti tumeweka nukuu kutoka kwa Mheshimiwa Baba wa Taifa katika Elimu ya Kujitegemea pale anaposema; "macho yetu lazima yawaangalie walio wengi katika kuweka uzito." Na wakati aliandika lile andiko la Elimu ya kujitegemea, walio wengi hawakuwa wanasonga mbele kwa ngazi inayofuata ya Elimu na *data* ziko wazi katika vitabu hivi.

Hata katika vitabu ambavyo tumevitoa hapa, ukitazama katika *BEST,* kitabu kile cha *National Data.* Ukiangali mwaka 1980, darasa la saba walifanya mtihani 212,000. Waliokwenda Kidato cha Kwanza walikuwa 17,166, hao ni asilimia 4.8. Kama asilimia 4.8 ndiyo iliyosonga mbele, una asilimia 95.2 ilikuwa haina nafasi ya kusonga mbele katika kupata taaluma. Kwa hiyo, walio wengi walikuwa ni wale wasio songa mbele, ndiyo maana kulikuwa na kuingiza kwingi kwa masuala ya Elimu ya Kujitegemea katika shule za msingi. Ilitizama mazingira ya wakati ule. Lakini mambo yamekwenda yakibadilika, ukitizama takwimu za mwaka 2003, waliofanya mtihani wa darasa la saba 490, 018. Waliokwenda kidato cha kwanza 180, 239. Ukichukua asilimia ni asilimia 36. Umekwishafika *by 2003* una asilimia 36 wanakwenda kidato cha kwanza ukichukua shule za Serikali na shule zisizo za Serikali, *36 percent.*

Lakini pia tunayo sasa MMES, Mpango wa Maendeleo ya Sekondari. Tunazungumzia ifikipo mwaka 2010, wanaosonga mbele kutoka *Primary* kwenda *Secondary Ordinary Level* wawe asilimia 50 na wakimaliza *Form Four* wanaosonga mbele kwenda *Form Six* tunataka nao wawe asilimia 50 na ngazi inayofuata wenzetu wa *Higher Educationa Development Plan* watakavyoandaa, nao tunalenga wanasonga mbele wazidi kuongezeka. Baba wa Taifa anasema macho yetu yawatazame walio wengi. Unapoona mwaka 2010 utafika asilimia 50 kwa asilimia 50, huwezi ukaka na mtaala ule wa kule tunakotoka. Lazima mtaala uanze kwenda kule tunakokwenda. Ndiyo maana umekuja sasa mtaala huu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala hii mabadiliko yake hayakurupuki tu. Napenda niwarejeshe kwamba kunako miaka ya 1980 mwanzoni. Tulikuwa na Tume inayojulikana sana kama Tume ya Jackson Makwetta. Ilikuwa ni Tume maalum iliyoundwa wakati huo kutizama masuala ya elimu. Lakini Tume ya Makwetta upeo wake, ilikuwa mwaka 1980 mpaka mwaka 2000, ndiyo ilikuwa upeo wake. Ndiyo maana mapendekezo ya Tume ile yalikuja yakaleta masuala ya kuleta mchepuo na kadhalika.

Lakini ukitoka Tume ya Makwetta, uchambuzi mwingine uliofanywa *seriously* ni ile Tume Maalum ya Serikali ya Wataalam iliyoandaa *report* inayojulikana kama *The*

*Tanzania Education System for the 21st Century*. Ile Tume ndiyo iliyosema tuangalie mfumo wa Elimu yetu uweje karne ya 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayesimama na kuongea mbele ya Bunge hili ndiye Waziri wa Elimu wa Kwanza katika karne ya 21. Mambo haya tunayoyafanya tunapokuwa madarakani huwa tunakuja kupimwa na historia. Historia ingekuja kunipima vibaya sana kama nitakaa na kuna *report* inayoitwa *The Tanzania Education System for 21st Century* nikaiacha kwenye *shelves* bila kuisimamia utekelezaji wake na hicho ndicho nilichokuwa najaribu kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalam mmoja alipokuwa anafafanua, Kaimu Mkurugenzi wa *Institute of Education* alipokuwa anafafanua suala hili la mchepuo alitumia maneno haya, alisema neno mchepuo linatokana na neno chepuka. Chepuka unapata mchepuo yaani umeacha njia, ulikuwa unakwenda uko katika mkondo, mkondo wa kutoa taaluma. Lakini ukafika mahali ukakuta unalo tatizo kwa sababu taaluma unaitoa siyo wote wanakwenda mbele. Ukaamua kuchepuka kidogo, fanya na hii kazi nyingine ambayo haina mfanyaji wakati ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huchepuki halafu ukabaki umechepuka, hutafika katika safari yako. Lazima ukichepuka, urudi uanze kusonga mbele kwenye *direction* inayohitajika na hivi ndivyo tulivyofanya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawa unatoka hapa Dodoma unakwenda Morogoro, ukafika sehemu za Kongwa pale ukakuta umepungukiwa mafuta ukachepuka ukaenda Kongwa ukapate mafuta. Lakini huendelei huko huko, ukizidi kuendelea huko huko hutafika Morogoro, lazima urudi barabarani uweze kusonga mbele. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatuwezi tukabakia, wengi wa waliokuwa wanapinga suala la mtaala mpya walikuwa bado wamejikita kwenye Tume ya Makwetta. Wamejikita hapo hapo, sasa hizo ndiyo wanaita wataalam fikra za mgando. Unaganda hapo hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nilikuwa namshukuru Mwenyekiti Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwa kunifafanulia hili jambo. Nisiendelee zaidi kwa sababu naona Waheshimiwa Wabunge na wananchi wamelielewa vizuri sana.

Napenda niwashukuru na Wabunge wengine, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, kwa kunipongeza na kwa kufafanua mafanikio ya MMEM na MMES. Pamoja na matatizo yaliyopo akasema tatizo la uhaba wa kidato cha kwanza limepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nikubaliane naye kwamba pamoja na kwamba MMEM na MMES kuna matatizo mengi ambayo tunayazungumzia hapa, lakini angalau tatizo moja la nafasi za kidato cha kwanza kwa watoto wetu, limeanza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, hebu tufikirie hali ambayo ingekuwepo katika Bunge hili kama tungekuwa tuna MMEM na hatuna MMES. Haya

yote tuliyofanya na MMES yangekuwa hayajaanza, nina hakika hapa Bungeni kungekuwa na malumbano makubwa sana ya watoto walifaulu wanakosa nafasi za kidato cha kwanza. Kwa hiyo, naomba tulione fanikio hilo. Mafanikio yapo lakini na matatizo yapo. Nakubaliana na ushauri wake kwamba tuna haja ya kuzingatia zaidi mafunzo kwa walimu, akapendekeza katika vile vyuo ambata tungechukua na cha Tukuyu, Uyole KKKT na Chuo cha Marangu.

Katika hotuba yangu ya Bajeti nimesema kwamba jambo moja ambalo tunalifanya kuhusu Vyuo vya Walimu tunavitenganisha. Tutakuwa na Vyuo vya *Diploma* na Vyuo kwa ajili ya *Grade A.* Tunavitenganisha na kwenye hotuba ya Bajeti tumetoa na namba, vipi, vingapi vitakuwa vya *Diploma* na hii itatuwezesha katika hatua zinazofuata. Vyuo vile vinavyofundisha Stashahada, tutaanza kuvibadilisha kuelekea kwenye kile cha Mtwara tunachoanza nacho mwaka huu kukifanya kuwa chuo ambata. Neno ambata naambiwa ni tafsiri ya *associate.* Kitakuwa *associate College of the University of Dar es Salaam* kwa maana ya kwamba vitatoa Stashahada ile ile. Tumeanza na hicho kimoja cha Mtwara lakini tutaendelea kuviongezea vingine kwa sababu watu wa Chuo Kikuu nao wana masharti yao. Hutamki tu kwamba kimekuwa chuo ambata, lazima mbadilishe *Faculty,* mbadilishe walimu wanaofundisha na lazima mbadilishe maabara na vitu kama hivyo, waangalie watu wa Chuo Kikuu ndipo waruhusu *Diploma* yao ianze kufundishwa katika vyuo vyetu. Kwa hiyo, mapendekezo haya ya vyuo vinavyoweza kuchukuliwa kwenda katika utaratibu huo yanaweza yakashughulikiwa wakati huo.

Mheshimiwa Margareth Mkanga, namshukuru sana kwa kutukumbusha kwa mara nyingine tena masuala yanayohusu Elimu kwa Walemavu. Mimi napenda niseme kwa niaba ya wenzangu wote katika Wizara, tumesikia ujumbe wake. Najua hatujafanya cha kuridhisha, tutaendelea kujitahidi. Tumesikia mashaka aliyoayasema kwamba elimu jumuisho tusiende nayo pupa, tukadhani hiyo ndiyo aina peke yake ya kufanya.

Nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kufanya tathmini. Kama kweli kuacha shule maalum tukaingio katika Elimu Jumuisho, kweli tunatoa kwa ukamilifu Elimu kwa Walemavu hususan ndugu zetu viziwi, ndugu zetu wasioona kwamba ukiwachanganya tu shuleni wanapata elimu ya kutosha, hata mimi nina mashaka. Kwa hiyo, hilo ni jambo nakifiri inabidi tuendelee kulifanyia kazi pamoja na alilosema la elimu ya kompyuta kwa ajili ya walemavu.

Mheshimiwa Nimrod Mkono, namshukuru sana kwa pongezi zake. Lakini nilipenda nimfafanulie kidogo, katika suala la kuelekeza rasilimali katika elimu. Napenda niseme kwamba akianagalia vizuri katika *record* tulizozitoa katika *BEST* hasa kule mwisho viambataniso, ataona kwamba Serikali ya Rais Benjamin William Mkapa ya Awamu ya Tatu, kati ya mwaka 1995 na 2004 imeongeza uelekezaji wa rasilimali kutoka asilimia 2.2 ya *GDP* mwaka 1995 mpaka asilimia 4.3 ya *GDP* mwaka 2004. *That is nearly doubling.* Napenda kulinganisha, ulinganishe na wenzetu katika Afrika. Wastani wa *Sub-Sahara Africa* ni *2.4 percent of GDP* ndiyo inayopelekwa katika Sekta ya Elimu. Sisi sasa tumefikia asilimia 4.7 ya *GDP.*

Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ukiangalia katika *table 8.8* ukurasa wa 85 ya *National Data* utakuta kama asilimia ya *Discretionally Budget,* fedha ulizokusanya ambazo una uhuru nazo kuzipanga Serikali ya Awamu ya Tatu imeongeza kutoka asilimia 22.6 mpaka asilimia 37.3 kwa Sekta ya Elimu nzima. Hilo ni ongezeko zuri sana katika kipindi hiki. Katika kipindi hicho hicho tuelewe hizo asilimia ni za *GDP* inayokua. Katika kipindi hicho hicho kukua kwa uchumi kumeongezeka kutoka asilimia 3.6. Hii ni kukua kwa uchumi kwa mwaka. Kumeongezeka kutoka asilimia 3.6 mwaka 1995 mpaka asilimia 6.7 mwaka huu.

Kwa hiyo, hizo asilimia tunazozitaja ni za keki inayozidi kuwa kubwa. Kwa kweli tunapaswa kumpa hongera na nashukrani sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Sisi wengine ni watendaji wake, lakini kama alivyosema Lin Piao, alisema *sailing the seas depends on the helmsman, making revolution depends on Mao Tse Tung.* Kwa hiyo, kwa kweli ninachotaka kusema hapa, maamuzi haya makubwa yanategemea sana kiongozi anayewaongoza, anawaelekeza namna gani katika kufanya mambo. *(Makofi)*

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, kwa pongezi alizonipa. Narudia tena kusema kwamba nime-*take note* ya yale matatizo aliyoyasema. Lakini napenda niseme kwamba kwa ujumla tunakubaliana kwamba masuala ya elimu siyo *partisan.* Kwa hiyo, aliposema yeye kwamba kule wamejenga shule Kiboriloni mpaka kiwango cha asilimia 99, mimi kwa kweli kwa niaba ya Serikali nawapa hongera sana wote walioshiriki katika kujenga kwa sababu ni kwa faida ya watoto wetu wote. Sasa kama yeye anatoka chama cha Upinzani anaona mambo haya ya Elimu nafanya vizuri, basi kule Mufindi Kaskazini wasiweke mtu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mheshimiwa Anne Makinda, kwa mchango wake na kwa pongezi ambazo ulinipa. Kweli kasoro hazikosekani, tuna matatizo ya walimu, jambo hili limeelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Lakini pia napenda ifahamike kwamba katika mpango huu tulitegemea tufungue takribani shule 230. Lakini mwamko wa wananchi na MMES mwaka huu tumefungua *record* ya shule 486, haijawahi kutokea. Sasa ukiwa na shule 486 na wewe ulidhani utakuwa na 200 na kitu, *definitely* unakuwa na tatizo la walimu. Ndiyo maana tunachukua hatua mbalimbali za dharula kama vile niliposema wakati najibu swali jana, tunachukua *ex-form six* tunaendelea kuwafundisha na tunapata ushauri katika Bunge hapa kwamba tuangalie uwezekanao wa kupata walimu kutoka nchi za jirani. Ushauri wote huo tunauchukua kama kama shida hiyo itaonekana bado tunayo. *(Makofi)*

Nimshukuru Mheshimiwa George Mlawa, Mbunge wa Kalenga kwa pongezi zake na kwa *quotation* yake kutoka kwa John Maxwell kwamba, *a leader is the one who knows the way, goes the way, shows the way.* Namshukuru sana kwa kuniona hivyo, lakini napenda niseme na mimi najifunza, najifunza kutoka kwa wenzangu, najifunza kutoka kwa viongozi wangu wa humu Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu. Lakini mambo ya kitaalam, mimi nimesema siku zote si mwanataaluma ya elimu. Lakini mtu ukiwa na usomi unatambua kwamba yako

unayoyajua na yako usiyoyajua. Yale usiyoyajua unatakiwa wewe kama msomi ujue wapi pa kuyajua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilijua nilipofika pale Wizarani, Wizara ya Elimu, nizame kuchota kutoka kwa wataalam wangu. Timu yangu ya Wataalam wale pale nawashukuru sana kwa kunielimisha niyajue mambo ya taaluma na kwa msaada wao katika kusimamia masuala ya utekelezaji. *(Makofi)*

Nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa George Mlawa, kwamba umeme shuleni ni *input* muhimu sana. Tutaendelea kushirikiana na mwenzangu Waziri anayesimamia sekta hiyo ya umeme na tumekubaliana kwa ujumla utaratibu katika ule mpango mkubwa wa Benki ya Dunia wa *ruletification* kwamba unapofika umeme shuleni lazima *target* i-*target* vituo vya Afya, *Dispensaries* na shule. Isiwe tena unasema umeme uko mbali na shule. Itakuwa ni *target* muhimu, umeme unapofika kijijini, hilo tumekwisha kuelewana ndani ya Serikali.

Namshukuru sana Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa mchango wake, kwa pongezi alizonipa na kwa mapendekezo yake kwa uzito sana na hii anarudia karibu mara ya pili au mara ya tatu kwamba tupeleke madaraka ya usimamiaji wa Sekondari Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ushauri huu nimeushiba kabisa na nitajitahidi kusimamia kuhakikisha unatekelezwa na hii maana yake kuimarisha Ofisi ya Afisa Elimu wa Mkoa awe na *staff* wa kuweza kumsaidia waweze kusimamia masuala ya uhamisho wa walimu ndani ya Mkoa, walimu wa sekondari, masuala ya uteuzi wa *Headmasters,* nimeyaona tunavyoyafanya ovyo ovyo kutoka Wizarani kwa sababu shule 1,700 si rahisi kuzisimamia kutoka kwenye *centre* moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amependekeza tena tuwe na aina ya shule tusifute, ziwepo shule za kitaifa, iwepo shule katika Mkoa unayosema ni ya Mkoa inashindaniwa kwenda na katika Wilaya iwepo shule ya Wilaya. Mimi naona haya ni maoni mazuri tunayapokea yakafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza *technical education* iko wapi? Mimi nimependekeza, nadhani Mheshimiwa Jackson Makwetta, alinisikia kwamba kuna haja ya kukamilisha mapema iwezekanavyo, *Vocational Education Development Plan.*

Mheshimiwa mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, kwa hongera alizonipa. Pendekezo la kusema tuongeze Elimu ya Msingi iwe ya miaka tisa, mimi nimeona wenzetu waliowahi kujaribu kunyumbua Elimu ya Msingi, *you are not achieving much* kwa kweli, unachofanya unajaribu kuchanganya. Unachanganya elimu ya msingi na sekondari. Elimu iko katika ngazi, una elimu ya awali, una elimu ya msingi, una elimu ya sekondari, una elimu ya juu. Kila ngazi ina umri wake na mitaala imeandaliwa kwa kuangalia umri.

Kwa hiyo, ukisema tu utaita *primary* ya miaka kumi, hakuna *primary* ya miaka kumi au *primary* ya miaka kumi na mbili hakuna, una Elimu ya Msingi, una Elimu ya

Sekondari, unaoona wanazitoa kwa pamoja utakuta *primary* kuna *Head-teacher, secondary* kuna *headmaster* halafu *college.* Kwa hiyo, nadhani utaratibu ni huu na wala tusikate tamaa, tumeanza kufikia hasa Elimu ya Msingi kwa wote, tunao mpango wa kuifikisha Elimu ya Sekondari kwa nusu ya watoto wetu. Ukishafika nusu kwenda asilimia 100 ni suala la uamuzi na kuelekeza raslimali zaidi. Tusibabaike katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa amezungumzia suala la mimba kwa wanafunzi katika shule zetu. Napenda nirudie kutoa onyo kali. Tumetunga sheria kali zenye adhabu kali, lakini namshukuru sana mwenzangu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Anna Abdallah, sasa ameleta kifaa kinachoitwa *DNA,* yule anayetuhumiwa kwamba ndiye aliyempa mimba mtoto wa shule atajulikana kwa urahisi. Zamani walikuwa wana tabia ya kukataa, mimi sihusiki, lakini kifaa hicho cha *DNA* kinapima mate yako wewe uliyetuhumiwa na mate ya yule mtoto, yakikubaliana inalia kengere ngengereeee, ni wewe na ni ushahidi wa kutosha kukupeleka gerezani miaka sita. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, kwa kutueleza mafanikio ya kule Ukonga ya Mpango huu wa MMEM. Sina haja ya kurudia kwa sababu pamoja na kwamba ametoa hoja za utamaduni ni nini, lakini yeye mwenyewe alikuwa anafafanua na kutoa maelezo. Kwa kweli, kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba utamaduni ndiyo utambulisho wa Kitaifa, ndiyo utambulisho wa kwamba sisi ni Taifa, ni mambo fulani fulani tunayoyafanya yanayotutofautisha na wengine. Sehemu fulani niliulizwa nikasema kwamba, kwa kweli nchi isiyo na utamaduni ni sawasawa na uso usio na pua, utakuta haupendezi hata kidogo! Lakini ufafanuzi wa zaidi juu ya tunavyoliona sisi jambo hili utaukuta ndani ya Sera ya Utamaduni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa pongezi zake, lakini napenda nieleze kwamba *teaching allowance* siyo kwamba ilifutwa, *teaching allowance* iliunganishwa katika mshahara. Hili jambo napenda turudie tena kulisema, iliunganishwa katika mishahara ili mafao ya walimu ya *pension* yawe makubwa zaidi. Kwa hiyo, *teaching allowance* haikufutwa na hoja kwa kweli haipo maana mwalimu ameajiriwa kufundisha na anatakiwa afundishe, kinachohitajika alipwe mshahara anaostahili, kama ni mdogo tuzungumzie juu ya namna ya kumwongeza mshahara wake, la sivyo mwalimu ataomba *teaching allowance,* daktari ataomba *doctoring allowance* na kadhalika. Nadhani hatutafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kutukumbusha kuhusu shule ya *Tabora School.* Mimi nilisoma pale *Tabora Boys* na yeye alisoma *Tabora Girls,* wakati ule yeye alikuwa *Warsaw,* mimi nilikuwa kule Berlin, tulifahamiana tangu wakati huo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah! *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Ndiyo, kwa sababu pale *Tabora School* tulikuwa na utaratibu wa *social evening,* wanatoka *Tabora Girls* wanakuja *Tabora*

Boys kwa ajili ya *social evening,* mnasakata rumba na kadhalika, kwa hiyo, tumefahamiana tangu hapo mpaka leo. Kwa hiyo, *concern* yake kwa Shule za Tabora ni yangu pia. Napenda niseme kwamba katika bajeti hii tumeweka fedha za ukarabati wa shule hizi na tutaangalia uwezekano kiasi gani kipangwe kwenda katika shule ya Sekondari ya Tabora. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Omba radhi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Wengine wanasema nimwombe radhi Mheshimiwa kaka yangu George Kahama, hakuna sababu ya kuomba radhi kwa sababu nilimfahamu tangu wakati huo kama kaka yangu na nilivyojua anaelekea upande huo mimi nilikaa mbali kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda napenda nimalizie kwa kusema kwamba, nina hakika tunakubaliana kuwa katika suala hili la elimu katika kipindi hiki cha miaka mitano ya Ilani na miaka 10 tumekuwa na mafanikio makubwa na kwa *summary* naweza nikasema leo asilimia 95 ya watoto wa miaka 7 mpaka 13 wako shuleni mwaka huu. Mwaka 1995 walikuwa asilimia 55, leo asilimia 95, hayo ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2000 Bunge hili lilipochanguliwa asilimia 58 tu walikuwa shuleni, inamaanisha asilimia 42 walikuwa nje ya shule, leo asilimia 95 wako shuleni, walio nje ya shule maana yake ni asilimia 5. Lakini pia huko shuleni wanafaulu mitihani. Wastani wa kufaulu mwaka jana ilikuwa asilimia 49, lakini shule nyingi na Wilaya nyingi ufaulu wao ni zaidi ya asilimia 50. Kwa hiyo, kwa kweli tunaweza tukajipongeza, lakini hasa hasa tuwape pongezi walimu wanaofundisha watoto hawa katika shule zetu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni kwamba tunayo MMES. Tunao mpango ambao unalenga kupeleka nusu ya vijana wetu wanaomaliza darasa la saba kwenda sekondari ifikapo mwaka 2010. Matatizo yapo. Mawili makubwa yamesemewa sana, lakini lipo pia moja la wanafunzi wanaofaulu bado wengi wanabaki. Kwa hiyo, tunahitaji kuendelea na utekelezaji wa MMES wa kujenga sekondari nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la wahitimu wa kidato cha sita. Mwaka huu zimekutana *co-halt* mbili, waliomaliza mwaka jana na waliomaliza mwaka huu. Hapo napo tunahitaji kufanya *expansion* ya *Higher Education.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la *funding gap,* kwamba bajeti yetu ya MMES bado haijapata kila kitu kinachohitajika. Kuna shule nyingi hazina maabara, natudia tena kutoa wito kwa wenzetu, washiriki wetu katika maendeleo kwamba tushirikiane. Haya maabara ninayozungumzia yanahitajika kwa ajili ya wanafunzi ambao tayari wako shuleni. Wakubwa hawa wametuambia, nchi yoyote yenye mpango mzuri haitakosa fedha, ndiyo maana kwa imani kubwa tulianza utekelezaji kwa nguvukazi za Wananchi na tayari mwaka huu tumefungua shule 486. Ninachosema ni kwamba,

naomba *our development partners* wajitokeze haraka tukamilishe *shortcoming* hizi za kutokuwa na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda nimalizie kwa kusema kwamba, matatizo haya yote na ningeweza kuorodhesha mengi na Waheshimiwa Wabunge wameyasema mengi, tunayaona kwa sababu tumethubutu, tungekuwa hatukuthubutu tusingekuwa tunazungumzia haya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahehe huwa tukisalimiana tunasema; *Kamwene, kamwene.* Rahisi kabisa *kamwene, kamwene.* Lakini neno linalofuata ni *makasi,* yule anayesalimiwa anaweza akajibu, *gawenu mili. Mili* ni mwili, *makasi* maana yake ni habari ya kazi. Mwenzake anamjibu, aah, yaliona mwili. Kwa hiyo na hayo matatizo napenda niseme yaliona miili yetu sisi viongozi ili tuweze kuyashughulikia mpaka tuyamalize. Hatuwezi tukamaliza kila kitu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba katika awamu hii tumefunga kazi kwani tumefanikiwa kupeleka watoto shuleni na tumefanya maamuzi makubwa na mazito. Tumefuta ada katika Shule za Msingi, leo Elimu ya Msingi ni ya bure na ya lazima na tumepunguza ada katika Shule za Sekondari. Kutokana na sera sahihi za CCM, tunataka kupiga vita umaskini katika nchi yetu, lakini watoto hao wanafaulu, hatukuridhika na kufaulu tu, tumesema tuangalie na mtaala mpya. Watoto wanaweza wakawa wanafaulu kwa mtaala wa zamani, tumeangalia tumeweka mtaala mpya unaoendana na Karne ya 21, unaochukulia changamoto za soko huria na changamoto za *globalization. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Vyuo vyetu vya Ualimu tumeanzisha mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), tunaanza na walimu. Kila anayemaliza mafunzo ya ualimu atatoka anajua namna ya kutumia kompyuta. Huu ndiyo mwanzo mzuri wa kuanza kufundisha kompyuta katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo yote, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ..7,818,946,500/=

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kuwa nimeridhika kwamba kuna fungu bado litakuwa limewekwa kwa ajili ya *Tabora Schools,* lakini nafikiri kwa sababu Mheshimiwa Jackson Makwetta alizungumzia suala la *territorial,* ni kwa nini basi isianzishwe katika shule hizi za *Tabora Secondary?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba, niliomba kama kuna uwezekano Kamati ya Huduma za Jamii itembelee shule hizo, lakini bado sijaridhika kama kweli hilo limekubalika au vipi. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo kama Kamati watapenda kufanya hivyo na kama muda utaruhusu. Ninavyofahamu kwa taratibu za Bunge ni kwamba, Kamati hizi karibu zitafikia muda wa kutokuwepo, lakini kama muda utapatikana, hilo ni jambo ambalo ningelifurahia sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kuzungumzia katika *vote* hiyo hiyo 46, *sub-vote 1001,* kifungu cha 250100. Shule ya Sekondari ya Maposeni Songea mwaka 2002 ilipata ufadhili wa ujenzi wa bweni la wasichana kutoka Ubalozi wa Japan, lakini makubaliano ya ujenzi wa bweni hilo Serikali ilikubali kwamba itatoa fedha kwa ajili ya vitanda katika bweni hilo na hivyo Ubalozi utoe fedha kwa ajili ya kujenga bweni lenyewe katika shule hiyo. Ubalozi umeshafanya kazi ile na imekamilika kwa asilimia 100, lakini bweni hilo linashindwa kufunguliwa mpaka sasa hivi kwa sababu Serikali bado haijatoa fedha hiyo kwa ajili ya kuweka vitanda kwenye hilo bweni la watoto wa kike kwenye shule ya Sekondari ya Maposeni, Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri akubali kupokea ombi hilo tena rasmi na kulifanyia utekelezaji ili basi Ubalozi huo utakapokuja kufungua bweni hilo la wasichana, Serikali yetu ya Tanzania pia ionekane imetimiza ahadi yake iliyotoa katika mkataba ule wa kujenga bweni hilo la wasichana katika Shule ya Sekondari ya Maposeni na kama anakubaliana, ningependa kufahamu ni lini basi Serikali itatoa hiyo fedha ili wale watoto wa kike waweze kupata mahali pa kulala katika hiyo Shule ya Sekondari? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mwalimu Jenista Mhagama, alinisikiliza vizuri nilisema kwamba, siwezi kujibu kila kitu hapa kutokana na kwamba wachangiaji kuwa wengi sana na nikasema mambo mengine tumeyarekodi, ni pamoja na hilo alilolisema.

Mimi niko hapa na timu nzima, Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari yuko hapa, Mkurugenzi wa Mipango yuko hapa na tumekwisharekodi hilo jambo, hatuwezi tukaacha msaada tuliopewa na rafiki zetu wa kutoka Japan uwe hauna faida kwa wanafunzi wale kwa sababu ya hiyo ahadi ndogo ya vitanda. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami naomba nipate maelezo tu kuhusu *vote* hiyo 46, programu ya 10, *sub-vote 1001.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa namkumbusha Mheshimiwa Waziri majibu yake ya swali langu namba 37 lililojibiwa tarehe 10 Juni, 2005 linalohusu MMES.

Katika majibu yake alisema kwamba amekwishatoa shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 54 na nyumba 8 katika Wilaya ya Kondoa. Mimi nikaongeza swali la nyongeza nikamwambia, hapana, hizo pesa bado hazijafika. Leo nimechangia kutaka kujua kama hiyo pesa imefika na iko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi kwamba, pesa iliyofika ni ya madarasa 26 shilingi milioni 182 na nyumba 8 shilingi milioni 72, jumla shilingi milioni 254 na siyo shilingi milioni 450 kama yeye alivyojibu katika swali langu.

Sasa, naomba niulize kwamba, milioni 196 za vyumba vya madarasa 28 kama kweli zimetumwa ziko wapi? Ni *specific* tu kwamba angetakiwa kuniambia kwamba ziko Shule ya Sekondari fulani ili mimi nifuatilie kwa sababu nimeulizia viongozi wote wa Wilaya wamesema fedha hizo bado hawajapokea. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Paschal Degera, kwamba, majibu niliyomjibu hapa Bungeni ni kutokana na taarifa zilizo katika *record* ya Wizara yangu. Sasa kama kumetokea kasoro au nyingine ziko njiani katika utaratibu, si jambo rahisi kuweza kulijibu hapa. Kama lile jibu nililitoa kwa makosa inabidi tuangalie kweli ilikuwa ni kwa makosa, lakini si jambo ambalo naweza kulijibu tukiwa hapa kwenye Kamati ya *Supply* kwa sababu sina *record* za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, wataalam wangu wako hapa tunaweza tukakaa naye na kama tu imetokea makosa bado tunazo fedha katika Bajeti ya mwaka huu. Tumepanga fedha kwa ajili ya madarasa, ni suala tu la Mheshimiwa Mbunge, *DO* na *REO* watuambie yale majengo ambayo wamekwishayajenga yanahitaji vifaa vya kumalizia yaani vifaa vya kuyaezekea ili yaweze kutumika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Pascal Degera awe mvumilivu kwani mvumilivu hula mbivu, tutachambua tukiwa hapa ili tuweze kumaliza hilo tatizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal Degera, nadhani umeridhika.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya pili, lakini pia namshukuru Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa majibu yake. Kwa sababu hili jibu liko kwenye *Hansard,* naomba angetekeleza kwa kunihakikishia kwamba kabla ya Kikao cha Bajeti hii kuisha anipatie hizo shilingi milioni 186 ili niweze kukamilisha hayo majengo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa fedha za Serikali, mali ya umma, hicho anachoomba Mheshimiwa Mbunge hakiwezekaniki kabisa. Mimi siwezi kuahidi hapa tu kwamba, baada ya siku chache nitamwambia milioni 150 hizi hapa, hapana, ni lazima twende ndani ya utaratibu wa Serikali na mimi naongea hapa kama Serikali na nimesema tutachambua tuone kasoro hiyo iko wapi. Kama kulikuwa na makosa, napenda niseme MMES inaendelea na katika Bajeti ya mwaka huu tumepanga fedha kwa ajili ya majengo ya shule. Kama kuna

majengo na kweli Mheshimiwa Mbunge ananiambia yapo, ni lazima tutayapatia fedha kwa sababu yatakuwa katika mpango.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti,katika mchango wangu wa maandishi ambao nimempelekea Mheshimiwa Waziri nilizungumzia suala la udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali kwamba sasa Wizara hii ni moja ya Wizara ambazo zinatengewa fedha za kutosha, lakini pia kwa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bado kuna mianya mingi ambayo inasababisha upotevu wa fedha katika Wizara ya Elimu na Utamaduni na nikapenda anipe maelezo kwamba nimewahi kuzungumzia hoja ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi wakati wa kunyunyizia dawa katika shule tatu Mkoani Mara na katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri ndani ya Bunge lako Tukufu amekuwa akizungumza kwamba angenipatia maelezo ya hatua ambazo zimechukuliwa. Sasa ningependa kupitia katika Kamati hii anieleze ni hatua zipi ambazo zimechukuliwa kutokana na hili tatizo la ukiukwaji wa taratibu katika manunuzi ya vifaa vya Serikali.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, aliwahi kuleta hilo jambo na hilo jambo tulilisimamia tukalifikisha kwa vyombo vya dola vinavyohusika na uchunguzi na taarifa ya mwisho niliyopewa ni kwamba katika uchunguzi wao hawakuona kama kulikuwa na kosa linaloshtakika, ila kulikuwa na kukosewa kwa taratibu. Ndivyo jambo hili lilipofikia.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukipitisha Sheria ya Manunuzi *(Procurement Act)* katika Bunge lako iliainisha kwamba endapo mtumishi wa umma anakwenda kinyume na ile sheria ni hatua zipi anastahili achukuliwa. Kwa hiyo, ningependa Waziri aniambie kama mtumishi alikiuka taratibu za manunuzi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya *Procurement* kuna hatua ambazo inabidi achukuliwe. Ni hatua zipi ambazo Serikali imewachukulia watumishi ambao walivunja hiyo Sheria ya Manunuzi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si rahisi kwa mimi sasa hivi kusema ni hatua gani zilichukuliwa kwa huyo mtumishi. Kama Mheshimiwa Mbunge atahitaji maelezo ya sura hiyo inabidi ama aniandikie, ama aulize swali la Bunge nitakuwa tayari kutoa majibu, lakini katika Kamati ya Matumizi sikujiandaa kwa jambo la nyuma kiasi hicho.

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa Waziri unaweza kumpa majibu wakati tukiwa hapa kabla hatujaondoka.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Sawa.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwani ametoa majibu ya mengi niliyouliza, lakini ningependa kusisitiza machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *vote 46, sub-vote 1001,* niseme *basic salary* au hicho kifungu cha 260200 nataka tu kufahamu kwa sababu moja ya matatizo ya elimu maalum ni ukosefu wa vifaa na nilishatoa mfano hapa kwamba ule mtambo uliopo Shule ya Uhuru Mchanganyiko ufanyiwe kazi ili baadhi ya matatizo yaweze kutatulika hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kutoona. Je, katika bajeti hii Serikali imetenga kiasi gani cha fedha za kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia watoto wenye ulemavu nchini kwa levels zote za msingi na sekondari? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba ndani ya mchango wa maandishi nilieleza kuwa katika ziara zangu kuna mahali nilikuta watoto wenye ulemavu ambao wako kwenye vitengo, wataalam pale wanafahamu, hawahesabiwi ndani ya *total* ya wanafunzi wa shule nzima ili kusudi fedha za ruzuku ambazo ni *capitation fees* ziweze kuwa *calculated* kutokana na idadi hiyo, wanatengwa. Kwa hiyo, wao katika ile *capitation fees* hawamo, lakini shule iko ndani ya mazingira ya wale wengine wote ambao hawana ulemavu, kwa misingi hiyo hawapati huduma wala uji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii niliikuta Songea katika Mkoa wa Ruvuma ambako watoto wale hata hela ya uji wa asubuhi hawapewi kwa sababu ni hawa wenye matatizo ya akili ambao wanahitaji kula, wao kula kula kidogo ndiyo moja ya njia za kujifunza maana tunatofautiana katika hali ya ulemavu, hawana uji wala hawana chochote. Lile darasa sijui liliochwa na Wamisionari tangu mwaka gani, ni mashimo matupu na wale watoto ndiyo hivyo *balance* ya akili haipo, kuanguka ni rahisi, lakini ndiyo wako hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nataka kufahamu, walimu wa shule za msingi wanapaswa kufanya nini na utaratibu ni upi na kama huyu mmojawapo ambaye alishakiuka wale watoto hawakuwa kwenye hesabu, Serikali itamfanyia nini huyu? Nataka kufahamu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajili ya vifaa, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tutakapofika kwenye *vote* ya Afisa Elimu Kiongozi ambako ndiko zinatengwa fedha kwa ajili ya *Special Education* hapo tutaweza kufafanua ni fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Capitation Grants,* inatolewa kwa wanafunzi wote, hakuna ubaguzi. Kwa hiyo, hilo tatizo analolielezea Mheshimiwa Margareth Mkanga nashindwa kabisa kulielewa. *Capitation Grant* ni kiwango kinachotolewa kwenye shule. Ile *capita* maana yake ni *per capita,* unahesabu wanafunzi mara fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya shule ile. Kwa hiyo, hilo tatizo labda nikilijua kwa undani tunaweza tukalitafutia jawabu.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata mwongozo kwamba suala la vifaa niulize kwenye *development.* Lakini kuhusu suala hili ni kwamba haya mambo tunayaona tunakotembea.

Ushauri wangu ni kwamba, basi Wizara itoe maelekezo tena kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kwa sababu suala hili lipo. Pale Peramiho Shule ya Msingi kuna watoto wa mtindio wa ubongo wala siyo uongo nimekuta jambo hili. Kwa hiyo, watoe maelekezo upya kwa sababu mwingine anaweza akasikia, akapuuzia tu, sasa lawama inakuwa kwa Wizara. Kwa hiyo, naiomba Wizara iandike maelekezo upya ili suala hili lisijitokeze tena.. Inatia huruma, huku ndiyo kutengwa. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huo narudia kuukubali kwa sababu kama nilivyosema kwamba Mheshimiwa Margareth Mkanga, alitoa ushauri mwingi ambao nilisema tumeusikia, tunaupokea. Kwa hiyo, kama kunahitajika ufafanuzi zaidi kuhusu suala la *Capitation Grant* kwenye shule za wenye ulemevu, nitamwagiza Afisa Elimu Kiongozi atoe ufafanuzi huo.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sikuwa katika *list* ya kwanza nimeona nihamishe swali langu mpaka *sub-vote 4001.* Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 466,476,300/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,301,864,200/=
Kifungu 2001 - *Chief Education Officer* ... ... ... ... ... ... ... ... 5,404,684,300/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margareth Mkanga, bado una swali hapo?

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Hapana.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Inspectorate* ... ... ... .... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 3,612,351,200/=

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza katika *sub-vote 2002, sub-vote* tena 250100 katika Jimbo la Kibiti tulikuwa na shule mbili za sekondari ambazo wakaguzi walikagua mapema kabisa lakini wakachelewa kupeleka ripoti Wizarani mpaka muda ule wa kusajili shule hizo umepita na tulitegemea mwaka huu tuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza. Lakini Waziri anasema kwamba shule zimechelewa kusajiliwa. Sasa kosa ni la *inspectors* wao hawakupeleka ripoti mapema Wizarani kwa nini waadhibiwe wananchi ambao walijenga shule zile na ambao wanataka kuchukua wanafunzi zaidi waweze kuongeza idadi ya wanafunzi katika shule ya sekondari? Kwa hiyo, mimi naomba Waziri, atoe maelezo sababu gani zilizofanya tuadhibiwe sisi wakati kosa ni la *inspectors.*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasikitika sana kusikia kwamba shule hizo zilichelewa kufunguliwa kwa sababu

ya makosa ya *inspector* kutokana na anavyosema Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi. Lakini hata ukichukulia nani amekosa maana yake sasa hivi ili niridhike makosa kutokana na *inspectors* inabidi niangalie pia taarifa zao walizozitoa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge, anaweza akafikiri ni makosa ya *inspectors* kumbe ni yale waliyoyaona kwa sababu lazima tunaweza kusajiri shule kutokana na yale ambayo wameyahakiki wakaguzi.

Mimi ninavyofahamu na ndiyo utaratibu taarifa za ukaguzi ni *confidential.* Kwa hiyo, siamini kama Mheshimiwa Mbunge, aliziona hizo taarifa. Kwa hiyo, akitaka maelezo sahihi mpaka niziangalie zile taarifa nione kosa lilipo. Lakini sasa ikishafikia kwamba muda umepita hakuna tunachoweza kufanya, hatuwezi tukaruhusu shule ifunguliwe wakati karibu muhula mzima umepita. Shule hizi zinaendeshwa kwa kufuatwa *syllabus* ambazo zina muda wake kufundisha. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Mbunge, avumilie mpaka nitakapopata nafasi ya kuona ripoti za wakaguzi ndipo nitakapoweza kumpa maelezo ya usahihi.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini Mheshimiwa Waziri, anajua hilo kwa sababu tumemlalamikia kwa kitambo lakini Mheshimiwa Waziri, akasema tuandike barua ili shule hizo mwakani zisajiliwe na wachukuliwe watoto katika mwaka huu ili wahamishiwe mwakani. Lakini hakutaka maelezo ya hao *inspectors* walikuwa wamechelewa, kwa nini na angetaka hayo tungemweleza, bahati mbaya hakuyataka hayo maelezo ingawa hiyo ripoti ni *confidential,* sawa sawa haturuhusiwi kuona, lakini sisi wengine ni wana taaluma tunajua, mimi nimefundisha katika *primary schools,* nimefundisha katika *secondary schools,* nimefundisha Chuo Kikuu kwa hiyo, nafahamu ikiwa kuna kosa lolote katika shule katika mambo ya ukaguzi nayafahamu. Sasa angalitaka hayo Mheshimiwa Waziri, tungemweleza. Lakini pengine ingekuwa imefaa zaidi kuwaona hawa ambao walikuwa wamefanya makosa ili kuwaadhibu kwa kosa hilo kwa sababu wamefanya makusudi.

Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ingawa hiyo ripoti ni *confidential* lakini ni kwamba kwa sababu gani sisi hatuwezi kujulishwa kwamba shule zenu haziwezi kusajiliwa kwa sababu zina makosa kadhaa, kadhaa, ili wananchi waweze kufahamu, vinginevyo wananchi hawaweze kujua chochote wakati wanaposubiri viongozi wao tumechukua uzito huo wa kuweza kuyajua katika Wizara. Kwa hiyo, inamwomba Waziri aweze kutoa ahadi hapa si suala la kuzisajili tu mwakani hapana, ni kwamba hawa vijana waliokuwa waingie mwaka huu *form one* wataingia *form two* mwakani? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, kama ifuatavyo:-

Suala siyo la kupanda tu madarasa kwamba utoke darasa hili kwenda darasa lile, lazima upate elimu inayohitajika kwa darasa lile ndiyo uende katika darasa lile ndiyo uende katika darasa lingine. Kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii napenda nifafanue anayosema tulizungumza.

Mimi ni kweli alinileteа hilo lalamiko nikamwambia Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa tumekwishamaliza karibu muhula mmoja kwa hiyo, hata tufanye jitihada ya namna gani ya kuiona hiyo ripoti haitawezekani kuruhusu shule ifunguliwe mwaka huu. Isipokuwa kama nitapokea ombi kutoka kwako Mheshimiwa Mbunge, kama kweli wanafunzi walikwisha kuwa tayari kuanza ninachoweza kuruhusu kwa madaraka niliyonayo ni kwamba wale ambao walikwishateuliwa na kuandikishwa, tuwaandikishe kwa maana ya kuwa kidato cha kwanza Januari mwaka kesho. Wakati huo huo tutoe ruzuku ya maendeleo kuongeza mikondo pale ili wale wa darasa la saba mwaka huu nao tuwawekee mikondo miwili. Nilisema tulipata maombi hayo tunaweza ku-*accommodate* tatizo hilo kwa sura hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hawawezi kuruka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *MANTEP Institute* ... .... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 45,826,300/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu kifungu kidogo cha 2003 kifungu kidogo cha 250100 mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MANTEP* ni Taasisi ambayo tulikuwa tunajua iko chini ya Wizara ya Elimu. Lakini kutokana na taarifa tulizonazo kutoka kwenye tovuti, hii Taasisi sasa inaendeshwa na shirika binafsi na ushahidi mwingine ni katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa pili kifungu cha nne (f) ameorodhesha Taasisi zilizo chini ya Wizara na *MANTEP* haiko katika orodha ile. Lakini *MANTEP* inatengewa mishahara katika Bajeti hii na imetengewa mshahara tu haikutengewa kitu kingine chochote. Sasa je, tunalipa mishahara hewa ama tunafanya nini? *(Makofi)*

Pili, ninavyojua *MANTEP* ilitolewa kwa Wizara ya Elimu na Kanisa la Katoliki. Ikiwa ni pamoja na nyumba ya kwanza ya Mapadri pale Bagamoyo Mjini. Kama ni kweli inaendesha sasa na shirika binafsi ambalo vinatengewa mishahara na Serikali je na zile za Mapadri hili shirika limekabidhiwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika kitabu hicho hicho cha Bajeti aliposoma *paragraph* ya nne, sasa atoke ukurasa wa pili aende ukurasa wa tatu. Anapoona wakala wa maendeleo ya uongozi wa Elimu *ADEM* ndiyo *MANTEP.* Imebadilisha kuwa *agency* ya Serikali. Lakini kwa sababu haijitegemei basi inapewa fedha katika Bajeti kwa ajili ya kulipa mshahara.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kama Taasisi imebadilishwa jina na labda ikapewa majukumu zaidi au pungufu Bunge lako Tukufu lingeambiwa hivyo, siyo kupewa Bajeti kuwa Marehemu tuwe tunapewa fedha kwa ajili ya kitu ambacho hakipo Waziri akiri sasa hivi kwamba

*MANTEP* haipo, kwa hiyo, hamna haja ya kuipigia Bajeti. Halafu alete maombi kwa hiyo, Taasisi nyingine ambayo anaisema. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni makosa katika uchapaji tu. Ninachopenda kusahihisha ni kwamba hapo ilipoandikwa *MANTEP Institute* ni *ADEM* na sheria na taratibu za kuanzisha *ADEM* zimepita katika utaratibu wote wa sheria. Ni chombo cha Kiserikali ni *agency* ya Serikali sasa inawezekana kwamba katika *typing* labda kwenye *computer* kwenye mitambo hawajabadilisha tu, vitabu vya hazina hawajabadilisha tu hilo jina. Inabidi isomeke kama *ADEM* kwa hiyo, mimi nakiri kama anavyotaka nikiri Mheshimiwa Wakili msomi nakiri kwamba inayoonekana kama *MANTEP* ndiyo *ADEM* alikubali hilo badiliko.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect* ni tofauti kufanya marekebisho kwenye hotuba ya Waziri ambayo ni yake na kufanya kwenye marekebisho kwenye kitabu cha hazina ambacho ni cha Wizara ya Fedha ni kitabu cha Serikali.

Sasa je, Waziri atakubali kuondoa hii *item* kutoka kwenye Bajeti kwa sababu hana hiyo *institute* kwa hiyo, hawezi kuiombea fedha halafu akaja kwa njia nyingine baadaye baada ya kuomba fedha kutoka kwa hii *institute. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ndivyo anavyosema kwamba ni makosa. Ndivyo anavyo sahihisha kwenye *document* ya Serikali. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Basic Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 582,447,500/=
Kifungu 4001- *Secondary Education* ... .... ... ... ... ... ... ... ... 40,139,691,600/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kutumia kifungu kidogo cha 4001 na kifungu kidogo zaidi 250100 mishahara. Katika mchango wa maandishi nilikuwa nimeomba msaada kuhusu shule ya Karatu Sekondari au *Karatu High School* wengine wanavyoita.

Shule hii watoto wameandamana mara kadhaa kwa sababu ya kukosekana kwa walimu na kwa safari hii shule hii imefanywa kuwa ipokee kidato cha tano tu jambo ambalo linazidi kuongeza tatizo la Walimu.

Sasa mimi sina ugomvi sana na Waziri, nilitaka uhakika ni lini Walimu watapelekwa ili wale watoto wasikae kwenye hiyo shule kwa muda mrefu na kukosa

maana yake kuchelewa kufungua shule ni kitu kimoja lakini kuwepo shuleni na kutokuwa na Walimu ina athari ile ile ya kutokuwepo shuleni vile vile.

Lakini ya pili nilikuwa nimeeleza kwamba shule hii imekumbwa pia na tatizo la uongozi. Mwalimu aliyeko pale Mkuu wa Shule nimeeleza pale kwamba ana tatizo na uongozi umeshindikana bodi haikutani, *Procurement Act* haifuatwi, fedha zinatumika.

Sasa nilitaka uhakika kwamba Waziri  si lazima anipe jibu sasa hivi kwamba itakuwaje, lakini anihakikishe kwamba itachukuliwa hatua kwa sababu linahitaji uchunguzi. Nilikwisha kulieleza kwenye vikao mbalimbali mpaka kwenye vikao vya Mikoa lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Naona kuna athari itatokea na itakapotokea athari hii shule ni ya Serikali ni jina letu wote na Elimu ya watoto wetu inaathirika. Nilitaka tu uhakika kwamba Waziri atalichukulia hatua au vipi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubali kwamba Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ameyasema hayo anayoyasema katika mchango wake aliotoa kwa maandishi. Sikuweza kupata maelezo ya ufasaha juu ya jambo lenyewe kwa sababu mchango wake umefika dakika za mwisho mwisho kabisa, nimeusoma, nimeyaona hayo matatizo anayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwahidi kwamba tutayafanyia kazi. Ningekuwa niliyapata mapema huenda wakati Bunge lilipokuwa limesitishwa ningekuwa nimepata maelezo zaidi. Kwa hiyo, tutalishughulikia. *(Makofi)*

**MHE. *MAJOR* JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niko kwenye hii *sub vote 4001,* kifungu kidogo cha 250300 na kabla sijasema hili napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kazi nzuri aliyoifanya kipindi chote cha miaka mitano. Hongera sana mwalimu, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Lakini pia tumeweza kupata *secondary schools* nyingi kwa kipindi hiki na katika jimbo langu la Vunjo zimepatikana *secondary school 32.*

Sasa kutokana na wingi huu wa sekondari imepelekea walimu kuwa wachache, lakini pia tumewapata wale waliomaliza kidato cha sita kusaidia kufundisha ili shule hizo zikisubiri walimu wenye taaluma waingie ili wasaidiane. Swali langu ni kwamba katika hili watu wanapopewa wapo katika kifungu cha *basic salary* au kifungu cha *employment allowance?* Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, kwamba maelezo hayo

nilikwishayatoa kwamba tumefanya utaratibu, mpango maalum wa kuwapata walimu wanaohitajika wa ziada baada ya kuajiri wale wote wenye sifa.

Sasa hivi tunao karibu 600 wanapewa *induction course* yaani mafunzo maalum, yeye kama afisa wa Jeshi anajua *induction course* ni kitu gani, wanapewa *induction course* ili waende kujaza hayo mapengo. Katika Bajeti hii fedha ziko katika kifungu cha mishahara kwa ajili ya kuwalipa hao ambao tunawachukua. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Teachers Education*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 5,548,228,000/=
Kifungu 6001- *Culture and National Languages* ... ... ... .... 1,149,895,100/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ... 230,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ...... ... ... ... ... ... ... 2,870,000,000/=
Kifungu 2001 -*Chief Education Officer* ... ... ... ... ... ... ... ... ...1,235,933,600/=
Kifungu 2002 - *Inspectorate* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 100,000,000/=
Kifungu 3001 - *Basic Education*. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... .. 36,730,617,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 - *Secondary Education*... ... ... ... ... ... ... ... ... 64,343,312,800/=

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha 4001 kifungu kidogo cha 4301 ujenzi wa maabara na ununuzi wa vifaa vya maabara huu ni mkopo katuko Benki ya Maendeleo ya Afrika na hii siyo mara ya kwanza tunakopa kwa ajili ya maabara. Siku zilizopita ujenzi wa maabara hizi imekuwa kama siri kubwa. Narejea huu ni mkopo lakini ujenzi wa wapi kujenga maabara imekuwa siri kubwa.

Sasa mkopo wa sasa ni mkubwa zaidi inategemewa maabara zaidi 80 zitajengwa. Wizara itatumia vigezo gani sasa kwa sababu tulishaanza kunung'unika mara nyingi. Umeweza kujenga Wilaya moja maabara mpaka tatu katika mikopo ya awali, Wilaya

zingine zaidi ya 100 hazina maabara hata moja. Sasa Waziri atuambie ni vigezo gani hasa vinatumika kutumia mkopo huu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na pengine kabla hatujaondoka hapa maabara hizi 80 zitajengwa wapi? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti tunatenga fedha kwa ajili ya kazi maalum kama ujenzi wa maabara. Sasa upangaji tuanze na wapi ifuatiwe na wapi hilo ni jambo ambalo liko katika utekelezaji, linasimamiwa na wataalam kwa kuangalia ukubwa wa shida zilivyo na zinavyozidiana tuanze na wapi, tufanye wapi hivyo ndiyo utaratibu tunaoutumia.

Kwa hiyo, nikiulizwa hapa mimi niseme hizi fedha zitakwenda kujenga maabara za wapi, jibu sina kwa sababu bado hazijapangwa ni katika utekelezaji na kwa kadri fedha zinavyotoka kutoka hazina ile *realise of funds* ndiyo tunapanga tuanze na wapi halafu tufuatie wapi. Huu ndiyo utaratibu wa Bajeti hizi za Serikali na ninahakika Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge mwenzangu ambaye pia amewahi kuwa Waziri anaelewa kwamba huu ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunanung'uka kwamba haki haikuwa inatendeka kila Wilaya kwa sasa ina haja ya kuwa angalau na shule moja yenye maabara nzuri. Sasa ili haki itendeke sasa Waziri angalau atupe hata vigezo basi itakavyotumika ili ujenzi wa maabara uweze ukaelezeka kwa sababu miaka zamani haielezeki kuna Wilaya nyingine najua zimeshajengewa zaidi ya maabara tatu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, anasema niseme sasa hivi, mimi naweza kusema sasa hivi ni yale ambayo tumekwisha yafanya haya ambayo yatashughulikiwa ndani ya utaratibu ningemshauri Mheshimiwa Philip Marmo, tuyaache yabakie ndani ya utaratibu, *after all* tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu ndiyo unaweza ukaahidi hapa jambo ambalo halafu tunakwenda kwenye uchaguzi huu, ama usichaguliwe ama Serikali ikaundwa siyo wewe ni mwingine kwa hiyo, tunataka kujipeleka mahali ambapo tutakuwa tunasema tu maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema jambo hili litasimamiwa kwa kuzingatia utaratibu wapi kuna shida zaidi na kama Mheshimiwa Philip Marmo, anachopendekeza tusirundike katika Wilaya moja kabla ya Wilaya nyingine tutafanya mambo haya kwa uwazi na ukweli na Mheshimiwa Philip Marmo, anaweza akaangalia kwamba katika kitabu hiki cha Bajeti nimetoa maelezo ukurasa wa 50 shule 26 ambazo zimejengewa maabara na kupelekewa samani zimeorodheshwa zote na ndivyo tunavyofanya.

Kwa hiyo, kama ni ushauri wake kwamba zisiende eneo moja tu namhakikishia kwamba mimi na wataalam wangu tutazingatia hilo na pia tutatoa taarifa kama tulivyotoa katika ukurasa wa 50. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Teacher Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...2,992,000,000/=

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuomba nipate ufafanuzi. Katika michango moja ya nililolishauri lakini nilijua tu kwamba nitapata jawabu ni kwa kiasi gani Wizara imejiandaa katika utaratibu huu wa kufundisha somo hili kuwa la lazima kwa walimu watarajali wote watakaoanza nadhani mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu gani umeshapangwa mzuri wa kuwawezesha wanafunzi wa Tarajali, wanachuo watakaokuwa na matatizo ya ulemavu wa macho kwa sababu hata kwenye *Policy and Planning* nimeona kwa hiyo ni kitu ambacho naamini Wizara inaweza ikanisaidia tu kunijibu au nitoke na wazo kwamba hao wasioona basi tena hawawezi ku-*qualify* kusomea ualimu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Margareth Mkanga, kwamba kama inavyosema kwenye kifungu hiki fedha hizi zimepangwa kwa ajili ya vyuo vyote vya ualimu pamoja na Chuo cha Patandi ambacho kime-*specialize* kwenye walimu wenye ulemavu. Sasa teknolojia hiyo ya mawasiliano kwa wenzetu wasioona inafanywaje katika chuo hiki.

Kama nilivyosema mimi kwamba mpango huu ni pamoja na *technical assistance* kutoka Sweden na nchi ya Sweden ni miongoni mwa nchi ambazo zina programu nzuri kwa ajili ya walemavu na hasa wasioona. Kwa hiyo, mimi nina imani kubwa, lakini ukitaka nieleze hapa itakuwaje mimi ninachoweza kusema na mimi *I look forward to visit,* kuona wanafanyaje kwa wasioona. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 - *Culture and National Languages*... ... ... ... ... 862,232,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kifungu kwa

kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Jumatano saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.29 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano*
*Tarehe 6 Julai, 2005 saa tatu asubuhi)*